

## SURA YA 1

# MWANZO


HADITHI HII IMEHADITHIWA KATIKA KITABU CHA ZAMANI, KITABU CHENYE MAELFU YA MIAKA. KILA NENO NITAKALO KUAMBIA NI KWELI. BAADHI YAKE ITAKUWA NGUMU KUAMINI,
LAKINI UKWELI KWA MARA NYINGI NI MGUMU KULIKO TAMTHILIYA YA UONGO


HAPO MWANZO, KABLA YA MTU WA KWANZA KUUMBWA, KABLA YA DUNIA, JUA, NYOTA, HATA KABLA MWANGA NA WAKATI KUUMBWA, KULIKUWA NA MUNGU.


YEYE PEKE YAKE ALIKUWEPO BILA MWANZO, LAKINI HAKUWA NA UPWEKE. TOFAUTI NA MTU MWENYE MWANZO MWISHO, MUNGU ANADUMU KWA PAMOJA KAMA NAFSI TATU. NAFSI ZOTE TATU ZINA USAWA WA UMILELE NA UMOJA WA KIASILI, KIMATENDO NA NGUVU. KABLA YA MWANADAMU, ALIDUMU YEYE MWENYEWE NA UPENDO WENYE USAWA.
LAKINI MUNGU ALITAKA KUSHIRIKI MAISHA YAKE. ALITAKA MARAFIKI NA MAJIRANI.


BIBLIA* INATUAMBIA KWAMBA MUNGU ALIUMBA AINA TOFAUTI YA VIUMBE VYA KIMALAIKA KWA MADHUMUNI YA KUTOA SIFA KARIBU NA KITI CHAKE CHA ENZI, LAKINI MMOJA ALIYEITWA LUSIFA ALIONGOZA THELUTHI MOJA YA WAO KATIKA KUMUASI. MUNGU ALIWAFUKUZA KUTOKA MBINGUNI NA JINA LA LUSIFA LILIBADILISHWA KUWA SHETANI.


LAKINI HII SIO HADITHI YAO.
HII NI HADITHI YA MUNGU AKIFANYA KAZI KUPITIA WANADAMU.
ISAYA 45:18 - * TAZAMA UKURASA WA 322 KWA MAELEZO MAFUPI YA KITABU KINACHOITWA BIBLIA. KWA HABARI ZAIDI JUU YA SHETANI, TAZAMA: ISAYA 14: 12-14; EZEKIELI 28: 13-19; MATHAYO 25:41; LUKA 10:18; UFUNUO 12: 4, 20: 2


HAPO MWANZO MUNGU ALIUMBA MBINGU NA DUNIA. WAKATI HUU DUNIA ILIKUWA HAINA UMBO, TENA ILIKUWA KUBWA. GIZA LILIKUWA JUU YA USO WA VILINDI VYA MAJI, NAYE ROHO WA MUNGU ALIKUWA AMETULIA JUU YA MAJI


GHAFLA MUNGU AKANENA GIZANI...
"KUWE NA MWANGAZA"


HAIKUWA JINSI BAADHI YA WATU LEO WANADHANIA. MUUMBAJI HAKUTUMIA NJIA YA KISAYANSI YA EVOLUSHENI. ALIUMBA VITU VYOTE KWA KUTUMIA MANENO; KWA KUTAMKA VYOTE VILIVYO VIKAWA. KATIKA SIKU SITA ZA MASAA 24 KILA SIKU, MUNGU ALIFANYA MIMEA NA WANYAMA ILI WAIJAZE DUNIA.
TAKRIBAN MWAKA 4004 B.C. - MWANZO 1: 2-3 3



SIKU YA SITA, WAOVU WAKIWA WANATAZAMA, MUNGU AKAUMBA KIUMBE KIPYA KUTOKA MAVUMBINI YA ARDHI.


MUNGU ALIPUMULIA PUMZI YAKE MWENYEWE KWA UDONGO USIO NA UHAI, NA MTU AKAWA NAFSI HAI. NA AKAWA AMEUMBWA KWA MFANO WA MUNGU - NA ASILI YAKE IKIWA KUU KULIKO YA WANYAMA.




MWANZO 1:31, 2: 7


KILA SIKU, MUNGU ALIKUWA ANAZUNGUMZA NA ADAMU, NA MAISHA YALIPENDEZA NA KUFANA SANA. MUNGU ALIMLETEA ADAMU WANYAMA WOTE ILI AWEZE KUWAPA MAJINA. ALIPOKUWA ANAWAPA MAJINA, ALIGUNDUA KUWA ALIKUWA MPWEKE NA HAKUWA NA MWENZAKE KAMA VILE WANYAMA WALIVYOKUWA.


NA MUNGU AKASEMA ...
NITAFANYIA ADAMU MWENZI WA KUMSAIDIA.
MUNGU ALISABABISHA ADAMU KUPATA USINGIZI MZITO NA KISHA KUCHUKUA UBAVU KUTOKA UPANDE WAKE. KUTUMIA HICHO KIPANDE, MUNGU AKAMFANYIA MWANAMKE AMBAYE NI MSAIDIZI MPENZI WA ADAMU.


MUNGU ALIMWAMSHA ADAMU NA KUMLETA MWANAMKE KWAKE. AKAWAAMBIA WAPATE WATOTO NA KUJAZA DUNIA, NA ADAMU AKAMPA JINA EVA HUYO MKE WAKE MPYA NA MZURI.
YEYE NI MFUPA WA MIFUPA YANGU NA NYAMA YA NYAMA YANGU.
SHETANI, YULE MWOVU, ALIKUWA ANATAZAMA.
WOTE WAWILI WALIKUWA UCHI, LAKINI, KAMA WATOTO, HAWAKUTAMBUA UCHI WAO.


WALIKUWA NA FURAHA KATIKA BUSTANI. HAKUKUWA NA DHAMBI, WALA NJAA; HAKUKUWA NA JOTO SANA WALA BARIDI SANA.
MUNGU AKANENA KUHUSU MITI, AKISEMA ...
UKO HURU KULA MATUNDA YA MTI KATIKA BUSTANI, LAKINI KAMWE USILE MATUNDA YA MTI ULIO KATIKATI YA BUSTANI, KWA MAANA SIKU UTAKAPOKULA MATUNDA YAKE, HAKIKA UTAKUFA.
MWANZO 1:28, 2: 2, 16-22, 25


SHETANI ALIMCHUKIA MUNGU NA ALITAKA KUHARIBU KILE MUNGU ALIKUWA AKIFANYA, LAKINI ALIHITAJI NJIA YA KUWASILIANA NA EVA, KWA HIVYO ALIINGIA MWILI WA KIUMBE KIZURI NA KUSEMA NA EVA KUPITIA KINYWA CHA KIUMBE HICHO
JE, MUNGU ALIKUAMBIA KUWA HUWEZI UKALA KUTOKA KWA KILA MTI ULIO KATIKA BUSTANI?


ALISEMA SISI TUNAWEZA KULA KUTOKA KWA KILA MTI ISIPOKUWA HUU, IWAPO TUTAUGUZA, HAKIKA TUTAKUFA.
HA! HAUTAKUFA. UTAKUWA KAMA MIUNGU UTAKAPOKULA. BADALA YAKE UTAPATA MAARIFA KAMA SISI, NA UTAFAHAMU WEMA NA UOVU.




EVA HAKUFAHAMU MAANA KAMILI YA WEMA NA UOVU.


EVA AKAMUASI MUNGU NA AKALA LILE TUNDA
KWA KUCHELEWA SANA, EVA ALITAMBUA KWAMBA AMEKWISHA KUHADAIWA, HILO LIKAMSABABISHA YEYE KUELEWA WEMA NA UOVU, KISHA UOVU UKACHUKUA USHUKANI




MWANZO 3: 1-6; UFUNUO 20: 2


WAKAPATA MAARIFA KISHA WALIAIBIKIA UCHI WAO.
HA, HA, HA! MUNGU ATAWAUA SASA! TAZAMENI ALICHONIFANYIA MIMI


TUMEFANYA NINI JAMANI?
TUMEMUASI MUNGU. ANAKUJA HIVI KARIBUNI. LAZIMA TUFUNIKE UCHI WETU


ADAMU, UKO WAPI?
NIMESIKIA SAUTI YAKO NA NIKAOGOPA KWA SABABU NIKO UCHI.
NANI ALIKUAMBIA WEWE UKO UCHI? JE, ULINIASI NA KUKULA LILE TUNDA HARAMU?




MWANZO 3: 6-12



HISSSSS ...
NYOKA ALINIDANGANYA. AKANIAMBIA MIMI NISINGEKUFA, KWAMBA NITAKUWA KAMA WEWE MUNGU, LAKINI MIMI SIKO KAMA WEWE. NINAJUTA!


KWA HIVYO MUNGU ALILAANI NYOKA NA AKAMWAMBIA ...
KWA SABABU WEWE UMEFANYA HIVI, NITAKUFANYA UWE UNATAMBAA KWENYE TUMBO LAKO NA KULA VUMBI KWA KINYWA CHAKO
NITAUFANYA UZAO WAKO NA UZAO WA MWANAMKE KUWA MAADUI. MBEGU YAKO ITAPONDA KISIGINO CHA UZAO WA MWANAMKE, LAKINI ATAPONDA KICHWA CHAKO.


HAPA IPO AHADI YA VITA VYA BAADAYE. WAKATI UTAFIKA AMBAPO UZAO WA MWANAMKE UTAMSHINDA SHETANI. MTU HUYU ATAWAKOMBOA WANADAMU NA KURUDISHA UHUSIANO WAO NA MUNGU KISHA AWAOKOE KUTOKA KWA LAANA YA DHAMBI NA MAUTI.
MUNGU ANGEWEZA KUMUANGAMIZA SHETANI NA MALAIKA WAKE WOTE KWA MUDA MFUPI TU, LAKINI ALIWARUHUSU KUISHI KAMA MTIHANI KWA JAMII YA WANADAMU. JE! WATU WATAMFUATA MUNGU, AU WATAMFUATA SHETANI KATIKA UASI WAKE?
MWANZO 3: 13-15



MUNGU AKAMLAANI WANADAMU AKISEMA ...
ADAMU, KWA SABABU WEWE ULITII USHAWISHI WA MKEO NA KUNIASI, NITAILAANI DUNIA HII NA NITAFANYA MIBA KUMEA KWA UBORA KULIKO MBOGA NA UTALAZIMIKA KUFANYA KAZI NGUMU ILI ARDHI IKUPE MAZAO MAADAMU UNAISHI, UTAKUWA NA HUZUNI, UTAFANYA KAZI NA JASHO LITAKUTOKA USONI MWAKO MPAKA UTAKAPOKUFA NA KURUDI MAVUMBINI KWENYE ARDHI ULIOUMBWA KUTOKA KWAYO.


ILIKUWA SASA WAKATI WA ADAMU NA EVA KUFA JINSI MUNGU ALIVYOAHIDI IKIWA WATAKULA LILE TUNDA. LAKINI BADALA YA KUWAUA MUNGU ALIWAUA WANYAMA KWA NIABA YAO NA AKUCHUKUA NGOZI NA KUWATENGENEZEA NGUO ADAMU NA EVA ILI KUJIFUNIKA UCHI WAO.


HAKUTUUA! BADO TUKO HAI!
ALIWAUA WANYAMA BADALA YETU!
ADAMU NA EVA HAWAKUFA SIKU HIO HIO WALIOASI MUNGU, KWA SABABU WANYAMA WASIO NA HATIA WALIKUFA BADALA YAO. LAKINI HUKUMU YA KIFO ILIKUWA IMEKWISHA PITISHWA JUU YAO, NA HATIMAYE WAO PIA WANGEKUFA. KIFO NI ADHABU YA DHAMBI.


KWA KUWA ADAMU NA EVA WALIKUWA SASA WENYE DHAMBI, MUNGU ALIWATIMUA NJE YA BUSTANI NZURI LA EDENI HIVYO WASIJE WAKALA ULE MTI WA UZIMA WAKAISHI MILELE KATIKA HALI ZAO ZA DHAMBI.



MUNGU ALIWEKA AINA MAALUM YA MALAIKA AITWAYE KERUBI MLANGONI KWA BUSTANI LA EDENI ILI KUZUIA MTU YEYOTE ASIWEZE KUUFIKIA ULE MTI WA UZIMA. BUSTANI HIYO YA EDENI HATIMAYE ILIHARIBIWA NA MTI HUO WA UZIMA UKAHAMISHWA KUTOKA DUNIANI. SIKU MOJA UTAREJESHWA DUNIANI, LAKINI MIMI NINASONGA MBELE YA HADITHI YANGU.
MWANZO 3: 17-24; EZEKIELI 18: 4


ADAMU NA EVA WALIKUWA NA WATOTO WENGI. BAADAYE, WANA NA BINTI ZAO WANGEOANA NA KUWA NA WATOTO WAO WENYEWE.
WAKATI MWANADAMU ALIUMBWA KWANZA, JENI ZA KIBIOLOJIA AMBAZO HUSABABISHA ULEMAVU WAKATI WATU WA UKOO AU FAMILIA MOJA WANAPOOANA NA KUZAA WATOTO HAZIKUWA BADO ZIMEPATIKANA LAKINI BAADAYE WAKATI ULIFIKA IKAWA SHIDA, MUNGU ALIAMURU KWAMBA JAMAA WA KARIBU HAWAPASWI KUOANA.

KAINI, MTOTO WA KWANZA WA ADAMU NA EVA, ALIKUWA MKULIMA WA MBOGA NA MATUNDA. MWANA WAO WA PILI, ABELI, ALIKUWA MFUGAJI WANYAMA. JE, INAWEZEKANA MMOJA WAO ATAKUWA NDIYE MWANA ALIYEAHIDIWA AMBAYE ATAMHARIBU SHETANI?



KAINI NA ABELI WALIFAHAMU KUHUSU MUNGU NA MATUKIO KATIKA BUSTANI. LAKINI MUNGU HAKUTEMBEA TENA NA KUMZUNGUMZIA MWANADAMU KAMA ILIVYOKUWA KABLA UASI ADAMU NA UZAO WAKE WOTE WALIKWISHA KUTENGANISHWA NA MUNGU KUPITIA UASI WA ADAMU. MAISHA YALIKUWA MAGUMU KWELI BILA MUNGU.


EEH MUNGU WANGU, MIMI NI MTU MWENYE DHAMBI; NINAMCHINJA HUYU KONDOO NA KUMTOA KWAKO KAMA DHABIHU BADALA YA KIFO CHANGU MWENYEWE.
IKAJA WAKATI WALE WANA WAWILI WALIAMUA KUMWABUDU MUNGU. BABA YAO ALIKUWA AMEKWISHA WAAMBIA JINSI MUNGU ALIUA WANYAMA KATIKA BUSTANI LA EDENI, KWA HIYO KWA IMANI ABELI AKAMCHINJA MNYAMA NA KUMTOLEA MUNGU DHABIHU.


KAINI AKAMTOLEA MUNGU DHABIHU BORA ALIYOKUWA NAYO, LAKINI ILIKUWA SIO DHABIHU YA DAMU. KAINI HAKUELEWA KWAMBA DHAMBI ZAKE ZILIMWUDHI MUNGU.
MUNGU, TAFADHALI KUBALI ZAWADI HII NDIO BORA NILIYO NAYO NAKUTOLEA.
JE, MMOJA WA WATU HAWA ATAKUWA MKOMBOZI ALIYEAHIDIWA?
MWANZO 4: 1-4; WARUMI 3:23; WAEBRANIA 11: 4


HAPANA, KAINI!
MUNGU ALIIKATAA DHABIU YA KAINI KWA SABABU HAIKUWA NA DAMU.


MUNGU ALIFURAHISHWA NA ABELI NA SADAKA YAKE. WAKATI YEYE ALIONA KUMWAGIKA KWA DAMU YA MWANA-KONDOO ASIYE NA HATIA, MUNGU ALIONDOA DHAMBI YA ABELI.
MUNGU AKAMWAMBIA KAINI, “IKIWA UTAFANYA IKUPASAVYO, NITAPENDEZWA NA WEWE. PIA, UTATAWALA JUU YA NDUGU YAKO ABELI, NAYE ATAISHI CHINI YAKO.”


HIVI UNADHANIA WEWE NI NANI? MATUNDA YANGU NA MBOGA NI ZENYE THAMANI ZAIDI YA YULE KONDOO ULIYEMCHINJA. NI NINI KINACHOKUFANYA UWE BORA KUNILIKO?
KAKA YANGU, BADO KUNA MUDA UNAWEZA KUMTOLEA MUNGU DHABIHU YA DAMU.


NIMESKIA YA KUTOSHA!
WHACK!
MWANZO 4: 5-8
ABELI AKAFARIKI, NA KAINI AKAJARIBU KUFICHA DHAMBI YAKE YA MAUAJI.


LAKINI KAINI HANGWEZA KUFICHA TENDO LAKE OVU KUTOKA KWA MUNGU. MUNGU ANAONA NA ANAJUA YOTE.
KAINI, YUKO WAPI NDUGU YAKO HABILI?
NIPASWA KUJUA VIPI? JE, MIMI NDIYE NINAPASWA KUMTUNZA KAKA YANGU?
DAMU YA NDUGU YAKO BADO IKO JUU YA ARDHI. INANENA KUHUSU TENDO LAKO LENYE UOVU

MUNGU ANAJUA KILA KITU. ANAONA KILA MTU KILA WAKATI. HAKUNA KINACHOWEZA KUFICHWA MBELE ZAKE YEYE. ALIONA KILE KAINI ALIFANYA KWA ABELI. MUNGU AKAMLAANI KAINI, NAYE AKAKIMBILIA JANGWANI, AKAMCHUKUA MKEWE PAMOJA NAYE. HATIA YAKE ILIMSABABISHIA HUZUNI KUBWA NA MATESO.



BASI, KAINI HANGEWEZA KUWA MKOMBOZI ALIYEHAIDIWA, KIUKWELI YEYE MWENYEWE ALIHITAJI MKOMBOZI





MWANZO 4: 9-16, 5: 4; MATENDO 17: 24-26



SETHI AKAWA NA MTOTO WA KIUME, NA MTOTO WAKE AKAWA NA MWANA, NA WANA WENGINE WENGI WALIZALIWA, LAKINI BADO HAKUNA ALIYEJITOKEZA KUONDOA LAANA YA DHAMBI NA KUHARIBU KIFO. MUDA SIO MREFU DUNIA ILIJAA WATU, MIJI MINGI, VIJIJI, NA MASHAMBA.


KWA KILA KIZAZI KIPYA, JINSI WATU WALIVYONGEZEKA, DHAMBI NAYO ILIONGEZEKA. WATU WALITENDA DHAMBI ZA USHERATI NA UOVU UKAZIDI. MAWAZO YAO YALIJAA DHAMBI. HAKUNA ALIYEISHI KWA HAKI NA UTAKATIFU. ADAMU ALIFANYA DHAMBI MOJA LAKINI WATU WALIZIDI NA KUFANYA NYINGI.
MUNGU AKASEMA, "NINAJUTA KWAMBA NILIUMBA MTU DUNIANI. NITAHARIBU KILA KITU KILICHO NA UHAI DUNIANI.
"SHETANI, AMBAYE ANACHUKIA UFALME WA MUNGU ANGEPENDEZWA SANA KUONA MUNGU AKIUA MTU NA KUMALIZA KILA KITU DUNIANI.


VIZAZI TISA VILIKUWA TAYARI VIMEPITA (MIAKA 1,400) NA ULIMWENGU ULIJAA DHAMBI.
WANADAMU WAKAWAFANYA WENZAO WATUMWA WAO.
JE, MUNGU ATAWAHI KUWA NA FAMILIA ITAKAYOMPENDA NA KUMTII?
MWANZO 6: 5-7; WARUMI 5:12 13




LAKINI KULIKUWA NA MTU MMOJA ALIYEKUWA MWENYE HAKI NA SIKU ZOTE ALIFANYA LILILO NJEMA . INGAWA MUNGU ANGEWAUWA WATU WOTE DUNIANI, ALIAMUA KUONYESHA NEEMA KWAKE MTU HUYU PAMOJA NA FAMILIA YAKE.


NUHU,
MIMI NAENDA KUTUMA MAFURIKO MAKUBWA YA MAJI JUU YA DUNIA YOTE. KILA KITU AMBACHO KINA PUMZI KITAKUFA. ILI KUPONEA WEWE NA FAMILIA YAKO PAMOJA NA WANYAMA, UTAJENGA SAFINA KUBWA.


CHUKUA PAMOJA NA WEWE KWENYE MASHUA KUTOKA KWA KILA AINA YA MNYAMA ALIYE JUU YA USO WA DUNIA, WAWILI WAWILI WA KIUME NA KIKE. KISHA UTACHUKUA SABA KUTOKA KWA WANYAMA WANAORUHUSIWA KULA. NITAKUELEKEZA JINSI YA KUJENGA MASHUA NA CHOCHOTE UTAKACHO HITAJI ILI KUJITAYARISHA KUTOKANA NA MAFURIKO




GENESIS 6: 8-9, 17-22, 7: 2


NINAWAAMBIENI NYINYI KWA MARA YA MWISHO. MUNGU ANAENDA KUHARIBU DUNIA KUPITIA MAFURIKO MAKUBWA. LAZIMA MNIAMINI NA MJIUNGE NAMI KWENYE MASHUA.
ILIMHUZUNISHA NUHU KUWAZA JINSI KILA MTU ATAKAVYO ANGAMIA KWA MAFURIKO YANAYOKUJA, KWA HIVYO KILA NAFASI ALIYOPATA, ALIWAONYA WATU KUACHA KUTENDA DHAMBI.


WEWE NI MZEE MJINGA!
KWA SABABU YA DHAMBI. LAZIMA UACHE KUTENDA DHAMBI, UMPENDE JIRANI YAKO NA PIA UMFANYIE HAKI
KWA NINI MUNGU MWENYE UPENDO AHARIBU WATOTO WAKE?


MIAKA 120 BAADAYE, WAKATI MASHUA LILIKWISHA KUMALIZIKA, MUNGU ALISABABISHA WANYAMA KUJA KWA NUHU KUTOKA KOTE DUNIANI.
TAZAMA, WANYAMA ZAIDI WANAENDELEA KUKUJA WENYEWE, NI KAMA VILE MTU ANAWAITA.




MWANZO 7: 7-9; 2 PETRO 2: 5


NAFASI IMEBAKAIA KIDOGO TU.
HII NDIO YA MWISHO.
NUHU, WAKATI UMEWADIA, INGIA NDANI YA MASHUA PAMOJA NA FAMILIA YAKO NA WANYAMA PIA. HIVI KARIBUNI WAKATI UTAKUWA UMEKWISHA KWA WALIO KATAA KUACHA DHAMBI ZAO.



MUNGU ALIFUNGA MLANGO WA MASHUA, NA KWA MUDA WA SIKU SABA HAKUNA KILICHOTOKEA.
HA, HA! TAZAMA HAWA WAPUMBAVU, WALIOJIFUNIKIA NDANI YA MASHUA KUBWA KATIKATI YA JANGWA LISILO NA TONE LA MAJI.
NDIO, NINAHAKIKA HAO SIMBA WAMESHA WASHAMBULIA NA KUWALA HUMO NDANI.
NI JUMA MZIMA TANGU WAINGIE HUMO NDANI.



LAKINI SIKU YA SABA MVUA KUU IKAANZA KUNYESHA, MAJI YAKAJAA VIDIMBWI VYOTE NA KUANZA KUFUNIKA ARDHI.
LO! SIJAWAHI KUONA MVUA KAMA HII; UNAFIKIRI WALE WAZIMU WALIOINGIA NDANI YA HIYO MASHUA WANAWEZA KUWA HAWAKUKOSEA KUHUSU MUNGU KUTUANGAMIZA KWA SABABU YA DHAMBI ZETU?




KABLA YA WAKATI HUU, MVUA ILIKUWA HAIJAWAHI KUNYESHA. HALI YA HEWA ILIKUWA NZURI KILA WAKATI NA UKUNGU ULIPANDA KUTOKA ARDHINI KUMWAGILIA ARDHI MAJI. HAKUNA MTU ALIYEWAHI KUONA AU KUSIKIA JUU YA MVUA, KWA HIVYO WATU WENGI WALIDHANI NUHU ALIKUWA MWENDAWAZIMU KWA KUFIKIRIA MAJI YANGEMWAGIKA KUTOKA ANGANI, LAKINI NUHU ALIAMINI KILE MUNGU ALISEMA.




MWANZO 7: 9-12, 16


TAKRIBAN MWAKA 2348 B.C.
WAKATI HAO WATU WALIGUNDUA KWAMBA NUHU AMEKUWA AKIWAAMBIA UKWELI, WALIKUWA WAMECHELEWA SANA.
MVUA ILINYESHA KWA MUDA WA SIKU 40 USIKU NA MCHANA. MAJI YAKAFUNIKA KILA MLIMA NA KILA KITU DUNIANI KOTE. KILA NAFSI ILIYOKUWA HAI IPUMUAYO HEWA ILIKUFA, ISIPOKUWA WALE WALIOKUWA NDANI MASHUA PAMOJA NA NUHU. IKAWA KAMA MWAKA MMOJA KABLA WATOKE KWENYE MASHUA.


MWANZO 7:12, 19-23, 8: 9-12
NITAFURAHI WAKATI MAJI YATAPUNGUA ILI TUWEZE KUTOKA KWENYE MASHUA.
HATIMAYE NUHU AKATUMA NJIWA NA IKAREJEA NA TAWI KINYWANI MWAKE, ISHARA KWAMBA KULIKUWA NA MITI TAYARI INAKUA. BAADAYE, TENA AKAITUMA LAKINI KWA WAKATI HUU HAIKUREJEA, ISHARA KUWA ILIPATA MAHALI PAZURI PA KUISHI.


MUDA SI MUDA MASHUA IKATUA JUU YA MLIMA UITWAO ARARAT. WOTE WAKASHUKA NA KUPATA ULIMWENGU USIOKUWA NA DHAMBI.

NUHU AKAJENGA MADHABAHU NA AKAMTOLEA MUNGU DHABIHU ZA WANYAMA. INGAWA NUHU ALIKUWA MWENYE HAKI, BADO KULIKUWA NA DHAMBI NDANI YA MOYO WAKE. DHABIHU HIZI ZA DAMU ZILITOLEWA KWA MUNGU BADALA YA MAISHA YA NUHU NA FAMILIA YAKE YOTE.



WANYAMA HAO WALITOLEWA KAMA DHABIHU KUWAKILISHA WATU HAO WANANE AMBAO WANGEKUFA KWENYE MAFURIKO LAKINI MUNGU AKAWAOKOA KWA NEEMA. LILIKUWA TUKIO KAMA LILE LILIFANYIKA KWENYE BUSTANI LA EDENI WAKATI MUNGU ALIUA WANYAMA ILI KUWATENGENEZEA NGUO ADAMU NA EVA.


NITAKUONYESHA UPINDE WA MVUA MBINGUNI KAMA ISHARA NA UKUMBUSHO KWAMBA SITAWAHI HARIBU TENA DUNIA KUPITIA MAJI. BASI TANGU SASA UNAPASWA KUZAA WATOTO WENGI ILI WATAWANYIKE NA KUIJAZA TENA DUNIA.



NITAWAFANYA WANYAMA KUWA WANAOGOPA WANADAMU. UKO HURU KULA KIUMBE CHOCHOTE KILICHO UHAI NA KITAMBAACHO JINSI ULAVYO MBOGA NA MIMEA, LAKINI KAMWE USIDHUBUTU KULA DAMU YA KIUMBE CHOCHOTE. PIA USIUE MTU YEYOTE.
IKIWA MTU YEYOTE ATAPATIKANA NA HATIA YA KUUA MWINGINE, BASI YEYE PIA AUAWE NA WATU WENGINE. IKIWA MTU YEYOTE ATAMWAGA DAMU YA MTU MWINGINE, BASI WATU WENGINE WANAPASWA KUMWAGA DAMU YAKE PIA ILI KULIPA UHALIFU WAKE, KWA SABABU UHAI UKO KATIKA DAMU.



NUHU AKAWA MKULIMA NA AKAPANDA ZABIBU. ULIMWENGU HUU MPYA ULIKUWA MPWEKE NA FAMILIA ZILIKUWA NNE PEKE YAKE DUNIA NZIMA, LAKINI MUDA SI MREFU WANAWE WAKAWA NA WATOTO WAO WENYEWE.






NUHU ALIGUNDUA KWAMBA AKIWEKA MATUNDA KWENYE CHOMBO NA KUYAACHA KWA MUDA WA WIKI CHACHE, ILIFANYIKA KUWA KINYWAJI CHA KILEO KILICHOMFANYA KUJIHISI VIZURI BAADA YA KUKINYWA. NUHU AKAPENDA KINYWAJI HICHO SANA, BAADA YA KUKIZOEA WAKATI MWINGINE HAKUWEZA KUFANYA KAZI. KINGEMFANYA ALALE CHINI KWA KUTOJIFAHAMU NA PIA KUMSABABISHA KUTENDA MAMBO AMBAYO HAYAKUMPENDEZA MUNGU.



SIKU MOJA NUHU ALILEWA CHAKARI KIASI KWAMBA ALIJIFUNUA UCHI WAKE NA AKAPOTEZA FAHAMU AKIWA UCHI. MWANAWE HAMU, AKAUONA UCHI WA BABA YAKE NA BILA AIBU AKAONEA FAHARI KITENDO HICHO. KISHA AKAWAHADITHIA NDUGU ZAKE KWA SAUTI YA KEJELI NA DHARAU KILE ALICHOONA.


WAKATI NUHU ALIAMKA, WANAWE WAKAMWELEZEA KILE HAMU ALICHOFANYA.
MWANAO, KANAANI, MALI YAKE YOTE PAMOJA NA UZAO WAKE WATAKUWA WATUMISHI WA KAKAKO SHEMU.


MIAKA MINGI BAADAYE, HUU UNABII ULITIMIA. WAKANAANI WALITUA PALESTINA NA WAKAISHIA KUWA WATUMWA WA WAYAHUDI.
MWANZO 9: 21-27; 1 MAMBO YA NYAKATI 4:40; ZABURI 78:51, 105: 23,27, 106: 22


SETHI
ADAMU NA EVA
KAINI
ABELI
MUNGU ALIUA KILA MTU ISIPOKUWA HAO WATU WANANE.


NUHU NA FAMILIA YAKE WALIPATA KIBALI MBELE ZA MUNGU.
ULAYA
YAFETHI
UTURUKI
SHEMU
ASIA
HAMU
AFRIKA
MISRI
BAADA YA MUDA YAFETI AKAENDA MAGHARIBI NA KASKAZINI KUISHI NA KUONGEZEKA.
SHEMU ALIKWENDA MASHARIKI NA AKATULIA ASIA.
HAMU AKAENDA KUSINI NA KUKAA BARANI AFRIKA NA KUSINI MWA ASIA. UZAO WA MWANAE, KANA, UKAISHI MAHALI PAITWAPO SASA PALESTINA.
NA KWA HIVYO ULIMWENGU UKAJAA TENA.


TAKRIBAN MWAKA 2247 B.C.
MWANAE NUHU, HAMU, ALIKUWA NA MTOTO WA KIUME JINA LAKE KUSHI, HALAFU KUSHI ALIKUWA NA MTOTO WA KIUME ALIYEITWA NIMRODI. NIMRODI ALIKUWA MWINDAJI HODARI, NA ALIJULIKANA SANA KATIKA DUNIA YOTE. ALIASI MUNGU NA AKAANZA DINI LAKE LA UWONGO MAHALI PAITWAPO BABELI.


WATU WA BABELI HAWAKUTAKA KUTAWANYIKA DUNIANI NA KUIJAZA TENA DUNIA KAMA MUNGU ALIVYOKUWA AMEAMRISHA, KWA HIVYO WAKAJIKUSANYA NA KUJENGA MNARA MKUBWA NA MREFU KAMA KITUO CHA IBADA.




LAKINI HAWAKUABUDU MUUMBA WAO. SHETANI ALIWAONGOZA KUUNDA MIUNGU YAO WENYEWE KUTOKA KWA MBAO, MAWE, NA CHUMA.

MUNGU ALIGADHABISHWA NA MAAMUZI YAO YA KUKATAA KUTAWANYIKA JUU YA DUNIA, KWA HIVYO ALIWASABABISHA KUONGEA KWA LUGHA NYINGI TOFAUTI.





KILA KIKUNDI CHA LUGHA WAKAENDA NJIA YAO WENYEWE. BAADHI YAO WALIKWENDA MAENEO YA MBALI KATIKA DUNIA, WENGINE WALISAFIRI KUTUMIA MELI HADI VISIWA VYA MBALI, WENGINE HADI KASKAZINI AMBAPO KULIKUWA BARIDI NA WENGINE WAKAELEKEA CHINI NDANI YA MAJANGWA KWENYE JOTO. KWA HIYO AMRI YA MUNGU YA KUJAZA DUNIA ILITIMIA.



DUNIA ILIPOJAA WATU TENA, DHAMBI TENA IKAONGEZEKA. WATU WAKAANZA TENA KUABUDU SANAMU NA WAKAMSAHAU MUNGU ALIYE HAI.

MWANZO 10: 6-10, 11: 1-9



## SURA YA 2


# IBRAHIMU

KULIKUWA NA MTU MMOJA ALIYEITWA IBRAHIMU AMBAYE HAKUAMINI KWAMBA SANAMU ZILIKUWA MIUNGU YA KWELI. ALIJUA KWAMBA MUNGU WA KWELI ALIKUWA MUNGU MUUMBAJI NA HAKUFAA KUABUDIWA KUPITIA SANAMU



MUNGU AKANENA NAYE, AKISEMA, “IBRAHIMU, ONDOKA KATIKA MJI HUU ULIOJAA IBADA ZA SANAMU. ACHA FAMILIA YAKO YOTE PAMOJA NA NCHI YAO, NA NITAKUONYESHA PA KWENDA. NITAKUFANYA KUWA BABA WA TAIFA KUU. NITAWABARIKI WALE AMBAO WATAKUBARIKI NAMI NITALAANI WALE WANAOKULAANI. KUPITIA KWAKO MATAIFA YOTE YA DUNIA YATABARIKIWA.”




TAKRIBAN 1921 B.C.
IBRAHIMU ALIIJUA SAUTI AMBAYO ALISIKIA ILIKUWA SAUTI YA MUNGU, KWA HIVYO ALITII, BILA KUJUA NI WAPI ALIKUWA ANAENDA. ALIJUA KWAMBA ALIKUWA AKIACHA IBADA YA SANAMU NYUMA NA ALIKUWA AKIMFUATA MUNGU ALIYE HAI. HIYO ILITOSHA KWA IBRAHIMU. LAKINI AKAMCHUKUA LUTU MPWA WAKE.


SAFARI YA IBRAHIMU ILIMCHUKUA KUSHUKA MPAKA NCHI YA KANAANI, AMBAPO MTOTO WA HAMU ALIISHI PAMOJA NA UZAO WAKE. LEO, INAITWA PALESTINA. HUKO MUNGU ALIZUNGUMZA NAYE:
IBRAHIMU, TEMBELEA ENEO HILI KUTOKA MWISHO HADI MWISHO. MIMI NAKWENDA KUKUPA ARDHI HII YOTE YA KANAANI KWA AJILI YAKO NA UZAO WAKO WA BAADAE. NITAKUFANYA KUWA NA WATOTO WENGI AMBAO HAWAWEZI KUHESABIKA. WINGI WAO UTAKUWA KAMA VUMBI YA DUNIA.




MWANZO 12: 1-3, 13: 14-17



IBRAHIMU ALIPOKUWA AKISAFIRI KWENYE NCHI, MARA KWA MARA ALISIMAMA NA KUMTOLEA MUNGU DHABIHU YA DAMU. KAMA ABELI, ALITOA DHABIHU HIZO KWA IMANI, AKIELEWA KUWA YEYE NI MWENYE DHAMBI ALIYESTAHILI KUFA KWA SABABU YA DHAMBI ZAKE MWENYEWE.
DHABIHU YA MWANA-KONDOO HAIKUWEZA KUONDOA DHAMBI ZA IBRAHIMU, LAKINI MUNGU ALIPOONA IMANI YAKE, ALIFUNIKA DHAMBI ZAKE.


MIAKA KUMI BAADAYE.
IBRAHIMU, MIAKA KUMI ILIYOPITA ULIESEMA MUNGU ALIKUAMBIA KWAMBA NINGEKUZALIA MTOTO. SASA NINA MIAKA 75 NA WEWE 85. TUNAZIDI KUWA WAZEE, LAKINI BADO HATUNA MTOTO. HIVI KARIBUNI UTAPITISHA UWEZO WA KUPATA MTOTO. JE, UNA HAKIKA ULISIKIA KUTOKA KWA MUNGU?


NAJUA ILIKUWA MUNGU ALIYESEMA NAMI, LAKINI SIELEWI KWA NINI ANASUBIRI KWA MUDA MREFU HIVYO. ALISEMA NITAKUWA BABA WA TAIFA KUBWA, LAKINI NILICHO NACHO SASA NI MWILI WENYE UZEE, MKE MZEE AMBAYE HANA UWEZO WA KUPATA WATOTO, NA KUNDI KUBWA LA KONDOO.


USIOGOPE IBRAHIMU, MIMI NI NGAO YAKO, NA THAWABU YAKO KUBWA SANA.
NI DHAWABU GANI UTANIPA, ILHALI SINA MTOTO?
WEWE NA SARA NITAWAPA MTOTO WENU.


NJOO, IBRAHIMU, TAZAMA NYOTA NA UONE IKIWA UNAWEZA KUZIHESABU. KAMA NYOTA, WATOTO WAKO WATAKUWA WENGI KWAMBA HAWAWEZI KUHESABIKA
NAAMINI ITATIMIA KAMA ULIVYO SEMA.


MWANZO 15: 1-6, 13-14
KWA KUWA UNANIAMINI, NITAENDA KUHESABU IMANI YAKO KANA KWAMBA WEWE NI MWENYE HAKI. FAHAMU KWA HAKIKA WATOTO WAKO WATAKUWA WAGENI KATIKA NCHI ISIYO YAO. BAADA YA KUTESEKA KATIKA UTUMWA KWA MIAKA 400, NITALIADHIBU TAIFA HILO, NA WANA WAKO WATAONDOKA KWENYE TAIFA HILO WAKIWA NA UTAJIRI MWINGI. KISHA WATARUDI HAPA NA KUISHI KATIKA ARDHI HII.


IKO WAPI AHADI YA MTOTO? MIMI NAZIDI KUWA MZEE KILA SIKU. HIVI KARIBUNI HAUTAKUWA NA UWEZO KUZALISHA MBEGU. IBRAHIMU, KAMWE SITAWEZA KUKUPA WATOTO.


MILA NA DESTURI ZA HUKU NI KWAMBA MJAKAZI WANGU ANAWEZA KUNIZALIA MTOTO.


IBRAHIMU, HUONI HII NI NAFASI YETU YA MWISHO SISI KUWA NA MTOTO? KABLA HATUJACHELEWA SANA, LAZIMA UMCHUKUE KISHA MZAE MTOTO. ATAKUWA UZAO WAKO. NI MAPENZI YA MUNGU. JE, KUNA NJIA MBADALA YAKO KUWA BABA WA TAIFA KUBWA?


NDIO NJIA PEKEE.
IBRAHIMU HAKUMWOMBA MUNGU. ALISAHAU AHADI YA MUNGU NA AKATII SAUTI YA MKEWE.

MWANZO 16: 1-4


MIEZI KADHAA BAADAYE.
NINAKWENDA KUZAA MTOTO WA IBRAHIMU.
WAKATI HAJIRI ALIJUA KUWA YEYE ALIKUWA NA MIMBA YA IBRAHIMU, ALIJIVUNA NA KUMDHARAU SARA. NAYE SARA AKAKOSA FURAHA NA AKAWA MWENYE WIVU.


SARA ALIMFANYA HAJIRI AFANYE KAZI NGUMU SANA BILA HURUMA. HAIKUWA KUSUDI LA MUNGU KAMWE MTU KUWA NA WAKE WAWILI AU KUWA NA WATOTO KUPITIA WAJAKAZI.
UKIMALIZA KUTEKA MAJI, NENDA KAKATE KUNI.
HAJIRI AKAANZA KUFANYA MIPANGO YA KUTOROKA.


HAJIRI ALIMKIMBIA SARA NA KUKIMBILIA NYIKANI. ALIPOCHOKA ASIWEZE KWENDA MBALI ZAIDI, ALIZIRAI KWA UCHOVU. MUNGU AKAMWONA HAJIRI KATIKA SHIDA YAKE NA KUZUNGUMZA NAYE.
HAJIRI, RUDI KWA SARA NA UNYENYEKEE KWAKE. UTAPATA MTOTO WA KIUME NAWE UTAMUITA ISHMAELI, AMBAYO MAANA YAKE NI “MUNGU HUWA ANASIKIA.”


KUTOKA KWAKE WATAPATIKANA WATOTO WENGI, ZAIDI YA UWEZO WA KUHESABIWA. ISHMAELI ATAKUWA KAMA PUNDA-MWITU. ATAKUWA DAIMA WA KUPIGANA NA KILA MTU NA KILA MTU ATAKUWA ANAPIGANA NA YEYE. ATAISHI DAIMA KARIBU NA NDUGU ZAKE WOTE.


HAJIRI AKARUDI NYUMBANI NA BAADA YA MUDA MTOTO ALIZALIWA.
MUNGU ALINIAMBIA KWAMBA SABABU HUYU MTOTO NI WA IBRAHIMU, ATAKUWA BABA WA MENGI MENGI.
ISHMAELI BAADAYE AKAWA BABA WA MATAIFA YOTE YA KIARABU.
MWANZO 16: 4-16


IBRAHIMU ALIKUWA NA UMRI WA MIAKA 86 WAKATI ISHMAELI ALIZALIWA. SIO MUDA MREFU BAADA YA KUZALIWA KWA ISHMAELI, IBRAHIMU AKAWA MZEE SANA KUPITA UWEZO WA KUPATA WATOTO. JE, ISHMAELI ANGEKUWA MTOTO AMBAYE MUNGU ALIAHIDI IBRAHIMU? LAKINI MUNGU ALISEMA MTOTO ANGEZALIWA KUPITIA SARA NA IBRAHIMU.
JE, MUNGU ANAWEZAJE KUTIMIZA AHADI YAKE IKIWA WOTE WAWILI IBRAHIMU NA SARA WAMEKUWA WAZEE SANA KUPITA UWEZO WA KUZAA WATOTO?


WAKATI ISHMAELI ALIKUWA NA MIAKA KUMI NA TATU NA IBRAHIMU ALIKUWA NA MIAKA 99, MUNGU ALIZUNGUMZA NAYE TENA.
IBRAHIMU, MIMI NDIMI MWENYEZI MUNGU. FANYA YOTE NITAKAYO KUAMBIA, NA USITENDE DHAMBI. KAMA NILIVYOKUAMBIA HAPO AWALI, MIMI NITAWAZIDISHA WATOTO WAKO, NAWE UTAKUWA BABA WA MATAIFA MENGI. NITAFANYA AGANO LANGU NA WEWE NA PIA WATOTO WAKO BAADA YAKO.


NITAWAPA WATOTO WAKO NCHI YA KANAANI KUWA MILKI YAO YA MILELE. SARA ATAPATA MIMBA NA KUWA NA MTOTO KAMA NILIVYOAHIDI, AMBAYE ATAKUWA MKUU WA MATAIFA MENGI.
HA, HA! ITAKUWAJE HIVYO? MIMI SASA NINA UMRI WA MIAKA 99, NA SARA ANA MIAKA 89. MWILI WANGU NI KAMA ULIOKUFA TAYARI. HATUWEZI KUPATA WATOTO. TAFADHALI, MUACHE ISHMAELI AWE NDIYE MTOTO ALIYEAHIDIWA.


HAPANA, KAMA NILIVYOSEMA TANGU MWANZO, WEWE NA SARA MTAZAA MTOTO WENU WENYEWE, KUTOKA KWA MIILI YENU WENYEWE. AHADI YA BARAKA ITAKUWA KUPITIA YEYE MBALI SIO ISHMAELI. BAADA YA MUDA WA MWAKA MMOJA SARA ATAZAA MTOTO WA KIUME.


INAWEZEKANA KWELI? ... NDIO! MUNGU ALIYEUMBA MWILI WA MWANADAMU ANAWEZA KUCHUKUA MIILI MIWILI ILIYOZEEKA NA KUFA AKAIFANYA KUWA NA UWEZO WA KUZAA TENA. HAKIKA. MUNGU ANAWEZA KUFANYA HAYO!


BAADA YA SIKU CHACHE, WANAUME WATATU WAKATOKEA JANGWANI. KWA MTAZAMO HAWAKUONEKANA KANA KWAMBA WALISAFIRI TOKEA MBALI, WALA HAWAKUONEKANA KAMA WENYEJI WA MTAA HUO. WALIONEKANA WENYE NGUVU, USHUPAVU NA WASIO WACHANGA AU WAZEE.


IBRAHIMU ALIPOWATAZAMA WALIPOKUWA WAKIKARIBIA, ALIGUNDUA KUWA WALIKUWA NA UTOFAUTI WASIO WA KAWAIDA, LAKINI ALICHOKUWA HAFAHAMU NI KWAMBA WAGENI HAWA HAWAKUWA WENYEJI WA DUNIA HII.
WAWILI WAO WALIKUWA MALAIKA WENYE HAKI, NA WA TATU ALIKUWA MUNGU MWENYEWE, AKIONEKANA NDANI UMBO LA MALAIKA ILI AWEZE KUONGEA NA IBRAHIMU. IBRAHIMU AKATOKA KWENDA KUKUTANA NAO.
MWANZO 17: 1-21, 18: 1-2


IBRAHIMU, MKE WAKO SARA ATAZAA MTOTO WA KIUME.
HE, HE, HE
NILIVYO MZEE HIVI, NA IBRAHIMU HATA MZEE ZAIDI, NAWEZA KUWA NA FURAHA TENA KWELI?


KWA NINI SARA ANACHEKA WAKATI MUNGU ANASEMA ATAKUWA NA MTOTO?
MIMI SIKUCHEKA.
HAKIKA UMECHEKA. WEWE HUAMINI. JE, NI JAMBO GANI NGUMU SANA KWA MUNGU? NITAKUJA TENA WAKATI MWAFAKA WA KUPATA UJAUZITO UKIFIKA, NA UTAPATA MTOTO.


JE, NIMWAMBIE IBRAHIMU KILE AMBACHO NAKUSUDIA KUFANYA? ANAENDA KUWA BABA WA WATOTO WENGI, NAYE ATAWAFUNZA WATOTO WAKE NA WAJUKUU WAKE KUNITII.
NDIO ANAHITAJI KUJUA.


DHAMBI YA SODOMA NA GOMORA IMEKUWA MBAYA SANA. NITAHARIBU KILA NAFSI KATIKA MIJI YOTE MIWILI: WANAUME, WANAWAKE, NA WATOTO.
LAKINI MPWA WANGU LUTU NA FAMILIA YAKE WANAISHI HUMO!
MWANZO 18: 10-22


ISINGEKUWA HIVYO MUNGU KUWAANGAMIZA WENYE HAKI PAMOJA NA WAOVU. JE, IKIWA KUNA WATU HAMSINI WENYE HAKI KATIKA MJI? UTAHIFADHI MJI MZIMA KUOKOA MWENYE HAKI? NAJUA KWAMBA HAKIMU WA WATU WOTE ATAFANYA KILICHO SAWA.
IKIWA NITAPATA WATU HAMSINI WENYE HAKI NITAUSAMEHE HUO MJI.


MIMI NI UDONGO TU, SISTAHILI KUZUNGUMZA NA MUNGU, LAKINI VIPI IKIWA KUNA AROBAINI NA TANO TU WENYE HAKI? JE, UNGEHARIBU WOTE KWA KUKOSA WATANO?
IKIWA WATAKUWA 45 SITAUHARIBU MJI HUO.
JE, IKIWA KUNA AROBAINI TU WATAPATIKANA?
SITAUHARIBU IKIWA KUNA AROBAINI WENYE HAKI.


KUNRADHI NAOMBA USINIKASIRIKIE JE, IKIWA KUNA THELATHINI?
SITAIHARIBU IKIWA THELATHINI WATAPATIKANA.
JE, IKIWA KUNA ISHIRINI?
SITAUANGAMIZA MJI HUO MUOVU IKIWA KUNA ISHIRINI WENYE HAKI NDANI YAKE.


SAMAHANI USIGHADHIBIKE JUUU YANGU. HII NI MARA YA MWISHO NITAKUULIZA. JE, IKIWA KUNA WATU KUMI TU WENYE HAKI KATIKA MJI? BADO UTAUANGAMIZA?
LA HASHA, IKIWA MIMI NINAWEZA KUPATA ROHO KUMI ZENYE HAKI, MIMI SITAUANGAMIZA MJI.
IKIWA HUWEZI KUPATA KUMI, TAFADHALI WAWEZA KUMUONYA MPWA WANGU LUTU?
TUTAMTEMBELEA USIKU WA LEO.


MALAIKA HAO WAWILI WALIKWENDA NDANI YA JIJI HILO JIONI NA KUTEMBELEA KARIBU NA NYUMBA YA LUTU.
HII IMEPOTOKA, VIBAYA ZAIDI KULIKO NILIVODHANI.
SASA NIMEELEWA KWANINI MUNGU ANAENDA KUANGAMIZA KILA MTU, HATA WATOTO NA WANYAMA.


ENYI WAGENI, HAMUWEZI MKAKAA KWENYE MITAA HII USIKU; SIO SALAMA. NJOONI MPUMZIKE KATIKA NYUMBA YANGU USIKU HUU.
*JAMANI!* WANAPENDEZA SANA. TUTAWAAMBIA WANAUME KUWAHUSU.
MWANZO 18: 23-19: 2


ANAFIKIRI YEYE NI NANI, MWENYE NGUVU NA MKUU? MNAFIKI MKUBWA YEYE.
LUTU, TUMA HAO WANAUME NJE KWETU SISI TUFANYE NGONO NAO!
NENDENI HUKO; HAMUWEZI KUFANYA UOVU HUO.


TUTAUVUNJA MLANGO NA KUKUFANYIA VIBAYA ZAIDI, WEWE MGENI.
MWENYE CHUKI!
NDIO, SISI HATUWATAKI BINTI ZAKO; TUNATAKA HAO WANAUME WAREMBO!


MUNGU MWENYENZI NA AWAFANYE NYIE VIPOFU.
WAKO WAPI SIWAONI?


NI NANI AMEZIMA TAA?
SIONI MWANGAZA? KIPI KIMETOKEA.
HIZI NI NGUVU ZA AINA GANI?


LAZIMA UONDOKE MJI HUU KESHO ASUBUHI. WAONYE UTAKAO. MUNGU NI MWENYEHAKI NA HAWEZI KUVUMILIA ZAIDI UOVU HUU.
KESHO MUNGU ANAENDA KUSHUSHA MOTO MAHALI HAPA. KILA MMOJA KATIKA SODOMA NA GOMORA ATAANGAMIA.


FANYA HARAKA, HIVI KARIBUNI MOTO UTASHUKA. HAKUNA ATAKAYE PONEA.
MUNGU AMEAMRISHA YEYOTE ASIDHUBUTU KUTAZAMA NYUMA MJI UNAPOCHOMEKA.


USITAZAME NYUMA!
EEEK!


JAMANI! BABA, MAMA HAKUMTII MUNGU. AMEGEUKA JIWE LA CHUMVI.
USIDHUBUTU KUANGALIA! TUENDELEE KUENDA!


KILA KITU KILICHOKUWA HAI KATIKA SODOMA NA GOMORA KIKAFA SIKU HIYO. MUNGU NI MWENYE HAKI NA ANACHUKIA DHAMBI, HASWA NGONO ILIYOPOTOKA, WANAUME NA WANAUME NA WANAWAKE KWA WANAWAKE. DHAMBI ZA KINGONO ZINAZOHUSISHA WATOTO NI MBAYA ZAIDI KULIKO ZOTE. MUNGU ALIKUWA AMEAHIDI KAMWE HATAANGAMIZA ULIMWENGU KWA MAJI, LAKINI HAKUSEMA CHOCHOTE KUHUSU MOTO.


WAKATI MWINGINE ITAKUWA KWA MOTO. ADHABU YA DHAMBI YOYOTE NI MAUTI: KIFO CHA MWILI NA MAUTI YA MILELE KATIKA ZIWA LA MOTO. KUPITIA KWA NEEMA YA MUNGU, LUTU ALIOKOLEWA KUTOKA KWA HUKUMU YA MUNGU. MKEWE HAKUAMINI MUNGU ALIKUWA ANAMAANISHA WAKATI ALIONYA WAO WASIANGALIE NYUMA.
ADHABU YA KILA DHAMBI DAIMA NI MAUTI, HAKUNA UBAGUZI.




MWANZO 19: 24-26; MAMBO YA WALAWI 18:22; WARUMI 1: 23-32, 6:23; 1 WAKORINTHO 6: 9-11; UFUNUO 21: 8


MUNGU ALIKUWA AMEAHIDI KWAMBA SARA ANGEPATA MTOTO. IBRAHIMU NA SARA WAKAANZA KUWA NA HISIA ZA KIMAPENZI ZILIZOKUWA ZIMESAHAULIKA.
IBRAHIMU, NINI IMEKUJA JUU YAKO? IMEKUWA MUDA WA MIAKA MINGI TANGU UNITAZAME... KWA NJIA HIYO.


ULIKUWA NI MUUJIZA! MUDA SI MUDA, KILA MTU AKAJUA KWAMBA SARA ALIKUWA NA MIMBA!


KAMA VILE MUNGU ALISEMA, TUTAMUITA ISAKA*. ATAKUWA BABA WA TAIFA KUU.
NDIO, WAKATI MUNGU ALITUAMBIA KWAMBA NINGEZAA MTOTO, ILINIFANYA MIMI KUCHEKA. NANI ANGEMEAMINI KUWA KATIKA UZEE WANGU NINGEKUWA NAMPAKATA MTOTO WANGU MWENYEWE?
MUNGU ALITIMIZA AHADI YAKE. VILE YEYE HUFANYA KILA WAKATI.

ISHMAELI, MTOTO WA IBRAHIMU NA HAJIRI, SASA ALIKUWA NA UMRI WA MIAKA KUMI NA MINNE, NA ALIMCHUKIA MTOTO MPYA WA SARA.




MFUKUZE HUYO MTUMISHI MWANAMKE NA MTOTO WAKE. HAWAWEZI KUPOKEA URITHI WOWOTE PAMOJA NA ISAKA, MTOTO WA AHADI.
MUNGU AKANENA NA IBRAHIMU NA KUSEMA, “SARA HAJAKOSEA. MFUKUZE HAJIRI NA ISHMAELI. ISHMAELI HATAKUWA MRITHI PAMOJA NA ISAKA. LAKINI USIHUZUNIKE; NITAWAJALI NA KUWATUNZA.





MWANZO 21: 1-3, 9-14 * JINA ISAKA LINAMAANISHA KICHEKO.


WEWE NI MTOTO WA MIUJIZA. JE, UTAUOKOA ULIMWENGU KUTOKA KWA DHAMBI?
IBRAHIMU ALIMPENDA MTOTO WAKE ISAKA, NA WAKAPENDANA KWA KIWANGO KISICHOWEZA KUTENGANISHWA.


BABA, KWANINI UNAWAUA HAWA WANA-KONDOO WADOGO WAZURI NA KUWACHOMA KWENYE MAWE ULIOWEKA KWA PAMOJA?
MUNGU MUUMBA MBINGU NA NCHI NI MTAKATIFU NA MUADILIFU, SANA KWA MTU MWENYE DHAMBI KAMA MIMI. MTU WA KWANZA ADAMU, HAKUMTII MUNGU NA JAMII YA WANADAMU IMEKUWA KWENYE DHAMBI HADI SASA.
MUNGU ALIMWAMBIA ADAMU KWAMBA IKIWA ANGETENDA DHAMBI ANGEKUFA, LAKINI BAADA YA ADAMU KUTOTII NA KUTENDA DHAMBI, MUNGU ALIUA WANYAMA NA KUTUMIA NGOZI ZAO KUFUNIKA AIBU YA ADAMU NA HAWA.


WAKATI MIMI HUUA MWANA-KONDOO NA KUMTOLEA MUNGU, NI ISHARA KWAMBA MIMI NINATAMBUA HALI YANGU YA DHAMBI NA MWANA KONDOO ASIYE NA HATIA HUFA KWA NAFASI YANGU.


ISAKA ALIKUA AKIWA NA NGUVU NA AKAJIFUNZA KUMTUMAINI MUNGU WA BABA YAKE. IBRAHIMU ALIMPENDA SANA NA MARA NYINGI WALIENDA PAMOJA KUABUDU NA KUTOA DHABIHU. MWANA-KONDOO ALIPOUAWA ALIKUWA ANAWEKWA JUU YA MADHABAHU AMBAPO DHABIHU ILITEKETEZWA.


IBRAHIMU, NATAKA UMCHUKUE MWANAO WA PEKEE ISAKA, AMBAYE UNAMPENDA, NA UMTOE KAMA DHABIHU YA KUTEKETEZWA KWANGU.


MUNGU, ITAKUWAJE UNAWEZA KUNIULIZA KUFANYA JAMBO KAMA HILO? HIVI SIVYO ULIVYO. WAPAGANI NDIO HUTOA KAFARA ZA WANADAMU! UMEHAIDI UTAFANYA TAIFA KUBWA KUTOKA KWA MWANANGU ISAKA. IKIWA NITAMUUA AHADI YAKO HAITATIMIA.




MWANZO 22: 2; WARUMI 5:12


NI SAFARI YA SIKU TATU, KWA HIVYO TUTAKUWA TUMEENDA KARIBU WIKI NZIMA
MUWE MAKINI SANA, NITAWAOMBEENI ENYI WANAUME WANGU.

SIKU TATU BAADAYE...




BABA, SISI TUMELETA KUNI, NA TUMEJENGA MADHABAHU, LAKINI IKO WAPI DHABIHU?
ISAKA, UNAKUMBUKA JINSI NILIVYOKUAMBIA JUU YA MUNGU KUZUNGUMZA NAMI NA KUSABABISHA MAMA YAKO NA MIMI KUWA NA MTOTO KATIKA UZEE WETU? KWELI, ALIZUNGUMZA NA MIMI TENA.


WAKATI HUU ALISEMA MIMI NIKUTOE KAMA SADAKA YA KUTEKETEZWA.
MIMI? BABA, UNA HAKIKA KWELI?


JE, MUNGU HAKUKUAMBIA KWAMBA NITAKUWA MRITHI, MKUU WA TAIFA KUBWA, NA KWAMBA WATOTO WANGU WANGEKUWA WENGI KAMA NYOTA ZA MBINGUNI? IKIWA NITAKUFA SASA, VIPI KUHUSU AHADI YA MUNGU?
NIMEJIFUNZA KWAMBA KILE AMBACHO MUNGU ANAAHIDI ANAWEZA KUTEKELEZA. IKIWA ANASEMA UTAFANYIKA KUWA BABA WA TAIFA KUU, BASI, HATA UKIFA HAKIKA UTAKUWA BABA WA TAIFA KUU.


LAKINI ITAWEZEKANA AJE KAMA MIMI NIMEKUFA?
SIJUI ITAKAVYOWEZEKANA, ISIPOKUWA YEYE AKUFUFUE KUTOKA KWA WAFU.
BABA, LAZIMA TUMTII MUNGU KWA VYOVYOTE VILE.
MWANZO 22: 3-9


INGAWA IBRAHIMU ALIJUA KWAMBA ALIKUWA AKIMTII MUNGU, LAZIMA IWE ILIUPA MOYO WAKE HUZUNI NA KUFANYA MIKONO YAKE KUTETEMEKA ALIPOKUWA AKIFUATA TARATIBU ZA KAWAIDA ZA KUTOA SADAKA YA KUTEKETEZWA.
ALIFUNGA MIKONO NA MIGUU YA MWANAE NA AKAMWEKA JUU YA MADHABAHU. HATUA INAYOFUATA ILIKUWA KUTUMBUKIZA KISU KWENYE KOO LAKE.

KWA MAOMBI YA IMANI KWAKE MUNGU, IBRAHIMU AKANYANYUA KISU. ALIPOKUWA KARIBU KUKITUMBUKIZA KWA MWANAWE, GHAFLA AKASIKIA SAUTI KUTOKA MBINGUNI:




IBRAHIMU! IBRAHIMU! USIMDHURU MWANAO.



SASA NAJUA KWAMBA UNANIAMINI, KWANI ULIKUWA TAYARI KUTII, HATA KWA UHAKIKA KUNIPA MWANA WAKO WA PEKEE.


WAKATI IBRAHIMU ALIANGALIA JUU, AKAONA MWANA KONDOO WA KIUME AKIWA AMEKWAMA KWA KICHAKA.
BABA, TAZAMA! MUNGU AMETOA MWANA KONDOO WA KIUME KUCHUKUA MAHALI PANGU!


IBRAHIMU, KWA SABABU UMEFANYA JAMBO HILI KWA KUTOKUZUIA MWANAO WA PEKEE, NITAKUBARIKI NA KUZIDISHA WATOTO WAKO KAMA NYOTA ZA ANGANI, NA WATOTO WAKO WATACHUKUA ARDHI HII NA KUANGAMIZA MAADUI WAKO. PIA, KUPITIA MMOJA WA WATOTO WAKO, AMBAYE BADO HAJAZALIWA, MATAIFA YOTE YA DUNIA YATABARIKIWA
BABA, YEYE NDIYE MUNGU MWENYE HURUMA, KAMA ULIVYOSEMA!
MWANZO 22: 9-18; WAEBRANIA 11: 17-19


IBRAHIMU ALIKUWA NA WANA WAWILI, ISHMAELI NA ISAKA. ISAKA ALIKUWA MWANA ALIYECHAGULIWA NA MUNGU ILI KUENDELEZA AHADI ILIYOTOLEWA KWA IBRAHIMU. ISAKA ALIKUWA NA MTOTO WA KIUME ALIYEITWA YAKOBO, AMBAYE JINA LAKE LILIBADILISHWA BAADAYE KUWA ISRAELI. YAKOBO ALIKUWA NA WANA 12 AMBAO, BAADAYE, WALIKWENDA NA FAMILIA ZAO HADI MISRI AMBAPO MWISHOWE WALIKUWA WATUMWA (1706 B.C.).

## MWANZO 21: 5, 13, 24:67, 25: 12-18, 21-26, 29: 23-30







SURA YA 3

# MUSA


1706 B.C.
WAKATI WA NJAA, YAKOBO, AMBAYE ALIKUWA MJUKUU WA IBRAHIMU, ALICHUKUA WANAWE KUMI NA WAWILI NA WATOTO WAO WOTE PAMOJA NA WATUMISHI MPAKA MISRI KUISHI HUMO. KATIKA MISRI WALIONGEZEKA KAMA MAVUMBI YA DUNIA.


MUDA SI MUDA WANA WA YAKOBO, AMBAO JINA LILIBADILISHWA KUWA ISRAELI, WAKAONGEZEKA NA KUZIDI WAMISRI.


FARAO, MTAWALA WA MISRI, AKAWAFANYA WANA WA YAKOBO WATUMWA NA KUWALAZIMISHA KUFANYA KAZI YA KIKATILI, KUTENGENEZA MATOFALI. BAADA YA KUWA HUKO ZAIDI YA MIAKA 300, WALIKUWA WAMESAHAU AHADI ZA MUNGU ALIZOFANYA KWA IBRAHIMU NA KWA BABA ZAO.


MUNGU ALIKUWA AMEMWAMBIA IBRAHIMU KUWA WATU WAKE WANGESHUKA HADI NCHI YA UGENI NA KUFANYIKA WATUMISHI HAPO. PIA ALIAHIDI KWAMBA BAADA YA MIAKA 400 YEYE ANGEHUKUMU TAIFA HILO NA KUWARUDISHA WATU WAKE KUINGIA KATIKA NCHI YA AHADI.


NAKUAMBIA KWELI! FARAO ANATUOGOPA KWA KUWA TUMEKUWA WENGI MNO. ANAUA WATOTO WETU WOTE. WAMISRI NI WADHAIFU NA WAVIVU. WANAUME WETU WANA NGUVU KUTOKANA NA KAZI NGUMU WAFANYAO. WAMISRI WANATUOGOPA.
HAWATAUA MTOTO WANGU, MUNGU ATAMLINDA.
HA! NI NINI MUNGU ANAWEZA KUFANYA KINYUME YA FARAO MWENYE NGUVU?




FARAO, AKIOHOFIA KWAMBA WAYAHUDI WALIKUWA KUW WENGI SANA, ALIAMUA KUUA WATOTO WOTE WA KIUME.

MWANZO 46: 5-7; KUTOKA 1: 1-12, 22


LAKINI MAMA, NITAWAAMBIA ASKARI NINI NA MAJIRANI WAKATI WATANIULIZA YUKO WAPI MTOTO WETU?
UTAWAAMBIA UKWELI. KWAMBA MAMAYAKE ALIMTUPA MTONI MWENYEWE ILI ASKARI WASIMTUPE WENYEWE.


TAKRIBAN 1525 B.C.
MAMA, UNA UHAKIKA HAITAVUJA MAJI IINGE?
IMEFUNIKWA NA LAMI. ITAELEA WALA HAITAZAMA.


JE, SISI TUTAWAHI KUMWONA KAKA YETU TENA? HAWA WAMISRI WAOVU KWELI!
MUNGU ATAMLINDA, WEWE KAA KARIBU UTAZAME.



BINTI YA FARAO ALIKUJA MTONI ILI KUOGA.
TAZAMA! HAPO KUNA SAUTI YA KULIA KUTOKA KWA HICHO KIKAPU!


ANAWEZA KUWA MMOJA WA HAO WATOTO WACHANGA WA KIEBRANIA.
LO, YEYE SI NI MZURI KWELI?
LAZIMA AWE ANA NJAA KWELI.


NINGEPENDA NIMUWEKE AWE WANGU IKIWA NINGEWEZA KUPATA MTU AMBAYE ANAWEZA KUWA MLEZI WAKE.
HUYO, MMOJA WA HAO WATOTO WA KIEBRANIA. LABDA ANAJUA MTU AMBAYE ANAWEZA KUMLEA.


NITAKWENDA KUANGALIA IKIWA NAWEZA KUPATA MTU AMBAYE ANAWEZA KUMLEA. NAJUA MWANAMKE WA KIEBRANIA AMBAYE MTOTO WAKE ALITUPWA NDANI MTO. YEYE BADO ANA MAZIWA MENGI.

KUTOKA 2: 3-9


ILIKUBIDI KUFANYA HIVO. HUNGEWEZA KUMFICHA MILELE. HIVI KARIBUNI AU BAADAYE ASKARI WANGEMPATA NA WAMUUE. NI LAZIMA UEDNDELEE KUMTUMAINIA MUNGU.
NAJUTA NILICHOKIFANYA! JE, NITAWAHI KUMUONA MWANANGU TENA? JE, MUNGU ANAJALI?
MAMA, MAMA!


MAMA, BINTI YA FARAO ALIKUJA MTONI NA AKAMPATA KAKA YANGU MDOGO. ANATAKA KUMUWEKA KWA AJILI YAKE NA KUMLEA, NA ANATAFUTA MTU WA KUMUUGUZA! YEYE ANAKUJA HAPA SASA!
ATUKUZWE MUNGU WA MILELE!


NIMESIKIA ULIPOTEZA MTOTO WAKO. SAMAHANI KWA HILO. NIMEMPATA HUYU MTONI. NITAKULIPA WEWE UMUUGUZE KWA AJILI YANGU.
WAKATI ATAKUA NA KUPITA UMRI WA KUNYONYA NITAMKUJIA NIMPELEKE KWA IKULU AMBAPO ATALELEWA KUWA FARAO WA MISRI. JINA LAKE TUTAMUITA MUSA.
WAKATI MUSA ALIPOKUWA AKIKUA, MAMAKE ALIMFUNDISHA KUHUSU MUNGU WA KWELI WA BABA ZAKE. MUNGU ALIKUWA NA KUSUDI MAALUM KWA KIJANA HUYU MDOGO.


PANDA JUU KIJANA SHUPAVU, TWENDE HADI IKULU.
HAWA WANA MBIO SANA?
ASANTE KWA KUMLEA MUSA. ANAONEKANA MWENYE AFYA NZURI. YEYE ATAKAPOKUA ATAKUWA TAJIRI NA MWENYE NGUVU
KUTOKA 2: 8-10


KAMA MWANA WA KULELEWA KWA BINTIYE FARAO, MUSA ALIKUA NA AKAWA MTU MKUU HUKO MISRI. ALIKUWA AMEKUSUDIWA KUWA TAJIRI NA MWENYE NGUVU, LAKINI HAKUSAHAU URITHI WAKE.


NAKUAMBIA, MUSA, MUNGU WA BABA ZETU; IBRAHIMU, ISAKA, NA YAKOBO, ALIMWAMBIA IBRAHIMU KUWA UZAO WAKE UNGEONGEZEKA NA KWAMBA WATAKUWA WAGENI KATIKA NCHI AMBAYO SIO YAO. NAAM, NDIO HAPA TULIPO!
NDIO, NA PIA ALIMWAMBIA IBRAHIMU KWAMBA TUNGETESWA KATIKA HIYO NCHI YA UGENI KWA MIAKA 400. KUFIKIA SASA TUMEKUWA HAPA KWA MUDA WA MIAKA 359, MIAKA 41 TU NDIO IMEBAKI.


HILO LINAONEKANA KUWA LA AJABU. FARAO HANGERUHUSU WATUMWA WAKE WOTE WANAONDOKE, NA YEYE HAKIKA ASINGEWARUHUSU KUONDOKA NA UTAJIRI. LAKINI LABDA KUNA NJIA. KWA NINI TUSUBIRI MIAKA 41 ZAIDI?
NA PIA ALIMWAMBIA IBRAHIMU KWAMBA ANGELIHUKUMU TAIFA HILO KWA UOVU AMBAO WANGETUTENDEA, NA KWAMBA TUNGEONDOKA NA UTAJIRI MKUBWA NA KURUDI KWENYE ARDHI AMBAYO MUNGU ALIWAPA BABA ZETU.


WANA WA KIEBRANIA WALITESEKA CHINI YA UTAWALA WA MABWANA ZAO. WALILAZIMIKA KUFANYA KAZI KWENYE MASHIMO YA LAMI, KUTENGENEZA MATOFALI. MUSA HAKUWEZA KUVUMILIA KUWAONA WAKITESEKA, KWA HIVYO ALIAMUA KUFANYA KITU KULIHUSU JAMBO HILO
SIMAMA KABLA AKUPIGE HADI UFE!
SIMAMA, NGURUWE MCHAFU WEWE!
EBERI, TAFADHALI AMKA
KUTOKA 2: 10-11



SIKU MOJA MUSA ALIONA MMOJA WA WAMISRI AKIMPIGA KIKATILI MMOJA WA WATU WAKE MWENYEWE.
WAKATI WA UKOMBOZI UMEFIKA. HILI LAZIMA LISIMAME.


WHACK!
IMETOSHA!
MUSA ALIMUUA YULE MMISRI NA KUUZIKA MWILI WAKE, LAKINI MTU MMOJA ALIMWONA NA AAKAMRIPOTI KWA FARAO.


MUNGU WANGU! NIMEFANYA NINI SASA?
SIMAMA! LAZIMA UFIKISHWE KOTINI KWA MAUAJI!
NI MUSA HUYOO!


TAKRIBAN 1491 B.C.
MUSA ALIONDOKA MISRI NA KUKIMBILIA JANGWANI. ALIKUWA PEKE YAKE, BILA FAMILIA AU MARAFIKI. YEYE HAKUOKOA WATU WAKE. HAKUWEZA HATA KUJIKOMBOA.
KUTOKA 2: 11-15


MUSA ALITEMBEA KWA MUDA WA SIKU NYINGI. WAKATI HAKUWEZA KWENDA MBALI ZAIDI, YEYE AKAFIKA KWENYE KAMBI YA WACHUNGAJI.
TAZAMA! MTU!
ANAONEKANA MCHOVU SANA KUFA, LETA MAJI.
YEYE NI MMISRI!


MUSA ALIPATA MAISHA MAPYA KATI YA WAMIDIANI. ALIJIFUNZA NJIA ZA NYIKANI, ALIOA HUKO, NA AKAWA MCHUNGAJI. MIAKA AROBAINI ILIPITA NA MISRI IKAWA KUMBUKUMBU YA MBALI. MUSA ALIKUWA AMEKATA TUMAINI YA KUWAONA WATU WAKE TENA.


AJABU SANA! JE, KICHAKA HICHO KILISHIKAJE MOTO, NA KWANINI MOTO HAUKICHOMI? KINAWAKA TU BILA KUCHOMEKA.


MUSA, VUA VIATU ZAKO. ULIPOSIMAMA NI MAHALI PATAKATIFU. MIMI NI MUNGU WA BABA ZAKO IBRAHIMU, ISAKA, NA YAKOBO.


NIMEONA MATESO NA KUSIKIA MAOMBI YA WATU WANGU HUKO MISRI. NI WAKATI WA KUWAOKOA KUTOKANA NA MATESO YAO NA KUWARUDISHA KUINGIA KATIKA NCHI NILIYOAHIDI BABA ZAO.
NITAKUTUMA KWA FARAO NAWE UTAWATOA WATU WANGU KUTOKA KWA UTUMWA. UTAMWAMBIA AWACHE WATU WANGU WAENDE, NAYE ATAKATAA. KISHA NITAONYESHA NGUVU YANGU KWA MISRI. BAADA YA HAPO ATAWAACHA WAENDE.
KUTOKA 2: 16-3: 10



LAKINI HAWATAAMINI KWAMBA WEWE UMENITUMA. WAO WATACHEKA TU.


TUPA FIMBO YAKO CHINI.


IMEKUWAJE? FIMBO YANGU?


IMEBADILIKA KUWA NYOKA HATARI!


ICHUKUE HIYO NYOKA KWA MKIA!


IMEGEUKA TENA KUWA FIMBO YANGU!


NENDA MISRI. NITAKUFUNDISHA NINI CHA KUSEMA NA KUKUAMBIA KIPI CHA KUFANYA. NDUGU YAKO HARUNI ATAKUWA MSAIDIZI WAKO.
KUTOKA 4: 1-4, 12-16


1445 B.C.
IMEKUWA MIAKA AROBAINI. WOTE AMBAO WANAJUA CHOCHOTE KUHUSU MAISHA YANGU YALIYOPITA WAMEKUFA. HAKUNA MTU ATAKAYENITAMBUA.
UNARUDI MISRI! LAKINI VIPI KUHUSU WOTE WALE WANAOTAFUTA KUKUUA?
MPAKA FARAO ARUHUSU WATU WA MUNGU KUENDA
MUDA GANI UTAKUWA UMEKWENDA?


WAITE WAZEE WOTE KWA PAMOJA! WAKATI WA UKOMBOZI UMEFIKA!
HAO NI KINA NANI?
HUYO NI HARUNI MLAWI. MWINGINE MMOJA ANAONEKANA KAMA SISI, LAKINI YEYE SI MTUMWA.


MUSA ALIZALIWA MIAKA THEMANINI ILIYOPITA WAKATI FARAO ALIPOANZA KUUA WATOTO WOTE WACHANGA WA KIUME. MAMA YAKE AKAMFICHA KWENYE KIKAPU MTONI. NA KWA MAJALIWA YA MUNGU, BINTI YA FARAO ALIMPATA MUSA NA AKAMLEA KAMA MMISRI.
NJOONI KARIBU, NINYI WAZEE WOTE WA ISRAELI.
KUTOKA 4: 29-31


MIAKA AROBAINI ILIYOPITA, MUSA ALIAMUA AFADHALI ATESEKE NA WATU WAKE MWENYEWE KULIKO KUTAWALA KAMA MMISRI. ALIAMUA KUTUKOMBOA KWA NGUVU ZAKE MWENYEWE NA AKASHINDWA. KWA MIAKA 40 ILIYOPITA, AMEKUWA AKIISHI JANGWANI YA NCHI AMBAYO MUNGU ALIAHIDI BABA ZETU. HIVI MAJUZI MUNGU ALIZUNGUMZA NAYE NA KUMUONYESHA YEYE JINSI YA KUTUOKOA KUTOKA KWA FARAO! SASA, MUSA ATAWAONYESHA ISHARA AMBAZO YEYE ATATUMIA KUMSHAWISHI FARAO KUTUACHA TUENDE.


MUNGU WA IBRAHIMU ALIZUNGUMZA NAMI KUTOKA KWENYE KICHAKA KINACHOWAKA NA KUNITUMA KUWAONGOZA KURUDI KATIKA NCHI YA BABA ZETU. HII HAPA NDIO ISHARA.


ALAA! FIMBO YAKE IMEAGEUKA KUWA NYOKA
MSIOGOPE.


TAZAMA HII SASA.


MUNGU AMETUMA MKOMBOZI.
NDIO, FARAO ATAKIONA.



NI MUUJIZA!
SASA TUNAKWENDA KWA FARAO!
MUNGU WA IBRAHIMU!
KUTOKA 4:17, 30


HAKUJABADILIKA HUKU TANGU NILIONDOKA HAPA MIAKA AROBAINI ILIYOPITA. KUMBUKA KUSEMA KILE TU MIMI NILIKUAMBIA.


MUNGU WA ISRAELI ALIONGEA NA MUSA. MUNGU ALISEMA UWAACHILIE WAISRAELI WAENDE SAFARI YA SIKU TATU KUINGIA JANGWANI KUABUDU NA KUTOA DHABIHU.
*HA!* MUNGU WA ISRAELI? *HA, HA, HA!* SIJUI MUNGU WAKO. NI NANI HUYU MUNGU AMBAYE MIMI NAPASWA KUMTII? HUO NI MZAHA TU. SIWEZI KUWAACHA WATUMWA WANGU WAENDE SAFARI YA SIKU TATU NYIKANI.


NIMESIKIA JINSI UNACHOCHEA WATU WANGU, KUSABABISHA WAO KUACHA KUFANYA KAZI. NA SASA WANATAKA KUCHUKUA SAFARI YA SIKU TATU KUABUDU MUNGU AMBAYE HATA SIMJUI WALA KUMFAHAMU. NITAHAKIKISHA KUWA WAO WATAKUWA NA KAZI ZAIDI YA KUFANYA.
KUANZIA SASA, WATALAZIMIKA KUTOA NYASI ZAO ZA KUTENGENEZA MATOFALI. SASA, TOKA MBELE YA MACHO YANGU NA URUDI ULIKOTOKA MARA MOJA.

KUTOKA 5: 1-7


ANATOA WAPI UJASIRI KAMA HUO?
INACHEKESHA KWELI. WALIANDAMANA HAPA KANA KWAMBA WALIKUWA SAUTI YA MUNGU.


UNAMAANISHA KWAMBA WEWE ULICHOFANIKIWA KUFANYA NI KUZIDISHA MZIGO WETU WA KAZI? HUO SASA NDIO UKOMBOZI. NA UNAFIKIRI MUNGU ALIKUTUMA?
ANAFIKIRIA YEYE NI NANI?
SIAMINI TULIKUBALIANA NA UPUUZI WAKE.
HUU NI MZAHA TU!


KWA HIVYO, HUNA KAZI YA KUTOSHA YA KUFANYA. UNATAKA KWENDA KUMWABUDU MUNGU WAKO. TUTAKUFUNZA JINSI YA KUTOKUWA MVIVU.


YEHOVA, TANGU NILIPOKUJA KUZUNGUMZA KWA JINA LAKO, YAMENIPATA MABAYA. KWA NINI ULINITUMA?
MIMI NDIMI BWANA, MUNGU WA BABA ZAKO, NA MIMI NIMEONA MATESO NA NIMESIKIA KILIO CHA WATU WANGU ISRAELI.
NI WAKATI WA KUTIMIZA AHADI YANGU KWA IBRAHIMU NA KUONGOZA WATU HAWA MPAKA NCHI YA KANAANI. WEWE, MUSA, NDIO UTAWAONGOZA.


LAKINI MIMI SIWEZI KUZUNGUMZA VIZURI. FARAO HATANISIKILIZA.
HARUNI ATAZUNGUMZA KWA NIABA YAKO; WEWE NISIKILIZE TU NA UMWELEZE CHA KUSEMA. MWANZONI, FARAO HATAKUSIKILIZA, LAKINI NITAMUONYESHA ISHARA KUBWA HADI WAMISRI WATAJUA YA KUWA MIMI NDIMI BWANA MUNGU WA KWELI PEKEE.


*HA, HA!* NI NINI KIMEWALETA HAPA TENA?
YEHOVA ANASEMA, "ACHILIA WATU WANGU WAENDE. "


HII HAPA ISHARA KWAMBA YEHOVA AMENENA.
*HA, HA, HA!* HIZO NI HILA YA KICHAWI TU. HAZIWEZI KUNITISHA. WAITENI WACHAWI WETU.




KUTOKA 5: 10-23, 7: 7-11


NJOONI HARAKA NA MLETE HIZO HILA ZA KICHAWI ZA KUGEUZA VIJITI KUWA NYOKA.


MUNGU WETU WA NYOKA, NESETI, AMETUTUMA KUKUAMBIA UTENGENEZE MATOFALI ZAIDI. *HA, HA, HA!*




KUTOKA 7: 11-12


TAZAMA!
NYOKA YAKE INATAKA KUPIGANA NA NYOKA ZETU.


NYOKA YAKE INAKULA MOJA YA NYOKA ZETU!


IMEMEZA NYOKA YETU KABISA!


USINIAMBIE ITAJARIBU KULA INGINE! MUNGU WETU WA NYOKA, NESETI, ATAKASIRIKA.


NASHINDWA KUAMINI! NYOKA YAKE IMEKULA KILA MOJA YA NYOKA ZETU.
INAWEZEKANA AJE KWELI?


YEHOVA NDIYE BWANA MUNGU WA UUMBAJI. ANASEMA, "WACHILIA WATU WANGU WAENDE. "

KUTOKA 7:12


SIJUI ULIVYO WEZA KUFANYA HIVYO, LAKINI SITALIPA MAONYESHO YAKO YA SARAKASI ZA KICHAWI KWA WATUMWA MILIONI. *ONDOKA MACHONI PANGU!*
KUTOKA 7:13 "NAYE (MUNGU) AKAUFANYA MOYO WA FARAO MGUMU, KWAMBA HAKUWASILIKIZA; KAMA BWANA ALIVYOKUWA AMESEMA. "


KWA NINI YEHOVA ATUTUME NA ISHARA AMBAYO WACHAWI WA FARAO WANGEWEZA KURUDIA HAPO KWA HAPO? ILITUFANYA TUONEKANE KAMA WAPUMBAVU.
SIJUI VIPI, LAKINI MUNGU ALISEMA KWAMBA ANGEFANYA MOYO WA FARAO MGUMU. HICHO NDICHO KIMETOKEA. ULIONA JINSI ALIVYOKASIRIKA WAKATI FIMBO YANGU ILIPOKULA NYOKA ZAKE?
LAZIMA NITAFUTE PAHALI NIZUNGUMZE NA YEHOVA. SIJUI KIPI CHA KUFANYA KUTOKA HAPA.



MUNGU ALIKUTANA NA MUSA TENA NA KUMWAMBIA ATAKACHOFANYA. WAMISRI WALIKUWA WAMEMDHIHAKI MUSA. WATU WAKE MWENYEWE WALIMKATAA KWA SABABU FARAO ALIFANYA UTUMWA WAO KUWA MGUMU ZAIDI, LAKINI MUSA ALIMWAMINI MUNGU NA KUTII INGAWA HAKUELEWA.
***BWANA ANASEMA,*** "KWA SABABU UNAKATAA KUWACHILIA WATU WANGU WAENDE, NA NDIVYO MPATE KUJUA YA KUWA MIMI NDIMI MUNGU WA KWELI, MAJI YOTE YA MISRI YAT***AGEUKA*** KUWA DAMU."




KUTOKA 7: 15-21


UNAONA? WACHAWI WANGU WANAWEZA KUFANYA HIVYO PIA. SIWEZI KUSHAWISHIKA NA HILA ZAKO ZA KICHAWI.


SIJAWAHI KATIKA MAISHA YANGU YOTE KUONA KITU KAMA HICHO. HATA CHEMCHEMI PAMOJA NA MABWAWA MADOGO YAMEGEUKA DAMU. ETI ALISEMA NI NINI JINA LA MUNGU WAKE?
KAMWE SIJASIKIA JINA LAKE. ANA UTOFAUTI GANI KWELI? TUNA MAELFU YA MIUNGU. MUNGU WA MTO NILE MTO LAZIMA AWE NDIYE AMEKASIRIKA.


HUYO JAMAA MUSA ANASEMA KWAMBA MUNGU WAKE NDIYE BWANA MUNGU WA KWELI PEKEE.
MUNGU MMOJA? **HIYO NI MZAHA TU.**


SIKU SABA BAADA YA MAJI KUGEUKA KUWA DAMU, MUSA TENA ALILETA HUKUMU ZA MUNGU JUU YA MISRI.
ACHA MAJI YALETE VYURA KWA WINGI.




KUTOKA 7: 21-25, 8: 6


NYUMBA YANGU IMEJAA VYURA.


MISRI YOTE IMEJAA VYURA. MIUNGU *IMEGHADHABIKA!*
WAKO WAPI MAKUHANI WETU? HAWAWEZI KUFANYA KITU?


EIIIII!


KWANINI WANATENGENEZA VYURA ZAIDI? HUYO MUSA HAKUTUPA VYA KUTOSHA? SASA FARAO ANATUPA ZAIDI.
FARAO, TAZAMA, SISI WACHAWI TUNAWEZA KUTENGENEZA VYURA PIA.


KWANINI USIWAACHILIE WAENDE JANGWANI KAMA WALIVYOULIZA? HATUWEZI KUVUMILIA ZAIDI YA HII.


ITENI MUSA. MWAMBIE NINGEPENDA KUONGEA NAYE.
NDIO BWANA, KAMA USEMAVYO.


OMBA YEHOVA AONDOE HAO VYURA. IKIWA ATAFANYA HIVYO, NITAWACHILIA WATU WAKO WAENDE WAKAFANYE DHABIHU.
SEMA TU NI WAKATI UPI UNGETAKA HAO VYURA WAFE KISHA ITAKUWA HIVO.


KESHO ASUBUHI.
KULINGANA NA MANENO YAKO MWENYEWE ITAKUWA HIVYO, ILI WOTE WAPATE KUJUA HAKUNA MUNGU KAMA YEHOVA MUNGU.

KUTOKA 8: 7-10


FARAO ALIPOONA KUWA CHURA WALIKUFA WAKATI AMBAO ALIAMURU, ALIUFANYA MGUMU MOYO WAKE NA KUKATAA WAEBRANIA WAONDOKE.
HUYU YEHOVA NI MUNGU WA AINA GANI ANAJAZA VYURA NCHINI KWETU?
KIPI KINACHOKUFANYA UFIKIRI NI MUNGU ALIYEFANYA HAYA? LABDA TU NI MAJIRA YAKO HIVI NDIO MAANA KUNA VYURA.


BASI MUSA ALIJUAJE HADI KUTABIRI KUWA INGEFANYIKA HIVI? NA ALIJUAJE WAKATI HASWA AMBAPO WANGEKUFA?
EH. NYAMAZA NA UCHOTE, AMA HATUTAMALIZA LEO.


NA YEHOVA AKAMWAMBIA MUSA, "MWAMBIE HARUNI AUNYOSHE MKONO WAKE NA APIGE VUMBI ARDHINI HADI KUWE NA CHAWA MISRI YOTE."


VUMBI YOTE MISRI IKAGEUKA CHAWA.
IEEEEE!


UNAAMANISHA NINI HUWEZI TENGENEZA CHAWA? ***WATU WATAFIKIRI MUNGU WAKE MUSA ANA NGUVU KULIKO WETU.*** JARIBU TU ATA KUWAHADAA.
LAKINI KWA KWELI HII NI KAZI YA MUNGU. HAKUNA MTU ANAYEWEZA KUFANYA YALE AMBAYO MUNGU AMEFANYA. HATUNA NGUVU.


LAZIMA KUWE NA SABABU YA KIASILI. ILA HATUWEZI KUENDELEA HIVI. MWAMBIENI MUSA IWAPO MUNGU ATAONDOA CHAWA HAWA BASI NITAWAACHILIA WAEBRANIA WAENDE WAKAMUABUDU MUNGU WAO.
KUTOKA 8:13-19


CHAWA WAMEONDOKA LAKINI SITAWAACHILIA WAEBRANIA WAENDE. HAKUNA LINGINE ANALOWEZA KUFANYA ZAIDI.


MUNGU AMEZUNGUMZA NA MUSA NA KUMUELEZA, "NITATUMA NZI WENGI MISRI. VYUMBA VYENU VITAJAA NZI. MARA HII NITAWEKA TOFAUTI KATI YA WAMISRI NA WAEBRANIA.
HAKUTAKUWA NA NZI KATI YA WATU WANGU. NA KWA HILI WATAJUA KUWA MIMI NDIYE MUNGU WA DUNIA NZIMA."


BABA, MBONA MAKUHANI WETU HAWAWEZI KUMSIMAMISHA MTU HUYU? KWANI HAWANA UWEZO?
SIJUI LOLOTE KUHUSU DINI. MIMI HUSHUGHULIKA NA MAMBO YANGU.


NI KAMA TU ALIVYOSEMA. HAKUNA NZI KATI YA WAEBRANIA! KWELI HII NI KAZI YA MUNGU.
NENDA UKAMTAFUTE MUSA.


NENDENI MKAMTOLEE MUNGU WENU SADAKA LAKINI MSITOKE MISRI.
LAZIMA TUENDE ANGALAU SAFARI YA SIKU TATU.
NIMESEMA MNAWEZA KUENDA ILA MSIENDE MBALI SANA. ZUNGUMZENI NA MUNGU WENU ATUONDOLEE HAWA NZI.




KUTOKA 8:20-32


MUNGU ALITUMA JANGA LINGINE MISRI. MIFUGO YOTE YA WANAMISRI ILIGONJEKA NA KUAGA. MIFUGO YA WAEBRANIA ILIBAKI HAI NA WALA HAIKUGONJEKA.
MIFUGO YETU YOTE IMEAGA NA YENU INA AFYA. MTAELEZAJE HAYA?
MUSA ALITUELEZA KUWA MUNGU WA BABA ZETU AMEKUJA KUTUOKOA KUTOKANA NA JANGA. LAKINI MIMI SIJUI MENGI.


MAKUHANI WETU WANATOLEA MIUNGU YETU SADAKA. MIUNGU YA MAFAHALI ITAKASIRISHWA NA NYINYI NA HAYA YOTE YATAISHA.


MIUNGU YA MISRI IKO WAPI? HAWANGEWEZA KUWAOKOA?
MWAMBIENI FIRAUNI MSHACHELEWA. MAFAHALI WOTE WAMEAGA NA WATU HAWATAFURAHI WATAKAPOJUA KUWA MIUNGU YA MAFAHALI HAINGEWEZA KUWAOKOA.


ILA FIRAUNI ALIUKAZA MOYO WAKE.
KUTOKA 9:6-7

MARA NYINGINE MUNGU ALIMWAMBIA MUSA AMWAGE JIVU MJINI NA WANAMISRI WANGEPATA VIDONDA.




WAITE WACHAWI ILI WAWEZE KUPAMBANA NA HAYA.


UMEITANA MKUU.
WEWE PIA HAUNA UWEZO DHIDI YA MUNGU HUYU WA MUSA?


ONDOKENI MBELE YANGU NYINYI ***WAPUMBAVU.*** NYINYI HUFANYA VIFUMBA MACHO VIDOGO MBELE YA WATU. NYINYI NI WAONGO TU.


AMKA MAPEMA KISHA USIMAME MBELE YA FARAO NA KUSEMA, "BWANA MUNGU WA WAEBRANIA ANASEMA, 'ACHILIA WATU WANGU WAENDE. KWA MAANA PIGO LINALOFUATA LITAKUWA MBAYA ZAIDI. LITALETA UHARIBIFU ZAIDI NA LITAWAUA WATU WAKO WENGI. KWA HILI WEWE UTAJUA YA KUWA HAKUNA MUNGU KAMA MIMI.
LABDA HAUTAMBUI, LAKINI MIMI NDIYE AMBAYE NILIKUFANYA UWE FARAO. UNAONA, NILIJUA UNGEUFANYA MOYO WAKO KUWA MGUMU NA KUKATAA KUWAACHA WATU WANGU WAENDE."


'UKAIDI WAKO UNANIPA FURSA YA KUDHIHIRISHA UWEZO WANGU NA KULETA HUKUMU JUU YA MISRI KWA UKATILI WALIOUFANYIA WATU WANGU. UNAKUZA MASLAHI YAKO MWENYEWE NA KUPINGA KUFANYA MAPENZI YANGU,
...HIVYO KESHO KWA WAKATI KAMA HUU MIMI NITALETA MVUA YA BARAFU NA MOTO. KAMA VILE DUNIA HAIJAWAHI KUSHUHUDIA KABLA YAKE."


"NAWAAMBIA HIVYO ILI MUWEZE KUONYA KILA MTU KUJIWEKA MWENYEWE AU WANYAMA ANAOWEZA KUWA NAO NDANI YA NYUMBA, KWA SABABU WOTE WALIO NJE WATAKUFA."
KUTOKA 9:8-19


IFANYIKE KAMA YEHOVA ALIVYOSEMA.


INAWEZEKANAJE MOTO NA BARAFU KUCHANGANYIKA?
MUNGU MKUU SETHU, UTUOKOE.
AHHH!
WALE AMBAO HAWAKUJALI ONYO NA KUPATIKANA NJE WALIKUFA.


BABA, MUSA ANAFANYAJE HIVYO? MUNGU WAKE NI MWENYE NGUVU ZAIDI KULIKO MUNGU SETHU? BWANA WA MACHAFUKO NA DHORUBA?
ANADAI KUNA MUNGU MMOJA NA KWAMBA HAWA WAEBRANIA NI WATOTO WAKE.
LAKINI HAKUNA MTU ALIYEWAHI KUMWONA HUYO MUNGU WAKE, HATA WAEBRANIA. MUNGU WAKE AMBAYE ANADAI NI ROHO TU, KUJARIBU KUMSHAWISHI FARAO KUWAACHA WAINGIE JANGWANI KUABUDU.


EEH MUNGU MKUU SETHU, BWANA WA MACHAFUKO NA DHORUBA, TUNAKUSIHI, USIMAMISHE DHORUBA HIZI HATARI. HAKIKA WEWE MKUU KULIKO HUYU MUNGU ASIYEWEZA KUONEKANA WA MUSA.
KUTOKA 9:23-26


HAIKUJI KARIBU NA SISI, WA MISRI PEKE YAO.
BABA NAOGOPA. MOTO NA BARAFU UTATUFIKIA PIA?


LA MWANANGU, YEHOVA ANAWAADHIBU WAMISRI PEKEE.
INASIKITIZA.


NIMETENDA DHAMBI DHIDI YA YEHOVA. MUNGU WA WAEBRANIA NI MWENYE HAKI NA MIMI NA WATU WANGU NI WAOVU. ULIZA YEHOVA ASIMAMISHE MOTO NA BARAFU, NAMI NITAWAACHA WATU WAKO WAONDOKE MARA MOJA.


MARA TU NITAKAPOKUWA NJE YA MJI NITAINUA MIKONO YANGU MBINGUNI NA PIGO LITAKOMA. KUPITIA HILI UTAJUA YA KWAMBA NCHI NI YA MWENYEZI MUNGU, LAKINI BADO HUNA UKWELI KATIKA MANENO YAKO, WEWE BADO SIO MCHA MUNGU.
FARAO ALIPOONA YAMEISHA, ALIUFANYA MOYO WAKE KUWA MGUMU TENA NA KUKATAA WAEBRANIA WAONDOKE.


MUNGU ALITUMA PIGO LINGINE. NZIGE WALIKUJA NA KUKULA KILA KITU CHA KIJANI AMBACHO DHORUBA HAIKUWA IMEHARIBU. KISHA NZIGE WAKANGIA NDANI YA NYUMBA.
KUTOKA 9:26-35, 10:13-15


MAMA!
MAMA!
AHHHEEE!
SHIKA
HIYO.


GEBU, MUNGU WA MIMEA, HIVI HUONI YALE HUYU MUNGU WA WAEBRANIA ANAFANYIA MAZAO YETU?
OSIRI, ONYESHA NGUVU YAKO LEO.
FARAO ALIMUITA MUSA NA KUAHIDI KUWAACHA WAEBRANIA WAENDE, LAKINI MUNGU ALIPOONDOA NZIGE, BASI FARAO AKAUFANYA MOYO WAKE MGUMU, NA AKAKATAA KUWAACHILIA WATUMWA.
KUTOKA 10:14-20

KISHA MWENYEZI MUNGU AKAFANYA GIZA KUSHUKA JUU YA MISRI. KWA SIKU TATU KULIKUWA NA GIZA KULIKO USIKU WA MAWINGU, LAKINI KATIKA NYUMBA ZA WAEBRANIA HAKUKUWA NA GIZA.




ONDOKA MACHONI MWANGU. KWA KUWA SIKU AMBAYO NITAKUONA TENA UTAKUFA.
UMEONGEA UKWELI KWA MARA YA KWANZA. KWA SABABU HATUTAWAI ONANA TENA.


RA, MUNGU MKUBWA WA JUA, TUSIKILIZE. KWA SIKU TATU WEWE UMEJIFICHA MWENYEWE. HIVI HUWEZI KUMSHINDA HUYU MUNGU WA WAEBRANIA?



NDILO HILI! PIGO MOJA LA MWISHO, NA FIRAUNI ATAFURAHI KUONA TUKIONDOKA MISRI. USIKU WA MANANE MHARIBIFU ATAPITA KATIKA NCHI YA MISRI. MTOTO WA KIUME ALIYEZALIWA WA KWANZA KATIKA KILA FAMILIA ATAKUFA. NI MAPENZI YA MUNGU KUADHIBU DHAMBI USIKU HUU.
NA JE WAZALIWA WA KWANZA WETU? WATAAGA PIA?


MUNGU ANA MPANGO WA *KUWAOKOA* WOTE WANAO AMINI, HATA WAMISRI. NENDENI SASA, TAFUTENI MWANAKONDOO AU MBUZI MCHANGA, KISHA MMUUWE USIKU WA LEO, ALAFU MPAKE DAMU YAKE KWENYE UPANDE WOWOTE WA MLANGO.
YEHOVA ANASEMA, "NINAPOPITA KWENYE NCHI USIKU WA LEO, KUUA WANAUME WOTE WALIO WAZAWA WA KWANZA, NITAKAPO ONA DAMU NJE YA MILANGO YENU NITAPITA JUU YA NYUMBA HIYO, NA MZALIWA WA KWANZA HATAKUFA." KAENI KATIKA NYUMBA ZENU USIKU WA LEO NA KULA MWANAKONDOO MNAYEMUUA..
KUTOKA 10:22-29, 11: 4-5, 12: 3-7


KESHO NENDENI KWA MABWANA ZENU WAMISRI NA KUKOPA VITU VYAO VYA THAMANI, DHAHABU, VITO, NA FEDHA. MWENYEZI MUNGU AMEGUZA MIOYO YAO NA WATATOA KWA UHURU NA WINGI.
PAKIENI VITU VYENU NA KUWA TAYARI KUONDOKA KESHO ASUBUHI. HAMTAREJEA MISRI TENA. HUU UTAKUWA MWANZO MPYA KWENU NYIE.


BABA, HUYU NI MWANA-KONDOO WETU WA PEKEE, HATUNGETUMIA RANGI NYEKUNDU AU KITU KINGINE?
MWANAGU, MUNGU ALIAGIZA KUWA TUMUUE MWANAKONDOO NA KUPAKA DAMU YAKE KWENYE MLANGO. LAZIMA TUFANYE JINSI ALIVYOSEMA. UMEONA JINSI ANAVYOWAPIGA WALE WASIOMTII. MWANAKONDOO HUYU NI WA KUTUOKOA KUTOKANA NA KIFO.


KWA HIVYO MWANAKONDOO HUYU AMEFARIKI KWA AJILI YANGU?
NA KWA AJILI YANGU PIA. MIMI PIA NI MZALIWA WA KWANZA.


MAMA, KWA NINI BABA ANACHORA MLANGO WETU NA DAMU?
YEHOVA ALISEMA, "NITAKAPOONA DAMU KWENYE MLANGO NITAJUA HAKIKA NYINYI MNANIAMINI, BASI SITAMUUA MTU YEYOTE ALIYE NDANI YA NYUMBA."
KUTOKA 12:26-28, 35-36


KWA NINI HAMKUMUUA MWANA-KONDOO NA KUWEKA DAMU KWENYE MLANGO WENU?
HA! UNAAMINI HUO UPUZI? **ITAWEZEKANAJE DAMU** KIDOGO KWENYE MLANGO ISIMAMISHE KIFO KUJA? SISI HATUOGOPI, AU SIO MWANANGU JOIKIM?


BILA SHAKA, SIOGOPI.
DINI NI KWA AJILI YA WADHAIFU.


BABA, KWA NINI USIKU HUU NI TOFAUTI NA SIKU ZINGINE?
KWA SABABU USIKU WA LEO MUNGU ATATUMA MUARIBIFU WAKE KUUA WANAUME WOTE WALIO WAZAWA WA KWANZA AMBAO HAWAMUAMINI. NA ANAPO IONA DAMU ATAPITA JUU YA NYUMBA HIYO.
HUU NI MWANZO WA SIKU KWETU. KILA MWAKA KWA WAKATI KAMA HUU TUTASHEREHEKEA PASAKA HII NA KUKUMBUKA KWAMBA MUNGU ALITUOKOA KUTOKA MIKONONI MWA FIRAUNI.


EE BABA, SIKILIZA WANAVYOPIGA MAYOWE! MHARIBIFU LAZIMA AWE HAPA!
MSIOGOPE.TUMEMTII MUNGU. DAMU IPO KWENYE MLANGO. SISI TUNAKULA MWANA-KONDOO.


MWANANGU AMEKUFA! LO, MUNGU WANGU FANYA KITU. MUITENI MUSA!
KUTOKA 12:28


IEEEEE!
LA, MUNGU! MWANANGU ASIFE!
LAAA!


SAMAHANI, LAKINI UMECHELEWA SANA. MLIONYWA LAKINI HAMKUAMINI. WENGI WAMEKUFA USIKU WA LEO.
WAKATI MHARIBIFU ALIPOPITA KWENYE MJI USIKU HUO, MAELFU WALIKUFA. WALIOKUWA WAMEAMINI NA KUPAKA DAMU KWENYE MILANGO YAO WALIPONEA.


MTOTO WETU AMEKUFA!
HARAKISHA, MLETE MUSA HAPA!


MAMBO GANI HAYA...
NI MZALIWA WA KWANZA KWAO.
KUTOKA 12:29-31



FIRAUNI ALIMUITA
MUSA TENA.


LAKINI FIRAUNI HAKUANGALIA USO WA MUSA.




KAMA VILE MUNGU ALIVYOWAAHIDI BABA ZAO, BAADA YA MIAKA MIA NNE WALIKUWA WANAONDOKA MISRI. WAMISRI WALIWAPA WAEBRANIA DHAHABU, VITO, CHAKULA -- CHOCHOTE WALICHOTAKA NA WANGEWEZA KUBEBA. ILIKUWA TUKIO LA FURAHA KWA WANA WA KIEBRANIA: SIKU YA KWANZA YA TAIFA JIPYA.




KUTOKA 12:31-38, 13:21-22



## SURA YA 4

# KUTOKA


WALITEMBEA HADI KUFIKA MILIMANI KANDO YA BAHARI YA SHAMU. WALIPIGA KAMBI HUKO WAKIZUNGUMZA JINSI WANGEWEZA KUVUKA BAHARI SHAMU.


BAADA YA FARAO KUOMBOLEZA MWANAWE ALIJAWA NA HASIRA ZAIDI.
TAYARISHENI MSAFARA! MUWAFUATE WAEBRANIA. MUWARUDISHE HUKU AMA MUWAUE.
TUTAFANYA UTAKAVYO, MKUBWA.
KUTOKA 14:5-7


TAZAMA, JESHI LA MISRI LINAKUJA! TUMEFUNGIWA JANGWANI.
MUSA ALITULETA HAPA TUFE. INGEKUWA VYEMA TUBAKI WATUMWA KULIKO KUFIA HUKU.


WAMISRI WALIPOWAONA WAEBRANIA NA WALIPOKUMBUKA JINSI MUSA ALIFANYA MISRI ITESEKE, WALIKUWA TAYARI KUWAUA.
HAKUNA LOLOTE MUNGU ANAWEZA FANYA KUTUOKOA SASA.
MILIMA IKO MBELE YETU NA BAHARI PIA. TUMETEGWA.


SIMAMENI MLIKO. MUNGU ATATUOKOA KWA NJIA KUU.
MUNGU AMEUKAUSHA MOYO WA FARAO TENA. BAADA YA LEO HAMTAWAHI KULIONA JESHI LA MISRI TENA.
KUTOKA 14:5-13


JESHI LA MISRI LILIPOKUWA KARIBU KUFIKIA WAEBRANIA, MOTO MKUBWA ULITOKA MBINGUNI NA KUFUNGA NJIA. USIKU HUO, WAEBRANIA WALIONA MWANGAZA ILHALI WA MISRI WALILIONA GIZA TUPU.


MUSA ALIINUA FIMBO YAKE JUU NA UPEPO MKUBWA ULIKUJA TOKA MBINGUNI, UKAGAWANYA MAJI NA KUKAWA NA NJIA KATI YA BAHARI.
HUU ULIKUWA MUUJIZA MKUBWA SANA. WANA WA ISRAELI WALITEMBEA KATI YA BAHARI KWA NCHI KAVU.
SIKU ZILIZOKUJA WALIIMBA KUHUSU MUNGU ALIYEFANYA NJIA KATIKATI YA BAHARI. KILA MTU ALIFAHAMU KUWA KUNA MUNGU MMOJA TU NA JINA LAKE NI YEHOVA.
KUTOKA 14:15-22


HII IMEPITA KILA KITU TULICHOKIONA MISRI.
KWELI MUNGU WETU NI MWEMA KULIKO WOTE.


JOSAYA! UNA WAZIMU? ONDOKA HAPO. UNAJUA HUWEZI KUOGELEA.


NATAKA KUWAGUZA SAMAKI HAWA WANAOPENDEZA.


WAEBRANIA WALIPOKUWA KARIBU KUVUKA, MUNGU ALIONDOA MOTO ULIOKUWA UMEPINGA WAMISRI. HAWAKUWA WAMEONA BAHARI IKIWA IMEJIGAWANYA, KWA HIVYO WAKAKIMBIA KUWAFIKIA WAEBRANIA.
MBELE, WAUENI WAEBRANIA!
KUTOKA 14:22-23


LEO MUMEONA UWEZO WA YEHOVA.
TAZAMA, MAJI YANARUDI. WATAZAMA.


KILA MWANAJESHI WA MISRI AZLIZAMA KWENYE BAHARI. MIUNGU YAO YA MBAO NA MAWE HAINGEWASAIDIA.
KUTOKA 14:27-28


TAZAMA MIILI HII YOTE. BAHARI IMEJAA WANAJESHI WA MISRI WALIOKUFA.
KWA KWELI YEHOVA NDIYE BWANA MUNGU PEKEE. HAKUNA MUNGU MWINGINE AWEZAYE KUTENDA HAYA. TUTAIKUMBUKA SIKU HII MILELE NA MILELE.

WALIPOACHA BAHARI NA JESHI LILILOKUFA LA MISRI, WATOTO WA KIEBRANIA WALIMFUATA MUSA NA LILE WINGU NYIKANI. WALIENDELEA KULA NA KUNYWA CHAKULA WALICHOTOKA NACHO MISRI.



BAADA YA SAFARI YA SIKU CHACHE, WINGU LILILOKUWA LIKIWAONGOZA LILISIMAMA KARIBU NA KISIMA CHA MAJI. WAEBRANIA WALIPIGA KAMBI HAPO HADI CHAKULA CHAO KIKAKWISHA. HAWAKUWA NA MAHALA PENGINE PA KUPATA CHAKULA. HAPAKUWA NA MATUMAINI.


TUNGEBAKI MISRI NA TUNGEISHI VYEMA KULIKO HIVI. TULIPOKUWA WATUMWA TULIKUWA NA CHAKULA CHA KUTOSHA. HAPA HAMNA CHOCHOTE.
NDIO. ULITULETA HAPA TUFE KWA NJAA?


NISIKILIZENI, HAMNILALAMIKII MIMI BALI MNAMLALAMIKIA MUNGU TUNAYEMFUATA.
YEHOVA ASEMA ATASHUSHA MKATE KUTOKA MBINGUNI. KILA ASUBUHI MTAPATA MKATE ARDHINI. MTAKACHOFANYA NI KUOKOTA NA KULA.


MUSA AMESEMAJEE? TUTAPATAJE CHAKULA? WATOTO WETU WANATESEKA.
ANASEMA KUWA YEHOVA ATASHUSHA MKATE KUTOKA MBINGUNI KILA ASUBUHI.


NI WAKATI JUA LIPAE SASA. UNAAMINI KUTAKUWA NA MKATE ARDHINI KAMA MUSA ALIVYOSEMA?
TUTATESEKA KWA NJAA TUKIKOSA MKATE.
USHAWAHI KUSIKIA MKATE UKIANGUKA KUTOKA MBINGUNI?
LA, ILA SIJAWAHI KUSIKIA KUHUSU NJIA KUFANYIKA KATIKATI YA BAHARI. MUNGU HUYU WA MUSA LAZIMA AWE MUUMBAJI WA ULIMWENGU. SIDHANI NI NGUMU KWAKE KUSHUSHA MKATE KUTOKA MBINGUNI. NJOO, NI WAKATI TWENDE TUKAANGALIE.
KUTOKA 14:21-22, 30, 16:2-3, 7-8


MKATE ULIOTOKA MBINGUNI. KAMA ALIVYOSEMA.
MBONA SISI HUWA NA SHAKA?


*TAZAMA!* IKO KILA MAHALI.
AH, NI TAMU. ***INAONJA*** KAMA ASALI.
KWA KWELI YEHOVA NI MUNGU NA MUSA NI NABII WAKE.


WALIPOKUWA NYIKANI MUNGU ALIWALISHA CHAKULA KILA SIKU NA CHAKULA CHA MALAIKA CHA MBINGUNI.
WINGU LILIPOKUWA JUU YA KAMBI WALIENDELEA KUKAA KANDO YA KISIMA CHA MAJI NA KULA MKATE ULE, LAKINI PINDI WINGU LILIPOANZA KUONDOKA WALIPANGA VIRAGO VYA NA KUANZA KUSAFIRI WAKILIFUTA NYIKANI.


ILA ILIFIKA WAKATI AMBAPO MAJI YALIWAISHIA.
KWA HIYO ALITUPATIA MKATE NA SASA ANATAKA KUTUUA KWA KIU?
MSICHANA WANGU MDOGO ATAAGA ASIPOPATA MAJI YA KUNYWA.




KUTOKA 16:14-15, 17:2-4, ZABURI 78:24-25


MUNGU ALIMWELEZA MUSA CHA KUFANYA.
NJOONI MUONE UWEZO WA YEHOVA. HAMUMUAMINI, MNALALAMIKA TU.


ALIWAPATIA MKATE, NA SASA ANAWAPATIA MAJI KUTOKA KWA JIWE HILI.


WHAAACK!
IEEE!
KUTOKA 17:5-6


MAJI YALITIRIRIKA KAMA YA MTO.


TENA WINGU LILISONGA NA WAEBRANIA WAKAPANGA VIRAGO NA KUANZA SAFARI WAKILIFUATA WINGU NYIKANI KULEKEA KWA MLIMA ULIOULIKANA KAMA SINAI.



HUKO MUSA ALISALI NA MUNGU ALIZUNGUMZA NA YEYE.
WAKUMBUSHE YALE YOTE NILIYOWAFANYIA WANA WA MISRI, NILIVYOWAOKOA, NIKAWALISHA NA KUWANYWESHA KUTOKA KWA JIWE.
KUTOKA 17:6, 19:1-6, 9


WAELEZE IWAPO WATATII AMRI ZANGU NIATAWAFANYA WATU WANGU WA KIPEKEE DUNIANI KOTE. WAKITII AMRI ZANGU NITAWAFANYA UFALME WA MAKUHANI.
MUSA, NIKIZUNGUMZA NANYI NITAKUJA KAMA WINGU NONO ILI WATU WAWEZE KUONA NA KUSIKIA KWAMBA NI MIMI.


MUSA ALITOKA JUU MLIMANI NA AKAWAELEZA WATU YOTE MUNGU ALIYOYASEMA.
TUTATII KILA KITU AMBACHO MUNGU ATASEMA.
BASI NENDENI MKAOGE NA KUFUA NGUO ZENU. MJITAYARISHE KUMUABUDU MUNGU. SIKU TATU KUTOKA LEO MUNGU ATAWATEMBELEA.


KAMA MUNGU ALIVYOAMURU, BAADA YA SIKU TATU WATU WALIKUSANYIKA MLIMANI WAKINGOJA MUNGU AWAZUNGUMZIE. WINGU LISILOKUA LA KAWAIDA LILITUA JUU YA MLIMA ALAFU....
MUSA, NJOO JUU MLIMANI.


MUSA, MIMI NDIYE YEHOVA MUNGU, NILIYEWATOA MISRI. UKIRUDI, WEKA UA KILA MAHALI KUZINGIRA MLIMA HUU.
IWAPO MTU MWINGINE YEYOTE AKIUSHIKA MLIMA HUU ATAKUFA. NITAKUPA AMRI KUMI AMBAZO LAZIMA UWAELEZEE WATU.
KUTOKA 19:7-25



KUTOKA 20:3-17


MUSA ALIPOSHUKA KUTOKA MLIMANI ALIWAKUSANYA VIONGOZI SABINI WA ISRAELI NA KUWAELEZA KUHUSU AMRI ZA MUNGU.
TUTAFANYA HIVYO.
NI AMRI NZURI.
NYINYI WATU SABINI MTARUDI MLIMANI NA MIMI. MTAPATANA NA MUNGU NA MTAJIONEA WENYEWE. LAKINI KWANZA LAZIMA NIANDIKE KWA KITABU AMRI AMBAZO MUNGU ALINIELEZA.

MUSA ALIKUWA MAKINI KUANDIKA AMRI AMBAZO MUNGU ALIMUELEZA. ROHO MTAKATIFU ALIMUONGOZA ASIFANYE MAKOSA YOYOTE.




MUSA ALIPOMALIZA KUANDIKA ALIWAKUSANYA WATU ILI KUWASOMEA MANENO YALE.
YOTE AMBAYO MUNGU AMESEMA NI MEMA. NA TUYAFUATA.
KWA HIVYO TAIFA LA ISRAELI LILIFANYA AGANO NA MUNGU. ANGWABARIKI, AWAPATIE UHAI NA KUWAOKOA KUTOKA KWA MAADUI WAO. WANGEFUATA AMRI ZOTE ZA MUNGU NA KUTEMBEA KWA WEMA.

MUNGU ALIMUUAMURU MUSA ATOE DHABIHU YA DAMU NA AWANYUNYUZIE WATU DAMU.




WOTE WALIKUWA WATENDA DHAMBI, WALIFAA KIFO HATA MUSA NA HARUNI. ILA MUNGU ALIKUWA NA HURUMA. ALIWAPA NJIA YA KUTOROKEA.

KWA KUNYUNYUZIA DAMU YA MWANA KONDOO, MUNGU ANGEWASAMEHE DHAMBI ZAO NA HANGEWAUA KAMA WALIVYOFAA. MWANAKONDOO AMBAYE HANGEFAA KIFO ALIKUFA KWA AJILI YA WENGI WALIOSTAHILI KUFA KWA AJILI YA DHAMBI ZAO.




KWA HIVYO VIONGOZI SABINI WALIKWENDA NA MUSA JUU YA MLIMA AMBAKO MUNGU ALIZUNGUMZA NA MUSA.

GHAFLA, KITI CHA ENZI CHA MUNGU KILITOKEA MBELE YAO.




VIONGOZI SABINI WALIMTAZAMA MUSA AKIENDA JUU YA MLIMA NA KUPOTELEA KATIKA UTUKUFU ULIONG'AA WA MUNGU.
INAPENDEZA SANA!
NA UTUKUFU.
HAKUNA MTU KAMA MUSA ANAYEWEZA KUZUNGUMZA NA MUNGU MOJA KWA MOJA.
KUTOKA 24:9-10


MUSA, UTAWAELEZA WATU WAJENGE HEKALU AMBALO WATAKUWA WAKINIABUDIA. LITAKUWA NA MADHABAHU AMBAKO MTATOLEA SADAKA. NA MAHALI PATAKATIFU AMBAKO NAWEZA KUKUTANA NA KUHANI MKUU MARA MOJA KWA MWAKA KATIKA VIZAZI VYAO VYOTE.
NITAKUELEZA JINSI LILATATAKAVYOJENGWA. KABILA LA LEVI WATAKUWA MAKUHANI WANGU. HARUNI, PAMOJA NA WANAWE WATAKUWA MAKUHANI WANGU. WATAWAFUNZA WATU KUWA WATAKATIFU NA WATAWATOLEA WATU SADAKA WATAKAPOTENDA DHAMBI.


IMEKUWA NI WIKI KADHAA TANGU APOTELEE KATIKA MWANGAZA HUO. LAZIMA AWE AMEKUFA.
NDIO. HATUWEZI KUISHI NYIKANI MILELE.
TUNAHITAJI MUNGU WA KUTUONGOZA KAMA MUSA ALIVYOFANYA.
TUTENGENEZENI PICHA YA MUNGU WA DHAHABU.


MUSA AMEKUFA. HARUNI ATATUTENGENEZEA MUNGU WA DHAHABU AMBAYE ATATURUDISHA MISRI.
TUPATIENI DHAHABU YENU.


KWA KUTUMIA MIKONO YAO WAJINGA WALE WALITENGENEZA FAHALI WA DHAHABU NA KUIITA MUNGU. SURA YA SHETANI KABLA YAKE KUTENDA DHAMBI ILIKUWA NI FAHALI, ILA WATU HAWAKULIJUA HILO.
HARUNI ALIFUATA KAMA WATU WALIVYOTAKA NA KUWASAIDIA KUJENGA FAHALI YULE.
KUTOKA 20:4, 25:8-9, 28:1-3, 32:1-4, EEKIELI1:10, 10:14,28:14

HARUNI ALIKUWA MPUMBAVU SANA. ALIJUA KUWA FAHALI HAIKUA MUNGU LAKINI ALIOGOPA KUWAAMBIA WATU.




WATU WALICHEZA NA KUWA UCHI. WALILEWA NA KUTENDA DHAMBI NYINGI. MUNGU ALIKUWA TAYARI KUWAANGAMIZA NA KUWATUPA KWENYE MOTO ULIOTAYARISHIWA SHETANI NA MALAIKA WAKE.
MUNGU ALIZUNGUMZA NA MUSA NA KUMWAMBIA, "NENDA CHINI SASA. WATU WAMETENDA DHAMBI KUBWA. WAMEJIFANYA UCHI NA KUCHEZA MBELE YA SANAMU. INAFAA NIWAANGAMIZE. MIOYO YAO NI MIGUMU HAWATEMBEI KWA HAKI."
KUTOKA 32:5-10


MUSA ALIKASIRIKA ALIPOONA KWAMBA WATU WALITENGENEZA SANAMU NA KUMSAHAU MUNGU.
MUMEVUNJA AMRI ZA MUNGU.


MUSA ALIVUNJA JIWE ALILOKUWA AMEANDIKIA AMRI ZA MUNGU.




KUTOKA 20:3-4, 32:15-20


IWAPO UKO UPANDE WA YEHOVA BASI KUJA HUKU USIMAME NAMI. IWAPO UTAABUDU MIUNGU YA MISRI BASI KAAENI MLIKO.
NI HERI NIMFUATE MUNGU AWEZAYE KUGAWANYISHA BAHARI YA SHAMU HATA KAMA HANA PICHA.
TUTAMFUATA MUNGU WA IBRAHIMU, ISAKA NA YAKOBO.


MSHAHARA WA DHAMBI NI MAUTI. ***YEHOVA*** ASEMA NI LAZIMA WAFE. BASI CHUKUENI PANGA ZENU NA MUWAANGAMIZE WALE WANAOABUDU SANAMU.


WATENDA DHAMBI 3,000 WALIUAWA SIKU HIYO.
KSSHHH!
LAAA!
HURUMIA!
KUTOKA 32:26-28

MUSA ALIKWENDA TENA MLIMANI NA KWA MARA NYINGINE MUNGU ALIANDIKA AMRI ZAKE KATIKA MAWE MAWILI NA KUMKABIDHI MUSA. MUSA ALIPOREJEA ALIWAONYESHA WATU AMRI NA WAKAKUBALI KUZIFUATA.




MUNGU ANASEMA NYINYI NI WATU WENYE ROHO NGUMU. MLIPOTENDA DHAMBI ALISEMA MTAKUFA NYOTE ILA NILIWAOMBEA NYOTE NA ATASAHAU DHAMBI ZENU. KWA KWELI YEHOVA NI MWENYE HURUMA NA MSAMAHA.


MUNGU AMEPEANA MWELEKEO WA KUJENGA MASKANI. TUKILIJENGA KULINGANA NA ANAVYOTAKA, ATAPATANA NASI HUKO. KWA KUWA SOTE NI WATENDA DHAMBI, MUNGU AMETENGENEZA NJIA AMBAYO TUNAWEZA KUMFIKIA.
WANA WA LEVI WATATOA SADAKA YA DAMU KILA SIKU. MARA MOJA KILA MWAKA DAMU ITAPAKWA KWENYE SADUKU LA AGANO. MUNGU ATAKAPOONA DAMU HIYO ATAFUTILIA DHAMBI ZETU, NA HATUTAKUFA. NI NJIA YA MUNGU YA MSAMAHA.


NA KWA HIVYO HEKALU LILIJENGWA KAMA WALIVYO AMURIWA NA KILA KITU KILITENDEKA KAMA WALIVYOAMBIWA.
LAKINI WATU HAWAKUFURAHISHWA NA KUISHI KWA NYIKANI HIVYO WALILALAMIKA KILA WAKATI.
ILIKUJA SIKU AMBAYO MALALAMIKO YAO ILIMFANYA MUNGU KUWAADHIBU.




KUTOKA 34:28-32, 39:32, NAMBARI 21:5-6


KAMBI LILIKUA LIMEJAA NYOKA WENYE SUMU.


MUNGU TUSAIDIE!


NYOKA WALIWAPATA HADI KWA HEMA ZAO USIKU WALIPOKUA WAMELALA.
HISSSSS


NISAIDIE. NIMEUMWA.


LAAAA!




HATA WATOTO WALITESEKA KWA DHAMBI ZA WAZAZI WAO.

HESABU 21: 6


KILA MAHALI KWEYE KAMBI VILIO VYA WATU VILISIKIKA. GADHABU YA DHAMBI NI KUBWA.
KILA MAHALI KAMBINI KUKO HIVI. TAYARI WENGI WAMEKUFA.
LAZIMA TUMTAFUTE MUSA. KWA KWELI HII NI KAZI YA MUNGU. AMEKASIRISHWA NA DHAMBI WANAZOTENDA WATU.
WHAACK!


LAZIMA UUNGUMZE NA MUNGU. *TUNASTAHILI* GADHABU HII ILA MSIHI ATUHURUMIE.
WATU WATAJUA LINI KUWA MUNGU HAPENDI *DHAMBI? LA*ZIMA WATII AMRI ZAKE NA WAKUWE TAIFA TAKATIFU.


EH MUNGU. TAFDHALI WAHURUMIE WATU WAKO NA UWASAMEHE DHAMBI ZAO.
NENDA. TENGENEZA JOKA LA SHABA KAMA ZILE ZINAZOWAUMA WATU KISHA UWEKE KATIKA KIKINGI ILI WATU WAONE. WAAMBIE WATAZAME NYOKA YA SHABA NA WATAPONA.

HESABU 21: 7


MUNGU AMETENGENEZA NJIA. TAZAMENI NYOKA YA SHABA NANYI MTAPONYWA.


ATAKUFA.
LA! MUNGU AMETENGENEZA NJIA. FUNGUA MACHO YAKO NA UTAZAME. TAZAMA NA UISHI!


NI MUUJIZA!
LAZIMA TUWAELEZE WENGINE.
IMEFANYA KAZI KWANGU HIVYO ITAFANYA KWA WENGINE.


TAZAMA NA UISHI.
HESABU 21: 9


MBONA UNAMTANIA NA TUMAINI LA UONGO?
WENGINE WAMETAZAMA NA WAMEKUWA WAZIMA.
HUONI MIMI NAAGA? MBONA UNANISUMBUA NA UJINGA KAMA HUO?


AMEKUFA.
POLE HAKUAMINI.
ALIKUWA NA KIBURI SANA.


KWA MARA NYINGINE WATU WALIUONA UWEZO WA MUNGU. KAMBI LILIONDOKA KWENYE MAJOKA NA MAISHA YAKARUDI KAMA KAWAIDA.
LAKINI WATU WALIENDELEA KUFUATA NJIA ZAO, NA KUKOSA KUFUATA AMRI ZA MUNGU.




HESABU 21:9, 32:13


MUSA, UNAFIKIRI NI WEWE TU ULIYE KARIBU NA MUNGU? SISI PIA NI WATAKATIFU KAMA WEWE NA MUNGU ANAISHI KATI YETU. HATUKUHITAJI WALA HARUNI KUTUAMURU. TUNAWEZA KUWAAMURU NYINYI PIA.
NDIO, NIMECHOKA KUZURURA HUKU KOTE NYIKANI NA MUNGU KUTUUA KWA SABABU NDOGO NDOGO.
NDIO, HAYA NI MAKOSA YA MUSA.



MUSA ALIKWENDA KWENYE MASKANI NA KUMUULIZA MUNGU ALILOHITAJI KUFANYA.


MUNGU AMEZUNGUMZA, "MNACHUKUA JUKUMA ***JUU YENYU NYINYI*** WANA WA LEVI. MNAWAFANYA WATU MAKUHANI KABLA YA MUNGU KUWACHAGUA."
KESHO MUNGU ATATOA HUKUMU NA TUTAWEZA KUBAINI NANI KUHANI KATI YETU. MJE HEKALUNI KESHO ASUBUHI.
NAMBARI 16:2-6


SIKU ILIYOFUATA.
KARIBIENI, NYINYI **MNAOTANGAZA** UTAKATIFU WENU, NYINYI AMBAO MNGEKUWA MAKUHANI NA KUWAONGOZA WENZENU.


MUNGU ATAKUTANA NASI LEO HAPA NAYE ATACHAGUA. TUTAONA NGUVU ZAKE NA UTUKUFU.


JITENGENI NA WATU HAWA WAOVU KWA DAKIKA MOJA NITAWAANGAMIZA.


ONDOKENI KATIKA HEMA ZAO. MSIWAKARIBIE AMA NYINYI PIA MTAKUFA NAO.
HESABU 16:19-24


HAPA KUNA JARIBIO: WATU HAWA WAKIFA KIFO CHA KAWAIDA MTAJUA MIMI NI NABII WA UONGO NA MUNGU HAZUNGUMZI NAMI.
LAKINI IWAPO LEO MTAONA JAMBO JIPYA LIKITENDEKA, DUNIA IKIFUNGUKA NA IWAMEZE PAMOJA NA VITU VYAO HADI JEHANAMU, MTAFAHAMU KUWA WALITENDA DHAMBI DHIDI YA MUNGU NA KUWA MIMI NI NABII WAKE.


SAIDIA!
YIEEE!
LAAAA!

HESABU 16:28-33



WATU WOTE WALIOJIFANYA MAKUHANI
WALIMEZWA MZIMA MZIMA HADI
KWENYE MOTO WA JEHANAMU.


CHUKUA VYOMBO VYAO VYA SHABA NA UVITUMIE KUTENGENEZA KIFUNIKO CHA MADHABAHU.
MTAKAPO ONA SHABA IKIFUNIKA MADHABAHU MTAKUMBUKA SIKU HII, AMBAYO WATU WALIASI AMRI ZA MUNGU NA WAKATAKA KUJIFANYA MAKUHANI WENYEWE.
HIO ILIKUA NI SIKU AMBAYO WANA WA ISARAELI HAWANGEWAI SAHAU. MUNGU ALIDHIBITISHA KUWA MUSA ALIKUWA NABII WAKE, NA WALE TU AMBAO ANGEWACHAGUA NDIO WANGEKUWA MAKUHANI WAKE.


UTUKUFU WA MUNGU SIKU ZOTE ULISIMAMA JUU YA MASKANI NA WATU WALIMFUATA MUSA NYIKANI KWA MIAKA 40 KWA HIARI YAO.
UTUKUFU WA MUNGU UPO NASI NAYE HUTUPATIA MKATE KUTOKA MBINGUNI.
MUNGU ALIENDELEA KULETA MKATE TOKA JUU MBINGUNI, NA ALIWAPA MAJI KUTOKA KWA MWAMBA. ILE NGUZO YA MOTO ILIWAFUNIKA USIKU NA WINGU MCHANA. WAKATULIA NA WAKAJIFUNZA KUFUATA AMRI ZA MUNGU.
HESABU 16:37-38



MAKUHANI WALISHUGHULIKIA HEKALU NA WALITOA SADAKA KILA SIKU KAMA MUSA ALIVYOAMURU.


BAADA YA MIAKA 40 NYIKANI, KILA MTU ALIPOKUWA AKIJITAYARISHA KUINGIA KWENYE ARDHI ILIYOAHIDIWA, MUNGU ALIMUITA MUSA MLIMANI. HUKO BAADA YA KUZUNGUMZA NA MUNGU KWA MARA YA MWISHO, ALILALA CHINI KWA UPOLE NA KUAGA DUNIA.


GHAFLA, ROHO YAKE ILIELEKEZWA KWENYE UWEPO WA MUNGU. HAPO, ANGEKAA HADI MWISHO WA NYAKATI AMBAPO ANGEUNGANIKA TENA NA WATU WAKE KWENYE NCHI AMBAYO MUNGU ALIAHIDI IBRAHIMU.
TAKRIBAN MIAKA 1451 KABLA YA KRISTO - KUMBUKUMBU LA TORATI 34:4-5



KARIBU MIAKA 500 ILIPITA BAADA YA IBRAHIMU KUELEZWA NA MUNGU AWACHE WATU WAKE NA KUENDA AMBAKO MUNGU ANGEMUELEKEZA.
AHADI YA MUNGU KWA IBRAHIMU NA SARA YA KUWAPA TAIFA KUBWA KUPITIA KWA MWANAO ISAKA ILITIMIA. WATOTO 12 WA YAKOBO, AMBAYE JINA LAKE LILIBADILISHWA NA KUWA ISRAELI, WALIKUWA NI KABILA 12 YA WATU.


WALITOKA UTUMWANI, WAKAZURUZA JANGWANI, WAKAPOKEA AMRI ZA MUNGU NA SASA HATIMAYE WALIKUWA WANAINGIA KWENYE NCHI WALILOAHIDIWA. ***WALIPOKUWA*** NYIKANI KULIKUWA NA KIJANA MMOJA MDOGO AMBAYE ALITEMBEA KANDO YA MUSA AKIJUFUNZA JINSI YA KUONGOZA TAIFA LA ISRAELI.


KIJANA HUYO ALIKUWA MKUBWA NA ALIITWA YOSHUA.


BAADA YA MUSA KUFA, YOSHUA ALICHAGULIWA NA MUNGU ILI KUONGOZA WATU KWENYE NCHI ILIYOAHIDIWA IBRAHIMU.
WATU WALIKUMBUKA UNABII KWAMBA WANGEKUWA WATUMWA KATIKA NCHI YA UGENI NA KWAMBA BAADA YA MIAKA 400 WANGERUDI KWENYE CHI YA BABA ZAO. MUNGU ALITIMIZA HUO UNABII.


SIKU HIYO WALIVUKA MTO YORODANI, CHAKULA TOKA MBINGUNI KIKAISHA NA WAKALA CHAKULA KUTOKA KWENYE NCHI HIYO.
EEEH MUME WANGU. HUKU NI ***KUZURI AMBAKO*** MUNGU AMETULETA SISI.
KUMBUKUMBU LA TORATI 34:9, YOSHUA 5:12
NDIO. NI MAHALI PAZURI PA KUWALELEA WATOTO WETU KWA UNYENYEKEVU NA AMANI.



## SURA YA 5

# UFALME




WATU WALIOISHI PALESTINI, NCHI AMBAYO WANA WA ISRAELI WALIKUWA WAMEKUJA, WALIKUWA WAOVU. WALIITWA WAKANAANI NA WALIKUWA WA LUGHA TOFAUTI NA WAISRAELI. WALITOA DHABIHU ZA KIBINADAMU NA KUABUDU MIUNGU ILIYOTENGENEZWA KWA DHAHABU, FEDHA, SHABA NA MBAO.




MWANZO 14:18, 20:7: HESABU 22:4-8: KUMBUKUMBU LA TORATI 18: 9-11



WATU WALIO ABUDU SANAMU WALIOISHI KATIKA NCHI YA AHADI WALIPINGA UWEPO WA WANA WA ISRAELI NA WALIPIGANA KUITUNZA NCHI YAO, LAKINI MUNGU ALIWAPA WANA WA ISRAELI UWEZO WA KUWASHINDA


MNAWEZAJE KUDHUBUTU KUJA KATIKA HEKALU HILI TAKATIFU!
UMEMUUA MTOTO WAKO WA MWISHO


WAKATI VITA VYA UMWAGAJI DAMU VILIPOMALIZIKA HATIMAYE, WAEBRANIA WALIKUWA WAMEWASHINDA MAADUI ZAO, NA NCHI KUWEKWA MBELE YAO ILI KUICHUKUA. YOSHUA ALIHUTUBIA WATU
IBRAHIMU, MMOJA WA MABABU **ZETU,** ALIKUJA KUTOKA KWA WATU WALIO ABUDU MASANAMU. MUNGU ALIONGEA NAYE NA KUMUAHIDI KUMFANYA KUWA BABA WA TAIFA KUBWA




YOSHUA 24:2-14


KATIKA NCHI MPYA WALIKUWA NA AMANI. KILA MTU ALIMILIKI SHAMBA LAKE MWENYEWE NA KULIKUWA NA VINGI VYA KUKULA. MUNGU ALIWABARIKI JUU YA WATU WOTE.
CHAKULA CHAKO CHA JIONI KIPO TAYARI.
PINDI TUTAKAPOLITOA JIWE HILI



KAMA VILE MUNGU ALIVYOAHIDI, WAEBRANIA WALIONGEZEKA MPAKA WAO WAKAIJAZA NCHI. MIJI YAO ILIJAWA NA NIA NJEMA NA HAKI.TAIFA JIPYA LILIITWA ISRAELI.
*AMANI* IWE NAWE DADANGU. SAMAKI IKO VIPI LEO?
NI SAFI KUTOKA BAHARINI KAMA KAWAIDA.


YEHOVA AMEWASHINDA MAADUI WENU, LAKINI BADO KUNA IBADA YA SANAMU KATIKA NCHI HII. LEO HII MCHAGUE MTAKAYETUMIKIA! KAMA NI MIUNGU YA UONGO YA WATU HAWA, WANAOISHI NCHINI HUMU, AU MUNGU WA IBRAHIMU. KWANGU MIMI NA NYUMBA YANGU, TUTAMTUMIKIA BWANA.
NA ISHINDWE KWAMBA TUTAACHA KUMTUMIKIA BWANA KWA KUTUMIKIA MIUNGU MINGINE; KWA SABABU KATIKA NGUVU ZA YEHOVA ALITUOKOA KUTOKA UTUMWA WETU HUKO MISRI NA KUTUTUNZA NYIKANI.
TUNAAHIDI KUMTUMIKIA BWANA.


BWANA ALIWAONDOA WATU WOTE, HATA WAAMORI AMBAO WALIISHI KATIKA NCHI HII. KWA HIYO, TUNAMTUMIKIA BWANA; KWA MAANA YEYE NI MUNGU WETU.
MUNGU NI MUNGU MTAKATIFU; YEYE NI MUNGU MWENYE WIVU; NA MKIMGEUKA NA KUFUATA SANAMU, ATAWAGEUKA NA KUWAADHIBU.


MMEKUA MASHAHIDI KATI YENU, KWAMBA MMECHAGUA KUMTUKMIKIA BWANA.
SISI NI MASHAHIDI
NITAANDIKA KATIKA KITABU AGANO MLILOFANYA NA MUNGU LEO
TULIVYOMTII MUSA KATIKA YOTE NA SISI TUTAKUTII. BWANA, MUNGU WAKO, AWE PAMOJA NAWE, KAMA ALIVYOKUWA PAMOJA NA MUSA. NA ATAKAYE MUASI MWENYEZI MUNGU KATIKA AMRI ZAKE ATAUWAWA.


WATU WALITAWALIWA NA MAKUHANI AMBAO WALIONGEA NA MUNGU NA KUSOMA MANENO YA MUSA. WALIELEZA SHERIA YA MUNGU KWA WATU NA KUWAONGOZA KUMTII MUNGU.
JE, SHERIA YA MUNGU INASEMAJE KUHUSU FAHALI ILIYOMKWAZA MTU?
MUSA ALISEMA MMILIKI ATAWAJIBIKA KWA UHARIBIFU NA FAHALI ANAPASWA KUULIWA.
KUTOKA 21:28-29; YOSHUA 24:15-24


KWA MUDA MFUPI, WATU WALIKUMBUKA MIUJIZA AMBAYO MUNGU ALIFANYA CHINI YA MUSA NA YOSHUA. WALIKUWA NA SHUKRANI KWA HURU YA UTUMWA WA MISRI. WAO WALIMTUMIKIA YEHOVA MUNGU NA KUTOA DHABIHU KAMA WALIVYOAMRIWA.
BABA, KWA NINI MAKUHANI WANATAKA KUMUUA KONDOO ***WETU?*** JE MHARIBIFU ATAPITIA KAMA ALIVYOFANYA WAKATI BABA ZETU WALIKUWA MISRI?
LA MWANANGU, MHARIBIFU HATAKUJA, LAKINI DAMU YA MWANAKONDOO HUYU ITAFUNIKA DHAMBI ZETU NA KUTUFANYA KUKUBALIKA MBELE YA MUNGU


WATU WALIMWAHIDI YOSHUA KWAMBA WATAMUABUDU MUNGU NA KUZISHIKA AMRI ZAKE, LAKINI SIO KILA MTU ALIENDELEA KUMWABUDU YEHOVA.
NA MIUJIZA ILIPOISHA, KIZAZI KIJACHO KILIMSAHAU MUNGU ALIYE HAI NA KUABUDU PICHA ZISIZO NA UHAI. PIA WALIWAABUDU MABABU ZAO.


KAMA VILE YOSHUA ALIVYOONYA, MUNGU ALITUMA MATAIFA YALIYO ABUDU SANAMU KUWAANGAMIZA ISRAELI.
NIOKOE EEH BAALI!
NDIIOOO!
WAAMUZI 3:7-8, 12-13, 4: 1-2, 10: 6-7



WAKATI HUKUMU ILIWAPATA WATU WA MUNGU, WALIKUMBUKA SHERIA YAKE NA WALIKIRI DHAMBI ZAO.
EE YEHOVA, *TUSAMEHE* DHAMBI ZETU NA UIREJESHE AMANI YETU.
WALIPO KIRI DHAMBI ZAO, WALISAMEHEWA, NA KUREJESHEWA ARDHI YAO.


WATU WALIKUWA WAMECHOKA KUWAFUATA WAAMUZI AMBAO WALIWAELEKEZA NJE YA KITABU CHA MUNGU, HIVYO WAKAAMUA KUTAFUTA MFALME WA KUWATAWALA.
ARDHI ZENU ZITACHUKULIWA KWA AJILI YA MEMA YA UFALME. UNAWEZA ACHA BINTI YAKO HAPA. TUTAMTUNZA VYEMA.


NABII NA HAKIMU AITWAYE SAMWELI ALIWAONYA KWAMBA KATIKA KUTEUA MFALME WALIKUWA WAKIMKATAA MUNGU KAMA MTAWALA WAO, LAKINI HAWAKUTAKA KUTEMBEA KWA IMANI. MFALME SAULI ALIWANYANYASA, AKACHUKUA FEDHA ZAO, MALI, KUWAFANYA WAVULANA WAO WATUMISHI NA KUWANYANYASA MABINTI ZAO.


WAKATI MFALME SAULI ALIZEEKA, ALIINGIWA NA MAPEPO NA KUJAWA NA HASIRA ISIYOWEZA KUDHIBITIWA.
SIKU MOJA ALIJARIBU KUMUUA KIJANA MDOGO ALIYEITWA DAUDI, AMBAYE ALIKUWA AKIMCHEZEA MZIKI.
1 SAMWELI 8
SAULI ALITENDA DHAMBI ZAIDI NA ZAIDI. ALIKUWA NA WIVU KWA KILA MTU NA MWENYE HOFU. PEPO WALIAHIDI KUMPA NGUVU NA MALI, ILA WALILETA TAABU NA MATESO YA NAFSI.


SAULI ALIACHA MUNGU ALIYE HAI NA KUFUATA USHAURI WA WACHAWI.
NINAONA GIZA. SIO PAZURI. WEWE UTAKUFA KATIKA VITA NA MWINGINE ATACHUKUA MAHALI PAKO.
SAULI ALIKUFA KATIKA VITA NA NAFSI YAKE IKATUPWA KUZIMU.


MUNGU ALIMCHAGUA KIJANA MDOGO KUCHUKUA NAFASI YA SAULI KAMA MFALME. ALIKUWA MVULANA MCHUNGAJI ALIYEMPENDA MUNGU NA KUWEKA AMRI ZAKE; KIJANA AMBAYE SAULI ALIKUWA AMEJARIBU KUUA.
BWANA NI MCHUNGAJI WANGU. SITAPUNGUKIWA KITU. HUNILAZA KWENYE MAJANI MABICHI NA KURIDHISHA NAFSI YANGU
DAUDI ALIKUWA MWENYE HAKI NA MPENDWA WA MUNGU. ANGEWEZA KUWA YULE WA KUWAOKOA WANADAMU KUTOKANA NA DHAMBI NA KIFO? INGEKUWA NI DAUDI ALIYEAHIDIWA?
1 SAMWELI 18:10-11, 31:4, 16:1-13; ZABURI 23:1-3



DAUDI ALIANDIKA: AMEBARIKIWA MTU ASIYEMWASI MUNGU NA ASIYESIMAMA KATIKA NJIA YA WAKOSEFU, WALA KUKAA KATIKA KITI CHA DHARAU. LAKINI FURAHA YAKE IKO KATIKA SHERIA YA BWANA; NA KATIKA SHERIA YAKE ATATAFAKARI MCHANA NA USIKU.


ATAKUA KAMA MTI KANDO YA MTO KWANI HATANYAUKA. ATAFANIKIWA KWA KILA ATAKACHOFANYA.
WAOVU WATAANGAMIA KWA MAANA BWANA ANAJUA NJIA YA WENYE HAKI, NA WAOVU WATAANGAMIA.


WAKATI SAULI ALIPOKUFA, DAUDI AKAWA MFALME WA ISRAELI NA KUWAONGOZA WATU KWA KUMWABUDU MUNGU NA KUSHIKA AMRI ZAKE.
MREJESHEE MWANAMKE HUYU ARDHI YAE, NA ASITOZWE USHURU ZAIDI.
2 SAMWELI 2:4; ZABURI 1; MATENDO YA MT.13:22-23
CHINI YA UTAWALA WA DAUDI TAIFA LILIFANIKIWA NA WALIISHI VYEMA


MUNGU ALIONGEA NA DAUDI NA KUMFUNULIA MAMBO MENGI KUHUSU SIKU ZIJAZO. DAUDI ALIANDIKA UNABII HUO KATIKA KITABU CHA ZABURI. MENGI TAYARI YASHATIMIA.
ATAWAHUKUMU WATU KWA HAKI. ATAWAOKOA WATOTO WA MASKINI, NA KUVUNJA VIPANDE VIPANDE MKANDAMIZAJI. SIKU ZAKE WACHAMUNGU WATAISHI KWA AMANI TELE, NA ATATAWALA DUNIA NZIMA.


WAFALME WOTE NA MATAIFA YOTE YATAMUINAMIA, ATAOKOA NAFSI ZAO NA ATAISHI MILELE. MAOMBI PIA YATAFANYWA KWA AJILI YAKE DAIMA; NA KILA SIKU ATAPEWA SIFA. JINA LAKE LITATUKUZWA MILELE. WATU WATABARIKIWA NDANI YAKE: MATAIFA YOTE YATAMWITA HERI. (ZABURI 72)
DAUDI ALIKUWA MTU MWEMA, LAKINI ALIFANYA DHAMBI, HIVYO HAKUWEZA KUWA MKOMBOZI AILYEAHIDIWA ALIANDIKA HAYA YA MKOMBOZI ANAYEKUJA:


MUNGU AKAMWAMBIA DAUDI: BAADA YAKO KUFA, NITAANZISHA UFALME WAKO CHINI YA MWANAO. ATAJENGA HEKALU AMBAKO NITAABUDIWA, NAMI NITAIMARISHA UFALME WAKE MILELE.
BAADA YA DAUDI KUFA, SULEMANI MWANAWE AKAWA MFALME (971 B.C). KULINGANA NA MAELEKEZO AMBAYO MUNGU ALIMPA DAUDI, SULEMANI ALIJENGA HEKALU (966 B.C) AMBAYO ILICHUKUA NAFASI YA HEMA WALIYOKUWA WAKIITUMIA NYIKANI.


WATU WA ISRAELI WALIFANIKIWA KULIKO HAPO AWALI. HAKIKA MWENYEZI MUNGU ALITIMIZA AHADI YAKE YA KUWALETA KATIKA NCHI NA KUWABARIKI HUKO.
2 SAMWELI 7:12-16; ZABURI 72:1-20
LAKINI KULIKUWA NA AHADI MOJA MUNGU ALIKUWA BADO HAJATIMIZA-KUJA KWA MWOKOZI AMBAYE ANGEHARIBU KAZI YA IBILISI. WATU WALIENDELEA KUTENDA DHAMBI. LAKINI WALIKUWA WAKISHUKURU KWAMBA MUNGU ALIWAPA NJIA YA KUFUNIKA DHAMBI ZAO MPAKA WAKATI MWOKOZI ANGETEULIWA, NA KUONDOA DHAMBI MILELE.

WATU WALIKUJA HEKALUNI KUSIKIA MAFUNZO KUTOKA KWA MAANDIKO MATAKATIFU. HASA WALIFURAHIA UNABII WA MWOKOZI ANAYEKUJA.




DAUDI ALIANDIKA MAMBO MENGI KUHUSU MKOMBOZI BWANA AMWAMBIA BWANA WANGU:


"KETI MKONO WANGU WA KUUME, MPAKA NITAKAPOWAFANYA ADUI ZAKO KUWA MAHALI PA KUWEKA MIGUU YAKO."

(ZABURI 110:1)

EE MUNGU, KITI CHAKO CHA ENZI KITADUMU MILELE NA MILELE, FIMBO YA UTAWALA WA HAKI ITAKUWA FIMBO YA UTAWALA WA UFALME WAKO. UNAIPENDA HAKI NA KUCHUKIA UOVU; KWA HIYO MUNGU, MUNGU WAKO, AMEKUWEKA JUU YA WENZAKO, KWA KUKUPAKA MAFUTA YA FURAHA.

(ZABURI 45: 6-7)

# UNABII ZAIDI WA MWOKOZI ANAYEKUJA:




DAUDI ALIANDIKA ***JAMBO GENI*** KUHUSU MASIYA ANAYEKUJA:

NIMEMWAGIKA KAMA MAJI, MIFUPA YANGU YOTE IMETEGUKA, MOYO WANGU UMEKUWA KAMA NTA, NA KUYEYUKA NDANI YA MTIMA WANGU. NGUVU ZANGU ZIMEKAUKA KAMA GAE, ULIMI WANGU WAAMBATANA NA TAYA ZANGU; UNANIWEKA KATIKA MAVUMBI YA MAUTI KWA MAANA MBWA WAMENIZUNGUKA; KUSANYIKO LA WAOVU WAMENISONGA; WAMENIZUA MIKONO NA MIGUU. ***NAWEZA KUIHESABU MIFUPA YANGU YOTE;*** WAO WANANITAZAMA NA KUNIKODOLEA MACHO. WANAGAWANYA NGUO ZANGU, NA VAZI LANGU WANALIPIGIA KURA. (ZABURI 22:14-18)


SULEMANI ALIKUWA NA UTAWALA MREFU NA WENYE MAFANIKIO, LAKINI BAADA YA KUFARIKI NUSU YA KASKAZINI YA UFALME ILIVUNJIKA NA KUMFANYA MTU MWOVU ALIYEITWA YEROBOAMU MFALME WAO (975 B.C.).
HUYU NDIYE MWENYEZI MUNGU ALIYE WALETA KUTOKA MISRI, NA HAWA NI MAKUHANI WAKE.
LAKINI JE, VIPI KUHUSU SHERIA YA MUSA NA HEKALU LA MUNGU ALILOLIANZISHAYERUSALEMU?
1 WAFALME 12:20, 28-29; ZABURI 2:7,12, 22:6, 14-18, 40:8, 45: 6-7, 78:2, 89:27, 110:1, 4, 132:11; MATHAYO 13:34-35


UFALME WA KASKAZINI ULIKUWA MBALI NA HEKALU LA YERUSALEMU, KWA HIVYO WAKAJIJENGEA WENYEWE MAHALA PA IBADA, KAMILI NA SANAMU KATIKA MFANO WA NDAMA WA DHAHABU.
KUNA JINA NYINGI ZA MUNGU. BAADHI YA WATU WANAMWITA YEHOVA, WENGINE WANAMUITA CHEMOSH, LAKINI TUNAMWITA BAALI.
LAKINI VIPI KUHUSU MAANDIKO MATAKATIFU MUNGU ALIYOWAPA MANABII WAKE? INATUAMURU SISI TUSIWE NA MUNGU MWINGINE. INASEMA KUNA MUNGU MMOJA TU NA NJIA NI MOJA KWAKE.


WADHANI FIKIRA ZA MUNGU NI NDOGO?
*SITASKIZA ZAIDI YA HAYA!* IBADA YA BAALI SASA NI DINI RASMI YA NCHI. MAKAFIRI WATAUWAWA!


WAKATI MAKUHANI WALIPOCHAGUA NG'OMBE KAMA SANAMU YA KUABUDU, BILA KUJUA WALICHAGUA SURA YA LUSIFA, KERUBI WA DHAMBI. WAO WALIKUWA WAKIMWABUDU IBILISI, NA ALIFURAHISHWA; KWANI ALIKUWA AKIGEUZA WATU MBALI NA AHADI YA MUNGU KUHUSU MKOMBOZI ANAYEKUJA.
EWE BAALI! POKEA HII DHABIHU KUTOKA KWA MIKONO YETU.
UMEBARIKIWA SANA WEWE, MALKIA WA MBINGUNI, MAMA YA MUNGU. SIKIA MAOMBI YETU NA UTUSAMEHE DHAMBI ZETU.


UNAFANYA NINI HAPA KWENYE ARDHI TAKATIFU?
KWA JINA LA YEHOVA, SIKILIZENI NENO LAKE. MTOTO ATAZALIWA YA UZAO WA DAUDI. MKOMBOZI ATATOKA KWA UKOO WAKE DAUDI. JINA LAKE LITAKUWA YOSIA, NA KATIKA MADHABAHU HAYA ATAWAANGAMIZA MAKUHANI WA BAALI.
1 WAFALME 12:28, 13:1-2; YEREMIA 44:17-25; EZEKIELI 1:10, 10:14, 28:14


UNAWEZAJE KUSEMA KITU KAMA HICHO? HAKUNA AWEZAYE KUELEZA SIKU ZA USONI ILA MIUNGU.
KWA NENO LA BWANA, MIFUPA YA MAKUHANI HAWA WA BAALI ITAANGAMIZWA HAPA KWA ALTARI NA YOSIAH


MUNGU ATAKUPA ISHARA KWAMBA NINAONGEA NAYE. SIKU HIYO MADHABAHU HAYA AMBAYO MMEJENGA KUABUDU SANAMU ITAGAWANYIKA NA MAJIVU YAKE YATAMWAGIKA


HA HA HA! SIKILIZENI MCHAMUNGU HUYU SHAYIRI. ANAFIKIRI YEYE NI SAHIHI NA KILA MTU SI SAHIHI!
MSHIKENI! MUUENI! ANAWEZAJE THUBUTU KUONGEA VIBAYA KUHUSU DINI YA WENGINE?


MKONO WANGU UMEKAUSHWA! YEHOVA AMENIADHIBU. OMBA KWAMBA ANIPONYE.


BWANA MUNGU, FANYA UJULIKANE LEO NA UMPONYE MFALME MKONO WAKE




1 WAFALME 13:2-6



ÄJALI!
BOOOM
EIII!
LA!
YEHOVA HIVI MUDA SI MUDA?



HAKIKA WEWE NI MTU WA MUNGU! HAKUNA NABII WA BAALI ALIYEWAHI KUFANYA KITU KAMA HICHO. NJOO NAMI. TUTAJIBURUDISHA NA NTAKUPA ZAWADI KWA HUDUMA YAKO LEO.
HAPANA, SIWEZI KWENDA NA WEWE. MUNGU ALINIAMRISHA NISILE WALA KUNYWA HUMU ISRAELI.


AMENIANGAMIZIA DINI. HAKUNA KILICHOBAKI.
LAKINI ULISEMAMIFUPA YA MAKUHANI INGETEKETEZWA KWENYE MADHABAHU. MADHABAHU IMETOWEKA NA HAKUNA *MTU ALIYEKUFA*.
HAYO YALIKUWA MANENO YA MUNGU, WALA SI YANGU.
1 WAFALME 13:5, 7–9

HIVYO KAMA MUNGU ALIVYOAMURU, NABII WA MUNGU ALIRUDI KWA NJIA TOFAUTI. ALIKUWA BILA CHAKULA AU MAJI KWA SIKU MBILI NA ALIKUWA NA KIU KALI NA NJAA. VIJANA WAWILI,WALIO ABUDU NDAMA WA DHAHABU SIKU HIYO, WALIMFUATA ILI KUONA NI NJIA GANI ANGEENDA.




BABA NISINGEAMINI IWAPO SINGEONA. IMEKUWA TU KAMA ZAMANI KWA *MANABII WA ISRAELI!*
*HARAKISHA!* MTAYARISHE PUNDA! LAZIMA NIMFWATE NA NIMPATE!
BABA, WAFIKIRI ALICHOSEMA NI KWELI? YEHOVA NDIYE MUNGU ALIYE HAI TU? MIUNGU YETU SI KITU?


ALIMPATA NABII WA YEHOVA AMEKETI CHINI YA MTI. ALITAKA KUWA KARIBU NA MTU HUYU MWENYE NGUVU. ALIWAHI KUWA NABII WA YEHOVA LAKINI AKAMWASI MUNGU. ALIWAZA "JE, DINI ZOTE SI SAWA?"


LAZIMA UWE MTU WA MUNGU KUTOKA YUDA. UNAKAA MCHOVU. KUJA NYUMBANI PAMOJA NAMI NITAKUHUDUMIA KWA CHAKULA NA VINYWAJI.
SIWEZI MUNGU ALINIAMBIA NISILE WALA KUNYWA CHOCHOTE HUKU.
ILA MIMI NI NABII KAMA WEWE, NA LEO ASUBUHI MALAIKA WA YEHOVA ALINIZUNGUMZIA NA AKANIAMBIA NIKULETE NYUMBANI KWANGU TULE NA TUNYWE.
NAMSHUKURU MUNGU. NINA KIU SANA


HAKIKA HUO NI MLO MWEMA. LAKINI LAZIMA NIWE NJIANI NIKIRUDI YUDA.
YEHOVA AMESEMA: "KWA SABABU HUJATII AMRI YA YEHOVA MUNGU, UMEKULA NA KUNYWA MAHALI HAPA, MWILI WAKO ULIOKUFA HAUTARUDI YUDA KUZIKWA KATIKA MAKABURI YA FAMILIA YAKO."
BABA, UNATABIRI PIA JE, MUNGU ALIONGEA NA WEWE PIA?
NDIO MWANANGU. KWA MARA YA KWANZA BAADA YA MIAKA KUMI


1 WAFALME 13:10-22
UNA MAANA YA KUA ATAKUFA?
NINAOGOPA HIVYO, ILA SIO KOSA LANGU.


NABII ALIONDOKA NA MOYO MZITO, AKIJUA KWAMBA MUNGU DAIMA ALIKUWA MWAMINIFU KWA NENO LAKE. ALIJUA ANGEKUFA. HAKUTARAJIA TU NI HIVI KARIBUNI, AU KWA NJIA HII.
EIIII


YULE NI NABII KUTOKA YUDA!
CHA KUSTAABISHA ZAIDI NI KUA SIMBA NA PUNDA WAMEKETI HAPO NI KANA KWAMBA WANAMLINDA.
SIJAWAI **KUONA** JAMBO KAMA HILI. SIMBA AMEMUUA ILA HAJAMLA


NABII WA UONGO ALIMCHUKUA MTU WA MUNGU AKAMZIKA KATIKA KABURI LAKE MWENYEWE MIONGONI MWA MANABII WA BAALI, KARIBU NA MAHALI AMBAPO MUNGU ALIHARIBU MADHABAHU
MUNGU ALIMUUA KWA KUTOTMTII. KWA KWELI UTABIRI WOTE LAZIMA UNGEFANYIKA.
MTU WA MUNGU AZIKWA NA KUSAHAULIKA NA WOTE ISIPOKUA WACHACHE. MADHABAHU ILIKARABATIWA NA KARIBU MIAKA MIA TATU BAADAYE ILIKUWA BADO INATUMIWA NA WAABUDU WA BAALI, LAKINI HAKUNA MTU ALIYEWAHI KUTEKETEZA MIFUPA YAO JUU YA MADHABAHU KAMA MTU WA MUNGU ALIVYOTABIRI.
1 WAFALME 13:23-31; 2 WAFALME 21:24, 22:8-11, 23:1-3


MIAKA MIA TATU BAADAYE, MFALME AITWAYE YOSIA ALICHUKUA KITI CHA ENZI KATIKA YUDA (640 B.C.). ALIKWENDA HEKALUNI NA KUPATA NAKALA YA BIBLIA. ILIMSUMBUA WAKATI ALIGUNDUA KWAMBA TAIFA LILIKUWA LIMESAHAU MUNGU ALIYE HAI NA KUENDA KWA SANAMU, HIVYO YEYE ALIWAAMURU WAZEE WOTE, MANABII, MAKUHANI, NA WAKAZI WOTE WA YERUSALEMU WAUNGANE PAMOJA KUSIKIA MAANDIKO NA KUKISOMA KITABU.
WATU WALIHAIBIKA NA WAKAKUBALI KUKISOMA KITABU.


WATU WALITII SHERIA YA MUNGU NA KUHARIBU SANAMU ZOTE. WALIWAANGAMIZA PIA MAKUHANI WALIO ABADU SANAMU.
MAMA MTAKATIFU, TUOKOE!


SHERIA YA MUNGU, KAMA ILIVYOTOLEWA NA MUSA, ILIKATAZA USHOGA HIVYO MASHOGA WOTE WALIFUKUZWA KUTOKA NCHI.
WAPUUZI


PIA WALISAFISHA NCHI KWA WALE WOTE WALIOSHAURIANA NA ROHO ZILIZOZOELEKA, WASTANI, NA WACHAWI.
VUNJA MPIRA WAKE NA UITEKETEZE NYUMBA YAKE.
2 WAFALME 23:5, 7, 10, 24


WALIVUNJA MADHABAHU, KUHARIBU SANAMU ZOTE, WAKAKATA MITI, NA KUSAGA ZOTE KUA UNGA.
YOSIA ALIKWENDA MAHALI PA JUU AMBAPO NABII ALIKUWA AMEKABILIANA NA YEROBOAMU, MFALME WA KWANZA WAFALME WA KASKAZINI, MIAKA 300 MAPEMA.
KUNA MUNGU MMOJA TU. NA HAABUDIWI KUITIA PICHA. HAWA MANABII WA UONGO WAMEWAELEEKEZA WATU GIZANI.


LAZIMA UFE!
KWA MARA NYINGINE TENA MADHABAHU ILIZIMWA NA MAJIVU YALITAPAKAZWA.


MAKUHANI WOTE WA UONGO WALIUAWA NA MIILI KUTEKETEZWA KWENYE MAGOFU YA MADHABAHU.
KARIBU NAH APO YALIKUWA MAKABURI YA MAKUHANI WA UONGO. ILI KUWAZUIA WATU KUTOUABUDU MAKUHANI KATIKA MAKABURI, YOSIA ALICHIMBA MIFUPA YAO NA KUITEKETEZA KWA MOTO, JUU YA MADHABAHU.
2 WAFALME 23:15-16


NA HATIMAYE UTABIRI WA MIAKA 300 ILIYOPITA ULITIMIZWA, KAMA VILE MTU WA MUNGU ALIVYOSEMA.
CHOMA MIFUPA YOTE
LAKINI HILI NI KABURI LA MTU WA MUNGU ALIYETOKA YUDA KARIBU MIAKA MIA TATU ILIYOPITA NA KUTABIRI SIKU HII. ALISEMA KWAMBA MTU AITWAYE YOSIA, YAANI WEWE MWENYEWE, ANGEKUJA NA KUFANYA MAMBO ULIYOYAFANYA LEO.
BASI IWACHE MIFUPA YAKE. CHOMA INGINE YOTE. IBADA YA SANAMU LAZIMA IISHE ILI MUNGU ATUBARIKI.


AMEBARIKIWA MWENYEZI MUNGU, MFALME WA ULIMWENGU,
SASA IBADA HIYO YA SANAMU ILIKUWA IMETOWEKA, MFALME YOSIA ALIWAAMURU WATU WOTE KUWEKA PASAKA KATIKA UKUMBUSHO WA YEHOVA, AMBAYE ALIWALETA BABA ZAO KUTOKA MISRI NA KUWAPA NCHI HII.


2 WAFALME 23:17-18, 21-22
BABA VIPI MBONA LEO NI TOFAUTI NA SIKU ZINGINE?
HIVYO BABA ALIWAAMBIA HADITHI YA ZAMANI YA JINSI MUNGU ALIVYOWAOKOA KUTOKA UTUMWA WA MISRI NA ALIWAPA SHERIA NA TABENAKULO. ILIKUWA PASAKA KUBWA ZAIDI MILELE.



## SURA YA 6

# ELIYA



KULIKUA NA MTU MMOJA ALIYEJULIKANA KAMA AHABU. ALIKUJA ISRAELI, NUSU YA KASKAZINI MWA UFALME (1918 B.C) ALIISHI SAMARIA KARIBU NA WAZIDONI. WAZIDONI WALIABUDU BAALI. AHABU ALIMUOA YEZEBELI, AMBAYE ALIKUWA MTOTO WA MMOJA WA MAKUHANI WA BAALI.


YEZEBELI ALIJULIKANA KWA KUPENDA DINI YAKE SANA. ALIDHARAU SANA MUNGU WA ISRAELI NA KUHIMIZA WATU SANA KU ABUDU BAALI.


WATAFUTE MANABII WOTE WA YEHOVA NA MUWAUE. BAALI ATAKUA MUNGU WETU.
MFALME ALIKUWA NA MTUMISHI ALIYEJULIKANA KAMAA OBADIAH, AMBAYE ALIABUDU YEHOVA.
LAZIMA NIWATAFUTE MANABII WA YEHOVA ILI NIWAONYE


OBADIA ALIWAFICHA MANABII 100 CHINI YA MWAMBA NA ALIWALETEA CHAKULA NA VYA KUNYWA.
1 WAFALME 16:28, 31, 18:4


ILA KULIKUA NA NABII MMOJA AMBAYE HANGEJIFICHA, ELIYA.


MFALME AHABU, KWA SABABU UMEMUACHA YEHOVA NA KUMFUATA MKE WAKO YEZEBELI KATIKA MABAYA, YEHOVA AMESEMA ISRAELI ITAKUA NA KIANGAZI HADI NITAKAPO AMURU VINGINE.
*HA HA HA* KWA HIVYO WAJIONA NABII SIO? NINA MANABII 1000 NA HAKUNA ASEMAYE CHOCHOTE KUHUSU KIANGAZI. TUMEKUA NA MVUA KA MIAKA MINGI SASA. WEWE NI MUONGO TU. ONDOKA HAPA!


KIANGAZI KILIPOZIDI NDIVYO WATU WALIENDELEA KUUMIA KWA KUHISI NJAA. MANABII WALIMUITA BAALI, LAKINI HAKUITIKA. KIANGAZI ILIZIDI KUENEA. MUNGU ALIMTUMA ELIYA KWA NYUMBA YA MJANE, AKAMWELEZA KUWA MJANE YULE ANGEMPA NYUMBA NA CHAKULA HADI KIANGAZI KITAKAPOISHA.
WAWEZA KUNIPA MAJI NA KIPANDE CHA MKATE ILI NILE?
KWA KUSEMA UKWELI NINA UNGA NA MAFUTA KIASI TU YA KUPIKIA MIKATE MIWILI PEKEE. MKATE WANGU NA WA MWANANGU. ILIKUWA TULE KISHA TUKAE TUANGAMIE KWA KIANAGAZI. HAKUNA MATUMAINI. MUNGU ANATUADHIBU KWA DHAMBI ZETU.


USIWE NA HOFU, MUNGU ATAWASAIDIA.
TAYARISHA MKATE ULIONELEZA KUHUSU. LAKINI NILETEE MIMI KWANZA KISHA WE NA MWANAWE MTAKULA. KWA HAYA YEHOVA ASEMA KUA "HAMTAKOSA VYA KULA WALA KUNYWA HADI KIANGAZI KITAKAPOKWISHA ISRAELI."


NI KWELI!
BADO KUNA UNGA NA MAFUTA YA KUTOSHA!
1 WAFALME 17:1, 10-16


HATUEZI KUONDOA UNGA HUU WOTE! UNAZIDI KUONGEZEKA.
NI MIUJIZA! MUNGU NI MWEMA.
KWA MIAKA MIWILI ILIYOKUJA, WATATU HAO WALIKULA MKATE KUTOKA KWA UNGA ULE WALIOPATA.


SIKU MOJA ELIYA ALIRUDI KWA MJANE HUYO NA KUPATA KUA KIJANA WAKE ALIAGA DUNIA.
ALIJAWA JOTO MWILINI NA KUAAGA *DUNIA*.


NIMEFANYA NINI KUKUUMIZA? ULIKUJA HUKU ILI KUNIKUMBUSHA DHAMBI ZANGU NA KWA MUNGU KUMUUA MWANANGU?
BADO KUNA MUNGU ISRAELI.


O YEHOVA MFUFUE MTOTO HUYU.


MUNGU ALIYASIKIA MAOMBI YA ELIYA NA KUMFUFUA MTOTO YULE.




1 WAFALME 17:17-24



KIANGAZI KILIENDELEA KWA MIAKA MITATU. WATU WALIZIDI KUTESEKA, ILA WALIZIDI KUABUDU BAALI.
MBONA BAALI HATUSIKII NA KUTUPATIA MVUA?
LABDA BAALI NI SANAMU MJINGA. HANA ATA MASKIO.


YEZEBELI NA AHABU WALIMLAUMU ELIYA SABABU YA KIANGAZI. WALIWATUMA ASKARI KUMTAFUTA ELIYA ILI WAMUANGAMIZE.
TUPATIE ELIYA! IWAPO MNAMFICHA NTAWAANGAMIZA PIA NYINYI.



*AHABU!* MWANITAFUTA?
WEWE NDO UNATATIZA ISRAELI KWA KIANGAZI?
WEWE NDO WATATIZA ISRAELI VNA SANAMU. BASI TUWE NA MASHINDANO KATI YA YEHOVA NA BAALI. WALETE MANABII 850 KATIKA MLIMA KARMELI.
WASEMA MASHINDANO? HAYA BASI. *TUPATANE HUKO.*


SIKU KADHAA BAADAE KATIKA MLIMA KARMELI.
MTAGAWANYIKA HADI LINI? KUNA MUNGU MMOJA TU. IWAPO YEHOVA NI MUNGU, MUMUABUDU YEYE TU. IWAPO BAALI NI MUNGU, BASI MUMUABUDU YEYE. MUWE NA MSIMAMO DHABITI.
NAWAALIKA MANABII WA BAALI KWENYE MASHINDANO. TUTAWEZA KUFAHAMU MUNGU WA KWELI NI YUPI.
NDIO! MASHINDANO YA KUTAMBUA MUNGU WA KWELI. TUNAHITAJIKA KUFANYA NINI?
1 WAFALME 118:1, 17-21.


MTAOMBA KWA BAALI NAMI NITAOMBA KWA YEHOVA. MUNGU AMBAYE ATAJIBU MAOMBI KWA KUTUMA MOTO KWENYE SADAKA, NDIYE ATAKUA MUNGU WA KWELI NA TUTAMUABUDU SOTE. NA KWA SABABU MKO WENGI, BASI MTAANZA.
JENGENI MADHABAHU YA BAALI, NAMI NTAMJENGEA YEHOVA MADHABAHU. TUTAWEKA KUNI NA SADAKA JUU YA MADHABAHU, ILA HATUTAWASHA MOTO.


EEH *BAALI,*
TUSKIZE SIKU HII YA LEO.
TUNAKUKABIDHI SADAKA HII
KWA JINA LAKO KUU.


EEH BAALI, MKUU NA MUWEZA YOTE.
EEH MALKIA WA MBINGUNI,NJOO UMSAIDIE BAALI SIKU HII YA LEO.


IWAPO BAALI NI MUNGU BASI HAWATILII MAANANI. LABDA ANAONGEA NA HAWEZI KUWASKIA, AMA LABDA AKO KWENYE SAFAI, AU AMELALA.
*WEWE MPUZI.* HUWEZI KUFANYA VYEMA ZAIDI.
1 WAFALME 18:22-27


EEH! ANAWEZA KUA AMELALA. TUMUITE KWA SAUTI KUBWA ILI TUMUAMSHE.
TUSIFE MOYO. PENGINE TUKIJIKATA BAALI ATAFURAHISHWA NASI



MANABII WA BAALI WALICHANGANIKIWA NA WAKAANZA KUJIRUSHA KWA ARDHI, KUJIKATA MWILINI NA KUPIGA NDURU ILI BAALI AWASKIE.
EIIIII
AAAAAAAAAH!
NAKUKABIDHI DAMU YANGU, O BAALI. TUSKIZE! TUMA MOTO! JIONYESHE.
YAAIIIEEEE!



*HA HA.* EBU JIANGALIENI. KWA MUDA WA MASAA TISA SASA MMEKUA MKIMUITA MUNGU NA ATA HAWAJIBU. ANGEKUA NI MUNGU WA KWELI BASI KWA SASA ANGEKUA AMEJIONYESHA.
SASA NI WAKATI WANGU. KARIBIENI NA MUANGALIE KWA MAKINI KILE NINACHOFANYA.
*EEH BAALI,* MBONA HUTUJIBU?
1 WAFALME 18:28-30


MBONA ANACHIMBA SHIMO?
ANAPOTEZA TU MUDA, SI GIZA TU LIINGIE.
UTAANZA KUSALI SAA NGAPI? HAYA SI MASHINDANO YA KUCHIMBA.
NENDENI MKALETE MAPIPA MANNE VYA MAJI KISHA MMWAGILIE SADAKA HII NA KUNI HIZI PIA.
MAJI? HAITAWAKA IKIWA BARIDI.


HAIJAPATA MAJI YA KUTOSHA. ONGEZENI MAPIPA MENGINE MANNE YA MAJI.
NABII HUYU ANA KICHAA. HATAISHI KULIONA JUA LIKITWAA.
KWANI AMETUPA MBAO? MBONA MFALME ANAMSKIZA?
1 WAFALME 18:32-34


*HA HA!* KUNA KITU KIGUMU MBELE YA MUNGU ANAYEISHI? ONGEZEENI MAPIPA MENGINE MANNE YA MAJI. MTAJUA YA KUWA KUNA MUNGU ISRAELI NA WALA JINA LAKE SI BAALI.
AHABU ATAMUUA KWA SABABU YA HILI.



SONGENI NYUMA
TENA
SONGENI NYUMA


YEHOVA, MUNGU WA IBRAHIMU, ISAKA NA ISRAELI, NA IJULIKANE SIKU HII YA LEO KWAMBA WEWE NDIWE MUNGU WA KWELI, NA YA KUA MIMI NI MTUMISHI WAKO.



VAROOOOOOOM
AAAAAH
IEEEE
CRRACK
1 WAFALME 18:35-38


MUNGU WA IBRAHIMU!
NI MOTO SANA!
MOTO KUTOKA MBINGUNI!
SAIDIA!


MUNGU WA IBRAHIMU NA ISAKA AMEJIBU KWA MOTO.
HADI IMECHOMA MAWE NA *UCHAFU*
NI MUNGU MGANI HUYU AMBAYE ATA HANA PICHA WALA USO NA ANAYAFANYA HAYA YOTE?




KUMBUKUMBU LA TORATI 17:2-5, 1 WAFALME 18:38-40


WAUE! WOTE 850
LAKINI SISI HATUKUJUA
WAANGAMIZE KWA MIKUKI
MANABII WOTE WA BAALI WALIUAWA


MFALME, UTAHITAJIKA KUHARAKISHA ULE NA UNYWE KISHA UENDE NYUMBANI. NASKIA SAUTI YA MVUA MINGI.


MIAKA MITATU NA NUSU ILIYOPITA ELIYA ALIMUELEZA AHABU YA KUWA ISRAELI HAINGEPATA MVUA HADI SIKU AMBAYO ELIYA ANGEAMURU. BAADA YA VIFO VYA MANABII WA BAALI NA WATU KUMREJELEA MUNGU, ELIYA ALIAMURU KUNYESHE.
MVUA KUBWA INGENYESHA WAKATI WOWOTE KWA HIVYO ILIWALAZIMU WAHARAKISHE KURUDI NYUMBANI KABLA WAPATWE NA MAFURIKO.
ELIYA, KWA UWEZO WA MWENYEZI MUNGU ALIKIMBIA MBELE YA FARASI KUELEKEA KWENYE IKULU.


NATUMAI MULIMUUA HUYO ELIYA.
LA MPENZI. ELIYA YUPO HAPO NJE. ALIKIMBIA MBELE YA FARASI WANGU KUTOKA MLIMA KARMELI.
HIYO NI UONGO TU. HAKUNA ANAYEWEZA KUFANYA HIVO. MAKUHANI WA BAALI WAPO WAPI? TUNAHITAJI KUSHEREHEKEA MVUA.
1 WAFALME 18:40-41, 44-46, 19:1


WOTE WAMEANGAMIZWA. NI WAONGO.


UMEFANYA NINI WE MJINGA. UNGEMUANGAMIZA ELIYA.


LAKINI MUNGU WAKE ALIJIBU KWA MOTO. *ILIKUA NI MUUJIZA*. MAKUHANI WETU *WALIKUWA HA*WANA NGUVU. WATU WOTE WAMEMGEUKIA YEHOVA.


NINGEFANYA NINI LAKINI? NLIWAOGOPA WATU
ULIWAANGAMIZA MAKUHANI
WANGU. WE MJINGA.


HAKUNA MUUJIZA AMBAO UTAMLINDA ELIYA KUTOKANA NA BAALI.
NISPOMUUA ELIYA KWA HAYA BASI WACHA PIA MIMI NIFE.
LAZIMA NIONDOKE




1 WAFALME 19:1-4


EEH MUNGU. NIMEYAPITIA MENGI. NIRUHUSU NIFE SASA HIVI KABLA YA YEZEBELI KUNIPATA.
NINA AIBU MWENYEWE. NIMEKOSA KUKUAMINI. NIRUHUSU NIFE.


ELIYA ALITOROKA KWA SIKU ARUBAINI JANGWANI ILI KUJIFICHA. ALIFIKA KWENYE MLIMA SINAI, NA HAPO MUNGU ALIMWONGELESHA.


ELIYA, UNAFANYA NINI HAPA?
KILA MTU AMEKWENDA MRAMA NA AMRI ZAKO ISIPOKUA MIMI. MANABII WAKO WOTE WAMEANGAMIZWA ISIPOKUA MIMI NA WANATAKA KUNIANGAMIZA PIA.
NENDA KASIMAME JUU YA MLIMA MBELE ZA MUNGU.


1 WAFALME 19:4, 8-12
ELIYA ALIPOSIMAMA MBELE ZA MUNGU UPEPO MKALI ULIKUJA LAKINI MUNGU HAKUA KWENYE UPEPO.
KISHA MTETEMEKO WA ARDHI ILA MUNGU HAKUWEPO.
MWISHOWE KUKAWA NA MOTO KUTOKA MBINGUNI, ILA MUNGU HAKUWEPO PIA.
MUNGU ALIKUWA AKIMUONYESHA ELIYA KUWA ALIKUWA NA NGUVU KUMLIKO YEZEBELI.


KISHA BAADA YA UPEO, MTETEMEKO NA MOTO KUISHA, ELIYA ALIMSIKIA MUNGU AKIONGEA KWA SAUTI NDOGO NA KUMMULIZA
ELIYA, UNAFANYA NINI HAPA?
ELIYA HAKUWA AMEJIFUNZA CHOCHOTE KWA HIVYO AKAJIBU TENA..
KILA MTU AMEKWENDA MRAMA NA AMRI ZAKO ISIPOKUA MIMI. MANABII WAKO WOTE WAMEANGAMIZWA ISIPOKUA MIMI NA WANATAKA KUNIANGAMIZA PIA.


HAYA BASI. NENDA UKAMPAKE ELISHA MAFUTA AWEZE KUA NABII WANGU.
NA PENGINE KAMA HUJUI, KUNA WATU 7000 AMBAO HAWAJA ABUDU BAALI. SASA NENDA NJIA ZAKO. JAMII YOTE YA AHABU ITAANGAMIA.


ELIYA ALIMPATA ELISHA AKILIMA NA AKAMPAKA MAFUTA NA KUMFANYA NABII.
BWANA AMESEMA YA KWAMBA UTAKUA NABII WAKE.
NITAMTOLEA MUNGU FAHALI WANGU KAMA SADAKA NA NIMFUATE.
1 WAFALME 19:12-21


KANDO YA IKULU YA AHABU KULIKUA NA SHAMBA LA NABOTH. AHABU ALITAMANI SANA SHAMBA LA NABOTHI KWA HIVYO ALIAMUA KULINUNUA.


AHABU ALIKUWA NA PESA NYINGI KWA HIVYO AKAAMUA KULINUNUA SHAMBA LA NABOTHI.
NIUZIE SHAMBA HILI KISHA MIMI NTAKUPATIA SHAMBA LINGINE MAHALI PENGINE.
MUNGU HANGEKUBALI.


SHAMBA HILI LIMEKUWA KWA JAMII YANGU KWA MIAKA 500 SASA. SHERIA HAITURUHUSU KUUZA SHAMBA HILI NJE YA JAMII LETU.


NIELEZE MPENZI WANGU. MBONA HUKULI?
KWA SABABU **NABOTHI** AMEKATAA KUNIUZIA SHAMBA LAKE.


KUTOKA 20:17; 1 WAFALME 21:1-7
WEWE NDIWE MFALME. UNAWEZA KUFANYA CHOCHOTE UNACHOTAKA. NITALINUNUA SHAMBA HILO KWA AJILI YAKO.


NITAWALIPA ZAIDI MKIMALIZA KAZI HII. NA MSIAMBIE MTU YEYOTE.


SHERIA YA MUSA INASEMA
"USIMSEMEE MWENZAKO UONGO"
CLINK


NDO YULE.
ALISEMA MFALME ANAPASWA KUFA.
NA PIA AKASEMA MUNGU ATAMTUMIA MFALME MAPEPO
BASI ANASTAHILI KUAGA.
WALIMBEBA NABOTHI NA KUMUANGAMIZA


NDIO HII MPENZI. SHAMBA HILI NI LAKO SASA.
INAPENDEZA SIO?
KUTOKA 20:16; 1 WAFALME 21:10-16
YEZEBELI ALIJUA KWAMBA BAALI HAKUA NA UWEZO WA KUONA, LAKINI ALITAMBUA KWAMBA YEHOVA ANASIKIA NA KUONA NA HASAHAU.


ELIYA, AHABU AMAKWENDA KWENYE SHAMBA LA NABOTHI ILI KULICHUKUA. NENDA UKAPATANE NAYE NA UMUELEZE MANENO YANGU.


AHABU MUNGU AMENIELEZA KUWA UMEMUUA MTU ASIYE NA HATIA. PALE AMBAPO DAMU YAKE ILIMWAGIKA, HAPO NDIPO YAKO PIA ITAMWAGIKA NA KULAMBWA NA MBWA.
KWANI ADUI WANGU AMENIPATA HAPA?


HUWEZI KUJIFICHIA MUNGU. NA KWA SABABU YA DHAMBI *ULIYOTENDA MUNGU ATAIANGAMIZA* JAMII YAKO YOTE.
UMEIPANDISHA HASIRA YA MWENYEZI MUNGU. MBWA WATAMLA YEZEBELI KANDO YA NYUMBA YAKO. MTU YEYOTE WA JAMII YAKO AKIFA MWILI WAKE UTALIWA NA MBWA. HAKUNA ATAKAYEZIKWA KWA HESHIMA.


HILO NDILO NENO LA MUNGU. NA LAZIMA LITATIMIA.
*TAFADHALI,* NTAANZA KUMTOLEA YEHOVA SADAKA.
1 WAFALME 21:17-26


AHABU ALIMTOLEA YEHOVA SADAKA, ILA HAKUMFUATA KWA MOYO MKUNJUFU.
YALE YOTE AMBAYO ELIYA AMESEMA YAMETIMIA


BAADAE MANABII WAONGO WAKAMSHAURI AHABU KUHUSU JESHI.
NENDA KAPIGANE KATIKA RAMOTH GILEAD NA MUNGU ATAKUPA USHINDI.
NA MANABII WOTE *WANAKUBALIANA* NA HAYA?


MFALME AHABU, YEHOVA AMEONGEA NAMI. UTAKWENDA HUKO RAMOTH GILEAD NA UTAKUFIA HUKO.
USIMSKIZE MICAIAH. SI YEYE ***PEKEE NABII WA YEHOVA.*** KUNA SISI MANABII 400 AMBAO TUNASEMA KUTAKUA NA MAZURI HUKO RAMOTH GILEAD.
NAMCHUKIA MICAIAH. YEYE HUSEMA TU ***MABAYA.***


MFALME AHABU, UMEFANYA MAOVU MBELE YA MUNGU. WEWE HUWASKIZA MANABII WA UONGO NA KUWALIPA KWA KAZI YAO. WAO HUHUBIRI UONGO.


NILIMWONA MUNGU AMEKETI JUU YA KITI CHA ENZI, NA MALAIKA WOTE WA MBINGU WALIKUWA WAMESIMAMA MBELE YAKE. YEYE AKASEMA "TANGU ELIYA ALIPO MWAMBIA AHABU KWAMBA ATAKUFA, AMEKUWA MAKINI SANA KUTOINGIA KATIKA NJIA YA MADHARA. NANI ANAWEZA KUMSHAWISHI AHABU AENDE VITANI KATIKA RAMOTH-GILEAD AMBAKO ATAUAWA?"
NA MMOJA AKASEMA JAMBO MOJA NA MWINGINE AKATOA PENDEKEZO. BAADA YA KUJADILIANA BASI AKASIMAMA MBELE NA KUSEMA:



NINA WAZO AMBAYO ITAFANYA KAZI. NITAFANYA JUU CHINI NIWE ROHO MDANGANYIFU MDOMONI MWA MANABII WAKE WOTE WA UONGO. NITAWAAMBIA KWAMBA AHABU ANAPASWA KWENDA VITANI.
1 WAFALME 21:27, 22:6-22
HILO NI WAZO ZURI. WATATOA UNABII KWAMBA ATAKUWA NA USHINDI, LAKINI YEYE ATAKUFA. BASI NENDENI.


UNAFIKIRI ROHO WA YEHOVA ALINIACHA NA KUZUNGUMZA KWAKO?
SMACK!



UTAJUA NI NANI ANA ROHO WA YEHOVA SIKU UTAKAPO KWENDA KATIKA CHUMBA CHA NDANI CHA *KUJIFICHA* KWA HOFU *YA MAISHA YAKO*
NINI HII, UNABII MWIGINE? HA!


WEKA HUYU MTU KATIKA GEREZANI NA KUMLISHA *TU YA KUTOSHA* KUMWEKA HAI MPAKA NITAKAPORUDI KUTOKA KWENYE VITA. ***KISHA TUTAMUUA.***
***UKIRUDI*** KTOKA VITANI UKIWA HAI BASI MIMI NI NABII WA UONGO NA NINASTAHILI ***KUFA.***



HIYO ILIKUWA WAZO ZURI, *KUJIFICHA* MWENYEWE KAMA ASKARI WA KAWAIDA. WAO KAMWE HAWATAJUA WEWE NI MFALME. *SIWEZI* KUSUBIRI KUONA USO WA NABII *HUYO UTAKAPORUDI* UKIWA HAI.
NDIYO, NA SILAHA HII ATANILINDA DHIDI YA *MISHALE.*
1 WAFALME 22:24-30


A SOLDIER SHOT AN ARROW HIGH IN THE AIR, NOT AIMING AT ANYONE IN PARTICULAR, JUST HOPING TO HIT ONE OF HIS ENEMIES.











THUD
NINI?
UGGGHHHHHH


HARAKA, NATOKWA NA DAMU VIBAYA.
VUMILIA
1 WAFALME 22:34


NINA HOFU AMEAGA.
MSHALE ULIUPATA SEHEMU MOJA AMBAYO ILIKUWA HAIJALINDWA NA SILAHA. NADHANI ILIKUWA TU MUDA WAKE WA KUFA
EEH MUNGU, HAPANA!


WEKA MWILI WAKE KATIKA SHAMBA LA MIZABIBU LA NABOTHI MPAKA TUWE NA MUDA KUKABILIANA NAJAMBO HILIVIZURI.



KAMA VILE ELIYA ALIVYOSEMA, MBWA WALIKUWA WAKILAMBA DAMU YA AHABU CHINI YA DIRISHA LA YEZEBELI. ALIKUWA WA KWANZA WA NYUMBA YAKE; WENGINE WANGEFUATA.


BAADA YA KUOSHA DAMU KUTOKA GARI LA AHAB ASKARI ALIRUDI IKULU.
AKO WAPI MFALME AHABU? JE, YEYE ANASHEREHEKEA USHINDI?
1 WAFALME 22:37-38; 2 WAFALME 9:8-10


MJINGA WEWE! WEWE SI NABII WA MUNGU. WEWE NI MWONGO! AHABU AMEKUFA TU KAMA VILE MIKAYA NABII WA YEHOVA ALITANGAZA.
LAKINI HAIWEZI KUWA. WACHAMUNGU WOTE WALIKUBALIANA AHABU ANGEKUWA MSHINDI.
SIO WOTE. SI MIKAYA ULIYEMPIGA MAKOFI NA KUMWEKA KWENYE GEREZA. WATU WATAKAPOSIKIA HIVI NDIVYO WATAKAVYO KUJIA KICHWA CHAKO!


UKO HURU KWENDA. AHABU AMEFARIKI.
NDIYO NINAJUA NA BILA SHAKA MBWA WAMEILAMBA DAMU YAKE KAMA MUNGU ALIVYOSEMA. YEZEBELI ATAFUATA NA JAMII YOTE YA AHABU. MUNGU AMEZUNGUMZA.


LAZIMA NIJIFICHE.


LO, HAPANA! MIKAYA ALISEMA MIMI NINGEJUA NI NANI ALIYEPATA ROHO WA MUNGU SIKU AMBAYO NITAKWENDA MAFICHONI KATIKA CHUMBA KIDOGO.


WANA WA AHABU WANGETAWALA MAHALI PAKE, NA MIAKA KUMI NA MIWILI INGEPITA NA YEZEBELI BADO ANGEISHI KAMA MALKIA. ISRAELI INGEENDELEA KUABUDU MIUNGU NA KUVUNJA AMRI ZA MUNGU.
MUNGU ALIONGEA DHIDI YA NYUMBA YA AHABU, AKASEMA: WAKATI UMEFIKA. FAMILIA YOTE YA AHABU ITAANGAMIA, HATA WATOTO WADOGO. NA HAKUNA YEYOTE ATAKAYEPONEA. YEZEBELI ATALIWA NA MBWA, NA HAKUTAKUWA NA YEYOTE KUOMBOLEZA AU KUMZIKA."




2 WAFALME 9:30


NITASIMAMA HAPA AMBAPO WATAWEZA KUONA KWAMBA MIMI NDIYE MAMLAKA.


NANI AKO UPANDE WANGU?



TUPO NAWE, JENERALI.
BASI MRUSHENI YEZEBELI CHINI.
HAMUEZI KUFANYA HIVO. *MIMI NDIYE MALKIA.*




2 WAFALME 9:32-33


WACHENI MWILI WAKE HAPO


MBWA WALIKULA MWILI WA YEZEBELI, JINSI NABII WA MUNGU ALIVYOTABIRI.
GRRRR


2 WAFALME 9:33-37
LAKINI MBWA HAWANGEWEZA KULA MIKONO ILIYOTENDA MAOVU.
KAMA VILE MANABII WALISEMA, WATOTO WENGINE WA AHABU WOTE WALIUAWA NA WATU WA MJI, MPAKA WATU WOTE WA FAMILIA YAKE WALIUAWA.
WALE WALIOKUFA MASHAMBANI WALILIWA NA WANYAMA PORI NA WALE WALIOKUFA KATIKA MJI WALILIWA NA MBWA. HAKUNA KILICHOBAKI CHA KUZIKA. HAKIKA MSHAHARA WA DHAMBI NI MAUTI


ELIYA ALIPOOMBA, MANABII WADOGO WALIKUJA KWA ELISHA KUTOA UJUMBE.
MUNGU AMEZUNGUMZA KWA BAADHI YA MANABII WADOGO. JE UNAJUA KWAMBA ELIYA ATACHUKULIWA KWENDA MBINGUNI?
*NDIYO,* MUNGU ALINIAMBIA PIA, BALI *TULIENI NYINYI!* WALA MSISEME ZAIDI.


ELISHA, KAA HAPA. NITAKWENDA SAFARI KULE JERICHO.
KAMA MUNGU ANAVYOISHI, SITAKURUHUSU UONDOKE MACHONI PANGU. MIMI *NITAKWENDA* KOTE UTAKAPOENDA.


JE, ULIJUA KWAMBA ELIYA ATAKWENDA MBINGUNI LEO?
NDIO NAJUA. BASI JIWEKEE UNAYOJUA. SIFAI KUMWACHA ATOKE MACHONI MWANGU.


WE *KAA HAPA* JERICHO. LAZIMA NIFIKE MTO JORDAN.
HAKIKA KAMA MUNGU ANAISHI NA UNAISHI, *MIMI SITAKUACHA.*


KUNA MANABII HAO WADOGO, NA WANAT*UFUATA* TENA.
TUTAVUKEAJE MTO? MAJI NI MENGI SANA LEO.
KWA ARDHI KAVU
2 WAFALME 2:3-7


KOFI!
AHHH!
UMEONA HAYO? MAJI YAMEJIGAWANYA ILI WAWEZE KUPITA.
NDIO, KAMA TU ULE WAKATI WA MUSA.
SINGEKOSA KUONA HAYA KWA VYOVYOTE VILE.
NATAMANI MANABII WA BAALI WANGEYAONA HAYA.


UNGEPENDA NIFANYE NINI KABLA NIONDOKE?
NIGAWIE ROHO WA MWENYEZI MUNGU ALIYE NDANI YAKO.
UMEULIZA JAMBO GUMU ILA ITAFANYIKA NITAKAPO PAA KWENDA MBINGUNI.

2 WAFALME 2:8-11




WROOARRR
GARI LA MOTO LILIMTENGA
ELIYA NA ELISHA



ELIYA ALICHUKULIWA HADI MBINGUNI KATIKA KIMBUNGA


KISHA KUKAWA NA UKIMYA. ELIYA SASA ALIKUWA KATIKA UWEPO WA MUNGU.
AMEIACHA JOHO LAKE PEKEE ALILOTUMIA KUGAWA MAJI.
2 WAFALME 2:11-13


YUPO WAPI MUNGU WA ELIYA?



ROHO WA ELIYA YUKO JUU YA ELISHA!
WHOP!
JAMANI, LEO NI SIKU YA KIPEKEE



ELISHA ALIENDELEA KUFANYA MARA MBILI MIUJIZA MINGI KAMA ALIVYOFANYA ELIYA. ALIKUWA MWAMINIFU KWA MUNGU, LAKINI WATU HAWANGEACHA KABISA KUABUDU SANAMU.
ELIYA ALIKWENDA WAPI?
LAZIMA TUMTAFUTE.
HAKUNA HAJA, AMEENDA MBINGUNI.
2 WAFALME 2:!4-16




SURA YA 7

# UNABII WA KRISTO


BAADA YA ELISHA, MUNGU ALIWALETA MANABI WENGINE KAMA VILE ISAYA, YEREMIA, NA AMOSI AMBAO WANGE WABADILISHA WATU DHIDI YA IBADA YA SANAMU NA DHAMBI. MUNGU ALIZUNGUMZA KUPITIA MANABII HAWA, NA KUWAFANYA WAO KUANDIKA UNABII WA MAMBO AMBAYAO YANGEFANYIKA SIKU ZA USONI.
ISAYA ALIKUWA NABII WAKATI WA UTAWALA WA WAFALME UZIA, YOTHAMU, AHAZI, NA HEZEKIA (TAKRIBAN 760-700 B.C.). MUNGU ALIONGEA KUPITIA ISAYA, "NIME WALISHA NA KULEA WATOTO, LAKINI HAO WALINIASI, FAHALI BUBU ANAJUA MMILIKI WAKE, LAKINI ISRAELI HAINIJUI MIMI. NYINYI NI TAIFA LA DHAMBI, WATU WALIOJAWA NA UOVU, WATOTO WA WATENDA MAOVU..."


“KAMA MTAONDOKEA UOVU WENU NA MUACHE KUKANDAMIZANA, KUTUNZA WASIO NA BABA, NA KUWAPA WAJANE WANACHOHITAJI, NITAREJESHA AMANI NA KUWAPONYA, LAKINI MSIPONIRUDIA BASI MTAKUFA KWA KWA UPANGA. ARDHI YENU YOTE ITAKAUKA, NA MJI WENU UTACHOMEKA KWA MOTO MKALI! NAO WATABEBA WAVULANA WENU NA KUWAPELEKA BABELI NA HUKO WATAWAFANYWA WATUMISHI KUHUDUMU KATIKA IKULU YA MFALME WA BABELI.”




YEREMIA ALIKUWA NABII WAKATI WA UTAWALA WA WAFALME YOSIA, YEHOYAKIMU, NA ZEDEKIA (TAKRIBAN 630- 590 B.C.). ALISEMA, "BWANA ASEMA HIVI, TAZAMA, NIMEWEKA MBELE YENU NJIA YA UZIMA, NA NJIA YA KIFO. YEYE ADUMUYE KATIKA MJI HUU ATAKUFA KWA UPANGA, NA KWA NJAA, NA KWA TAUNI; ATAKAYE TOKA NA KUANGUKA KWA WAKALDAYO WALIOWAKASIRISHA, ATAISHI, LAKINI ATAKUWA MTUMWA KATIKA BABELI. KWANI NIMEUWEKA USO WANGU DHIDI YA MJI HUU KWA UOVU, ASEMA BWANA, UTATOLEWA MKONONI MWA MFALME WA BABELI, NAYE ATAICHOMA KWA MOTO."


BWANA ALISEMA KUPITIA YEREMIA AKISEMA, " MIMI MWENYEWE NITAPIGANA DHIDI YAKO NA MKONO ULIONYOSHWA NA WENYE NGUVU, HATA KWA HASIRA, NA KWA GHADHABU, NA KATIKA GHADHABU KUBWA. NAMI NITAWAPIGA WENYEJI WA MJI HUU, MTU NA MNYAMA:


WATAKUFA KWA TAUNI KUBWA.
NA BAADAYE, ASEMA BWANA,
NITAKOMBOA SEDEKIA MFALME WA YUDA, NA WATUMISHI WAKE, NA WATU, NA WALE WALIOBAKI KATIKA MJI HUU KUTOKANA NA TAUNI, KUTOKANA UPANGA, NA NJAA, NITAWAPEANA KATIKA MKONO WA MFALME NEBUKADREZA WA BABELI, NA KATIKA MKONO WA ADUI ZAO, NA KATIKA MIKONO YA WALE AMBAO WANATAFUTA MAISHA YAO: NA YEYE ATAWAPIGA KWA MAKALI YA UPANGA; HATAWAHURUMIA, WALA KUWAONEA REHEMA. HASIRA YANGU ITAWAKA KAMA MOTO NA HAKUNA ATAKAYEIZIMA. WATAWABEBA KAMA WATUMWA KWENDA BABELI, NA WATAWAUWA KWA UPANGA. WENGI WA WALE AMBAO WATAKAOBEBWA KWENDA BABELI WATAKUFA NA KUZIKWA HUKO."

YEREMIA 20:4-6, 21: 5-7, 10-12


AMOSI ALIKUWA NABII WAKATI WA UTAWALA WA WAFALME UZIA NA YEROBOAMU II (TAKRIBAN 765–750 B.C.). MUNGU ALIZUNGUMZA KUPITIA AMOSI, "WANAWAKE WENU NI KAMA NG'OMBE WANAOHITAJI WAUME KUWAWEKA VIZURI. HAMTAWATAWALA TENA WAUME WENU. MTAPOTOSHWA NA NDOANO KATIKA MIILI YENU NA KUWA WATUMWA KATIKA BABELI."




NYINYI HUKALIA VITI VYA DHAMANI KUBWA NA KULA VYAKULA VILIVYOJAA MAFUTA. KUSKIZA MZIKI NA KUNYWA DIVAI KWA WINGI. MMEITUPA HAKI, KUWANYANYASA MASKINI, KUDHULUMU WENYE HAKI NA KUCHUKUA HONGO. MTAPANDA MIZABIBU, ILA ADUI ZENU NDO WATAKUNYWA DIVAI. JESHI LENU LITATAWANYIKA NA KUANGAMIA, NANYI MTAKUA WATUMISHI KWA NCHI NYINGINE.


MUNGU ANASEMA, “NITAHARIBU MADHABAHU YA BETHELI PAMOJA NA VYUMBA VYENU VYA WAKATI WA BARIDI NA WAKATI WA JUA. MNAWAKANDAMIZA MASKINI, KUCHUKUA RUSHWA, NA KUWANYANYASA MASKINI. NIMEWATUMIA KIANAGAZI PAOMJA NA MAGONJWA ILA NYINYI HAMTUBU. MNAPANDA MIZABIBU ILI KUTENGEZA DIVAI, ILA NYINYI HAMTAIKUNYWA DIVAI HIYO.
MAMA NINA NJAA.
AMOSI 4-6


753 KABLA YA YESU.
HOSEA ALIKUWA NABII WAKATI WA UTAWALA WA WAFALME UZIA, YOTHAMU, AHAZI, NA HEZEKIA (TAKRIBAN 785-725 B.C. "ISRAELI WATAANGUKA KWA UPANGA, WATOTO WAO WATAPIGISHWA KWENYE ARDHI, MIMBA YA WANAWAKE WAO ITACHANWA WAZI."
"SIKU ITAKUJA AMBAPO MUNGU ATAWASAMEHE DHAMBI NA ATAPENDA ISRAELI. ISRAELI ITAPENDEZA NA KUFANIKIWA.


"KATIKA MIAKA IJAYO, BAADA YA BABELI, MTASAMBAZWA KWA MATAIFA NA MATAIFA HAYO YATAWAHUKUMU, KUCHUKUA MALI YENU NA HAMTAPATA MAHALA PA KUPUMZIKA.




ISAYA 10:21, SURA YA 35, 51:11; YEREMIA 30:11; EZEKIELI 17:21; HOSEA 13:16, 14:1-6; YOELI 3:2


KULINGANA NA NAKALA HII, WAYAHUDI WANAPASWA KUONDOKA HUMU NCHINI NA WASIBEBE *CHOCHOTE*.
NIMEKUWA NIKITAMANI KURIDHI NGOMBE HUYU.
KWA SABABU TAIFA LA ISRAELI LILIKATAA NENO LA MUNGU, WANGETAWANYIKA MATAIFA YOTE YA DUNIA; LAKINI HAWATAPATA MAPUMZIKO. MPAKA MWENYEZI MUNGU AWAREJESHE KWA NCHI YA BABA ZAO.



"NCHI YOTE YA ISRAELI ITAPATA UKIWA, NA MTAMTUMIKIA MFALME WA BABELI KWA MIAKA SABINI. LAKINI BAADA YA MIAKA SABINI NITAIADHIBU BABELI KWA AJILI YA UOVU NA WATAKAOBAKI NTAWAREJESHA KATIKA NCHI HII KUIJENGA UPYA."
"YERUSALEMU ITAACHWA HIVYO NA KULIMWA KAMA UGA."


UNABII HUU ULIKUJA KUTIMIA. LAKINI KATIKA SIKU ZA MWISHO HEKALU LITAJENGWA UPYA, NA WATU WATAJAA HUKO.
NABII MICAH, AMBAYE ALIISHI KUTOKA 750-686 B.C., ALITABIRI:


"NA MATAIFA MENGI YATAKUJA, NA KUSEMA, KUJA, TUENDE MLIMANI WA BWANA, NA NYUMBA YA MUNGU WA YAKOBO; NAYE ATATUFUNDISHA NJIA ZAKE, NASI TUTATEMBEA KATIKA NJIA ZAKE; KWANI SHERIA ITATOKA SAYUNI, NA NENO LA BWANA KUTOKA YERUSALEMU."
"NAYE ATAHUKUMU MIONGONI MWA WATU WENGI, NA KUKEMEA MATAIFA YENYE NGUVU MBALI;


TAIFA HALITAINUA JUU UPANGA DHIDI YA TAIFA, LAKINI ATAKETI KILA MTU CHINI YA MZABIBU WAKE NA CHINI YA MTI WAKE; NA HAKUNA ATAKAYE WAOGOPESHA, KWA AJILI KINYWA CHA BWANA WAMAJESHI KIMESEMA HAYO."
"NASI TUTATEMBEA KATIKA JINA LA BWANA, MUNGU WETU MILELE NA MILELE. KATIKA SIKU ILE, ASEMA BWANA, NITAMKUSANYA YOYOTE ALIYETIMULIWA NJE. NAMI NITAIFANYA TAIFA KUWA IMARA: NA BWANA ATAWATAWALA KATIKA MLIMA SAYUNI TANGU SASA, HATA MILELE."
YEREMIA 25:11-12; MICAH 3:12, 4:1-7


YEREMIA NA WENGINE WALITABIRI:
"MFALME ZEDEKIA AMETENDA MAOVU MACHONI PA BWANA. HATAUAWA. ATAKWENDA KATIKA BABELI AMBAKO ATAISHI MAISHA YAKE PAMOJA NA WATU WAKE, LAKINI MACHONI MWAKE HATAWAI KUONA BABELI. ATAPOFUSHWA. UTABAKI HUKO BABELI KWA MIAKA 70.
"MWISHONI MWA MIAKA 70, BABELI ITASHINDWA NA JESHI KUTOKA KASKAZINI NA SAZO LA WATU WETU WATARUDI KATIKA NCHI HII KUJENGA UPYA MJI NA HEKALU."


"BAADA YA MUDA WA HUKUMU MUNGU ATASAMEHE DHAMBI ZAO NA YERUSALEMU ITAJAA WATU KATIKA VIZAZI VYOTE."
"CHUKUA KITABU HIKI UENDE NACHO BABELI NA UKISOME HUKO MBELE YA WATU. WAVUMILIE KABLA WARUDISHWE HUMO.
"NITAREJESHA KITI CHA ENZI CHA DAUDI NANYI MTARUDI TENA NA KUMILIKI NCHI YENU YOTE."


EZEKIELI ALITABIRI: "WAO WATAGAWANYIKA KATIKA MATAIFA, LAKINI JINSI MUNGU ATAKAPOWAGANYA, BADO ATAWAREJESHA NCHINI"
"MUNGU ALIMWAHIDI IBRAHIMU KWAMBA UZAO WAKE UNGERIDHI NCHI HIYO MILELE, NA WALA HATAVUNJA AHADI YAKE. HATA HIVYO, WANAPOKUA WATENDA DHAMBI. MUNGU ATAWAPELEKA UTUMWANI AMBAKO WATATUMIKIA MIUNGU ILA MWISHOWE ATAWAREJESHA NCHINI.
YEREMIA 34:3, 39:7, 51:60-61, 52:11; EZEKIELI 12:13-16; YOELI 3:20-21; AMOSI 9:11-15


"MISRI PIA ITAHUKUMIWA NA BABELI, NA KWA MIAKA 40 MISRI ITAHANGAIKA. NA MISRI ITAKAPOTOKA BABELI, HAITAKUA NA SIFA KAMA ILIVYOKUWA HAPO AWALI, ILA WATAVUMILIA HADI MWISHO. NA KWA SIKU ZA USONI MISRI ITAUGANA NA ASIRIA NA ISRAELI KWA AGANO LA AMANI, NAMI NITAWABARIKI.


"WAFILISTI WATATESEKA NA WATAANGAMIA. VILE VILE ASHDODI, EKRONI NA AMMONI HAWATAKUWEPO TENA.


“ILA IRANI, UTURUKI, ETHOPIA NA LIBYA WATAISHI HADI MWISHO, NA WAKATI UTAFIKA AMBAO WATAVAMIA ISRAELI, LAKINI WATAKUFIA KWENYE MILIMA ILIYOKO ISRAELI.”


UNABII WOTE ULIOKO KWENYE BIBILIA HUTIMIA KWA KAWAIDA. MIJI NA MATAIFA YALIYOTABIRIWA KUISHA NA KUANGAMIA YALIANGAMIA.
YEREMIA 25:15-26, EZEKIELI 25, 26:15-19, 29:12-16, 30:1-8; AMOSI 1


KATIKA MWAKA 605 KABLA YA YESU, ISRAELI ILISHINDWA NA WABABELI KAMA ILIVYOTABIRIWA.
EEH BWANA, KWA DHAMBI ZA BABA ZETU TUNAADHIBIWA. TUSAIDIE TUWEZE KUFUATA AMRI ZAKO HATA TUKIWA HUKU KWENYE NCHI NGENI.


ZAIDI YA WAYAHUDI 5000 WALILETWA BABELI KAMA WAFUNGWA WA VITA. WALIWABEBA VIJANA NA WALIO NA HEKIMA ILI KUWATUMIA KWA MANUFAA YA UFALME WAO. KATI YA VIJANA HAO KULIKUA NA KIJANA ALIYEJULIKANA KAMA DANIELI. ALIZIFUATA AMRI ZA MUNGU, NA KUMHESHIMU MUNGU WA IBRAHIMU.


TUNAKUSHUKURU, EEH BABA WA MBINGU NAN NCHI, MFALME WA ULIMWENGU.
DANIELI ALIKUWA MFUNGWA KWA NCHI NGENI, ILA ALIAMUA KUA MWAMINIFU KWA MUNGU. WAFUNGWA WALITAMBUA KUA DANIELI ALIKUWA NA ROHO YA KIPEKEE KWA HIVYO WAKAMWEKA MAHALA KANDO NA WENGINE KAMA MMOJA WA MTU WA HEKIMA KATIKA BABELI.


NEBUKADINEZA, MFALME WA BABELI ALIAMSHWA NA NDOTO ISIYOKUA YA KAWAIDA.
MAMBO GANI HAYA? KA KWELI NDOTO HII IMETUMWA NA ***MUNGU*** ILI KUFICHUA ***YATAKAYOKUJA***.




DANIELI 1:2-7, 17-21, 2:1-11


NILIJUA NYINYI NI ***WALAGHAI.*** HAKUNA MUNGU ANAYEZUNGUMZA NANYI. ***NYOTE MTAUAWA*** PAMOJA NA JAMII ZENU NA NYUMBA ZENU ***KUHARIBIWA***.


POLE DANIELI ILA WEWE PAMOJA NA WAZEE WENYE BUSARA WA BABELI ***MTAUWAWA***. MFALME HAWAAMINI MAKUHANI WAKE.
LAKINI ***YEHOVA*** ANAWEZA KUMFICHULIA MAANA YA NDOTO YAKE. LAZIMA NIJITENGE ILI NIOMBE. JARIBU UMSIHI ANGOJE HATA ANGALAU SIKU MOJA.


BWANA, WEWE PEKEE NI MUNGU NA MFALME WA ULIMWENGU. TAFADHALI ONYESHA MTUMISHI WAKO YATAKAYOTENDEKA. HAKUNA MUNGU MWINGINE KAMA WEWE.
DANIELI, NISKIZE MIMI...


HARAKA, NIPELEKE KWA MFALME!
USIPOMWELEZA MFALME KUHUSU NDOTO YAKE BASI ATANIANGAMIZA PAPO HAPO.


USINIPOTEZEE MUDA. UNAWEZA KUNIFAFANULIA NDOTO YANGU AU LA?
EH MFALME, WEWE NDIWE MFALME WA *WAFALME,* KWA MAANA MUNGU WA MBINGUNI NDIYE AMEKUFANYA HIVO. AMEKUANGAZIA KWA NDOTO MAMBO YATAKAYOFANYIKA ***SIKU ZA USONI.***
MUNGU WA KWELI, ALIYEUMBA ULIMWENGU, AMEONYESHA NDOTO YAKO KWA MTUMISHI WAKO.
DANIELI 2:12-30


EEH MFALME, ULIONA PICHA NDOTONI. PICHA HIYO INAWAKILISHA UFALME WAKO NA ZINGINE TATU ZITAKAZOFUATA.
*NI KWELI! SIKUMUELEZA YEYOTE!* MUNGU WAKO NDIYE MUNGU WA KWELI.


WEWE NDIYE KICHWA HIKI CHA DHAHABU, MFALME WA WAFALME. KABLA YA KUSHINDA JUDA, MANABII WETU WALITUELEZA KUWA MUNGU ANGETUHUKUMU KWA DHAMBI ZETU NA KISHA KUKUPATIA UFALME. SASA UTAWALA WAKO UTAKUA WA UTUKUFU.


KIFUA CHA FEDHA KINAWAKILISHA UFALME MWINGINE, WAMEDE NA WAAJEMI. BAADA YA KIFO CHAKO, WAO WATASHINDA BABELI NA WATATAWALA NCHI YOTE KAMA WEWE ULIVYOTAWALA.


EEH MFALME, BAADA YA KICHWA CHA DHAHABU NA KIFUA CHA FEDHA ULIONA TUMBO LA SHABA. SHABA HIYO INAWAKILISHA UFALME WA TATU, ***WAGIRIKI***. ITAKUJA BAADA YA UAJEMI NA ITAKUA YA ***HARAKA***.
UFALME WA NNE UTAKUA NA TOFAUTI NA ZINGINE. MIGUU ITAKUA IMETENGENEZWA KWA ***CHUMA***. NAYO ITAVUNJIKA VIPANDE MATAIFA MENGI. LAKINI ULIONA KWAMBA VIDOLE VYA CHUMA VILICHANGANYWA NA ***UDONGO***. KATIKA SIKU ZA MWISHO UFALME UTAGAWANYWA NJIA KUMI NA UTAKUWA DHAIFU.
DANIELI 2:31-33, 39-43



KISHA, EE MFALME, WEWE ULIONA JIWE LIMEKATWA KUTOKA KWA MLIMA, LAKINI *SIO* KWA MIKONO YA *MWANADAMU*. ILIBINGIRIKA CHINI YA MLIMA NA KUICHAPA PICHA KATIKA MIGUU NA KUHARIBU FALME *ZOTE* KATIKA WAKATI MDOGO.


MWAMBA HUO UNAWAKILISHA MWANA WA MUNGU ATAKAYEKUJA NA KUUFANYA UFALME KUA MTUKUFU.
MWISHO WA WAKATI, WAFU WOTE WATAAMSHWA NA KUSIMAMA KATIKA HUKUMU. WALIOTENDA MAOVU WATAPOKEA AIBU. WALIO TENDA MEMA WATAPOKEA UZIMA WA MILELE.


BILA SHAKA MANENO HAYO YAMETOKA KWA MUNGU. NI JINSI GANI INGINE AMBAYO NINGEWEZA KUYAJUA HAYA? NITAKUFANYA ***KIONGOZI WA WAZEE WENYE BUSARA.***
DANIELI ALIENDELEA KATIKA BABELI KWA MIAKA 68. ALITAFSIRI NDOTO NYINGI NA KUTABIRI SIKU ZIJAZO MARA NYINGI. KWA WAKATI, MFALME NEBUKADREZA ALIKUFA NA MWANAWE BELSHAZA ALICHUKUA NAFASI YAKE.

USIKU MMOJA BELSHAZA ALIPOKUWA NA SHEREHE YA WALEVI, MKONO WA AJABU ALITOKEA NA KUANDIKA KWENYE UKUTA. DANIELI ALIITWA KUTAFSIRI. MUNGU ALIMPA UFAHAMU YA LUGHA HII ISIYOJULIKANA




MHUBIRI 12:13-14; ISAYA 9:6-7, 45:1; DANIELI 2:34-35, 44-48, 5:1-29; UFUNUO 20:11-21:5
MANABII WALITABIRI KWAMBA ADUI HUYU ANGESHINDA BABELI KWA KUINGILIA MILANGO MIWILI AMBAYO MAJI YANAYORUHUSIWA KUINGIA MJINI. WABABELI WANGEKUWA WALEVI SANA KUTAMBUA. HISTORIA INAREKODI KUANGUKA KWA BABELI KWA NJIA HIYO HASA.


BAADA YA WAMEDE NA WAAJEMI KUSHINDA BABELI, DANIELI ALIGUNDUA KITABU CHA ZAMANI KILICHOANDIKWA NA NABII YEREMIA, MOJA YA VITABU VYA BIBLIA. ALIPOKUWA AKISOMA, ALISHTUKA ALIPOGUNDUA KWAMBA MUNGU ALIKUWA AMETABIRI MAPEMA KWAMBA UTUMWA WA BABELI UNGEDUMU KWA MIAKA 70 TU.
BAADAYE MBAKI ANGERUDI KWENDA YERUSALEMU NA KUJENGA UPYA KUTA NA HEKALU. AKISOMA ZAIDI, ALIGUNDUA KWAMBA MIAKA 200 MAPEMA NABII ISAYA ALIKUWA AMEANDIKA JINA LA MFALME WA UAJEMI AMBAYE ANGEWAONGOZA BAADAYE.


SASA IMEKUWA KARIBU MIAKA 69... NI **MWAKA MMOJA TU ULIOBAKI.** INASEMA KWAMBA KORESI NI MTUMISHI WA MUNGU, ANAYEFANYA MAPENZI YA MUNGU. ATAAMURU KWAMBA **TUTARUDI KATIKA NCHI YETU!** UMEBARIKIWA WEWE, EE BWANA WETU MUNGU, MFALME WA ULIMWENGU.


KAMA VILE MUNGU ALIVYOAHIDI IBRAHIMU, AMETUPA NCHI HII ILI TUIMILIKI MILELE. ALIWAONYA BABA ZETU KWAMBA TUNGEPELEKWA MIKONONI MWA MAADUI KAMA TUNGETUMIKIA MIUNGU MINGINE, LAKINI ALIAHIDI KAMWE HATASAHAU WATU WAKE. MUNGU AMELITUNZA NENO LAKE. SASA KWA KUWA TUMERUDI, LAZIMA TUMTII.
KORESI ALITOA WAYAHUDI MIAKA 70 BAADA YA UTUMWA WAO KUANZA, KAMA VILE MAANDIKO YALIYOTABIRIWA, NA 52,000 ALIRUDI KUJENGA UPYA MJI.



LAZIMA TUJIPANGE. TUTAJENGA UPYA ***KUTA KWANZA*** NA KISHA TUNAWEZA KUANZA ***HEKALU***.
EE BWANA MUNGU WA IBRAHIMU, UMETURUDISHA KAMA ULIVYO AHIDI. TUFUNZE KUTEMBEA KATIKA NJIA ZAKO.
NIMELETA MAJI SAFI. SASA TUANZE KAZI.
ISAYA 44:28; YEREMIA 25:11-12, 29:10; DANIELI 9:1-2


DANIELI ALIKUWA MZEE SANA, KWA HIVYO HAKURUDI NA WENGINE. BADO ALICHUKUA JUKUMU MUHIMU ALIPOKUWA AKIWASHAURI WAFALME WA MEDO-UAJEMI HIMAYA, SASA IKO KATIKA MJI WA BABELI. MUNGU ALIMPA MAONO ZAIDI KUHUSU SIKU ZIJAZO, HATA HADI MWISHO WA SIKU. KATIKA MOJA YA NDOTO ALIMWONA MNYAMA WA CHUMA. MALAIKA ALIMWAMBIA MAANA YAKE.




MUNGU ANAKUONYESHA KITAKACHOFANYIKA SIKU ZA MWISHO. ALIMFUNULIA NEBUKADREZA KUA KUTAKUA NA FALME ***NNE***. SASA KUMEKUWA NA MBILI. BAADA YA HIMAYA HII YA MEDO-UAJEMI ITAKUJA KIGIRIKI. ITASHINDA LAKINI ITAGAWANYIKA MARA NNE. WATAPIGANA MIONGONI MWA KISHA ZIBAKI FALME ***MBILI***. WATAPIGANA HADI UFALME WA NNE USHINDE. HII NDIYO TAFSIRI YA MNYAMA WA CHUMA ULIYEONA.


DANIELI 7:17-28; MATHAYO 24:4-25
UFALME WA NNE UTAKUWA KAMA CHUMA, **NGUVU ZAIDI** NA MKALI KULIKO FALME ZOTE ZA ZAMANI. UTAWASHINDA WOTE, LAKINI KATIKA SIKU ZA MWISHO UFALME HUU UTAGAWANYWA KATIKA MATAIFA KUMI. KISHA KUTATOKEA MTU AKIONGEA AMANI. YEYE NDIYE PEMBE YA MWISHO ITAKAYO MEA KICHWANI CHA MNYAMA. KATIKA SIKU ZA MWISHO, **ATADANGANYA NA KUAHIDI AMANI,** ILI KUSHINDA NA KUHARIBU. KISHA SIKU ITAWADIA **YA SHIDA KUBWA** DUNIANI KOTE, LAKINI WATU WEMA WATAOKOLEWA.


"DANIELI, MUNGU ANATAKA UJUE KILE KITAKACHOTOKEA NA WAKATI. TANGU WAKATI AMRI INAPOTOLEWA KUREJESHWA NA KUJENGA UPYA HEKALU, KUTAKUWA NA MIAKA 483, AMBAYO MASIHI ATAUAWA KWA KULIPIA DHAMBI ZA WATU, NA KISHA HEKALU LITAANGAMIZWA TENA.
HUU UNABII UTATIMIA, NA MASIHI ATATIWA MAFUTA. KUTAFANYIKA UPATANISHO WA DHAMBI, NA HAKI YA MILELE ITALETWA KWA MWANADAMU".




MWANZO 49:9-10; ZABURI 22, 53; ISAYA 7, 9:1-2, 42:1, 49:6, SURA YA 53; DANIELI 9:25-26; MICAH 5:2; ZAKARIA 9:9; MATHAYO 24:1-2; WAEBRANIA 2:9

MUNGU ALIMWAMBIA IBRAHIMU KWAMBA MKOMBOZI ANGETOKA KWENYE UZAO WAKE KUPITIA MWANAWE ISAKA.

MUNGU ALIMWAMBIA ISAKA KWAMBA YULE ALIYEAHIDIWA ATAKUJA KUPITIA MWANAWE YAKOBO, NA ALIMWAMBIA YAKOBO KWAMBA KRISTO ANGEKUJA KUPITIA YUDA.

UNABII MWINGI MAALUM WA MAISHA YA MKOMBOZI ALIYEAHIDIWA ULITOLEWA NA MUNGU KWA MANABII MBALIMBALI.

WALISEMA KWAMBA KAZI YAKE NA UWEPO UMETOKANA NA MILELE, KWAMBA ANGEZALIWA NA BIKIRA KATIKA MJI WA BETHLEHEMU YA YUDA, ANGEKUWA MNYENYEKEVU KATIKA KUONEKANA, NA KUWA CHINI NA KUENDESHA PUNDA.

BWANA ATAWEKA ROHO WAKE JUU YAKE, NAYE ATALETA HUKUMU KWA WAYUNANI.

YEYE ATAKUWA NURU KWA MATAIFA NA ATACHUKUA WOKOVU KWA WOTE WALIOKO DUNIANI.

ATAKUWA MASIHI MWENYE MATESO NA ATAKUA AKIKATALIWA NA WATU WAKE, NA KUFA AKIWA AMEDUNGWA MIKONO NA MIGUU YAKE.

ATANING'INIA UCHI NA ATAPATA KIU YA MAJI LAKINI ATAPEWA SIKI YA KUNYWA BADALA YAKE.

ATAKUFA BAINA YA WEZI NA KUZIKWA KATIKA KABURI LA MTU TAJIRI.

UTABIRI WA DANIELI KUHUSU FALME NNE ULITIMIA KAMA ALIVYOTABIRI. KATIKA MIAKA 330 KABLA YA KRISTO, ALEXANDA KUTOKA UGIRIKI ALIWEZA KUSHINDA DUNIA. UGIRIKI ULITAWALA HADI MIAKA 167 KABLA YA KRISTO KISHA NCHI YA UFALME WA NNE, ROMA ILIPOANZA KUTAWALA.

ROMA, ILIVYOWAKILISHWA KATIKA NDOTO YA NEBUKADREZA, KAMA MIGUU YA CHUMA, NA KWA NDOTO YA DANIELI KAMA MNYAMA WA CHUMA ILIONGEZA NGUVU ZAKE, KAMA VILE MANABII WALITABIRI. MIAKA 5 KABLA YA KRISTO, ROMA ILITAWALA ISRAELI KWA MKONO WA CHUMA.

***IZAIDI YA MIAKA*** MIA TANO ILIKUWA IMEPITA TANGU UNABII WA DANIELI. KATIKA MWAKA 6 B.C WARUMI WALIWARUHUSU WAYAHUDI UHURU WA DINI LAKINI WALIWATOZA KODI SANA. HEKALU LILIKUWA LIMEJENGWA UPYA NA ILIKUWA KATIKATI YA MAISHA YA KIYAHUDI. WENGI WALIKUWA WAMESAHAU UNABII WA MASIHI ANAYEKUJA, LAKINI WENGINE BADO WALIITUNZA SHERIA NA KUTAFUTA KRISTO. MIONGONI MWAO ALIKUWA MZEE AITWAYE SIMEONI. ALIKUWA MTU MTAKATIFU AMBAYE ALITAMANI KUMWONA MMOJA WA MANABII WAKIZUNGUMZA. KWA MIAKA MINGI ALIKUWA AMESOMA UNABII NA KUJUA KWAMBA WAKATI ULIKUWA UNAKARIBIA. LAKINI SASA ALIKUWA MZEE NA LABDA HANGEISHI KWA MUDA MREFU ZAIDI. ILIKUWA MIAKA 4,000 TANGU MUNGU KUMWAHIDI EVA KWAMBA UZAO WAKE UTAKUJA NA KUHARIBU MATENDO YA YULE MWOVU.

***ILIKUWA WAKATI SASA***. ZAIDI YA UNABII 350 ULIKUWA TAYARI KUTIMIZWA.



SURA YA 8

# AGANO JIPYA



MAIKA 6 KABLA YA KRISTO
EH MUNGU WA IBRAHIMU, ISAKA NA YAKOBO, NIMEMGOJA MKOMBOZI LAKINI SITAISHI KWA MIAKA MINGI.
KWA KWELI HAUTAISHI SANA, ILA UTAMUONA MKOMBOZI.


SIMEONI ALITAFUTA MAANDIKO NA KUPATA UTABIRI MWINGI KUHUSU KRISTO.
SIMEONI, WEWE HUJA HUMU *KILA SIKU*. NATAMANI MAKUHANI WOTE ***WANGEJITOLEA*** KAMA WEWE
MAONI YAKO KULINGANA NA UTABIRI HUU WA ISAYA KUHUSU MKOMBOZI NI YAPI? INASEMA ***BIKIRA*** ATAJIFUNGUA MTOTO. LAZIMA IWE NI MBEGU YA ***MWANAMKE,*** KAMA HAWA ALIVYOELEZWA.
NDIO. NA ISAYA PIA ALISEMA KUA ATAITWA ***MUNGU MKUU.*** ILA UTABIRI *HUU NI NGUMU* KUELEWA.


KULINGANA NA MIKA 5:2 MWANA HUYU ATAISHI MILELE, KAMA MUNGU. JE KUHUSU UTABIRI WA ZABURI 45:6 AMBAPO MUNGU HUITA MWANAWE MUNGU?
WACHACHE WATAKUBALIANA NA WEWE, NDIO MAANA HUFAI KUYAONGEA MAMBO HAYA KWA UWAZI. UTAANGAMIZWA KWA KUPIGWA MAWE.
MTAONA KABLA NIAGE DUNIA, MASIHI ATAKUJA KWENYE HEKALU HILI NA MTAMUONA.


ANAWEZA KUA ANAZUNGUMZA *UKWELI*.
NA WEWE *NANI*? UNAJUAJE MAMBO HAYA?


NIMEPATA TU KUSIKILIZA MAZUNGUMZO YENU. MI PIA NLIYASOMA MAANDIKO NA MIAKA 500 ILIYOPITA DANIELI ALIKUWA NA MENGI YA KUSEMA KUHUSU SIKU HIZI ZA UJIO WA MASIHI.
NI YAPI AMBAYO WE WAJUA NA MAKUHANI HAWAJUI?
MWANZO 3:15, ZABURI 45:6, ISAYA 7:14, 9:6; DANILEI 9:25-26, MIKA 5:2, LUKA 2:25-26.


BABANGU NI KUHANI NA AMENIONYESHA UTABIRI HUU. MUNGU ALIMWELEZA DANIELI YA KUA INGEKUA NI MIAKA 483 KATI YA WAKATI AMBAPO YERUSALEMU INGEJENGWA UPYA NA KIFO CHA MASIHI.
IMEKUWA SASA MIAKA 449 TANGU YA HAYO. INA MAANA KUA TUMEBAKISHA MIAKA 34, KUMAANISHA MASIHI ANAWEZA KUA AKITEMBEA MTAA HUU ATA SASA HIVI.
LA HASHA. ROHO MTAKATIFU ALINIFUNULIA KWAMBA NTAMUONA MTOTO MASIHI NDANI YA IKULU HILI.
UNAJUAJE MAMBO HAYA?
MTAONA.

SIMEONI
ALIPOZEEKA
NA ALIPOKUWA
AKINGOJA HEKALUNI,
AKIMNGOJA MASIHI.
KUHANI KWA JINA
ZAKARIA ALIKWENDA
HEKALUNI KUSALI.
YEYE NA MKEWE
WALIKUWA WAZEE ILA
HAWAKUA NA WATOTO.


GHAFLA MALAIKA AKATOKEA UPANDE WA KULIA WA MADHABAHU.
USIOGOPE. SALA YAKO IMEPOKELEWA NA WEWE PAMOJA NA MKEWE ELIZABETI MTAPATA MTOTO WA KIUME NA MTAMWITA YOHANA.
WENGI WATAFURAHI WAKATI ATAZALIWA, KWA SABABU YEYE NDIYE ATAKAYEWAANDAA WATU KWA UJIO WAKE MASIHI. HATAKUNYWA DIVAI AU KILEO NA YEYE ATAPOKEA ROHO NA NGUVU YA ELIYA.


NITAJUAJE KUA UNAYOYASEMA **NI KWELI?** MIMI NA MKE WANGU TUMEZEEKA KUPATA WATOTO NA MKE WANGU AMEKUWA TASA MIAKA YAKE YOTE.
MIMI NI **GABRIELI,** NA HUSIMAMA MBELE YA UWEPO WA MUNGU, NA NILITUMWA KUWAELEZA MAMBO HAYA. MWATAKA ISHARA? BASI WEWE UTAKUA **BUBU** HADI SIKU AMBAYO MAMBO HAYA YATATIMIA.


NITAFURAHIA SIKU AMBAYO TUTAZUNGUMZIA MANENO HAYA. NYUMBA HII IMEKUWA KIMYA SANA. WAJUA HUFAI KUBISHANA NA *MALAIKA*.
ZAKARIA, BADO NI VIGUMU KUAMINI. KAMA SARA, MAMA WA TAIFA LETU, MUNGU ALISIKIA MAOMBI YETU, NA SASA NITAKUWA MAMA WA *NABII MKUU*.

KWA MIAKA 4,000 MANABII WALITABIRI UJIO WA MASIHI. MIAKA 700 MBELENI NABII ISAYA ALISEMA “BIKIRA ATAPATA MIMBA NA KUMZAA MTOTO WA KIUME,NAYE ATAITWA EMANUELI, MUNGU PAMOJA NASI.”




MARIAMU ALIKUWA AMEUNGANISHWA NA YUSUFU ILI WAOANE. HAKUWAI KUA NA UHUSIANO WOWOTE WA KIMAPENZI NA MTU YOYOTE. ALIZITII SHERIA NA AMRI ZOTE ZA MUSA.


GHAAFLA MALAIKA AKAMTOKEA!
MARIAMU UMEPATA **NEEMA KUBWA** MBELE ZA BWANA. UTAPATA MIMBA NA UTAMZAA MWANA WA MUNGU.
HAYO YOTE YATAFANYIKAJE NA MIMI SIJAWAI KUA NA UHUSIANO WOWOTE WA KIMAPENZI NA MTU YEYOTE?
ROHO MTAKATIFU WA MUNGU ATAKUONGOZA. MTOTO UTAKAYEBEBA NI MWANA WA MUNGU. BINAMU YAKO ELIZABETI ALIYEITWA *TASA SASA* ANA MIMBA. NA SASA AKO KATIKA MWEZI WA SITA.

ISAYA 7:14, LUKA 1:5-20, 26-40




I ELIZABETI!
MARIAMU, MWANANGU!


*UMEBARIKIWA* KULIKO WANAWAKE WOTE, NA UZAO WA TUMBO LAKO *UMEBARIKIWA*. MIMI NI NANI IWE MAMA WA BWANA WANGU AJE KUNITEMBELEA? KWANI PINDI NILIPOSIKIA SAUTI YAKO, MTOTO NDANI YANGU AMERUKA KWA FURAHA.
NAFSI YANGU INAKUTUKUZA MUNGU, NA ROHO YANGU IMEFURAHI KWA MUNGU MWOKOZI. BAADA YA HAYA, VIZAZI VYOTE VITANIITA MWENYE HERI, KWA SABABU AMETENDA MAKUU.
AMETUTUKUZA WALE WOTE AMBAO NI WA ASILI YA CHINI. KAMA ALIVYOONGEA NA BABA IBRAHIMU, AMETUKUMBUKA KWA *REHEMA*.
MARIAMU ALIKAA NA ELIZABETI KWA TAKRIBANI MIEZI MITATU.


WAKATI ULIKUJA WA ELIZABETI KUJIFUNGUA.
ZAKARIA ANA UHAKIKA ATAKUWA MVULANA; ANASEMA *MALAIKA* ALIMWAMBIA HIVYO.
BASI IKIWA NI MVULANA NADHANI JINA LAKE LITAKUWA ZAKARIA BAADA YA BABA YAKE.
NDIO HUYU ANAKUJA. EBU TUMUULIZE YEYE.



ALISEMA KUWA MALAIKA ALIMFANYA BUBU KWA SABABU HAKUAMINI.
UTAMUITAJE MTOTO?
ANATAKA KIBAO CHA KUANDIKIA.


ANASEMA ATAITWA *YOHANA,* KAMA MALAIKA ALIVYOSEMA.
LAKINI HAKUNA MOJA KATIKA FAMILIA KWA JINA LA YOHANA.


KWA HAKIKA NI *MVULANA*. NA ANA NYWELE KWA WINGI.


JINA LAKE NI YOHANA, KULINGANA NA NENO LA BWANA. ATAMTAMBULISHA MASIHI KWA WATU WA ISRAELI.
ANAONGEA! BAADA YA MIEZI HIYO YOTE SASA ANAONGEA!
INAWEZA KUA KWA HAKIKA YA KWAMBA HUYU NI ELIYA WA UNABII?
LUKA 1:41-64



WAKATI HUO HUO, YUSUFU ALIGUNDUA KWAMBA MARIAMU ALIKUWA MJAMZITO, NA ALIJUA HAIKUWA MTOTO WAKE.
MAMA BADO SIWEZI ***KUIAMINI***. HAJAKUWA NA WANAUME NA AMEKUWA KWENYE UWEPO WA JAMII YETU KILA DAKIKA. NA KILA MTU ANAJUA JINSI MARIAMU NI MSICHANA MWENYE HESHIMA. ***SIKUFANYA CHOCHOTE*** LAKINI NI KWELI NI MJAMZITO.


EH YUSUFU, UTAFANYA NINI SASA?
SIWEZI KUMUOA KWA SASA, ILA SITAKI WATU WAJUE. ANAWEZA *KUPIGWA MAWE* KWA *KUZINI.* LABDA TUTUPILIE MBALI USHIRIKIANO WETU BILA YA WATU KUJUA.


ANASEMA NANI NDIYE BABA?
ANASEMA BABA WA MTOTO NI *MUNGU*, NA ALIPANDIKIZWA NDANI YAKE NA ROHO MTAKATIFU BILA UHUSIANO WOWOTE WA KIMWILI.


OH! AMEPOTEZA AKILI?
ANASEMA MTOTO ATAKUWA MWOKOZI WA ULIMWENGU, MWANA WA MUNGU.
HICHOO NI KITU CHA KUFUKURU KWA MWANAMKE KAMA HUYO KUSEMA. LAZIMA NIMWEKE MBALI NA KWA UTULIVU KWA HARAKA IWEZEKANAVYO.


JIONI HIYO KAMA YUSUFU ALIPOKUWA AMELALA, MALAIKA ALIMTOKEA.
YUSUFU, WEWE MWANA WA DAUDI, USIFANYE HOFU YA KUMCHUKUA MARIAMU KAMA MKE WAKO, KWANI MTOTO ALIYE NDANI YAKE NI KWA UWEZO WA ROHO MTAKATIFU. ATAJIFUNGUA MTOTO WA KIUME NA UTALIITA JINA LAKE *YESU,* KWA MAANA ATAOKOA WATU WAKE KUTOKA DHAMBI ZAO.


HUU NDIO UTIMILIFU WA UNABII WA ISAYA: “BIKIRA ATAKUWA NA MTOTO NA KUZAA MWANA AMBAYE ATAITWA EMANUELI, AMBAYO KUTAFSIRIWA NI MUNGU PAMOJA NASI.’”


MARIAMU, UTAWEZA KUNISAMEHE KWA KUTOKUAMINI?
NAJUA, YOTE NI YA AJABU SANA. WANAWAKE WOTE WA ISRAELI NA WA KARNE NYINGI, KWAMBA MUNGU ANICHAGUE KWA KULETA MASIHI KATIKA ULIMWENGU!


MTOTO ATAKUWAJE? KWA KUWA ATAKUWA ***MUNGU*** KATIKA ***MWILI,*** ATAWEZA KUONGEA WAKATI ANAZALIWA? JE, TAYARI ATAJUA JINSI YA ***KUSOMA?***
EE, YUSUFU, SIJUI NA MWENYEZI MUNGU NI MJUZI, MWENYE KUJUA. TUTASUBIRI ILI TUWEZE KUJUA.


MWANZO 3:15; ISAYA 7:14, 9:7; MATHAYO 1:18-23; LUKA 1:32-33
SISI SOTE NI WA UKOO WA DAUDI, NA MANABII WALISEMA KWAMBA MASIHI ANGEKUWA YA UZAO WA DAUDI.
NILIFIKIRIA TU KITU KINGINE. KATIKA BUSTANI YA EDENI, MUNGU ALIAHIDI KWAMBA UZAO WA MWANAMKE ANGEMPONDA KICHWA CHA MBEGU YA NYOKA. NINAONA SASA! MTOTO HUYU HATAKUWA MBEGU YA MWANAUME, TU MBEGU YA MWANAMKE. MUNGU AMEKUWA NA MPANGO HUU TANGU MWANZO.


YUSUFU NA MARIAMU WALIISHI NAZARETI YA GALILAYA, LAKINI KULIKUWA NA UNABII WA ZAMANI KWAMBA MASIHI ATAZALIWA KATIKA BETHLEHEMU YA YUDEA (MICAH 5:2). SANA HIVI KARIBUNI, MARIAMU ANGEKUWA ANAMZAA MTOTO WAKE KATIKA MJI ULIO KUWA MBAYA. HAKIKA HAO WALIKUWA WATU WAPOTOVU. NA HAKUKUWA NA SABABU YA KUFANYA SAFARI NDEFU KWENDA BETHLEHEMU.
*SIKILIZENI, SIKILIZENI*, KWA TANGAZO RASMI KUTOKA ROMA, ILIYOSAINIWA NA KAISARI MWENYEWE HESABU *ITACH*UKULIWA NA WATU WOTE WA ISRAELI WATARUDI KWA MJI WA KUZALIWA KWAO KUJIANDIKISHA KWA AJILI YA USHURU.


YUSUFU
HIYO INAMAANISHA WEWE UTALAZIMIKA KWENDA BETHLEHEMU. HUTAKUEKO MTOTO ATAKAPOZALIWA.
WATU
HAWATAELEWA NIKIONDOKA HIVYO NTAONDOKA PAMOJA NA WEWE.


MARIAMU NISINGEKULETA KWENYE SAFARI HII. AMA TUGEUKE TU TURUDI.
*LA!* LAZIMA NIWE NAWE NITAKAPOMPATA MTOTO. WEWE NDIWE UNAYENIELEWA.


LAZIMA TUHARAKISHE KAMA ITAWEZEKANA. NADHANI WAKATI UMEFIKA.
ILICHUKUA ZAIDI YA WIKI MOJA KUFANYA SAFARI YA KARIBU MAILI 100.
NITAONA KAMA TUNAWEZA KUPATA CHUMBA.


MARIAMU, NIMEMPATA MKUNGA ATAKAYE TUSAIDIA.
HAKUNA CHUMBA HUKO?
LA. IMEJAA.


UMEFANYA VYEMA KWA MTOTO WAKO WA KWANZA. NI JAMBO LA HURUMA KUA AMEZALIWA KWA ZIZI LA **NGOMBE**.
USITATIZWE NA HILI KWANI SIKU MOJA ***ATATAWALA ULIMWENGU.***
NAAM, ANAONEKANA KAMA MTOTO WA KAWAIDA KWANGU.

LUKA 2:1–7


NI MALAIKA!
MAELFU YA MALAIKA.
MSIWE NA HOFU. MUNGU AMENITUMA KUWALETEA WATU WOTE HABARI NJEMA. SIKU YA LEO KATIKA MJI WA DAUDI AMEZALIWA *MWOKOZI* WA WA KIYAHUDI.
UTUKUFU KWA MUNGU JUU MBINGUNI. MUNGU HULETA AMANI ULIMWENGUNI SABABU ANA NIA NJEMA NA WATU WAKE.


KUTAKUA NA ISHARA, MTAPATA MTOTO AMEFUNIKWA KWA VITAMBAA NA ATAKUA AMELAZWA KWENYE ZIZI LA NGOMBE.


MNAAMINI, MALAIKA ***WAMETUTOKEZEA!***
NANGOJA KUMUELEZA MKE WANGU!
ULISIKIA ALISEMA NINI? ***MASIHI*** AMEZALIWA KATIKA ISRAELI.
NINATAKA KWENDA NIONE.
***MWOKOZI! AMANI KUELEKEA KWA WATU!*** MTOTO? ***HEBU TWENDE TUKAMUONE.***


MASIHI!
POLE KWA KUWASUMBUA ILA MALAIKA ALITUALIKA TUJE.
NANI ANGEWEZA KUFIKIRIA, *MUNGU* ANAKUWA *MTOTO?*
LUKA 2:8-20


WAKATI ULIFIKA KWA MARIAMU NA YUSUFU KUWASILISHA MTOTO MZALIWA KWA KUHANI NA KUTOA DHABIHU ZILIZOAMBATANISHWA NA SHERIA.
YUSUFU, HII ITAKUA MARA YAKE YA KWANZA KUJA HEKALUNI, NA HAKUNA ANAYEJUA KWAMBA YESU NI KRISTO.
NA SIDHANI KAMA TUNAPASWA KUMWAMBIA MTU YEYOTE. TUSUBIRI MPAKA YEYE AWE MKUBWA.


SIMEONI ALIKUWA HEKALUNI.
NI NANI, MARIAMU?
SIJUI. HAKUNA ANAYETUJUA HUKU.
YUKO HAPO! TUMESUBIRI KWA SANA.


UMEBARIKIWA WEWE, EE BWANA WETU MUNGU. SASA NAWEZA KUFA KWA AMANI, KWANI MIMI NIMEUONA WOKOVU WAKO, KAMA VILE ULIAHIDI. ATAKUWA NURU KWA MATAIFA PAMOJA NA UTUKUFU WA ISRAELI.
ULIJUAJE?


NISIKILIZENI, HUYU MTOTO ATASABABISHA WENGI KATIKA ISRAELI *KUPANDA* NA BAADHI *KUANGUKA,* NA YEYE ATAPINGWA.
NDIYO, NA MOYO WAKO UTAVUNJIKA KWA YALE UTAKAYOSHUHUDIA.


ANGALIA! MASIHI. AMEKUJA HEKALUNI. KAMA VILE MANABII WALIVYOSEMA.
HUYO NDIYE ANNA. YEYE AMEKUWA AKIMNGOJA MASIHI KWA SANA.


KIJANA, MTOTO HUYU NI ***KRISTO***, MWOKOZI WA ULIMWENGU. ATAOKOA ISRAELI KUTOKANA DHAMBI ZAO.
KUANZIA HATUA HIYO, ANNA ALIONGEA KUMHUSU KWA WOTE WALIOTAFUTA UKOMBOZI.

LUKA 2:27-38


KATIKA NCHI ZA MASHARIKI YA ISRAELI KULIKUWA NA WATU WENYE HEKIMA AMBAO WALISOMA ZAMANI MAANDISHI NA KUTAFUTWA KUJUA KUHUSU MUNGU. WALIJUA KUHUSU UNABII WA KUJA KWA MASIHI. KATIKA NDOTO NA MAONO, MUNGU ALIWAPA MAWAIDHA KUHUSU MASIHI.KISHA WALIGUNDUA NYOTA ISIYO YA KAWAIDA AMBAYO ILIASHIRIA TAIFA LA ISRAELI.
TUMEFIKA MBALI. HII NI NCHI YA AJABU TUNAKWENDA. TUMEKUA TUKISAFIRI KWA WIKI NYINGI.
NYOTA INAZIDI KUSONGA, TUTAIFWATA HADI MWISHO.


MFALME HERODE, KUNA WATU WATATU MATAJIRI SANA KUTOKA MASHARIKI YA MBALI. WAO WANASEMA WANAMTAFUTA MFALME MPYA WA ISRAELI, MTOTO MCHANGA.
ISRAELI HAIKUWA NA MFALME WAKATI HUO KWA SABABU RUMI ALIWATAWALA, LAKINI MFALME ALIYETEULIWA NA KIRUMI WA WAYAHUDI, HERODE, ALITAWALA YERUSALEMU. WATU WENYE HEKIMA WALIMTAFUTA HERODE ILI KUMUULIZA KUHUSU MFALME MZALIWA.
MTOTO? MFALME? MIMI NDIYE MFALME. WAKARIBISHE KISHA ULETE MAKUHANI WAKUU NA WAANDISHI KWANGU


MMESEMA MMEKUJA KUMUONA MTOTO MFALME? MLIJUAJE MAMBO HAYA?
TULIONA NYOTA YAKE MASHARIKI NA TUMEKUJA KUMUABUDU.
YUKO WAPI?
HATUJUI VYEMA NDIO *MAANA* TUMEKUJA KUULIZA.
NIMEWAITA WASOMI ILI KUFANYA UTAFITI. NJOONI NAMI KWA CHUMBA MAALUM.


WANASEMA WAMEKUJA KUABUDU MFALME WA WAYAHUDI, AMBAYE ALITABIRIWA KUJA NA KUWAOKOA WAPOTOVU. KUNA MAANDISHI YOYOTE INAYOSEMA KUHUSU *MFALME?*
NDIYO, MANABII WENGI WALISIMULIA KUHUSU KUJA KWAKE, LAKINI SISI HATUAMINI KWAMBA UNABII KAMA HUO UNAPASWA KUCHUKULIWA KWA *UHALISI*.
SINA HAJA NA MNAVYOELEWA. UNABII UNASEMAJE?
NABII MIKA ALISEMA KWAMBA MASIHI ANGEZALIWA KATIKA *BETHLEHEMU* KUTOKA KABILA LA *YUDA*.

MATHAYO 2: 1-8; MIKA 5:2




HERODE ALIKUWA NA HOFU YA MFALME ALIYEZALIWA HIVYO ALITAKA KUMUUA PINDI ALIPOJUA ALIKO.


ILISTAABISHA JINSI WASOMI WALIJUA KUHUSU UNABII LAKINI HAWAKUKUBALIANA NA MANABII.
MAANDIKO YA MANABII WA ISRAELI HAYAKUA KAMA MENGINE. SIJAWAI KUONA UTABIRI KAMA HUU.


ANGALIA! NYOTA KAMA TULIYO ONA MASHARIKI.
NA WALA HAIFANANI NA NYOTA ZINGINE. INANGAAA KWA MWANGAZA MKUBWA ZAIDI.
TIA ALAMA NAFASI YAKE NA KESHO TUTAIFWATA.


HUKO, INASIMAMA JUU YA NYUMBA HIYO. LAKINI HUKU SI *BETHLEHEMU!* IMEKUWA WIKI NYINGI. LABDA WAO WAMEHAMA.
IMEKUWA SAFARI NDEFU SANA, LAKINI TUKO KARIBU KUFIKA.
NI NYOTA YA *AJABU* KWA HAKIKA. HAIWEZI KUA JUU WA MAWINGU.


HATUTAKI KUKUSUMBUA, LAKINI TUMESAFIRI *WIKI NYINGI* KUONA NA KUABUDU MFALME MZALIWA.
MLIJUAJE?
TUMESOMA MAANDIKO MATAKATIFU YA WATU WOTE. MANABII WAKO WAMETABIRI KUJA KWAKE, NA KISHA NYOTA ILITUELEKEZA SISI HAPA. INASIMAMA JUU YA NYUMBA YAKO HATA SASA.



KWA UNYENYEKEVU SISI TUNATOA ZAWADI HIZI KWA HESHIMA YA MWOKOZI WA ULIMWENGU. ATAWAGEUZA ***WENGI KWENYE HAKI.***
USIKU HUO, MUNGU ALIZUNGUMZA NA WATU WENYE HEKIMA KATIKA NDOTO NA KUWAAMBIA WASISIMULIE HERODE AMBAPO WALIMPATA MTOTO, LAKINI KUCHUKUA NJIA NYINGINE YA KURUDI KWENYE NCHI. MUNGU PIA ALIZUNGUMZA NA YUSUFU AKAMWAMBIA AKIMBILIE MISRI, KWANI HERODE ANGETAKA KUMUUA MTOTO.
MATHAYO 2: 9-12


WATU HAO KUTOKA MASHARIKI ***WALINILAGHAI***. WALICHUKUA NJIA NYINGINE NYUMBANI. HIVYO INAMAANISHA KUWA WALIPATA MTOTO NA WAKAOGOPA KURUDI HIVI.
TUMA KIKOSI CHANGU MAALUM BETHLEHEMU. WAAMBIE ***WAUE KILA MTOTO WA KIUME*** CHINI YA MIAKA MIWILI.


MIAKA MINGI KABLA, MANABII WALITABIRI TUKIO HILI LA HUZUNI LINGETOKE KATIKA BETHLEHEMU.


YUSUFU NA MARIAMU WALIMCHUKUA MTOTO YESU KWENDA MISRI. ZAWADI ZA WATU WENYE HEKIMA ZILIWAWEZESHA KUSAFIRI NA KUISHI MIAKA MIWILI HUKO MISRI.
BAADA YA HERODE KUFA, WAKATI YESU ALIKUWA NA UMRI WA MIAKA MIWILI, MUNGU ALIWAAMURU WARUDI ISRAELI. HII PIA, ILIKUWA KATIKA KUTIMIZA UNABII WA BIBLIA: "NILIITA MWANANGU KUTOKA MISRI."


WALIPORUDI KUTOA MISRI MALAIKA ALIMWAMBIA YUSUFU WAHAMIE KATIKA MJI MDOGO WA NAZARETI.
HII ILIKUA PIA UTIMILIFU WA UNABII ULIOSEMA KUA YESU ANGEITWA MNAZARETI.
WANAUME WANGU TANO WATAFANYA KAZI SIKU YOTE? NJOONI MLE.
YESU ALIFANYA KAZI NA BABA YAKE WA KAMBO YUSUFU KATIKA DUKA LAKE LA USEREMALA. ALIKU KATIKA MWILI NA ROHO, NA AKAWA NA HEKIMA SANA.
YEREMIA 31:15; HOSEA 11:1; MATHAYO 2:13-23


YESU ALIPOKUWA MIAKA KUMI NA MIWILI, YUSUFU ALIICHUKUA FAMILIA YAKE NA KWENDA YERUSALEMU KUSHEREHEKEA PASAKA. WALIBEBA MWANAKONDOO WAO KAMA SADAKA KWA AJILI YA DHAMBI ZAO.
BABA, NAWEZA KUENDA NA YESU KULIONA *HEKALU?*
YESU, UNAWEZA KUWAPELEKEA MAKUHANI MWANA KONDOO. LAZIMA IIDHINISHWE KABLA YA DHABIHU KESHO. TUTATAFUTA MAHALI TUPIGE KAMBI USIKU HUU.


SIKU KADHAA BAADA YA DHABIHU...
YUSUFU, SIMUONI YESU. HAKUNA ALIYEMUONA SIKU YOTE.
LAKINI ALIJUA TUNAONDOKA. NLIDHANI ATAKUA NA WANAFAMILIA WETU.
PENGINE TULIMUACHA YERUSALEMU
ITATUBIDI TURUDI ILI KUMTAFUTA.


NYOTE MNAKUBALIANA KWAMBA MASIHI ATAKUWA ***MWANA WA DAUDI,*** KAMA WALIVYOSEMA MANABII. NYINYI PIA MNNAKUBALIANA KWAMBA DAUDI ALIMWITA BWANA, KANA KWAMBA MASIHI ALIKUWA MUNGU WAKE.
LAZIMA UWE ***MAKINI*** NA UNAYOSEMA ILI ***USIMKUFURU*** MUNGU.
LAKINI WEWE UNADHANI UFAFANUZI WAKO NI SAHIHI. ***WAZEE*** NI BORA ZAIDI KWA KUELEWA MAMBO HAYA ***KWA KINA.***


ISAYA 9:7; LUKA 2:42-46; 2 TIMOTHEO 3:16-17
MAANDIKO INAWEZA KUA YA KWELI AMA UONGO. SISI TUNAAMINI TU YANAYOAMBATANA NA MILA ZETU?
NDIO YULE PALE!
*UKWELI* UMEWAHI KUA KINA? SI TUMEPEWA MAANDIKO ILI TUELEWE?
LAKINI HUWEZI KUCHUKUA KILA KITU HALISI KAMA RABI ZETU WANAVYOSEMA ...


YESU TUMEKUA TUKIKUTAFUTA. *MBONA UMETUFANYIA HIVI?*
AMEKUWA NASI KWA SIKU MBILI. MNA MTOTO WA *KIPEKEE SANA.*


MBONA MLINITAFUTA *KILA MAHALI?* HAMKUJUA MIMI NLIKUA KWA NYUMBA YA BABA YANGU?


SIJAWAI KUMUONA MTOTO MDOGO ANAYEJUA MAANDIKO KAMA YEYE.
ALIMAANISHA *VIPI* *ATI AKO KWENYE NYUMBA YA BABA YAKE?* SI NI ***BABA*** YAKE ALIKUWA AKIMTAFUTA?


YESU ALIREJEA NA WAZAZI WAKE NA ALIWAHESHIMU. ALIENDELEA KUFANYA KAZI NA BABAKE NA ALIKUA NA KUWA MTU MWENYE BUSARA.
KWA SABABU ALITEMBEA KWA WEMA NA KUWATENDEA WENGINE MEMA ALIPENDWA NA WENGI.


VIJANA WENGI WALIPOTENDA DHAMBI, YESU ALITII AMRI ZA MUNGU.
SIKU ZOTE WEWE ***NI MZURI KWANGU,*** NA WALA HAKUNA SEREMALA ***MZURI ZAIDI YAKO*** NAZARETI YOTE KUKULIKO, NITACHUKUA SITA KAMA HIZI.
LUKA 2: 46-52


ELIZABETI ALIKUWA AMEJIFUNGUA MTOTO WA KIUME MIEZI SITA KABLA YA MARIAMU. MALAIKA ALIMWAMBIA ZAKARIA AMUITE MTOTO YOHANA NA KUWA ANGEKUJA KUTAYARISHIA MASIHI NJIA. HII ILIKUA IMETABIRIWA MIAKA 500 ILIYOPITA NA BAADHI YA MANABII.
LAZIMA MUACHE ***DHAMBI*** NA ***MUMFUATE MUNGU*** KWA SABABU UFALME WA MUNGU UPO KARIBU KUJA. MKITAYARISHA NYOYO ZENU KUMKARIBISHA MASIHI MIMI NITAWABATIZA KWA MAJI.


ILA KUNA MMOJA ATAKAYEKUJA BAADA YANGU NAYE ATAWABATIZA KWA ROHO MTAKATIFU WA MUNGU. WACHENI DHAMBI.
TUFANYEJE YOHANA? TUNAHITAJIKA KUFANYA NINI?


IWAPO UNA KOTI MBILI BASI MUAZIME MOJA ASIYE NA KOTI. IKIWA UNA CHAKULA BASI WALISHE WENYE NJAA.
WAFANYIE HAKI WATU WOTE.


YOHANA, SISI TUNAOFANYA KAZI NA SERIALI TUFANYEJE? MIMI NI MTOZA USHURU.
USICHUKUE HONGO NA PIA USITUMIE PESA ZA OFISINI KUITISHA ZINGINE KWA WATU.


MIMI SI MTU WA KWENU WALA SIFWATI *DINI YENU.* NIFANYEJE ***KUMFURAHISHA MUNGU?***
USIWE NA ***HASIRA*** KWA UNAOWASIMAMIA. PIA USITUMIE CHEO CHAKO ***KUIBA*** AU KUCHUKUA HONGO. TOSHEKA NA MSHAHARA WAKO.





MALAKI 3:1; LUKA 3:2-18, 7:24, 27


MIMI NI SIO MASIHI.
***WEWE NI NANI,*** KWAMBA UNAKUJA KUTANGAZA MASIHI? UNASEMAJE KUJIHUSU?
HAPANA, KAMA NABII ISAYA ALISEMA, "***MIMI*** NI SAUTI YA MMOJA ANAYELIA NYIKANI, ANDAENI NJIA KWA AJILI YA MASIHI."
WEWE NI NABII AMBAYE ***MUSA*** ALIZUNGUMZIA, YULE AMBAYE ALIKUWA AJE KUREJESHA WATU KWA MUNGU?


BASI UNA HAKI GANI YA *KUWABATIZA* WATU?
MIMI NI MTUMWA TU, NATAYARISHIA MASIHI NJIA. ILA NYINYI MNAFIKIRI SABABU NYINYI NI WAYAHUDI, NYINYI NI WANA WA MUNGU.
MNAHITAJI KUACHA KIBURI KWANI NI *DHAMBI*. MTAANGAMIA KWA MOTO MSIPOBADILISHA MIOYO YENU.


YOHANA, UNASEMA MASIHI ANAKUJA. TUTAJUAJE HILO?
MALAIKA WA MUNGU ALINIELEZA YULE NITAKAYEONA ROHO WA MUNGU ***AKIMSHUKIA KAMA NJIWA NDIYE MASIHI*** WA ISRAELI, MKOMBOZI WA ULIMWENGU.


YOHANA ALIKUWA AMEHUBIRI KWA MIEZI SITA NA YESU ALIKUWA NA MIAKA THELATHINI.
NILIJUA WAKATI HUU UMEFIKA. MALAIKA ***GABRIELI*** ALINIELEZA KUWA NINGEPITIA HUZUNI MINGI. NATAMANI BABA YAKO ANGEKUA KUSHUHUDIA HAYA.
UTAFANYAJE? UTAANZAJE? UTAENDA ***HEKALUNI?***
SIJUI. BABA YANGU ATANIONGOZA. LAZIMA NIKAMUONE YOHANA ILI ***ANIBATIZE***.


UTAREJEA NYUMBANI KUNIONA?
KUMBUKUMBU LA TORATI 18:15, ISAYA 40:3; MATHAYO 3: 1-12; LUKA 3:15-18, 23; 172 YOHANA 1:19-27, 33
NDIYO MAMA. SIWEZI KUKUACHA ILA LAZIMA UJITIE NGUVU. MAMBO YATANIFANYIKIA AMBAYO HAYATAKUWA RAHISI KWAKO.


JIANDAENI KWA UJIO WA *MASIHI*. NINYI AKINA BABA LAZIMA MGEUZE MIOYO YENU KWA WATOTO WENU. LAZIMA MUWE NA HEKIMA NA KUJITOLEA MUDA WENU NA NGUVU KUWAFUNDISHA SHERIA ZA MUNGU. IWAPO WATOTO WENU WASIOTII WATAONA UHALISIA WENU, NDIPO NDIPO MIOYO YAO ITAGEUKA NA FAMILIA *ZENU ZITAPONA*.
KAMA HUU NDIO MOYO WAKO, NA UKO TAYARI KUFUATA MASIHI, NJOO CHINI MAJINI NA MIMI NITAKUBATIZA KWA UBATIZO WA TOBA, NA WAKATI MASIHI ATAKUJA *ATASAMEHE DHAMBI ZAKO*.


YOHANA, UTANIBATIZA?
INGEKUA SAHIHI KAMA NI *WEWE* UNGENIBATIZA. HAKIKA WEWE NI *MWENYE HAKI*
YOHANA, LAZIMA NITII SHERIA ZOTE ZA MUNGU. NITAFANYA KAMA BABA YANGU ALIVYOAMURU WATU WAKE.








MATHAYO 3:13-17; LUKA 3:21-22


WEWE NDIWE MASIHI. LAITI NINGELIJUA!


HUYU NI MWANANGU MPENDWA AMBAYE NIMEPENDEZWA NAYE.
HUYU NDIYE MWANAKONDOO WA MUNGU AMBAYE ATAONDOA DHAMBI ZA ULIMWENGU WOTE!




LUKA 3:22; YOHANA 1:29-34; 1 YOHANA 2:1-2


KWA WAKATI, LAKINI KWANZA YEYE LAZIMA APITE **MTIHANI**.
*ANAKWENDA WAPI?* **HATALIKOMBOA** TAIFA?
*MTIHANI UPI?*
AMBAO ADAMU PAMOJA NA UZAO WAKE WOTE WALISHINDWA. LAZIMA AKUTANE NA MKUU WA GIZA.


BABA ALIMWAMBIA MWANAWE YESU AFUNGE KWA SIKU AROBAINI NA ASILE CHOCHOTE. MWILI ULIPOKUA MDHAIFU, SHETANI ALIJARIBU KUMSHAWISHI KUTOTII BABA NA KUKIDHI NJAA YAKE..
MTU WA KWANZA, ADAMU, HAKUMTII MUNGU NA KUPOTEZA NAFASI YAKE YA UPENDELEO. YESU ALIKUWEPO KAMA MUNGU TANGU MILELE, LAKINI SASA ALIKUWA MTU WA NYAMA YA KUFA. JE ANGEPITA MTIHANI WA MAJARIBU AMBAO WENGINE WOTE WALIKUWA WAMESHINDWA?

MWISHONI MWA SIKU AROBAINI ZA KUFUNGA, YESU ALIKUWA NA NJAA NA UDHAIFU. SASA ALIELEWA JINSI ILIVYOKUWA KUWA KATIKA UMASKINI, KUWA NA NJAA MPAKA MWILI WAKO UANZE KUJIKULA WENYEWE. SASA ALIELEWA JINSI ILIVYOKUWA KUWA MGONJWA, MNYONE NA MDHAHIFU.



KWA SIKU NYINGI, SHETANI ALIMSHAMBULIA YESU AKILINI KUPITIA MAWAZO YA SHAKA NA HOFU. KUJUA MAJARIBU YALIKUWA KARIBU KUISHA, NA KWAMBA YESU ALIKUWA KATIKA HALI YAKE DHAIFU, SHETANI ALIFANYA KITU AMBACHO MARA CHACHE HUFANYA; ALIJITOKEZA MBELE YA YESU.




MATHAYO 4: 1-3; LUKA 4:1-3; WARUMI 3:23, 5:12-21; WAEBRANIA 4:15


SHETANI ALIJARIBU MWANADAMU WA KWANZA, ADAMU, KATIKA KULA KITU KILICHOKATAZWA. ALIJARIBU JARIBIO HILI KWA YESU.
KWELI ILIKUA JARIBIO KWA MTU ALIYEKUWA NA NJAA KWA SIKU NYINGI.


HILI HAPA, UNAWEZA GEUZA JIWE HILI KUA MKATE NA ULE.


LA SITAFANYA HIVYO. KWA KUA MAANDIKO INASEMA KUA MWANADAMU HATAISHI KWA MKATE PEKEE ILA KWA KILA NENO AMBALO MUNGU HUNENA.
NJOO NAMI NIKUPELEKE MAHALI UTAKAPO MTII MUNGU.


UKIRUKA KUTOKA HAPA JUU MALAIKA WA MUNGU WATAKUSHIKILIA, NA WATU WATAKUKUBALI KAMA MASIHI.
UMETAJA MAANDIKO, NA MAANDIKO YANASEMA KWAMBA MALAIKA WATAKUBEBA WEWE KATIKA MIKONO YAO NA KUKUCHUNGA USIJE AKAJIKWAA KWENYE JIWE. SASA NI WAKATI WA KUONYESHA NGUVU YAKO.
MAANDIKO PIA YANASEMA KWAMBA *"HAUPASWI **KUMJARIBU** BWANA MUNGU WAKO."*


NAJUA UNAPENDA ULIMWENGU, KWA HIVYO NITAKUONYESHA JAMBO AMBALO LITAKUFURAHISHA.
MATHAYO 4:3-7


HAPO SASA. UKIWA HAPA JUU UNAWEZA KUONA MATAIFA MAKUBWA MAKUBWA. YAPENDEZA SIO? TANGU ADAMU AKOSE KUFUATA AMRI, NILIMILIKI ULIMWENGU HUU. MIMI NDIYE MUNGU WA ULIMWENGU HUU, NA WALA SIO WEWE. ILA NINAWEZA KUKUPATIA YOTE. UKINIPIGIA MAGOTI NA KUNIABUDU NITAKUPATIA YOTE PAMOJA NA WATU WALIOMO NDANI. UNAONAJE?




SHETANI ALIONDOKA NA KUTOROKA. KWA MARA YA KWANZA SHETANI ALIMJARIBU MTU AMBAYE HANGEWEZA KUMDANGANYA. YESU ALIPITA MTIHANI. DUNIA ILIKUA NA MTU MMOJA ALIYEMTUMIKA MUNGU KWA KWELI ZAIDI.

MTIHANI WA SIKU 40
ULIISHA ILA YESU
HAKUWA NA NGUVU.



MALAIKA WALIKUJA NA CHAKULA NA VINYWAJI NA WALIMHUDUMIA YESU. ALIPOPATA NGUVU ALIRUDI YOHANA ALIKOKUA AKIHUBIRI.



MATHAYO 4:8-11, LUKA 4:14



## SURA YA 9

# HUDUMA YA MAPEMA


TAZAMA, ANAYEKUJA NI *MWANAKONDOO* WA MUNGU, AONDOAYE DHAMBI ZA DUNIA.
*HUYU NDIYE MASIHI.*
YULE AMBAYE MANABII WALIMZUNGUMZIA.
ATAFANYAJE?


ILA SIWEZI KUKUACHA, MKUU.
MFUATENI YESU.
MIMI SIO MKUU. LAZIMA NINYENYEKEE. YEYE NDIYE MASIHI, MKOMBOZI WA ULIMWENGU. MFUATENI YEYE.


MKUBWA, TUNAWEZA KUKUFUATA NA TUWE ***WANAFUNZI*** WAKO. UNAISHI WAPI?
KUJENI MUONE.


FILIPO NIFUATE.
NDIO MKUU. ILA ACHA KWANZA NIMTAFUTE NATHANIELI.
YEYE PIA HUFUATA AMRI ZA MUNGU NA AMEKUWA AKIMNGOJA MASIHI.




YOHANA 1:35-39, 43-45, 3:30-31


NATHANIELI, UKO WAPI?
NIKO HAPA KAKANGU.
NATHANIELI, TUMEMPATA *MASIHI, YESU* MWANA WA MARIAMU.


MASIHI? UMEONGEA NAYEYE? ILA NAZARETI? HAKUNA KIZURI KISHAWAI TOKA NAZARETI. IMEKUWAJE MASIHI AMEZALIWA HUKU? ALIPASWA KUZALIWA BETHLEHEMU YA YUDA.
NJOO UJIONE MWENYEWE. YOHANA ALISEMA KUMHUSU, NA ANDREA YUPO PAMOJA NA YEYE.


KWELI HUYU NI MUISRAELI ALIYE NA *ROHO SAFI.*
FILIPO, ULIMWELEZA CHOCHOTE KUNIHUSU?
LA, SIKUMWAMBIA CHOCHOTE.


HUNIJUI. UNAWEZAJE KUSEMA KUA NINA ROHO NJEMA?
KABLA YA FILIPO KUKUITA ULIPOKUA UMEKAA CHINI YA MTI NILIKUONA.
ULINIONAJE? HAKUNA ALIYEJUA NILIKUA HAPO.


WEWE NDIWE MWANA WA MUNGU. MFALME WA ISRAELI.
HAYA YAMEKUFURAHISHA? BASI UTAYAONA MENGI. UTAONA MILANGO YA MBINGUNI IKIFUNGUKA NA MALAIKA WAKINISHUKIA. TUNA MENGI YA KUFANYA.
YOHANA 1:45-51


ANDREA PIA ALIONDOKA KUTAFUTA KAKA YAKE ILI KUMUELEZA KUHUSU YESU.
SIMEONI, TUMEMPATA *MASIHI* AMBAYE YOHANA ALIKUWA AKIMSEMA.
NJOO UJIONEE
*WAPI NA LINI?* KUNA WENGINE WANAMFUATA YEYE?


WEWE NI SIMEONI MWANA WA YONA, ILA UTAITWA PETERO.
NITAIREJESHA MASHUA KWA WANAFAMILIA KISHA NIKUFUATE.


YESU ALIKUWA NA WANAUME KUMI NWA WAWILI AMBAO WALIMFUATA NA KUSKILIZA MAFUNZO YAKE. WALIITWA WANAFUNZI KUMI NA WAWILI. WALITEMBEA KUTOKA MJI HADI MJI WAKIIHUBIRI INJILI.


YESU NA WANAFUNZI WAKE WALIKWENDA HEKALUNI KUSALI, ILA HEKALU LILIKUA LIMEJAA WAUZAJI.
MBONA NIBADILISHE PESA ZANGU KABLA NILETE HEKALUNI? NYINYI HUPATA *FAIDA KUBWA SANA.*
MAKUHANI NI WAFISADI. WAO HUCHUKUA FAIDA YOTE AMBAYO WAUZAJI HUPATA.
MAKUHANI WANAKUBALISHA.
MARKO 3:16, YOHANA 1:40-42, 2:12-14


ANAFANYA NINI? AMEKUWA AKISIMAMA HAPO KARIBU LISAA MOJA AKISHONA KAMBA HIYO.
TUMEPATA FAIDA KUBWA LEO.


KIBOKO! ANATENGEZA KIBOKO!


NYUMBA YA BABA YANGU NI MAHALA PA SALA, ILA NYINYI MMEIFANYA KUWA MAHALI PA WAKORA. ONDOKENI SASA!
NYUMBA YA BABA YAKE? ANAFIKIRI YEYE NDIYE MASIHI?


MSIIFANYE NYUMBA YA BABA YANGU KUWA SOKO!
KRRRR
YOHANA 2:15-16


SNAP!
NYINYI NI UZAO MNAFIKI. MNAWANYANYASA WAJANE.
AAAH!
ANAFIKIRI YEYE NANI?

MATHAYO 6:5-7, 12:34, YOHANA 2:15-16, 1 TIMOTHEO 6:10




WAKATI MWINGINE MKIJA HEKALUNI, MUWE MNAKUJA KUTUBU DHAMBI ZENU.


MNAKUMBUKA HADITHI AMBAYO DAUDI ALISIMULIA KUMHUSU MASIHI?
UNAJUA WAANDISHI WANAFUNDISHA KWAMBA MASIHI ATAKAPOFIKA, ATAKUJA GHAFLA HEKALUNI.
NDIYO, "ARI YA NYUMBA YA MUNGU ITANIANGAMIZA KWA SABABU MAADUI WA MUNGU WA WAMESAHAU NENO LA MUNGU."


NADHANI WEWE NI HUYU *YESU* WA *NAZARETI* WA AMBAYE YOHANA ANAONGELEA. UMESABABISHA SHIDA NYINGI SANA LEO. NI ISHARA GANI WEWE UTATUONYESHA?
*UTHIBITISHO* KWAMBA MIMI NI MASIHI UTAONEKANA SIKU MTAKAYOHARIBU HEKALU HILI. KATIKA ***SIKU TATU*** ***NITAIINUA TENA.***




ZABURI 69:9, 119:139; YOHANA 2:17-22


YESU NA WANAFUNZI WAKE WALIONDOKA YERUSALEMU NA KWENDA KURUDI KASKAZINI HADI NAZARETI, MJI WA YESU.
EEH *YESU* UMEKUJA NYUMBANI. WALETE MARAFIKI WAKO WOTE NA TUTAWAANDALIA *MLO MTAMU.*
MAMA TUTAKUWA HAPA KWA MUDA MFUPI TU, KUPITIA *SABATO.*




*SABATO NI SIKU YA KIDINI YA KILA WIKI YA MAPUMZIKO ILIYOANZISHWA NA MUNGU SIKU YA SABA NA KUTAWAZWA KAMA MOJAWAPO YA AMRI KUMI KWA WAYAHUDI (MWANZO 2: 2-3; KUTOKA 20:10). ISAYA 42:7, 61:1-2; LUKA 4:16-21


YESU ALIFUNGUA UNABII WA ISAYA NA ALIPATA UTABIRI MAARUFU WA MASIHI.
“ROHO WA BWANA YUKO JUU YANGU, KWA SABABU AMENITIA MAFUTA KWA KUHUBIRI INJILI KWA MASKINI, NA KWA VIPOFU, NA KUHUBIRI KWAMBA WAKATI UMEFIKA SASA WA MUNGU KULETA WOKOVU KWA WATU WAKE.”


LEO UTABIRI HUU UMETIMIA.


KUFURU!
WEWE NI MTOTO WA SEREMALA TU.
TULIA. TUNAONDOKA.
MUUWENI KWA MAWE. ANASEMA KUA YEYE NI MASIHI.


YESU NA WANAFUNZI WAKE WALIKUJA KAPERNAUMU AMBAKO BAADHI YA WANAFUNZI WAKE WALIISHI. TENA WAKAINGIA KATIKA SINAGOGI.


NA NABII AKASEMA MASIHI ATAKUWA NURU KWA WAYUNANI NA MATAIFA NA NDANI YAKE WANGEAMINI. ANAFURAHI ALIYE NA AMANI MOYONI MWAKE, KWA KUWA ATAMUONA MUNGU. MUNGU HAMTUPILII YEYOTE ANAYEKUJA KWAKE, AWE MYUNANI AMA MYAHUDI.
MTAKATIFU. ACHANA NA SISI.


NAKUJUA! MTAKATIFU WA MUNGU!
AMEJAWA MAPEPO! MUONDOENI HAPA.


UMEKUJA KUTUANGAMIZA SISI MAPEPO *KABLA YA WAKATI WETU?*
NI NANI ALIYEMRUHUSU HUMU? *MUANGALIENI.* YEYE *NI HATARI!*


MAPEPO! ***NINAWAAMRISHA*** MUMUONDOKE MTU HUYU NA WALA MSIMTESE TENA.

LUKA 4:28-35


ONDOKENI!
AAAAH


UMEMFANYIA NINI?
AMEAGA?


GHAFLA AKASIMAMA KWA MIGUU YAKE.
MUNGU ASIFIWE!
MAPEPO YAMETOWEKA SASA UKO ***HURU***. NENDA ZAKO NA USITENDE DHAMBI.
YESU ANA MAMLAKA JUU YA MAPEPO.


PETERO, MKE WAKO ANASEMA UENDE NYUMBANI KWANI MAMA YAKO ANAUGUA KWA SANA.
TUTAKUJA.


EH *PETERO,* MUME WANGU. NINA HOFU.
*USIOGOPE*. MKUU YUKO HAPA.


MWANAMKE, AMKA. UMEPONYWA.


MARKO 1:25-30,
LUKA 4:35-38
ANAAMKA! AMEPONYWA!
ALIAMKA KUTOKA KITANDANI
NA AKAWATUMIKIA YESU
NA WANAFUNZI WAKE.


MANENO YA UPONYAJI YALISAMBAA NA WAGONJWA WALIJAA WAKIMTAFUTA YESU.
MKUU, BABA YANGU AMEKUWA KIWETE TANGU ALIPOKUA MDOGO. ALIANGUKIWA NA MTI NA KUUVUNJA MGONGO WAKE. TAFADHALI MSAIDIE.
SIMAMA NA UTEMBEE.


UTUKUFU KWA MUNGU.




MARKO 1:30-34, LUKA 4:38-40


KAMA MAANDIKO YANAVYOSEMA, "*VIPOFU WATAONA*" MSICHANA WAKO ANAONA SASA.


BABA, NI WEWE?


EH BABA, SIKUWAI FAHAMU UNAVYOFANANA. WAPENDEZA KULIKO NILIVYOFIKIRIA.


YESU NA WANAFUNZI WAKE WALIENDA YERUSALEMU NA WANAFUNZI WAKE, SIKU ZA SHEREHE NA WALIFUNZA HEKALUNI.
MTU AKIKULAANI, USIMLAANI MBALI UMUOMBEE BARAKA.
MTU AKIKUKWAZA MSAMEHE. UTABARIKIWA. UKIFANYA AMANI UTABARIKIWA ZAIDI.


MMESKIA IKISEMEKANA KUWA MWAPENDE MARAFIKI WENU NA MWACHUKIE ADUI ZENU, ILA NAWAAMBIA MWAPENDE ADUI ZENU NA MUWATENDEE MEMA.
NA JE KUHUSU *KULIPIZA KISASI?*


MTU AKIKUPIGA KOFI UPANDE WA KUSHOTO, MGEUZIE NA SHAVU *LA KULIA PIA* AKUPIGE. USIWE MWENYE HASIRA. JIRANI YAKO AKIHITAJI KOTI NA UNA MBILI BASI MPE NA MOJA. IWAPO ANA NJAA MLISHE NA BABA WA MBINGUNI ATAKUBARIKI.




MATHAYO 5:8, 21-22, 38-44, 6:12, MARKO 1:34, LUKA 4:40


MMESIKIA IKISEMWA KUWA USIZINI, ILA NAWAAMBIA UKIMTAZAMA MWANAMKE KWA NJIA YA KUMTAMANI BASI ***UMEZINI***.


VIONGOZI WA DINI WANAPENDEZA NJE LAKINI NDANI NI WAOVU.
WAO NI KAMA KABURI ZILIZOPAKWA RANGI NYEUPE. NJE WANAPENDEZA ILA NDANI NI WAOVU TU.


KUNA NJIA KUBWA INAYOPELEKEA ***UHARIBIFU,*** NA WENGI WENU MWAIFUATA.
MIMI NDIYE NJIA YA MBINGUNI. UKIPITIA KWANGU BASI UTAPATA UZIMA WA MILELE, NA UKIPITIA NJIA ZINGINE UTAANGAMIA.


MBONA UNAWAPONYA WATU SIKU YA SABATO? ***MUSA ALISEMA*** TUSIFANYE KAZI YOYOTE SIKU YA SABATO.
BABA YANGU ALINITUMA DUNIANI KUFANYA KAZI ALIZONIAMURU MIMI.
WAJITOSHANISHA NA MUNGU. ***HIYO NI KUKUFURU!*** WAWEZA KUADHIBIWA KWA KIFO.


NI MAPENZI YA MWENYEZI MUNGU KWAMBA MWANAWE AHESHIMIWE NA KUABUDIWA KAMA YEYE MUNGU ANAVYOHESHIMIWA.
ITAFIKIA WAKATI AMBAPO WAFU WATAISIKIA SAUTI YANGU. WENGINE WATAKWENDA MBINGUNI NA WENGINE JEHANAMU.


KWELI HUYU NDIYE MASIHI, KWANZA MIUJIZA NA SASA MANENO HAYA.
NI TOFAUTI NA VIONGOZI WA KIDINI. ANAONGEA VYEMA. HOFU YANGU ***WATAMUUA***.
LAZIMA NIENDE NIMUELEZE MKE WANGU.
MATHAYO 5:27-28, 7:13-14, 28-29, 23:27-28, YOHANA 5:18-19, 23, 29-30, 14:16





HESABU 21:5-9; YOHANA 3:1-14 *MSHIRIKI WA MADHUBUTI YA KALE YA KIYAHUDI ALIBAINISHA KWA UTII MKALI KWA MILA ZA KIYAHUDI.


MKUU SISI VIONGOZI WA WAYAHUDI TUNAJUA WEWE NI MWALIMU TOKA KWA MUNGU. SABABU **HAKUNA MTU** AWEZAYE KUTENDA MIUJIZA KAMA WEWE.
IWAPO HUJAZALIWA MARA YA PILI, HAUTAUONA UFALME WA MUNGU.


WAJARIBU KUNIAMBIA ETI NIRUDI TUMBONI MWA MAMANGU KISHA NIZALIWE TENA?
LA. MWILI HUZAA MWILI NA ROHO HUZAA ROHO. NIKODEMA, NISKIZE, NI LAZIMA UZALIWE UPYA.
HIYO ITAWEZEKANAJE?


KUZALIWA KWA ROHO NI JAMBO LA KUTATANISHA KAMA UPEPO, ILA SOTE TUNAISHUHUDIA KWA USAWA. LAZIMA HII IFANYIKE IWAPO UNATAKA KUINGIA KWENYE UFALME WA MUNGU.
KAMA VILE AMBAVYO MUSA ALIINUA NYOKA KULE JANGWANI, BASI MIMI PIA LAZIMA NIINULIWE VIVYO HIVYO.
HESABU 21:5-9; YOHANA 3:1-14 *MSHIRIKI WA MADHUBUTI YA KALE YA KIYAHUDI ALIBAINISHA KWA UTII MKALI KWA MILA ZA KIYAHUDI.


LAKINI WALIKUWA WANAKUFA SABABU YA KUUMWA NA NYOKA KWA KUWA WALITENDA DHAMBI. WALIPOANGALIA NYOKA YA SHABA WALIPONA MARA MOJA.



INRI
NDIYO, NA HATA SASA WATU WOTE WANAKUFA KUTOKANA NA "NYOKA" WA DHAMBI. LAKINI WAKATI HUU NITAINULIWA KWA AJILI YA WATU WOTE KUNIONA. KAMA WALE AMBAO WALIUMWA NYIKANI WALIKOMBOLEWA KWA KUANGALIA JUU YA NYOKA WA SHABA, WALE AMBAO WANAUMWA NA DHAMBI WATAPATA UKOMBOZI KWA KUNIAMINI MIMI.


"KWA MAANA JINSI HII MUNGU ALIUPENDA *ULIMWENGU* HATA AKAMTOA *MWANAWE WA PEKEE,* ILI KILA MTU AMWAMINIYE ASIPOTEE, BALI AWE NA UZIMA WA ***MILELE***. YEYOTE AMWAMINIYE HAHUKUMIWI, LAKINI ASIYEAMINI AMEKWISHA KUHUKUMIWA
YOHANA 3:14-18


KWA HIVYO WASEMA HII KUZALIWA UPYA NDIO TIBA PEKEE YA DHAMBI? NA YA KWAMBA UTAWEKWA MTINI ILI WATU KUKOMBOLEWA?
NA WAKATI HUU WA KUZALIWA UPYA NI LINI?
BAADA YA KUINULIWA JUU NA WATU KUNIONA.


WASAMARIA WALIISHI KATI YA YERUSALEMU NA GALILAYA. WAYAHUDI WALIEPUKA MAWASILIANO YOYOTE NA WASAMARIA, HATA HAWAKUPITA KATIKA MIJI YAO, KWA SABABU WALIAMINI WASAMARIA KUWA KUNAJISIWA KIROHO. SIKU MOJA YESU ALIWASHANGAZA WANAFUNZI WAKE KWA KUSEMA:
NJOO, LAZIMA NIPITIE SAMARIA.
BWANA, WAO NI WACHAFU. ***WATU WASIOJUA!*** WAO NI MASKINI NA WASHERATI.
NI MAPENZI YA BABA KWAMBA NIENDE SAMARIA.


MCHANA WALIFIKA KISIMANI NJE YA MJI
NENDENI MJINI MNUNUE CHAKULA. MIMI NTAWANGOJA HAPA KISIMANI.
UTABAKI HAPA PEKE YAKO?
NDIO. LAZIMA NIFANYE KAZI YA BABANGU.


YESU ALIKUWA AMECHOKA, ALIKUWA NA NJAA NA KIU. MWANAMKE MMOJA ALIKUJA KISIMANI KUTEKA MAJI.
YOHANA 4:1-8


WAWEZA KUNISAIDIA MAJI YA KUNYWA?
HA! MBONA WEWE MYAHUDI UNANIOMBA MIMI MSAMARIA MAJI? NLIDHANI WAYAHUDI HAMPENDI KUHUSIANA NASI?
UNGALIJUA MIMI NI NANI BASI UNGENIAMBIA NIKUPATIE MAJI YA UZIMA.


UNATAKA KUNIPA MAJI NA HAUNA CHOMBO CHA KUTEKA MAJI. UTAYATOA WAPI MAJI YA UZIMA?
UKIKUNYWA MAJI KUTOKA KISIMANI HIKI BASI BADO *UTAPATA KIU*. MAJI NINAYOKUPA NI MAJI YA UZIMA
BASI NIPE MAJI HAYA YA UZIMA ILI NISIWAI PATA KIU TENA.


NENDA UKAMUITE MUME WAKO NA NITAKUELEZA KUHUSU MAJI HAYA.
SINA MUME.
ULIKUWA NA WAUME WATANO, ILA UNAYEISHI NAYE KWA SASA SIO MUME WAKO.



KWELI WEWE NI NABII KWA KUA UMEWEZA *KUJUA DHAMBI* YANGU YA SIRI.
NYINYI WAYAHUDI HUFANYA IBADA **YERUSALEMU** NA BABA ZETU HUFANYA IBADA MLIMANNI HUKU. NI WAPI SAHIHI KUFANYIA IBADA?


MUNGU NI ROHO. YEYE HAABUDIWI HEKALUNI ILIYOJEGWA KWA MIKONO YA WATU. MUNGU ANATAFUTA WATU WATAKAO AMINI UKWELI NA KUMUABUDU KWA ROHO.
TUNAJUA MASIHI ANAKUJA NA AKIJA ATATUELEZEA UKWELI.


UNAZUNGUMZA NA MASIHI KWA SASA.


LAZINA NIKAWATAFUTE MARAFIKI WANGU ILI NIWAAMBIE!
YESU ALIKAA SAMARIA SIKU MBILI NA ALIWAFUNZA WATU NENO LA MUNGU.
YOHANA 4:7-29, 40


SIKU MOJA YESU ALISIMAMA JUU YA KILIMA AKIANGALIA UPANDE WA ZIWA LA GALILAYA.
UKIMPA MASKINI PESA, USIMPATIE WATU WAKIONA
UKITENDA MATENDO MEMA ILI UONEKANE NA WATU NA WAPENDEZWE NA MATENDO YAKO, HAUTATUZWA NA MUNGU WA MBINGUNI. UNACHOFANYA NA MKONO WA KUSHOTO USIKUBALI MKONO WA KULIA UJUE.
MAELFU YA WATU WALIKUJA ILI KUMSIKILIZA AKIFUNZA MAANDIKO.


UKIOMBA USIWE KAMA WALIMU WA KIDINI WANAFIKI, AMBAO HUOMBA MBELE YA WATU ILI WAONEKANE.
NA UNAPO OMBA USISHINDE UKIJIRUDIA KAMA VIONGOZI WENU WA DINI. WAO HUSIMAMA MBELE YA WATU ILI KUJIONYESHA TU.


USITUMIE NGUVU NYINGI ILI KUTAFUTA UTAJIRI. MATAJIRI WENGI WANA SHIDA NYINGI NA WANAPENDA UTAJIRI WAO KWA SANA HIVYO INAKUWA VIGUMU SANA KWAO KUINGIA MBINGUNI.
USIWEKE HAZINA YAKO KATIKA ULIMWENGU HUU, BALI UIWEKE MBINGUNI AMBAKO ITAISHI MILELE. HUWEZI KUWATUMIKIA MABWANA WAIWILI, MUNGU NA PESA. UTABAKI UKICHUKIA MMOJA NA KUPENDELEA MWINGINE.


MKUU, SIKU IKO KARIBU KUISHA NA WATU WAMEKUWA HAPA NASI SIKU NZIMA. LAZIMA IWE WANA NJAA NA MJINI AMBAKO TUNAWEZA KUNUNUA CHAKULA NI MBALI SANA.
UNAEZA KUWATAWANYA SASA ILI WAKATAFUTE CHAKULA.


MKUU NAEZA KUPA CHAKULA CHANGU. MAMA YANGU ALIKUWA AMENITAYARISHIA SAMAKI WAWILI NA MIKATE MITANO.





MATHAYO 6:1-7, 19-21, 14:15


ACHA TUONE. HAPA TUNA SAMAKI NA MIKATE.
LAKINI MKUU, HII HAIWEZI TOSHA KUWASHIBISHA HAWA WATU WOTE.
NENDENI MKAOMBE *VIKAPU KUMI NA VIWILI* NA MJITAYARISHE KUWASAMBAZIA WATU CHAKULA.


TUNAKUSHUKURU EEH BWANA MUNGU WETU, *MFALME* WA ULIMWENGU ULETAYE CHAKULA *DUNIANI*.


ANAWEZAJE KUMWAGA CHAKULA HICHO KIDOGO NDANI KIKAPU KIKUBWA HIVYO?


TAZAMA!
CHAKULA HICHO CHOTE KIMETOKA WAPI?
MATHAYO 14:19-21, LUKA 9:16-17


MUNGU ASIFIWE!
AMETUPATIA CHAKULA KUTOKA MBINGUNI...KAMA TU MUSA.
MAMA HATAAMINI HAYA.


WATU WALIKULA KUTOKA VIKAPUNI, NA CHAKULA KILIZIDI KUONGEZEKA.


MKUU, WATU WAMEKULA, WAMESHIBA NA BADO KUNA CHAKULA KINGI KIMEBAKI.
KUSANYENI KILICHOBAKI KISHA MPANDE MASHUA MUENDE UPANDE ULE MWINGINE WA ZIWA. TUTAPATANA BAADAE. LAZIMA NIENDE MLIMANI ILI KUSALI.


YESU ALIKWENDA MLIMANI KUSALI PEKE YAKE NA WANAFUNZI WAKE WAKAENDA UPANDE MWINGINE WA ZIWA.
YESU ALIKUWA AKIENDA NYIKANI PEKE YAKE KUSALI.
MATHAYO 14:20-23


BAADA YA WANAFUNZI KUFIKA KATIKATI MWA ZIWA, UPEPO MKALI ULIWAPATA NA WALIOGOPA KUZAMA.
SIJAWAI KUONA UPEPO MKALI KAMA HUU.
HATUWEZI KUENDELEA HIVI.


TUTAZAMA!
TAZAMENI! KUNA KITU HUKO MAJINI!



NI JINNI!
NI JINNI!
NI MTU ANATEMBEA JUU YA MAJI!


PETRO, NI MIMI. USIWE N SHAKA.
BWANA, IKIWA NI WEWE BASI NIRUHUSU MIMI PIA NIWEZE KUTEMBEA JUU YA MAJI.
NJOO KWANGU PETRO.
MATHAYO 14:24-29


NINAKUJA, BWANA.
LA, PETRO!


PETRO ALITEMBEA JUU YA MAJI KWA HAKIKA.


PETRO ALIPOONA MAJI MENGI NA KUKOSA KUMUONA YESU, ALIANZA KUOGOPA.




MATHAYO 14:29-30


PETRO, ULIANZA KUNISHUKU.


YESU ALIMREJESHA PETRO KWENYE MASHUA, WOTE WAWILI WAKITEMBEA JUU YA MAJI.
PETRO, UMETEMBEA JUU YA MAJI!


YESU ALIKEMEA UPEPO NAO UKATULIA.
KUWE NA AMANI, TULIA.
MATHAYO 14:31-33, MARKO 4:38-41


NIONDOKEE, EEH BWANA. SABABU MIMI NI MTENDA **DHAMBI**.
KWA KWELI WEWE NI **MWANA WA MUNGU.**
**BWANA** WANGU NA **MUNGU** WANGU.
**KRISTO** WA ISRAELI.


BAADAYE....
SIKU HIZI ZA SHEREHE ZINA WATU WENGI, WATU WAMETOKA PANDE ZOTE ZA NCHI. WENGINE KUTOKA ***ROMA*** NA WENGINE ***MISRI***.
TWENDENI KANDO YA BWAWA.


AMEKUWA HAPA KWA MUDA MREFU SANA.


UNGEPENDA KUWA *MZIMA?*
SINA YEYOTE WA KUNISAIDIA MIMI.


INUKA, CHUKUA MALAZI YAKO NA UTEMBEE!
WEWE NI YESU, SIO? NIMESIKIA KUHUSU MIUJIZA YAKO.

YOHANA 5:1-8


UTANI MBAYA HUO. MTU YULE AMEKUWA MLEMAVU KWA MIAKA 38 SASA.
LEO NI SABATO TAKATIFU. HAFAI KUWA AKIHARIBU AMANI YETU.


NASKIA KUNA NJAMA YA KUMUONDOA. ANATAMBULIKA SANA.
HUYU YESU ANAFIKIRI YEYE NI *MASIHI*?
NDIO, AMEWAHSAWISHI WATU KWAMBA ANAWEZA KUTENDA ***MIUJIZA***.


MIGUU YAKE! INAKUA.


ANAAMKA!
HAIWEZEKANI!


BWANA ASIFIWE! BAADA YA MIAKA HII YOTE!
YESU NDIYE MASIHI!



MBONA UNAPONYA SIKU YA *SABATO?*
MUSA ALIAMURU WATU *WAPUMZIKE* SIKU YA SABATO.
INAKUBALIKA KUMTOA FAHALI WAKO KUTOKA SHIMONI NA SASA NINATENDA DHAMBI KUMPONYA MTU SIKU YA SABATO?
BABA YANGU HUFANYA KAZI SIKU YA SABATO NA NDIO MAANA MIMI PIA NAFUATA ANACHOFANYA.
LUKA 14:5-6, JOHN 5:9-17


ANASEMA MUNGU NI BABA YAKE. ANAJITOSHANISHA NA MUNGU.
MSHIKENI. ANAPASWA KUPIGWA MAWE HADI AFE.
MUUWENI!


ANAZUNGUMZA KANDO NA SHERIA.
MNAWEZA KUMUUA MTU SABABU YA KUPONYANA SIKU YA SABATO?
SKILIZENI ATAKACHOSEMA.
HAJASEMA CHOCHOTE KINACHOPINGANA NA SHERIA.


NISIKILIZENI! MNASTAAJABU KWA SABABU MIMI NIMETENDA MUUJIZA MMOJA. MTAONA MIUJIZA MIKUBWA KULIKO HII. KAMA BABA YANGU ANAVYOWEZA KUFUFUA WAFU, AMENIPA MAMLAKA HAYO HAYO.
MSIPONIHESHIMU BASI HAMUMHESHIMU MUNGU. KWA KWELI NAWAAMBIA, ANAYEAMINI ALIYENITUMA BASI ATAPATA UZIMA WA MILELE.
UNAWEZAJE KUPEANA UZIMA WA MILELE?


ITAFIKA WAKATI AMBAPO WAFU WATASIKIA SAUTI YANGU NA WATATOKA MAKABURRINI MWAO. WALIO TENDA MEMA WATAPATA UZIMA WA MILELE. ILA WATENDA DHAMBI WATAANGAMIA KWA MOTO.
HIYO NI ***KUFURU,*** HAKUNA MTU AWEZAYE KUFUFUA WAFU. NI ***MUNGU*** TU ANAWEZA KUTOA UZIMA WA MILELE.
YOHANA 5:18-29


HAMNIAMINI MIMI, LAKINI YOHANA ALITABIRI UJIO WANGU. MAANDIKO PIA YANANIZUNGUMZIA. PEKUA MAANDIKO, KWA UNABII MWINGI KUNIHUSU.
MSIFIKIRI NITAWASTAKI KWA MUNGU. SHERIA ZA MUSA, AMBAZO MMESHINDWA KUFUATA, ITAKUWA USHUHUDA DHIDI YENU.
HUYU NDIYE WANAJARIBU KUANGAMIZA NA ANAONGEA KWA UJASIRI HIVI. HAWA VIONGOZI WANAFAHAMU KUWA HUYU NDIYE YESU KRISTO, MASIHI WA ISRAELI?
MAANDIKO YANASEMA HATUTAJUA MAHALI MASIHI ATATOKA NASI TUNAFAHAMU MTU HUYU NI MTOTO WA SEREMALA KUTOKA GALILAYA.


MNASEMA MNANIFAHAMU NA MNAJUA NINAKOTOKA, ILA NAWAAMBIA SIKUJA ULIMWENGUNI HUU PEKE YANGU BALI NILITUMWA NA BABA YANGU. HAMUMJUI BABA YANGU ILA MIMI NAMFAHAMU NA NDIYE ALIYENITUMA MIMI KWENU.
AMEWEZAJE KUNISIKIA?


ANAFAHAMU KILA KITU.
HUYU NDIYE MASIHI ALIYETABIRIWA KUJA.
MNATARAJIA MASIHI AFANYE MIUJIZA MINGI KULIKO MTU HUYU ALIVYOFANYA?


YOHANA 5:30-39, 45, 6:42-43, 7:25-32, 40-41
NENDENI SASA HIVI NA *MKAMKAMTE* KUFURU YULE.
WATU WANAMUAMINI NA LAZIMA ANYAMAZISHWE.
WAKATI HUU NI KUBAYA.


WAMEBARIKIWA WALIO NA KIU CHA WEMA, KWANI WATAJAZWA WEMA.
MTU YEYOTE AKIWA NA KIU MUACHENI AJE KWANGU ILI ASITIRI KIU CHAKE. ROHO MTAKATIFU ATAISHI NDANI YAKE KAMA KISIMA CHA MAJI YAKITIRIRIKA HADI *UZIMA WA MILELE.*
WAMEBARIKIWA WAFANYAO AMANI, KWA KUWA WATAITWA WANA WA MUNGU. PENDENI MAADUI WENU NA MUWABARIKI.
HAONGEI KAMA JAMBAZI.
WANASEMA YEYE NI JIBU LA UTABIRI ULIOFANYIKA MIAKA 4000 ILIYOPITA.


MBONA HAMJAMLETA KWETU? ALIKUWA AMESIMAMA MBELE YENU. *KWA NINI HAMKUMSHIKA?*
HAKUNA YEYOTE ASHAWAI KUZUNGUMZA KAMA MTU HUYU.
ANAONGEA KUHUSU UPENDO NA MSAMAHA.
*AH!* AMEWADANGANYA NYINYI PIA? HUYU YESU ANAPASWA KUFA.




MATHAYO 5:6, 9, YOHANA 4:14, 7:45-52


ANAWADANGANYA WATU WA KAWAIDA.
NI KAMA ANA JIBU LA KILA KITU.
MBONA TUSIMTUME MMOJA WA WAKILI SHUPAVU ILI AMSHINDE KWA MANENO YAKE?


NIMEJUA WAKILI TUTAKAYETUMA. NI *SHUPAVU* NA HANA *HURUMA*.


WAKILI ALIKUJA KUMJARIBU YESU.
MKUU NIFANYE NINI ILI KUPATA UZIMA WA MILELE?
SHERIA INASEMAJE?
INASEMA UMPENDE BWANA MUNGU WAKO KWA MOYO WAKO *WOTE, ROHO, NGUVU* NA AKILI NA UMPENDE JIRANI YAKO KAMA UNAVYOJIPENDA.


NDILO HILO JIBU LAKO. *UPENDO* NDIO SHERIA KUU ZAIDI. UKIMPENDA JIRANI YAKO UNAVYOJIPENDA MWENYEWE UTAMFURAHISHA MUNGU.
NDIO, LAKINI NI JIRANI YUPI? HUMAANISHI NI KILA MTU HADI WARUMI.
NITAKUSIMULIA HADITHI.


KULIKUA NA MTU ALIKUWA AKISAFIRI KUTOKA YERUSALEMU KWENDA YERIKO. ALIVAMIWA NA WEZI, AKANYANGANYWA KILA KITUU, AKAUMIZWA NA KUACHWA NJIANI AFE.
KUHANI AILPOPITA HAPO ALIZUNGUKA AKIMWANGALIA NA HAKUMSAIDIA.
LUKA 10:25-31


VILE VILE, MLAWI, MTU ALIYECHAGULIWA KUTUMIKA HEKALUNI, ALIPITA, AKASIMAMA KUMTAZAMA MTU YULE LAKINI HAKUMSAIDIA.
INA MAANA GANI KUSEMA UNAPENDA ILHALI HUONYESHI KWA MATENDO? IWAPO HUMPENDI JIRANI YAKO BASI HUMPENDI MUNGU.


KISHA MSAMARIA AKAPITIA HAPO, MTU ANAYEDHARAULIWA NA WAYAHUDI. ALIPOMUONA MTU YULE AKIWA AMELALA CHINI HAKUTAKA KUJUA KAMA NI MYAHUDI.
MSAMARIA ALIMHURUMIA NA ALISIMAMA ILI KUMSAIDIA.


MSAMARIA ALIMPANGUZA NA KUMFUNGA VIDONDA VYAKE. UPENDO WAKE HAUKUA WA MANENO *BALI* MATENDO.


MSAMARIA ALIMCHUKUA MTU YULE NA KUMBEBA KWA PUNDA WAKE NA AKAMPELEKA HOTELINI.
POLE POLE SASA. UTAKUA KITANDANI HIVI KARIBUNI.


NITALIPIA CHUMBA PAMOJA NA CHAKULA CHA WIKI MBILI. MAHITAJI YAKE YAKIZIDI NITAKULIPA TENA NIKIRUDIA HAPA.

LUKA 10:32-35



ULINIULIZA NI NANI JIRANI YAKO. NIELEZE SASA KATI YA WATU HAO WATATU NANI ALIKUWA JIRANI KWA MTU HUYU?
ALIYEONYESHA HURUMA.
VYEMA.


BASI UNAWEZA KWENDA NA UTENDE MEMA KAMA ***MSAMARIA*** HUYU. UWAPENDE MAJIRANI WAKO.


MJINGA! MUONDOENI HAPO KABLA ABADILIKE NA KUMUAMINI YESU.
HAYA NI MAFUNDISHO YA AINA GANI? HAIWEZEKANI. WATU WENGINE HAWAWEZI KUPENDEKA.




MATHAYO 5:43-44, LUKA 10:36-37




## SURA YA 10

# MIUJIZA NA MAFUMBO


KWINGINEKO...
SIJAKULA CHOCHOTE KWA SIKU KADHAA SASA
UTAKUFA USIPOJIFUNZA KULA PANYA NA MENDE. HII NDIO NJIA PEKEE YA KUISHI
NITAKUFA KWANZA. MWAKA ULIOPITA NILIKUWA TAJIRI NA WA KUHESHIMIKA KATIKA JAMII. NITAZAME SASA.
HUHESHIMIWI TENA, WE NI MWENYE UKOMA ALIYETENGWA


HAPO MBELENI NILIKUWA NA IMANI KUWA NITAPONA NA KUWEZA KURUDIA MKE NA WATOTO WANGU. LAKINI NIMEKUWA HAPA KWA MIAKA KUMI SASA, NA SIJAWAHI SIKIA MTU YEYEOTE ALIYEPONA NA KURUDI KWA JAMII.


HAPO MBELENI MKE WANGU ALIKUWA AKILETA WATOTO NA KUSIMAMA KWA UMBALI WAKIONGEA NA MIMI. LAKINI WALIPUNGUZA KUKUJA. WATOTO WAMEKUWA WAKUBWA SASA NA HAWATANITAMBUA WAKINIONA.HII NI MBAYA ZAIDI KULIKO KUWA MFU.


AH, ACHA KUJIONEA HURUMA, HAKUNA ANAYEJALI HATA MUNGU.WACHA TUONE IKIWA TUNAWEZA KUOMBA CHAKULA.


TUTANATOKA KWENDA KWENYE BARABARA KUU LEO TUONE KAMA TUNAWEZA PATA HURUMA KIASI.
TUTASAFIRI PAMOJA, INAWEZA KUWA SALAMA.


NAONA WASAFIRI WENGINE WAKIJA BARABARANI


TAZAMA! NI WALE WAVULANA TENA
ONDOKENI HAPA NYINYI WATU WACHAFU WENYE UKOMA. NENDENI KWINGINE MFE.
NYIE FUNZA MCHAPU! MUNGU ANAWAADHIBU.
KIMBIA! KIMBIA


WACHAFU! WACHAFU, SISI NI WACHAFU.
NI WENYE UKOMA. USIRUHUSU WAKUKARIBIE. UNAWEZA PATA HUO UGONJWA.


UNAWEZA KUTUONEA HURUMA? UNAWEZA KUTUPEA ANGALAU CHAKULA KIDOGO?
WAPE KITU ILI WAENDE.
RUDI NYUMA! WEWE NI MCHAFU.


RUDI NYUMA NA TUTAIACHA HAPA CHINI.
SASA, USIKARIBIE. SUBIRI NIONDOKE KWANZA.


MKATE!
NIPATIE PESA
CHAKULA!
USICHUKUE YOTE


WEWE NGURUWE
NI YANGU.
MUNGU WANGU
MKATE! MKATE!


KUNDI KUBWA LA WASAFIRI LINAKUJA
LAZIMA TUWE WAANGALIFU WAPO WENGI SANA.
NA WOTE NI WANAUME.


HUYO NI YESU WA NAZARETI. NILIMWONA MARA MOJA, KABLA SIJAPATA UGONJWA HUU. YEYE NDIYE ANAYEPONYA WATU,
AANADAI KUWA AMETOKA KWA MUNGU. ANASEMA KWAMBA YEYE NA BABA NI KITU KIMOJA. NILIMWONA AKIPONYA MACHO VIPOFU NA VILEMA VIUNGO.


YESU! TUSAIDIE
MWALIMU, NI WAKOMA
USIWARUHUSU WAKARIBIE.


JE! NI NINI UNGETAKA NIFANYE?
UTUHURUMIE NA UTUPONYE.
UKIPENDA, UNAWEZA KUNISAFISHA.


HAUPASWI KUNIGUSA!
NI SAWA. NENDENI HEKALUNI MKAJIONYESHE KWA KUHANI. ATAONA KUWA MMETAKASWA NA KUWARUHUSU MRUDI NYUMBANI KWA FAMILIA ZENU.


ANASEMA TUMESAFISHWA.
WATZTUFUKUZA KABLA HATUJAKARIBIA HEKALU.
NITAFANYA KAMA ALIVYOSEMA.
NIKO PAMOJA NAWE. TWENDE
LUKA 17: 11-14


YESU ALISEMA TUMEPONA.
NINAJISIKIA VIZURI.


TUNABADILIKA!


NGOZI YANGU IMEPONA!
YESU AMETENDA! WEWE NI MZIMA!
WEWE SIO MBAYA TENA!
LAZIMA NIENDE KUTAFUTA MKE WANGU


MBARIKIWA NI WEWE, MWANA WA MUNGU, MFALME WA ISRAELI. UMENIRUDISHIA MAISHA YANGU. MUNGU NI WA REHEMA NA MWENYE NEEMA.
JE! HATUKUSAFISHWA? LAKINI NI MMOJA TU NDIYE ALIYRUDI KUTOA SHUKRANI, NA HATA SIO MYAHUDI. YEYE NI MSAMARIA
LUKA 17: 14-19


MTU MMOJA ALIMWULIZA YESU IKIWA WENGI WATAINGIA KATIKA UZIMA WA MILELE. YESU AKAJIBU:
UZIMA WA MILELE
NIGHT CLUB
CARLOS
club
NAWAAMBIA, NJIA INAYOELEKEA UZIMANI NI NGUMU NA NYEMBAMBA NA NI WACHACHE SANA WATAIPATA. LAKINI NJIA INAYOONGOZA KWENYE KUZIMU NI PANA NA IMEJAA WATU WANAOELEKEA KWENYE HUKUMU YA MILELE.




MATHAYO 7: 13-14, 22-23; UFUNUO 14:11


YESU ALISIMULIA HADITHI NYINGINE:
KULIKUWA NA MTU TAJIRI AMBAYE ALIVAA NGUO NZURI KABISA NA ALIKULA VYAKULA VYA KITAJIRI KILA SIKU. ALIKUWA MWAMINIFU NA MWADILIFU, SIO MTU MWOVU, LAKINI ALIJIFIKIRIA YEYE MWENYEWE.
ALIKUSANYA PESA ***ZAKE*** NA ALIZIDI KUTAJIRIKA KILA SIKU


CHUKUA MABAKI HAYA KUTOKA KWA SAHANI LANGU NA UMPE MWOMBAJI **LAZARO** AMBAYE AMELALA KWENYE LANGO LANGU. MIMI NI MTU *MWENYE HURUMA* YA KINA NA *FADHILI*.
NDIO BWANA, NINA HAKIKA ATASHUKURU.


BWANA AMENITUMA NIKUPE MAKOMBO HAYA.
*BWANA ASIFIWE!* MUNGU HUWAANDALIA WALIO WAKE. HII NI ZAIDI YA NINASTAHILI. *MSHUKURU* BWANA WAKO KWA NIABA YANGU.
NINA UTAJIRI MWINGI, NITAHITAJI GHALA *KUBWA* KUTUNZA MALI ZANGU ZOTE.


WEWE MJINGA. USIKU HUU UTAKUFA NA UTALAZIMIKA KUTOA HESABU KWA ROHO YAKO
GASP! BLOUBB-GU...
"IMEWEKWA KWA MWANADAMU KUFA MARA MOJA TU, NA BAADA YA HAPO HUKUMU."
LUKA 16: 19-22; WAEBRANIA 9:27


WAKATI MSAFARA WA MAZISHI YA YULE TAJIRI ULIPOKUWA UKIONDOKA KWENYE NYUMBA YAKE YA KIFAHARI, WALIGUNDUA KWAMBA MWOMBAJI, LAZARO, PIA ALIKUWA AMEKUFA.
NI MWOMBAJI MZEE, **LAZARO** YEYE, PIA, ALIKUFA USIKU. ANAONEKANA MWENYE AMANI SANA.
MWILI WA LAZARO ULIBEBWA BILA KUPENDEZA JUU YA MKOKOTENI NJE YA JIJI, AMBAPO ULIZIKWA KAMA MTU MASKINI. HAKUKUWA NA MAZISHI NA HAKUNA MTU ALIYEOMBOLEZA KUFA KWAKE.


LAKINI MALAIKA WALIKUJA WAKAMCHUKUA LAZARO KWENDA PARADISO.
***JAMANI! SAFARI NZURI!*** SIKUWAHI KUFIKIRIA ***KUFA*** ITAKUWA ***FURAHA*** SANA!
LAZARO, NDUGU YETU, KARIBU ***NYUMBANI***. HUTAPATA NJAA TENA NA MWILI WAKO HAUTAUGUA TENA. NJOO, TUNA MEZA ILIYOANDALIWA KWA AJILI YAKO.


ALIKUWA MTU MZURI. WAKATI MWINGINE ALIONEKANA KUWA MGUMU KWA WALE ALIOWAPENDA, LAKINI TUTAKUMBUKA KILA WAKATI KWAMBA ALIPENDA TAIFA LAKE NA ALIKUWA MWAMINIFU KATIKA SHUGHULI ZAKE.
AMEENDA KWENYE THAWABU YAKE. ROHO YAKE IPUMZIKE KWA AMANI YA MILELE
TAJIRI ALIKUWA NA MAZISHI MAZURI KABISA KATIKA KABURI ZURI, NA KILA MTU ALIYEPENDA PESA ZAKE ALIKUJA KUONA KILE ALICHOWAACHIA KATIKA MAPENZI YAKE.


LAKINI TAJIRI ALIPOKUFA, ALIJIKUTA AKIANGUKA NDANI YA SHIMO LISILO NA MWISHO,.

LUKA 16:22


NISAIDIE!
EE MUNGU, MTU ANISAIDIE! NIKO HAPA HAPA KWENYE MOTO!


BABA *IBRAHIMU, UNIREHEMU*. NAMWONA LAZARO KULE. MTUME ATUMBUKIZE KIDOLE CHAKE NDANI YA MAJI NA APOESHE ULIMI WANGU, KWA MAANA *NINATESWA* KATIKA MOTO HUU.
MWANANGU, NINGEKUSAIDIA IKIWA NINGEWEZA, LAKINI KUNA *PENGO KUBWA* KATI YETU, NA ZIWA LA MOTO CHINI. HATUWEZI KUVUKA ILI KUKUSAIDIA, WALA HUWEZI KUVUKA KUJA UPANDE HUU.
BASI NAKUSIHI UMTUME LAZARO NYUMBANI KWA BABA YANGU ILI KUWAONYA KAKA ZANGU WATANO ILI WASIISHIE KATIKA ENEO HILI MBAYA LILILOJAA *MATESO*.


LUKA 16:22-31
WANA MAANDISHI YA *MUSA* NA *MANABII*. WACHA WAAMINI MAANDIKO.
LAKINI HIYO HAITOSHI KWAO. IKIWA WATAONA MUUJIZA WA UFUFUO, WANGETUBU KWA KUTOKUAMINI KWAO..
IKIWA HAWAAMINI MAANDIKO, HAWATASHAWISHIKA WAKIONA MTU ANAFUFUKA KUTOKA KWA WAFU. UMECHELEWA SANA KWAKO. LAZIMA WAFANYE MAAMUZI YAO WENYEWE. SAMAHANI. HAKUNA KITU NAWEZA KUFANYA


VIPI,,, MNATAKA KUBURUDIKA? KWA BEI RAHISI TU.
BWANA, MPUUZE TU. WAKATI WAKE UMEPITA


MAANDIKO MATAKATIFU YANASEMA, "USIZINI."
WEYE, MIMI NI MWANAMKE **MTAKATIFU**. NINAMWAMINI MUNGU
IBILISI **AMEKUDANGANYA.** MWISHO WAKO NI KATIKA ZIWA LA MOTO


MWENZAKO AMESEMA KWELI. NIMECHELEWA SANA. NIMEKUWA NIKILALA NA WANAUME TANGU NILIPOKUWA MTOTO.
HUJACHELEWA KWA MUNGU. UKIMTAFUTA, UTAMPATA. ATAKUSAMEHE DHAMBI ZAKO NA KURUDISHA ROHO YAKO.


NAFSI YANGU NI YA IBILISI LAKINI NINGEMPA MUNGU IKIWA ANGEFANYA ... ANGE ... ANGE ... ... ...




KUTOKA 20:14; LUKA 8: 2; 1 YOHANA 1: 9


IEEE
SHETANI, TOKA NDANI YAKE!


NINAKUAMURU UTOKE NA USIRUDI.
KWA AMRI YA YESU, MASHETANI SABA WALIONDOKA KWA YULE MWANAMKE.


WAMEKWENDA!
WEWE NI NANI?
MIMI NI YESU


LUKA 8: 2, 11: 24-26
LAZIMA UACHE DHAMBI ZAKO NA UMWABUDU MUNGU AU SHETANI ATALETA WENGINE WABAYA ZAIDI KULIKO WAO.
NATAKA KUMTUMIKIA MUNGU. NITAKUFUATA NA KUJIFUNZA ZAIDI.
NINI KILIMTOKEA


MWALIMU, NILIONA KILE KILICHOTOKEA. NI AJABU. VIONGOZI WETU WA DINI WANGEMPUUZA MARIAMU MAGDALENE WAKATI WA MCHANA,
LAKINI WENGINE WAO WANGEKUJA KWAKE USIKU ILI KUZINI NAYE.
JE! WEWE NA WANAFUNZI WAKO MNGEKUJA NYUMBANI KWANGU NA KULA? NINGEPENDA MARAFIKI WANGU WENGINE WASIKIE ZAIDI JUU YA HAYA
TUTAFUATA


TUAMBIE, YESU, NI VIPI MTU ANAWEZA KUWA MWAMINIFU NA MSAFI KATIKA JAMII HII MBOVU? TUNGEKUFA NA NJAA IKIWA HATUTAKUWA WAFISADI KIDOGO.
USIFANYE KAZI KWA VITU VINAVYOANGAMIA, LAKINI KWA VILE VINAVYOENDELEA MILELE. USIFIKIRIE JUU YA UTAJIRI WAKO MWENYEWE, LAKINI FIKIRIA JINSI UNAWEZA KUWA BARAKA KWA WENGINE.


MAISHA NI ZAIDI KULIKO **CHAKULA** NA **MAVAZI**. IKIWA MUNGU HUVISHA MAUA YA SHAMBA, YEYE ATAWAVISHA NYINYI.
INAKUJA WAKATI AMBAPO KILA MTU ATASIMAMA KATIKA HUKUMU MBELE ZA MUNGU NA KUTOA HESABU YA KILA KITU ALICHOFANYIKA MWILINI, KIWE KIZURI AU KIBAYA.


USIFANYE KAMA VIONGOZI WAKO WA DINI, KWA KUWA WANAHUBIRI JAMBO MOJA NA KUISHI LINGINE. NI KAMA BAKULI ZILIZO SAFI NJE, LAKINI NDANI NI CHAFU.
IKIWA HAKI YAKO SI KUU KULIKO YAO, HUTAINGIA KAMWE KATIKA UFALME.

MHUBIRI 12:14; MATHAYO 23:25, 6: 19-21, 25, 28-30, 12:36;
LUKA 15: 1-3




MTU MMOJA ALIKUWA NA WANA WAWILI. MWANA MDOGO ALIKUWA *MUASI* NA ALITAKA KUISHI MAISHA ***YA UTASHI WA MWILI.***
***NDIO,*** NAPENDA HADITHI HII.


KWA HIVYO ALIDAI KUPOKEA URITHI WAKE.
BABA, IKIWA UTANIPA TU SEHEMU YANGU YA SHAMBA SASA, NITAENDA MJINI KUTAFUTA *UTAJIRI WANGU.*
LAKINI MWANANGU, YOTE NILIYO NAYO NI YAKO. SITAISHI KWA MUDA MREFU ZAIDI NA WEWE NA KAKA YAKO MTARITHI HAYA YOTE. MTAKUWA NA VYA KUTOSHA NA MAISHA YENU YOTE. TUNAO KONDOO NA NG'OMBE WENGI. MASHAMBA YETU YAMEJAA NAFAKA KILA MWAKA. TUNA WATUMISHI WENGI NA UTAJIRI MWINGI ...


LAKINI NATAKA KUTOKA NJE NA KUUONA ULIMWENGU. SITAKI KUISHI SHAMBANI NA KUFANYA KAZI KAMA MTUMWA KATIKA MAISHA YANGU YOTE. WAKATI MIMI NI MCHANGA NATAKA KUBURUDIKA. MARAFIKI ZANGU.....
MARAFIKI ZAKO, AMBAO HAWAFANYI KAZI KAMWE, FIKIRIA TU JUU YA FARASI GANI NI WA HARAKA ZAIDI, NI DIVAI GANI BORA, NA NI WANAWAKE GANI WANAOVUTIA


JE! MNAJUA NINI JUU YA MAISHA? WEWE HUFUNGWA KILA WAKATI KWENYE SHAMBA HILI LA ZAMANI. NATAKA SEHEMU YANGU YA SHAMBA SASA. NAENDA MJINI KUTENGENEZA NJIA YANGU MAISHANI
*MPE. TUNGEKUWA BORA* BILA YEYE. YEYE HUWA HAFANYI SEHEMU YAKE YA KAZI HATA HIVYO


BABA ALIMPA MTOTO WAKE MDOGO SEHEMU YA URITHI. KWA HIVYO MTOTO HUYO ALIVUKA BAHARI KWENDA KWENYE MIJI MIKUBWA AMBAPO ANGEWEZA KUPATA RAHA
SASA, ***HAYA NDIO MAISHA*** – HAKUNA MTU ANAYENIAMBIA NINI CHA KUFANYA.

LUKA 15: 11-13


MWANA MDOGO ...
WOW, HII NI TUKUFU KULIKO NILIVYOFIKIRIA. WATU HAWA WOTE NA MAJENGO. HAPA NDIPO PENYE RAHA.
LAZIMA NIPATE NYUMBA NZURI YA KUKODISHA


NDIO, HII INAONEKANA ***NZURI***. NITAICHUKUA
IKIWA UNAHITAJI KITU CHOCHOTE TU PIGA SIMU. TUNAYO HUDUMA MCHANA NA USIKU


SASA NI NANI ANAYEWEZA KUULIZA ZAIDI YA HII? KESHO NITATOKA NJE NA KUKUTANA NA BAADHI YA WENYEJI WA MJIWENGINE
LUKA 15: 13


VIPI, TUNA NINI HAPA? MVULANA WA MASHAMBANI? ANAWEZA KUWA MZURI IKIWA TUNAWEZA KUONA USO WAKE
VIPI, MWENZANGU, IKIWA UNATAFUTA MAISHA MJINI, NI BORA KUNYOA NDEVU HIZO NA KUVAA NGUO ZA KISASA.


WEWE *MPUUZI.* SIO MBAYA UNAONEKANA KATIKA NGUO HIZI MPYA..


NIMEFURAHI UMEWEZA KUUNGANA NASI KWA CHAKULA CHA JIONI
HIVI SI ANAPENDEZA SASA KWA KUWA AMEONDOA NYWELE ZOTE MBAYA ZA ZAMANI USONI MWAKE.


FURAHA KWA RAFIKI WETU MPYA. AWEZE KUPATA RAHA NA FURAHA KILA WAKATI.
...NA UPENDO ....




LUKA 15:13


JE! HATUWEZI KWENDA KWENYE NYUMBA YAKO, SISI WAWILI TU?


NA KWA HIVYO KIJANA HUYO, MBALI NA NYUMBANI, ALIISHI JUU KWA MIEZI MINGI. ALIKUWA NA MARAFIKI WENGI KWA MUDA MREFU KADRI ALIVYOKUWA NA PESA
SIKU ILIFIKA WAKATI KWENYE RAHA ZA KIPUMBAVU ALITUMIA PESA ZAKE ZOTE - LAKINI BADO ALIKUWA NA MARAFIKI WENGI AMBAO WALIKUWA MATAJIRI KABISA.


UNAMAANISHA NINI HAUNA PESA ZAIDI? NILIDHANI WEWE NI TAJIRI
KWELI, INAHITAJIKA HELA NYINGI KUISHI HUMU, NA NILIPOTEZA KAMARI YA MWISHO KWENYE MASHINDANO YA WIKI ILIYOPITA. NILIDHANI NILIKUWA NA USHINDI HAKIKA, NA NILITARAJIA ..


UNAMAANISHA KUSEMA KUWA *HUNA HELA?* UTANINUNULIA VIPI HIYO NGUO ULIYOAHIDI?
NILITUMAINI BABA YAKO ANGEWEZA KUNIPA *KAZI* YA KUSIMAMIA MALI ZAKE.
*KAZI?*


SIWEZI KUAMINI NINALISHA NGURUWE -- HAWA WANYAMA WACHAFU.
NILIDHANI NILIKUWA NA MARAFIKI. HATA HAWAZUNGUMZI NAMI SASA. LAKINI NITAPATA KAZI BORA NA KURUDI JUU
OINK
SLUUUKK
GRUNT
LUKA 15: 13-15


SIJALI WEWE NI MGONJWA KIASI GANI. TOKA HUKO NJE NA UANGALIE NGURUWE. NITAKUFUKUZA KAZI NA KUPATA MTU MWINGINE. SASA SONGEZA!
NDIO, BWANA, SAMAHANI. MARA MOJA, BWANA


KAZI HII HAILIPI YA KUTOSHA HATA MIMI KULA VIZURI. NADHANI MARAFIKI WANGU WALIPO WANAKULA VIZURI


NAJUTA YALIYONIKUTA. NINA **BARIDI** SANA, NINA **NJAA,** NA **NIMECHOKA**. NINGEWEZA KULA CHAKULA HIKI CHA NGURUWE. WATUMISHI WA BABA YANGU NYUMBANI WANA CHAKULA ZAIDI YA VILE WANAHITAJI. IKIWA NINGEWEZA TU ... LAKINI HAPANA, NISINGEWEZA KURUDI HUKO, SIO BAADA YA NAMNA NILIVYOONDOKA. WANGEWEZA **KUNIDHARAU**



NIMEKUWA **MJINGA** GANI. JE! IKIWA NITARUDI NYUMBANI NA KUMSIHI BABA KUWA *MTUMISHI WAKE?* NIMETUMIA SEHEMU YANGU YOTE YA SHAMBA. LAKINI NINGEWEZA KUWA MTUMISHI - IKIWA WANGENITAKA


NAENDA NYUMBANI.
WEWE MJINGA! HUNA PESA. UTALAZIMIKA KUTEMBEA MAILI ELFU MOJA.


BAADA YA KUTEMBEA KWA WIKI, ALIKUWA KARIBU NYUMBANI.
NIKO **KARIBU** PALE. SINA HAKI YA KUJA HAPA KUOMBA NEEMA. NITASEMA, "BABA, NIMETENDA *DHAMBI* NA SISTAHILI KUITWA MWANA WAKO TENA. NIFANYE KAMA MMOJA WA WAAJIRIWA WAKO.

LUKA 15: 16-19


JE! UNAMWONA MTU HUYO AKIJA PALE? MACHO YANGU YA ZAMANI HAYAWEZI KUONA KAMA VIZURI, KWELI NIMEZEEKA, LAKINI NAKWAMBIA ANATEMBEA KAMA ***MTOTO WANGU ALIYEPOTEA ZAMANI.***
NDIO, AMEKUA KIDOGO, NA NI MWEMBAMBA, LAKINI NAAMINI NI MTOTO WAKO


MWANANGU!


MWANANGU, **MWANANGU!** UMERUDI NYUMBANI!
BABA, NIMETENDA DHAMBI MBELE ZAKO...



... NA SISTAHILI KUITWA MWANAO..


LUKA 15: 20-22
TULIDHANI UMEKUFA, NA SASA UKO *HAI* TENA. TUTAKUSAFISHA MARA MOJA!
HUWEZI KWENDA KWENYE NYUMBA NAMNA HII. MTUMISHI WANGU ATALETA JOHO NZURI NA VIATU KWA MIGUU YAKO. PETE YAKO ULIPOTEZA. NDIO, UTAHITAJI PETE. MWANANGU AMBAYE ALIKUWA AMEPOTEA AMEPATIKANA SASA


MCHINJE NDAMA ALIYENONA, ANDAA KARAMU, WAALIKE WAGENI, NASI TUTAFURAHI, KWA MAANA HII NI SIKU YA FURAHA.


NIMEFURAHI SANA NINYI NYOTE MKO HAPA KUFURAHI PAMOJA NAMI KATIKA *HAFLA HII NZURI*. MWANANGU BADO NI DHAIFU KUTOKANA NA SHIDA YAKE, LAKINI AKIWA NA CHAKULA KIZURI ATAKUWA NA NGUVU HIVI KARIBUNI. HII NI ***SIKU BORA MAISHANI MWANGU***


KAKA MKUBWA ALIKUWA AMEENDA KWA SIKU KADHAA. ALIPORUDI NYUMBANI, ALIPATA SHEREHE IKIENDELEA.
JE! NI MUZIKI GANI HUU NA DENSI NINAYOISIKIA?
NDUGU YAKO MDOGO ***AMERUDI NYUMBANI KWA*** SURA YA KUSIKITISHA ZAIDI. YEYE NI MGONJWA NA MASKINI. BABA YAKO ANAFURAHI KUWA NAYE NYUMBANI TENA. HARAKA INGIA NDANI.
SITASHIRIKI KATIKA UPUMBAVU HUU. AMEISHI MAISHA YA DHAMBI NA AIBU
YULE MTUMISHI AKAMWAMBIA BABA YALE AMBAYO MTOTO WAKE ALIKUWA AMESEMA, AKATOKA KUZUNGUMZA NA MTOTO WAKE


KWA MUDA MREFU NILIMTAFUTA, NIKIFIKIRI ALIPOTEA MILELE. NILIKUWA KARIBU KUFA MOYO NA KISHA HAPA ANAKUJA AKITEMBEA BARABARANI. JE! UNAWEZA KUAMINI **BARAKA** KAMA HIYO? *MUNGU NI MWEMA!*
SIWEZI KUAMINI UNAFURAHI NA MWENYE DHAMBI KAMA HUYU. SITASHUGHULIKA KWA HAYA MNAYOFANYA.


HIYO NI HADITHI YA KUPENDEZA, LAKINI JE! UNADOKEZA KWAMBA SISI NI KAMA KAKA MKUBWA?
ALIYE NA MASIKIO YA KUSIKIA NA ASIKIE.

LUKA 15: 23-32


MTU HUYU NI **HATARI**. WATU WOTE WANAMPENDA.
ANAWAPA TUMAINI
NDIO, LAKINI NI TUMAINI LA UONGO. NANI ANAWEZA *KUAHIDI UZIMA WA MILELE* KWA MWENYE **DHAMBI?** LAZIMA AFE. WAITE WATU WOTE PAMOJA. TUTAKUTANA USIKU WA LEO NYUMBANI KWA KUHANI MKUU.


NJOONI, TUTARUDI GALILAYA NA KUPUMZIKA KIDOGO. WAKATI UTAFIKA HIVI KARIBUNI AMBAPO WATANITUPA *GEREZANI*. WATANIDHALILISHA NA KISHA ***WANISULUBISHE***. LAKINI SIKU YA TATU ***NITAFUFUKA*** KUTOKA KWA ***WAFU***.
ANAMAANISHA NINI, "*KUFUFUKA KUTOKA KWA WAFU?*"
SIELEWI KABISA. LAZIMA IWE MFANO


BWANA, HARAKA! MARTHA ALINITUMA NIKUTAFUTE. NDUGU YAKE LAZARO NI MGONJWA KARIBU KUFA. YEYE NI RAFIKI YAKO MPENDWA. IKIWA UNA HARAKA, UNAWEZA KUFIKA HAPO KABLA HAJAFA. TUNAJUA UNAWEZA KUMPONYA.
MWAMBIE MARIAMU NA MARTHA KWAMBA NITAKUJA. NA WAAMBIE KUWA UGONJWA HUU SIO KWA KUSUDI LA KIFO, BALI NI KUMTUKUZA MUNGU
LAZARO? MGONJWA? LAZIMA TUHARAKISHE



SIKU MBILI BAADAYE ...
BWANA, IMEKUWA KARIBU SIKU MBILI TANGU TUSIKIE KWAMBA RAFIKI YETU LAZARO NI MGONJWA HADI KUFA, NA ITATUCHUKUA SIKU MBILI KUFIKA HAPO. JE, HATUPASWI KWENDA?
KESHO TUNAONDOKA. UTAONA UTUKUFU WA MUNGU.




MATHAYO 20: 17-19; YOHANA 11: 1-15


YESU NA WANAFUNZI WAKE WAKO NJE YA MLANGO,
WAAMBIE WANINGOJEE HAPO. NI HATARI SANA KWAO KUINGIA NA MAFARISAYO NA MAKUHANI WOTE WAPO. BADO WANATAFUTA KUMUUA
HAPANAAA!
AAHHHHH
JAMANI LAZARO!


BWANA, KAMA UNGALIKUWA HAPA, KAKA YANGU HANGELIKUFA
NDUGU YAKO **ATAFUFUKA** KUTOKA KWA **WAFU**.
NAJUA KWAMBA ATAFUFUKA WAKATI WA **UFUFUO** MWISHO WA ULIMWENGU.


MIMI NDIMI UFUFUO NA UZIMA.
YEYE ANIAMINIYE, HATA KAMA ALIKUWA AMEKUFA, ATAISHI TENA NA WALIO HAI WANAONIAMINI HAWATAKUFA KAMWE. JE! UNAAMINI HILI?


NDIO, BWANA. NINAAMINI KUWA WEWE NDIYE MASIHI, MWANA WA MUNGU, ALIYETABIRIWA KUJA ULIMWENGUNI.


BAADA YA MARTHA KUONGEA NA YESU, ALIMTUMA MTUMISHI AMLETE MARIAMU.
NJOO. ANAENDA KABURINI KULIA.
OHHHHH!
YOHANA 11: 17-31


BWANA, KAMA UNGALIKUWA HAPA, KAKA YANGU HANGELIKUFA
UMEMLAZA WAPI?


TUNAMKOSA SANA.


ANGALIA JINSI YESU ALIVYOMPENDA LAZARO.
JE! YEYE AMBAYE AMESABABISHA VIPOFU KUONA ANGEWEZA KUMZUIA RAFIKI YAKE ASIFE


TOA JIWE.
LAKINI BWANA, KWA WAKATI HUU ANANUKA, KWANI AMESHAKUFA SIKU NNE
HIVI SIKUKUAMBIA KWAMBA IKIWA UTANIAMINI UTAONA UTUKUFU WA MUNGU? ONDOA JIWE.




YOHANA 11: 32-42


LAZARO, NJOO NJE
AMEKWENDA MBALI SANA WAKATI HUU.
NDIO, ANAJIFANYA MJINGA.


MWILI TAYARI UMEANZA KUOZA.
WAKATI WATU WOTE WATASHUHUDIA YEYE NI MPOTOSHAJI, ITAFANYIKA RAHISI KWETU KUMCHUKUA NA KUMUUA


NINI?
SIAMINI!
HAIWEZEKANI


UTUKUFU KWA MUNGU!
WHOEEEE!




YOHANA 11: 43-44


LAZARO, BAADA YA KUFA SIKU NNE, ALITOKA NDANI YA KABURI, AMEFUNGWA MIKONO NA MIGUU KATIKA NGUO ZA KABURINI.
MFUNGUENI NA MUMWACHE AENDE!
NANI ANGEWEZA KUFANYA KITU KAMA HICHO ISIPOKUWA MUNGU?


KUNA NINI KELELE YOTE HII? NITOE KWENYE HIZI NGUO ZA KABURINI.
UMEKUFA SIKU NNE.
BWANA, NI VIZURI KUKUONA. NADHANI WEWE NDIO UMENIRUDISHA HAI?


OH LAZARO, TUMEKUKOSA SANA
NINA NJAA. WARUDISHENI WAOMBOLEZAJI NYUMBANI NA TULE.
UBARIKIWE BWANA MUNGU WETU


UNAWEZA KUAMINI KILE TULICHOKIONA? HAKUKUWA NA NJIA AMBAYO ANGEWEZA KUDANGANYA KWA HILO. NILIMWONA LAZARO KABLA HAWAJAMZIKA. ALIKUWA AMEKUFA KABISA, BILA SHAKA HIYO ILIKUWA KWELI.
WAKATI WATU WA YERUSALEMU WATASIKIA HAYA, WATAMFANYA MFALME.
TUTAWAAMBIA WAANDISHI NA MAFARISAYO MARA MOJA.


KWAMBA YESU ALIFANYA HILA KUBWA LEO. HATA WATU WALIOSHUHUDIA WALIDHANI KWELI ALIMFUFUA MTU KUTOKA KWA WAFU.
IKIWA KUNA UASI MWINGINE, WARUMI WATATUONDOA MADARAKANI. WANATUTARAJIA TUDUMISHE AMANI.
HAIJALISHI ALIFANYAJE; IKIWA HATASIMAMISHWA, ATANASA MIOYO YA WATU WOTE.
YOHANA 11: 44-48


LAKINI YESU HAJAWAHI KUWA MKALI AU KUSEMA KINYUME CHA UTAWALA WA ROMA.
*MANENO* YAKE NI YA *VURUGU! ANATUITA* HADHARANI *WANAFIKI*. WATU WANATUCHEKA. WANATUDHIHAKI WAZIWAZI.


LAZIMA AONDOLEWE. HATAWEZA KUJIFUFUA KUTOKA KWA WAFU.
LAZIMA IWE HIVI KARIBUNI, KABLA HAJAHARIBU HESHIMA YOTE KWA DINI YETU.
KABLA YA WARUMI KUCHUKUA HATUA DHIDI YETU


WAMENIKATAA NA WANATAFUTA KUNIUA. HAWAELEWI KWAMBA NILIKUJA *KAMA MWOKOZI WAO.* NINAWAAMBIA KWAMBA BAADA YA MIMI KUONDOKA, ROMA ITAHARIBU HEKALU WANALOLIPENDA SANA. HAKUNA JIWE LITAKALOBAKI LIMESIMAMA JUU YA LINGINE.


WAKATI UTAFIKA AMBAPO WALE WANAONIPENDA WATATUPWA GEREZANI. WATACHUKIWA NA MATAIFA YOTE KWA SABABU TU WANANIPENDA. BAADHI YENU MTAKUFA MIKONONI MWAO. WENGINE WATAFUKUZWA KUTOKA MAJUMBANI MWAO NA HAWATARUHUSIWA KUFANYA KAZI. USISHANGAE UNAPOONA MAMBO HAYA YANATENDEKA, KWA MAANA KUTAKUWA NA VITA VINGI, MATETEMEKO YA ARDHI, MAGONJWA, NJAA, NA MAJANGA YA KILA AINA, LAKINI MWISHO HAUTALETWA NA VITU HIVI.


MAMBO HAYA YATAKUWA NI MWANZO TU WA HUZUNI. YERUSALEMU ITAMILIKIWA NA WATU WA MATAIFA MENGINE MPAKA WAKATI WA MATAIFA UTAKAPOKAMILIKA. MTU ANAPOKUAMBIA KUWA NIMERUDI NA KWAMBA UNAPASWA KWENDA HAPA AU KULE KUKUTANA NAMI, USIWAAMINI. KUTAKUWA NA WATAKAOKUJA WENGI WAKIJIFANYA MIMI AU WANAJIFANYA KUNIONGEA.


LAKINI NITAKAPORUDI, NITAKUJA KAMA UMEME. KILA JICHO LITANIONA. WAFU WATAFUFULIWA NA NITAWEKA UFALME WANGU DUNIANI. LAKINI KABLA YA HILI KUTAKUWA NA WAKATI WA DHIKI KUU, MBAYA KULIKO KITU CHOCHOTE AMBACHO ULIMWENGU UMEWAHI KUONA.
MATHAYO 10:22, 24: 2, 5-9, 21, 27-31; LUKA 19: 43-44, 21: 8; YOHANA 11: 49-53; UFUNUO 2:10


BWANA, MARTHA ALINITUMA NIKUTAFUTE. ALISEMA NIKUAMBIE KUWA WEWE NA WANAFUNZI WAKO MNAKARIBISHWA NYUMBANI KWAO. YERUSALEMU SI SALAMA TENA KWAKO. WATU WENGINE HAWAFURAHII KWAMBA ULIMFUFUA BWANA WANGU KUTOKA KWA WAFU. TUNAOMBA UJE UKAE NASI.
TUTAFURAHI KUJA. NINGEPENDA KUWAONA MARA MOJA ZAIDI KABLA YA SAA YANGU YA MAJARIBIO.


NI YESU NA WANAFUNZI WAKE.
BWANA, NYUMBA YANGU NI YAKO. TAFADHALI INGIA UPUMZIKE.
*LAZARO,* RAFIKI YANGU, UNAONEKANA BORA KULIKO MARA YA MWISHO KUKUONA. NI VIZURI KUJA NYUMBANI KWAKO BADALA YA KABURI LAKO.


TUNA KARAMU ILIYOANDALIWA. WAGENI WAMEALIKWA.
BWANA, WEWE NI UFUFUO NA UZIMA.




MATHAYO 20:19, 26: 2; YOHANA 12: 1-2, 14: 6


WEWE NDIYE UFUFUO NA UZIMA. YEYE ANAYEKUAMINI WEWE HATAKUFA KAMWE.


MARIAMU, UNAFANYA NINI NA MANUKATO HAYO?


BWANA WANGU, WEWE NI UFUFUO NA UZIMA. YULE ATAKAYEKUAMINI *HATAKUFA KAMWE.*


MARIAMU, MANUKATO HAYO YANA THAMANI YA MSHAHARA WA MWAKA. KWANINI UNAPOTEZA?
LAKINI YEYE ANAMTIA MAFUTA MWALIMU
INAWEZA KUUZWA NA PESA IKAPEWA MASIKINI.


MARIAMU ALIPANGUZA MIGUU YA YESU KWA NYWELE ZAKE.
ACHANA NAYE. AMEFANYA HIVI KWA KUTARAJIA MAZISHI YANGU YANAYOKUJA.


ANAMAANISHA NINI, ***MAZISHI?***
ALISEMA ANGEENDA KUSULUBIWA. LAKINI HAKIKA HAIMAANISHI KUSULUBIWA KWA KIFO.


NIMEKUAMBIA KWAMBA MCHUNGAJI MWEMA HUUTOLEA KONDOO WAKE UHAI. NITAKATALIWA, NITASULUBIWA, NA KUZIKWA, LAKINI SIKU YA TATU NITAFUFUKA.
MARIAMU ANAUANDAA MWILI WANGU KWA MAZISHI. SAA YANGU IMEFIKA, SAA AMBAYO NAPASWA KUTUKUZWA. NJOONI, LAZIMA TUENDE YERUSALEMU, AMBAPO ITAFANYIKA.
MATHAYO 20:19; YOHANA 10:11, 12: 3-8


BWANA, YERUSALEMU YOTE INAKUSUBIRI UJE!
NENDA UKANILETEE PUNDA NIPANDE. TUTAKWENDA YERUSALEMU MARA YA MWISHO.


BWANA, KUNA *MAELFU* WANAKUSUBIRI UINGIE YERUSALEMU. WATAKUFANYA UWE ***MFALME***.
NITAKATALIWA NA KUSULUBIWA, LAKINI SIKU YA TATU NITAFUFUKA KUTOKA KWA WAFU


MSIFUNI, MFALME WA WAYAHUDI
AMEBARIKIWA YEYE AJAYE KWA JINA LA BWANA
ASIFIWE MWANA WA DAUDI


FANYA NJIA KWA MFALME WA ISRAELI.
MUNGU ASIFIWE
MKOMBOZI ALIYEAHIDIWA.
YOHANA 12: 12-13


WATU HUMWITA MFALME WA WAYAHUDI
WANAFIKIRI YEYE NDIYE *MASIHI, ALIYEAHIDIWA!*
KWA NINI ANAKUJA HEKALUNI? LAZIMA AJUE KUWA MAISHA YAKE YAKO HATARINI.
MWANA WA DAUDI, UTUOKOMBOE


WANAENDELEA KUITUMIA VIBAYA NYUMBA YA MUNGU. INAONEKANA KAMA SOKO BADALA YA NYUMBA YA SALA
NAWEZA KUKUPA HII KWA BEI NZURI SANA. TAYARI IMEIDHINISHWA KWA DHABIHU.



SAMAHANI, LAKINI IKIWA UNATAKA KIWANGO BORA CHA UBADILISHAJI ITABIDI UENDE MAHALI PENGINE. HIYO NI OFA YANGU BORA
MATHAYO 21: 11-12


YESU KWA MARA INGINE. ALITAKASA HEKALU KWA WEZI NA MATAPELI
KRASH
ONDOENI UUZAJI HUU KWA NYUMBA YA BABA YANGU. NYINYI NI WEZI NA WANYANG'ANYI.
UNAKUJA HAPA KUPATA PESA KWA WALE WANAOKUJA HEKALUNI KUOMBA. NA PESA ZAKO ZIENDE KUZIMU PAMOJA NAWE.
TAZAMA!


UNAFANYA HIVI KWA MAMLAKA GANI?
BANG!
UNAFIKIRI WEWE NI NANI?
KRASH
USIFANYE NYUMBA YA BABA YANGU KUWA YA *WANYANG'ANYI*.


BWANA, MAKUHANI NA MAFARISAYO WAMETUMA WAPELELEZI KUTUANGALIA. KUNA UVUMI KWAMBA WATAKUWEKA GEREZANI KABLA YA PASAKA, AMBAYO NI SIKU CHACHE TU KUTOKA SASA.
UNAJUA INAMAANISHA NINI KWAKE KUTAKASA HEKALU BAADA YA KUINGIA KWA USHINDI HUKO YERUSALEMU?


NIMESHAWAAMBIA KWAMBA LAZIMA NITESEKE KWA MIKONO YAO NA NISULUBIWE, LAKINI BAADA YA SIKU TATU NITAFUFUKA.
NDIO, UNABII UNASEMA KWAMBA "*BIDII YA NYUMBA YA MUNGU IMEMLA*" NA KWAMBA "*ANGEKUJA KWA HEKALU LAKE GHAFLA.*" NI MADAI YA KUWA MASIHI.
LAZIMA ASIMAMISHWE KABLA YA PASAKA. TUNAYE MPELELEZI KATI YA WANAFUNZI WAKE.
ZABURI 69: 9; MATHAYO 21: 12-13


NINAWAONYA, BAADA YA MIMI KWENDA, WATAWAFUNGA GEREZANI, WATAWAPIGA, NA WENGINE WENU WATAWAUA. MTAWASHUHUDIA JUU YA UPENDO NA NGUVU ZANGU. WATAKAPOWAPELEKA KORTINI, NITATIA MANENO KINYWANI MWENU. WATOTO WATATOA USHAHIDI DHIDI YA WAZAZI WAO, NA WAZAZI DHIDI YA WATOTO WAO. MTACHUKIWA KWA SABABU MNANIJUA. MANABII WENGI WA UWONGO WATATOKEA NA KUDAI KUNIWAKILISHA MIMI. ROHO MTAKATIFU ATAKUWA PAMOJA NANYI.
MWALIMU, NI NINI ISHARA YA KURUDI KWAKO DUNIANI NA MWISHO WA ULIMWENGU?


MWALIMU, NI NINI ISHARA YA KURUDI KWAKO DUNIANI NA MWISHO WA ULIMWENGU?
MTU ANAPOSEMA KWAMBA NINARUDI WAKATI FULANI, AU KWAMBA NIKO MAHALI FULANI, MSIMWAAMINI, KWANI NITARUDI, LAKINI ITAKUWA KAMA KASI YA UMEME. KUWA MWAMINIFU KWANGU, NA MWISHOWE UTAOKOLEWA KUTOKA KWA HUKUMU ZITAKAZOWAJIA WENYE DHAMBI. KESHENI BASI, KWA MAANA HAMTAJUA SIKU WALA SAA NITAKAYORUDI.


KAMA ILIVYOKUWA KATIKA SIKU ZA NUHU, NDIVYO ITAKAVYOKUWA KABLA SIJARUDI. WATU WALIKUWA NA SHUGHULI NYINGI NA RAHA NA HAWAKUJUA WALIKUWA KATIKA HATARI MPAKA MAFURIKO YALIPOKUJA NA KUWAOSHA WOTE. NITAKUJA GHAFLA, KAMA VILE MWIVI HUJA USIKU.
WANAUME WAWILI WATAKUWA WAKIFANYA KAZI SHAMBANI. MMOJA ATACHUKULIWA KWENDA KUKUTANA NAMI NA MWINGINE ATABAKI NYUMA KUTESEKA.
WANAWAKE WAWILI WATAKUWA WAKISAGA UNGA PAMOJA. MMOJA ATACHUKULIWA NA MWINGINE ATAACHWA. ANGALIENI NA MWE TAYARI, KWANI NITAKUJA SIKU AMBAYO HAMTARAJII.


BWANA, LAZIMA NIENDE KUMUONA MTU KATIKA JIJI. NITARUDI BAADAYE.
NENDA, YUDA, UKAFANYE UTAKALO


IKIWA BEI NI SAWA, NAWEZA KUMTIA YESU MIKONONI MWAKO.
LAKINI WEWE SI YUDA, MMOJA WA WANAFUNZI WAKE?
NDIO, NIMEKAA NAYE KWA MIAKA MITATU, LAKINI NIMECHOKA NAYO. ANAONGEA KICHAA, NA NINGEWEZA KUTUMIA PESA.




MATHAYO 26: 14-16; MARKO 13: 5-13; LUKA 17: 26-37; YOHANA 12: 23-24; 2 PETRO 3:10


SASA ROHO YANGU *INA WASIWASI*. NAMI NISEME NINI, "BABA, NIOKOE KUTOKA SAA HII"? ***HAPANA,*** KWA SABABU NIMEKUJA ULIMWENGUNI KWA TUKIO HILI.



BABA, LITUKUZE JINA LAKO MWENYEWE.


TAYARI NIMELITUKUZA JINA LANGU NA NITAFANYA HIVYO TENA
ILIKUWA SAUTI KUBWA KAMA RADI
MUNGU AMESEMA NAYE!
MALAIKA AMEZUNGUMZA NAYE!


SAUTI HAIKUWA KWA AJILI YANGU, LAKINI KWA AJILI YENU. SASA UMEFIKA WAKATI AMBAPO MKUU WA ULIMWENGU HUU, SHETANI, ATASHINDWA. NA IKIWA NITAINULIWA JUU YA MSALABA KUFA, NITAWAVUTA WATU WOTE KWANGU.
TUNAJUA KWAMBA MANABII WALISEMA KWAMBA MASIHI ATAISHI MILELE, NA WEWE UNASEMA UTAKUFA; BASI MASIHI NI NANI?


MTAKUWA NA NURU PAMOJA NANYI MUDA KIDOGO TU. AMININI NURU WAKATI IPO, ILI MPATE KUWA WANA WA MUNGU.
ANAONEKANA WAZIMU HUYU.


MTU YEYOTE AKINIKATAA MIMI NA MANENO YANGU, HUYO ANAMKATAA MUNGU. MIMI NI NURU YA ULIMWENGU. UKINIAMINI MIMI HAUTAKAA GIZANI, LAKINI UTAKUWA NA UZIMA WA MILELE
YOHANA 12: 27-36



SURA YA 11

# PASAKA NA MATESO


NENDENI MKATUANDALIE CHAKULA CHA PASAKA TULE.



NIMETAMANI KULA PASAKA HII NANYI KABLA SIJATESEKA. SITAKULA TENA MPAKA UFALME WA MUNGU UTAKAPOKUJA HAPA DUNIANI. NA KISHA MTAKULA KATIKA MEZA YANGU, NA MTAKETI KATIKA VITI VYA ENZI MKIHUKUMU MAKABILA KUMI NA MAWILI YA ISRAELI.
NITAKUAMBIA JAMBO ILI LITAKAPOTOKEA UTAAMINI. MAANDIKO YALITABIRI KATIKA ZABURI 41: 9, *"ANAYEKULA MKATE NAMI AMEINUA KISIGINO CHAKE JUU YANGU."* KWA MAANA NAKWAMBIA KWAMBA MMOJA WENU AMBAYE MKONO WANGU UKO PAMOJA NAMI MEZANI ***ATANISALITI***.
HAPANA!


IMEDHAMIRIA SANA, LAKINI OLE WAKE MTU ATAKAYEFANYA JAMBO KAMA HILO.


BWANA, NI *MIMI?* SITAKI KUKUSALITI.
BWANA, SIO *MIMI,* SIVYO?
BWANA, SINGEKUSALITI KAMWE.

LUKA 22: 8-23


NI MMOJA WENU AMBAYE HUTUMBUKIZA MKONO WAKE PAMOJA NAMI KWENYE BAKULI.



TULIKUNJA MKATE WETU KWENYE BAKULI.
YOHANA ALINONG'ONA NA KUMWULIZA YESU NI NANI ATAMSALITI. YESU AKASEMA, "NI YULE NITAKAYEMPA MKATE HUU BAADA YA KUUTUMBUKIZA."


BWANA, NI MIMI?
UNASEMA HIVYO


YESU ALITUMBUKIZA MKATE NA AKAMPA YUDA.


UNAYOFANYA, FANYA HARAKA.


SASA NITATUKUZWA. WATOTO WADOGO, SITAKUWA NANYI TENA KWA MUDA MREFU
YUDA ANAENDA WAPI?
BWANA AMEMWAMBIA AENDE MAHALI PENGINE HARAKA; KWA KUWA YEYE HUBEBA BEGI LA PESA, LABDA ANAENDA KUTOA MISAADA KWA MASIKINI.


SASA NITATUKUZWA. WATOTO WADOGO, SITAKUWA NANYI TENA KWA MUDA MREFU.
HAMUWEZI KWENDA HUKO NIENDAKO. SASA NINAWAPA AMRI MPYA, KWAMBA MPENDANE. KWA HILI WATU WOTE WATAJUA YA KUWA NINYI NI ***WANAFUNZI*** WANGU, NA KWAMBA MNAPENDANA.
ZAKARIA ALITABIRI JUU YA SAA HII AKISEMA, *"NITAMPIGA MCHUNGAJI, NA KONDOO WATATAWANYIKA MBALI."* BAADA YA KUFUFUKA KUTOKA KWA WAFU NITATANGULIA KWENDA GALILAYA. NYOTE MTANIKANA USIKU HUU.


BWANA, INGAWA KILA MTU ANAKUKATAA, *MIMI* SITAKUKATAA
PETER, KABLA JOGOO HAJAWIKA MARA MBILI, UTANIKANA MARA TATU.


AFADHALI NIFE NA WEWE LAKINI NISIKUKANE.
HAKUNA NJIA AMBAYO NINGEKUKANA KAMWE!
HATA KWA MATESO SIWEZI KUKUKANA.


MAANDIKO YAKO WAZI: NYOTE MTANIKANA. TENA, NABII ISAYA ALISEMA JUU YANGU, *"ALICHUKULIWA KANA KWAMBA NI MKOSAJI."*
PETRO, BAADA YA KUREGESHWA KWA IMANI, WATIE ***NGUVU*** NDUGU ***ZAKO*** KATIKA IMANI.




MATHAYO 26: 33-35; YOHANA 13: 31-38; 1 WAKORINTHO 11: 24-25


MWILI WANGU UTAVUNJWA KWA AJILI YENU.


CHUKUA NA ULE YOTE.


KIKOMBE HIKI CHA DIVAI KINAWAKILISHA AGANO JIPYA LINALOTEGEMEA DAMU YANGU AMBAYO ITAMWAGWA ILI KULIPIA DHAMBI ZENU.


KUNYWA YOTE. SITAKUNYWA TENA TUNDA LA ZABIBU MPAKA NITAKUNYWA NA WEWE KATIKA UFALME WANGU.


KATIKA SIKU ZIJAZO WAKATI MTAFANYA HIVI, MTAKUWA MNAKUMBUKA KIFO CHANGU HADI NITAKAPORUDI TENA.




YOHANA 14: 1-3; 1 WAKORINTHO 11: 24-26


LAKINI BWANA, HATUJUI UNAKOKWENDA, TUNAWEZAJE KUJUA NJIA YA KUJA KWAKO?


UNAIJUA NJIA, KWA MAANA MIMI NDIYE NJIA, UKWELI NA UZIMA. HAKUNA MTU ANAYEWEZA KUJA KWA BABA ISIPOKUWA AJE KUPITIA MIMI. IKIWA UNANIJUA, UNAMJUA BABA, NA UMEMWONA.


MWALIMU, TUONYESHE BABA NA TUTARIDHIKA.
FILIPO, UMEKUWA NAMI KWA MUDA MREFU NA BADO HUJANIJUA? IKIWA UMENIONA, UMEMWONA BABA PIA. MIMI NA BABA NI KITU KIMOJA.


SITAWAACHA PEKE YENU, NITAKUJA KWENU NINYI. ULIMWENGU HAUTANIONA TENA, LAKINI NITAMTUMA ROHO MTAKATIFU AKAE NDANI YENU NA KUWAFARIJI. YEYE ATAKUWA NDANI YENU NA ATAWAONGOZA KWENYE UKWELI WOTE.
IKIWA MNANIPENDA, SHIKENI AMRI ZANGU. NITAWAPA AMANI AMBAYO ULIMWENGU HAUWEZI KUCHUKUA.



IKIWA MNANIPENDA MNGEFURAHI, KWA SABABU NINARUDI KWA BABA YANGU. NIMEWAAMBIA MAMBO HAYA KABLA HAYAJATUKIA ILI MPATE KUAMINI.
INUKENI, TUIMBE WIMBO KISHA TUTAENDA KWENYE BUSTANI TUKAOMBE.




MATHAYO 26:30; YOHANA 14: 5-10, 15, 25-30


FUATA KIMYA KIMYA. TUTAKWENDA KWENYE SEHEMU YETU YA SIRI KUOMBA.


MSIHUZUNIKE KWA SABABU NILISEMA KWAMBA KITAMBO KIDOGO NITACHUKULIWA KUTOKA KWENU, HALAFU BAADA YA KITAMBO KIDOGO MTANIONA TENA.
KWA MAANA INGAWA MTALIA, HUZUNI YENU ITAGEUZWA KUWA FURAHA ***KUU. NILI***TOKA KWA BABA, NA HIVI KARIBUNI NITARUDI KWAKE.
SASA UNAONGEA WAZIWAZI. TUNAAMINI.
JE! SASA UNAAMINI? KWA MUDA MFUPI SANA NYOTE MTANIA***CHA*** NA KUTAWANYIKA. KAENI HAPA NAENDA MBALI KIDOGO NA KUOMBA.


BABA, SAA IMEFIKA. NIMEMALIZA KAZI *ULIYONI*PA KUIFANYA. NA SASA NITUKUZE KWA UTUKU*FU NILI*OKUWA NAO PAMOJA NAWE KABLA YA KUUMBWA ULIMWENGU. NIMEWAFUNDISHA JUU YAKO NA WAMEPOKEA MANENO YANGU. ULIMWENGU UTAWACHUKIA KAMA VILE ULIVYONICHUKIA MIMI, KWA SABABU NINAWAAMBIA UKWELI JUU YA DHAMBI ZAO. WAO SIO WA ULIMWENGU HUU. SIOMBI UWATOE ULIMWENGUNI, BALI UWAZUIE NA YULE MWOVU.
NINAWAOMBEA PIA WALE WOTE WATAKAONIAMINI KUPITIA USHUHUDA WAO. MAPENZI YANGU NI KWAMBA WOTE WAWE PAMOJA NAMI KAMA MIMI NILIVYO NA WEWE. BABA, UPENDO AMBAO UMENIPENDA UWE NDANI YAO NA MIMI NDANI YAO.




MATHAYO 26:31, 38; YOHANA 16: 19-20, 17: 1-10


BABA, IKIWA INAWEZEKANA, ONDOA KUTOKA KWANGU KIKOMBE HIKI CHA GHADHABU AMBACHO LAZIMA NINYWE. HATA HIVYO SITAKI KUFANYA MAPENZI YANGU, BALI YAKO. NITAKUNYWA IKIWA NI LAZIMA.


YESU ALIKUJA ULIMWENGUNI KUWA MBEBAJI WA DHAMBI, LAKINI WAKATI ULIPOWADIA, ALIDHARAU AIBU YA MSALABA, KWANI ILIMAANISHA KWAMBA ALIFANYWA KUWA DHAMBI KWA WATU WOTE WA WAKATI WOTE.
BABA, IKIWA INAWEZEKANA, ACHA KIKOMBE HIKI KIPITE KUTOKA KWANGU.


LAKINI SIO MAPENZI YANGU; MAPENZI YAKO YATIMIZWE
YESU ALITOKWA NA JASHO, MATONE MAKUBWA YA DAMU.


MARA MALAIKA AKATOKEA, AKAMHUDUMIA YESU
MTAKATIFU, SAA YAKO YA MATESO IMEFIKA, LAKINI BABA YU PAMOJA NAWE. JESHI LOTE LA MBINGUNI LITATAZAMA KESHO UNAPOCHUKUA DHAMBI ZA ULIMWENGU JUU YAKO.
TULIKUWA HAPO ULIPOUMBA ULIMWENGU; TUTAKUWEPO UTAKAPOIKOMBOA


ZABURI 23: 5-6; LUKA 22: 41-44; YOHANA 17:12; WAEBRANIA 6: 6, 12: 2
KESHO SHETANI ATASHINDWA NA DENI LA DHAMBI LITALIPWA.
IBRAHIMU NA JESHI LOTE LA PARADISO WANANGOJEA KUJA KWAKO. WAMEANDAA MEZA MBELE YAKO MBELE YA ADUI ZAKO; KIKOMBE CHAKO KINAPITA. HAKIKA WEMA NA REHEMA ZITAKUFUATA, NAWE UTAKAA KATIKA NYUMBA YA BWANA MILELE.
SIMAMA. *YUDA,* MWANA WA UHARIBIFU, ANAKUJA KUKUSALITI.


BABA, KWA SABABU HII, NALIKUJA ULIMWENGUNI


MMELALA USINGIZI. JE! HAMNGEWEZA KUWA MACHO HATA KWA SAA MOJA? SIMAMENI, NASALITIWA KATIKA MIKONO YA WENYE DHAMBI.


BWANA, NI VIZURI KUKUONA HAPA. LAKINI NINAHOFU KWAMBA NIMEFUATWA


YUDA, *UNANISALITI* KWA *BUSU?*




MATHAYO 26:40, 45-50; YOHANA 12:27, 18: 1-4


YESU WA NAZARETI.
MIMI NDIYE.


TAZAMA! ANA NGUVU!
ASKARI WALIMWOGOPA YESU NA WAKAANGUKA CHINI CHINI.


HUYO NDIYE.
UNAOGOPA NINI?
MCHUKUE!


HAUTACHUKUA MWALIMU WANGU.




YOHANA 18: 4-6, 10


ACHA! HAKUTAKUWA NA UMWAGIKAJI DAMU TENA HAPA. PETRO, RUDISHA UPANGA WAKO MAHALI PAKE. IKIWA NINGETAKA, NINGEWEZA KUITA MALAIKA 10,000 KUJA KUNISAIDIA. HII NI SAA YA GIZA.
ALIKATA SIKIO LANGU!


MNANIJIA NA MAPANGA KANA KWAMBA MIMI NI MHALIFU. NILIKUWA PAMOJA NANYI KATIKA HEKALU. KWA NINI HAMKUNICHUKUA WAKATI HUO? NITAKUAMBIA KWANINI. NI ILI MAANDIKO YATIMIE.


MUNGU ANISAIDIE!


HII HAPA, NZURI KAMA MPYA.


NI *MIMI* MNATAKA. HATUTATOA UPINZANI WOWOTE. NICHUKUE NA UWAACHE HAWA WENGINE WAENDE.


NI *MUUJIZA!*
AMENIPONYA SIKIO!
***AMENIPONYA SIKIO!***




MATHAYO 26: 52-57; MARKO 14: 51-52;
LUKA 22: 50-51


ENDELEA KUSONGA; WANATAKA KUMALIZA HII KABLA WATU HAWAJASIKIA JUU YAKE.


WALIMLETA YESU MAHALI AMBAPO MAKUHANI NA MASHUHUDA WALIKUWA WAMEKUSANYIKA
WANANIAMBIA UNADAI KUWA *MASIHI*, NA KWAMBA UNASEMA *MUNGU* NI *BABA* YAKO. UMESEMA WEWE SI WA ULIMWENGU HUU. UNATOKA WAPI?
NIMEFUNDISHA KATIKA MASINAGOGI NA HEKALUNI. SIKUFUNDISHA KWA SIRI. KWANINI MNANIULIZA? WAULIZE WALE WALIONISIKIA. WANAJUA NILICHOSEMA


GLUNK


HAUWEZI KUJIBU KUHANI MKUU KWA NJIA HIYO.
IKIWA NIMESEMA MABAYA, BASI SHUHUDIA MABAYA HAYO. LAKINI IKIWA NIMESEMA VIZURI, KWA NINI UNINIPIGA




YOHANA 18: 19-23



ALISEMA ATALIHARIBU HEKALU NA KULIJENGA KWA SIKU TATU BILA MIKONO YAKE
HAPANA, ALISEMA IKIWA MTU MWINGINE ATAHARIBU HEKALU BASI ATAIJENGA TENA.
HAMKUWA HATA HUKO. NIKASIKIA ALICHOSEMA. ALIJIELEKEZA MWENYEWE ALIPOZUNGUMZA JUU YA KUHARIBU HEKALU. NADHANI ALIKUWA AKIONGEA JUU YA MWILI WAKE MWENYEWE KUHARIBIWA


HUO NI *UJINGA*. ANGEWEZAJE KUJENGA MWILI WAKE MWENYEWE BAADA YA SIKU TATU?
SIJUI. ANGEWEZAJE KUINUA HEKALU KWA SIKU TATU


HUSIKII WAKIKUSHTAKI? JE! HUTAJIBU MWENYEWE?


YESU ALIKAA KIMYA.
MPUMBAVU HATAJIBU


NINAKUAMURU KWA MUNGU ALIYE HAI KUSEMA NA KUJIBU IKIWA WEWE NDIYE KRISTO, MWANA WA MUNGU ALIYE HAI.
MIMI NI MWANA WA MUNGU. NA UTANIONA NIKIKAA MKONO WA KUUME WA NGUVU NA KURUDI DUNIANI HAPA KATIKA MAWINGU YA MBINGUNI


HATUHITAJI MASHAHIDI WOWOTE ZAIDI. TUMEMSIKIA KWA MASIKIO ***YETU*** WENYEWE. ANAKUFURU KWA KUDAI KUWA ***MWANA WA MUNGU.*** ANASTAHILI ***KIFO!***
KUHANI ALIRARUA MAVAZI YAKE KAMA ISHARA YA HUZUNI YAKE KUBWA.
*MFUNGE MACHO,* NA TUTAONA NI NABII WA AINA GANI
MATHAYO 26: 59-65


ANGALIA IKIWA ANAWEZA KUTABIRI.. NILIDHANI WEWE NI NABII.
*MPIGE!* ALIHARIBU BIASHARA YANGU HEKALUNI.
ACHENI AFANYE *MUUJIZA.*


MPIGE TENA!


CRACK!
ANGALIA JINSI ALIVYO DHAIFU!
WHOP!
TOA UNABII NA UTUAMBIE NI NANI ALIYEKUPIGA
PONYA VIDONDA VYAKO. TUONYESHE *MUUJIZA*.


WAKATI HUO HUO, NJE YA JUMBA LA KUHANI MKUU, PETRO ALIKUWA AMEMFUATA YESU KUTOKA MBALI.
*NAKUJUA!* NILIKUONA UKIWA NA HUYO MTU YESU. WEWE NI MMOJA WA *WANAFUNZI* WAKE, SIVYO?
SIMJUI *YESU*. NATAKA TU KUONA KINACHOENDELEA.




MATHAYO 26: 71-75, 27: 1-2; LUKA 22: 58-62, 23: 1


NDIO, HAKIKA WEWE NI MMOJA WA WANAFUNZI WAKE. NILIKUONA UKIWA PAMOJA NAYE KWENYE MIKUSANYIKO KADHAA.
$?! # & !, MWANAMKE, SIJAWAHI KUMUONA MTU HUYO HAPO AWALI MAISHANI MWANGU.


COCK-A-DOODLE-DO
COCK-A-DOODLE-DO
COCK-A-DO
JOGOO HUYO ANAWIKA MAPEMA KIDOGO, SIVYO?
WANAMLETA NJE. INAONEKANA WALIMPA WAKATI MGUMU.


WALISEMA WAMPELEKE KWA MAAFISA WA SERIKALI KWA HUKUMU.
WANAFIKI WANENE WANATAKA MTU MWINGINE AFANYE KAZI YAO CHAFU.
MPE KIBOKO
PETRO ALISIKIA JOGOO AKIWIKA NA AKAKUMBUKA MANENO YA YESU, KWAMBA KABLA JOGOO HAJAWIKA MARA MBILI, ATAMKANA YESU MARA TATU. ALIPATWA NA AIBU JUU YA UOGA WAKE.
MATHAYO 26: 71-75, 27: 1-2; LUKA 22: 58-62, 23: 1


WEKA PAKA-YA-MKIA TISA KWAKE
MUNGU, *NIMEFANYA NINI?* NILIMKANA MARA **TATU**, KAMA ALIVYOSEMA. KWA NINI HII INATOKEA? KWANINI ANATESEKA HIVYO?
HAYA. HATUNA USIKU WOTE.
BABA, NIPE NGUVU.


UNATAKA NINI HAPA? JE, HATUKUKULIPA VYA KUTOSHA KWA USALITI WAKO KWA BWANA WAKO?
NIMEBADILISHA MAWAZO YANGU. MFUNGUE NA NITAKUPA PESA
NI PESA YA *DAMU, ISISYOSTAHILI;* HATUTAIGUSA. BWANA WAKO ATAKUWA AMEKUFA KABLA YA SIKU HII KUPITA. HUNA CHA KUOGOPA. TUNAWEZA KUKUTUMIA KATIKA KUKUSANYA WENGINE.


CHUKUA PESA ZAKO. SITAKI. SIWEZI KUISHI NA HATIA YANGU
CLING
PING




MATHAYO 27: 3-6


SIWEZI *KUISHI* NA HILI


MUNGU, SHIDA YANGU NI NINI?


KWA NINI SIKUWEZA KUDHIBITI TAMAA YANGU?


LABDA KIFO KITANIPA AMANI ..


NILIMWONA LAKINI HAKUNA KITU AMBACHO NINGEWEZA KUFANYA KUMZUIA
HARAKA, LAZIMA TUMKATE; LABDA BADO YUKO HAI!


LAKINI HATA WALIPOKUWA WAKIPANDA JUU YA MTI, ROHO YA YUDA ILIKUWA TAYARI IKIINGIA KWENYE MOTO WA LAANA.


ANAPOANGUKA UTALAZIMIKA KUMKAMATA, AU ATAANGUKA KWENYE BONDE KALI.
MATHAYO 27: 5


YEYE YUKO MBALI SANA


NI FUJO GANI! AMEPASUKA NA KUMWAGIKA JUU YA SHAMBA
UGG! INANIFANYA NIWE MGONJWA.
HILI PIA LILITABIRIWA NA MANABII.


MMENILETEA NINI, MZUSHI MWINGINE? MCHUKUENI NA MMSHUGHULIKIE YEYE KULINGANA NA SHERIA ZENU.
UHALIFU WAKE NI NINI?
ANASTAHILI KUFA, AU TUSINGEMLETA KWAKO. UMECHUKUA NGUVU ZETU ZA KUMPIGA MAWE MTU ANAYEKUFURU HADI KUFA, KWA HIVYO TUNAKUJA KUOMBA RUHUSA YAKO


ANADAI KUWA MFALME.
JE! WEWE NI MFALME WA WAYAHUDI?
SASA UFALME WANGU SIO WA ULIMWENGU HUU. IKIWA NI HIVYO, WATUMISHI WANGU WANGEPIGANA KUHIFADHI MAISHA YANGU.


JE! WEWE NI *MFALME* BASI?


NILIKUJA ULIMWENGUNI KUSHUHUDIA UKWELI. KILA MTU ALIYE WA UKWELI ANASIKILIZA KILE NINACHOSEMA.




ZEKARIA 11: 12-13; MATHAYO 27: 8; MARKO 15:14;
LUKA 23: 1-4; YOHANA 18: 29-38; MATENDO 1:18


NI MIJELEDI NGAPI?
WALISEMA WAMPE KIWANGO CHA JUU, VIBOKO 39
TUTAONA JINSI MHUBIRI HUYO ALIVYO MGUMU.
MKIA WA PAKA-YA-TISA NI MJELEDI WENYE KIPINI CHA MBAO CHENYE UREFU WA INCHI KUMI NA NANE NA MIKANDA TISA YA NGOZI YENYE UREFU WA FUTI TATU NA MIAMBA MKALI AU MFUPA AU CHUMA ILIYOFUNGWA MWISHO WA KILA KAMBA


UAAAA
KWA NGUVU!
CRACK
MARAFIKI ZAKE WAKO WAPI SASA?
HAJAOMBA REHEMA.
LABDA HII ITAMUUA NA TUTAMALIZANA NA MIUJIZA YAKE.


THELATHINI NA TANO
THELATHINI NA SITA
THELATHINI NA SABA
THELATHINI NA NANE
THELATHINI NA TISA
LUKA 23:11; YOHANA 19: 1-2


MGONGO WAKE UMEHARIBIKA.
KWELI, SIKU ZOTE NILITAMANI KUMPIGA MJELEDI MFALME


ALISEMA ALIKUWA MFALME. VAA VAZI HILI LA ZAMBARAU.
MFALME ANAHITAJI TAJI.


HA, HA, HA! HII ITAFANYA TAJI NZURI
OUCH!


HAPA, CHUKUA FIMBO YAKO YA *ENZI*, EE MKUBWA. ***HA, HA, HA!***
WEKA TAJI JUU YA KICHWA CHAKE NZURI NA NGUMU.


TUNAKUTIA TAJI MFALME WA ULIMWENGU WOTE!
AAUUHHHH!


SASA SIMAMA WIMA.
SHIKA FIMBO YAKO YA ENZI, MFALME
HA, HA! UISHI MUDA *MREFU MFALME.*
NDIO, HADI JUA LITAKAPOTUA *AKIBAHATIKA.*
YOHANA 19: 1-3


MFALME WA KIRUMI HANA NDEVU.


SASA, HIYO INAONEKANA ZAIDI KAMA MFALME.


YEYE HAFURAHISHI; HATA HAOMBI AHURUMIWE. HEBU TUMRUDISHE KWA PILATO


TAZAMA *MFALME* WAKO
HATUNA MFALME ILA *KAISARI.*
ANGALIA MTU HUYO. UNGETAKA NIFANYE NINI NAYE
*MSULUBISHE! MSULUBISHE!*


UNAWEZA KUMCHUKUA NA ***KUMSULUBISHA***. SIONI KOSA KWA MTU HUYU.


UNAMAANISHA *HAKUNA KOSA?* ANADAI KUWA MWANA WA MUNGU.





ZABURI 22; ISAYA 50: 6, 53: 5, 7; LUKA 23: 13-22; YOHANA 19: 4-8


WEWE NI NANI? KWANINI HAUTANIJIBU? JE! HUJUI KWAMBA NINA UWEZO WA *KUKUUA?*
HUNGEKUWA NA NGUVU IKIWA BABA YANGU ALIYE JUU HANGEKUPA.


NAKWAMBIA, SIONI KOSA KWA MTU HUYU. NITAMWACHILIA
UKIMWACHILIA, WEWE SI RAFIKI WA KAISARI.
MSULUBISHE! MSULUBISHE!
MCHUKUE NA UFANYE UTAKAVYO. NITAANDIKA KARATASI ZINAZOELEZEA UHALIFU WAKE. LAKINI MIMI SINA HATIA KATIKA DAMU YA MTU HUYU WA HAKI.




MATHAYO 27:24; YOHANA 19: 9-17


NADHANI ANASHINDWA.
THUD.
CRUNCH.



AMKA, LA SIVYO NITAKUPIGA *MJELEDI.*
HAPA, ***WEWE!*** MSAIDIE MTU HUYU KUBEBA MSALABA WAKE.
***KWANINI MIMI?***


ALIFANYA NINI?
ALIMPENDA KILA MTU.


AH, YESU, TUNASIKITIKA SANA.
MABINTI WA YERUSALEMU, MSINILILIE MIMI. JILILIENI NINYI WENYEWE NA WATOTO WENU, KWA MAANA UTAKUJA WAKATI AMBAPO WALE WALIO YERUSALEMU WATAJIFICHA KWA HOFU NA KUOMBA KUFA.


YESU ALIBEBA MSALABA WAKE MPAKA MAHALI PA KIFO. KULIKUWA NA WEZI WAWILI AMBAO PIA WALIBEBA MISALABA YAO SIKU HIYO.
KULIKUWA NA WATU WENGI AMBAO BADO WALIMPENDA YESU NA KUMHESHIMU, LAKINI WALIOGOPA SANA KUSEMA.
MATHAYO 27:32; LUKA 23: 26-33


HAPA, KUNYWA HII. ITAPUNGUZA MAUMIVU.
*HAPANA*, LAZIMA NIFANYE MAPENZI YA BABA YANGU.
BADO ANAFIKIRIA YEYE NI MWANA WA ***MUNGU***.


MNYOOSHE.
LETA NYUNDO NA MISUMARI.


SHIKILIA SANA SASA. ATAPIGANA KAMA MWENDAWAZIMU KWA MPIGO WA KWANZA. LAZIMA UENDELEE KUMTULIZA MPAKA MSUMARI UPENYE KATI YA MIFUPA NA NDANI YA KUNI.


HAPANA! MWANANGU!
BAM
CRNCH


KWA NINI UNAFIKIRI ANAFIKIRIA YEYE NI MWANA WA MUNGU?
KITU KUHUSU UNABII WA ZAMANI. *NANI ANAJUA?*
ZABURI 22; ISAYA 53; MATHAYO 27: 33-34


SHIKILIA MIGUU HIYO BADO. KAWAIDA HII INACHUKUA KUGONGWA MARA KADHAA ILI MSUMARI KUPENYA KATI YA MIFUPA.


OH MARIAMU, SIAMINI NINAWEZA KUVUMILIA
SIKUWAHI KUFIKIRIA INGEKUWA HIVI.
VUTENI, NYINYI WAJINGA..
NINGEWEZA KUTUMIA MSAADA KIDOGO, NGURUWE WAVIVU.


BABA, WASAMEHE, KWA MAANA HAWAJUI WATENDALO.
SOTE *TULIMWACHA*
*YOHANA,* NIMEFURAHI SANA KUWA UKO HAPA. HALI NI *MBAYA ZAIDI.*
ZEKARIA 13: 6; LUKA 23: 32-34


HAPA KUNA NGUO ZAKE. NITACHUKUA HII MOJA TU.
HAPANA HUWEZI. TUTAGAWANYA MARA NNE
HATUWEZI KUGAWANYA HII. IMEUNGANISHWA
TUTARUSHA KETE KWA HIYO.
MAANDIKO YALITABIRI KWAMBA WANGEGAWANYA VAZI MOJA NA KUCHEZA KAMARI KWA ILE NYINGINE


MWENYE KETE YA JUU ZAIDI ATACHUKUA YOTE.
ANGALIA, LEO, DAMU INAKUTIRIRIKA



ALIOKOA WENGINE. YEYE MWENYEWE HAWEZI KUJIOKOA
WEWE, YESU, ULISEMA UNAWEZA KUHARIBU HEKALU NA KULIJENGA KWA SIKU TATU. JIOKOE MWENYEWE NA USHUKE MSALABANI.
HEBU KRISTO, MFALME WA ISRAELI, SASA ASHUKE KUTOKA MSALABANI ILI TUWEZE KUONA NA KUAMINI.
ULAGHAI
ALIMTUMAINI MUNGU, KWAMBA ATAMWOKOA. MUNGU NA AMWOKOE SASA, KWA KUWA AMEMPENDA MUNGU.
ZABURI 22:18; MATHAYO 27: 39-43; YOHANA 19: 23-24


HAPA, KUNYWA HII NA ITAPUNGUZA *MAUMIVU* YAKO.
HAPANA



IKIWA WEWE NI MWANA WA MUNGU, JISHUKISHE HAPA NA TUTAWAUA WARUMI KADHAA.
KWANINI UNAZUNGUMZA HIVYO? HUMWOGOPI MUNGU, UKIJUA UKO KARIBU KUFA?


TUNASTAHILI KILE TUNACHOPATA, LAKINI HUYU NI YESU. HAJAFANYA CHOCHOTE KIBAYA.
YESU, UNIKUMBUKE WAKATI UNAKUJA KATIKA UFALME WAKO


LEO HII UTAKUWA PAMOJA NAMI PARADISO.




ZABURI 69:21; LUKA 23: 36-43; YOHANA 19: 25-27


ANGA LIKAWA GIZA KAMA USIKU NA LIKAKAA HIVYO KWA MASAA MATATU WAKATI YESU ALIKUWA AKINING'INIA MSALABANI. ILIKUWA SAA YA GIZA. KRISTO YESU ALIKUWA AKIFIA DHAMBI YA ULIMWENGU

WAKATI UZITO WA DHAMBI ULIPOMJIA YESU KABISA, ALILIA




MUNGU ALIMFANYA KUWA DHAMBI KWA AJILI YETU.
MATHAYO 27: 45-50; LUKA 23: 44-46; YOHANA 19:30; 2 WAKORINTHO 5:21
BABA, NINAWEKA ROHO YANGU MIKONONI MWAKO
EE YOHANA, *ANAKUFA!* SIWEZI KUAMINI KUWA *ANAKUFA* KWELI!
*IMEKAMILIKA!*
NAYE AKAFA



NA GHAFLA KUKAWA NA TETEMEKO KUBWA LA ARDHI.
NI HUYU *YESU*, MFALME WA WAYAHUDI. ALIKUWA MTENDA *MIUJIZA*.
NINI KINAENDELEA? KWANZA ANGA LINAGEUKA GIZA KAMA *USIKU*, NA SASA ARDHI INATETEMEKA.
HAFANYI MIUJIZA YOYOTE SASA. AMEKUFA


KUMEKUCHA TENA. HII NI SIKU YA AJABU.
NDIO, NA INAFANYIKA TU BAADA YA MTU HUYU KUFA


KWELI HUYU ALIKUWA MWANA WA MUNGU.


TUMEAGIZWA KUVUNJA MIGUU YAO. WANATAKA WAFARIKI NA WATOLEWE KUTOKA KWENYE MISALABA YAO KABLA YA JUA. KESHO NI MOJA YA SIKU ZAO TAKATIFU.
ILITABIRIWA KWAMBA ATAKUFA MSALABANI LAKINI HAKUNA MFUPA MWILINI MWAKE UTAKAOVUNJIKA. NA NDIVYO ILIVYOTIMIA.
HAKUNA HAJA YA KUVUNJA YAKE. ALIKUFA TU. JE, UNAJUA ALISEMA NINI KABLA YA KUFA? ALIMWULIZA BABA YAKE ATUSAMEHE KWA KUMUUA. WANANIAMBIA ALIKUWA MTU MTAKATIFU ALIYEFANYA MIUJIZA.





ZABURI 34:20; ZEKARIA 12:10; MATHAYO 27:54; YOHANA 19: 31-37


ANGALAU HAWAKUMVUNJA MIGUU
MARIAMU, NITAONA IKIWA NITAWEZA KUPATA MSAADA WA KUMUANDAA KWA MAZISHI.


SABATO INGEANZA JIONI, NA ILIKUWA JIONI. ILIBIDI WAHARAKISHE KUUINGIZA MWILI KABURINI


YOHANA 19:31, 38
YUSUFU, TAJIRI, AMBAYE HAKUWA MMOJA WA WALE WANAFUNZI KUMI NA WAWILI, ALIJITOLEA KABURI LAKE KUMZIKA YESU.
ITAKUWA SABATO HIVI KARIBUNI. TUTAMWEKA KWENYE KABURI LANGU MPYA.
HIVYO NI VIZURI YUSUFU. UMEKUWA RAFIKI MZURI.



## SURA YA 12

# UFUFUKO NA KANISA LA KWANZA


UNAJUA ALITUAMBIA, MARA KATHAA KWAMBA HILI LINGEENDA KUTENDEKA. MIMI HUWA SIELEWI MBONA. NI KANA KWAMBA ALIKUWA ANATAKA AFE KWA JINSI HII. ALIJUA WAKATI NA KILA KITU. ALITUAMBIA TENA USIKU WA JANA.
HARAKISHA MUDA UNAYOYOMA


HATUJAKUWA NA MUDA WA KUTAYARISHA MANUKATO YA MWILI.
TUTARUDI BAADA YA SIKU ZA SABATO ZIKISHAPITA.
LAKINI HIYO ITAKUWA *SIKU TATU KUTOKA SASA.*
NI HAYO TU TUNAWEZA FANYA.
KUINGIA HIVI, KUWA MWANGALIFU USIANGUKE.


MAKUHANI WALIRUDI KWA PILATO.
BWANA, HUYU MDANGANYIFU ULIYE MSULUBISHA ALISEMA, BAADA YA SIKU TATU AKIWA KABURINI ATAFUFUKA.
UTAKUWA MSIBA KAMA WANAFUNZI WAKE WANGEPENYA NDANI NA KUUBEBA MWILI WAKE. UNAFAA KUWEKA WALINZI NJE YA KABURI KUZUIA HILI.
NITATUMA WALINZI. IFANYE IWE SALAMA UWEZAVYO.




MATHAYO 25:59-66, YOHANA 19-40


MSIJALI KUHUSU KUPOTEA KWA MASIHI WENU. HATUJAWAI POTEZA MFU AU SIO WANAUME?
HA HA HA


SIKU TATU BAADA YA KUZIKWA KWA YESU.
HUU NDIO WAKATI WETU WA KWANZA KUWAHI LINDA MTU ALIYEKUFA.
KUTAKUWA ASUBUHI HIVI KARIBUNI NA TUTAPUMZIKA.


KUTAKUWA ASUBUHI HIVI KARIBUNI TUHARAKISHE, SIKU TATU ZIMEPITA TAYARI.
NATAMANI TUNGEKUWA TUMEFANYA HILI MAPEMA.




MATHAYO 28:1-2, LUKA 24:1


NA KWELI NI KUBWA
SIKILIZA WALE WANAUME WANAOPIGA MAYOWE. MTU ANAEZA KUWA AMEUMIA.


NI NINI SASA?
ALAAAA...


NI MIUNGU
ATATUUWA
ANASONGESHA MAWE
MAMA WA MUNGU TUHURUMIE


USINIACHE MUNGU. NIHURUMIE
HAIWEZEKANI
KIMBILIENI UHAI WENU
MATHAYO 28:2-4


LILE JIWE NI KUBWA MNO. TUTAPATAJE WANAUME WA KULISONGESHA?
SIJUI LAKINI IMEKUWA SIKU TATU BILA HIVI VIUNGO MWILI UNANUKA.
HAWAKUFAHAMU KUWA ASKARI WALIKUWA WANALINDA KABURI


DAKIKA CHACHE BAADAE
JAMAA ASHASONGESHA JIWE


MWILI WAKE UMEENDA. KABURI LI TUPU


ALAA NYIE NANI. UKOWAPI MWILI WA YESU?
YALE PALE NI MAVAZI YA KABURI
MSISHAGAE NAJUA MNAMTAFTA YESU ALIYESULUBISHWA. HAYUKO HAPO. ALISHAFUFUKA JINSI ALIYOSEMA.
NJOO MUONE MAHALI ALIPOKUWA AMELAZWA KISHA MUENDE NA KUWAAMBIA WANAFUNZI WAKE KWAMBA YESU ATAWAPATA GALILAYA.


YESU YU HAI! UNASEMA ASHAFUFUKA KUTOKA KWA WALIO WAFU; KAMA LAZARO;
HARAKISHA LAZIMA TUENDE NA TUWAMBIE WANAFUNZI.
WALE WATU NI MALAIKA
YESU YU HAI
MARKO 16: 3-8


YESU YU HAI. TUMETOKA KABURINI HIVI SASA
YESU HAKUWA PALE LALINI KULIKUWA NA MALAIKA.
TUKAKUMBUKA KWAMBA YESU ALISEMA ATAFUFUKA TENA SIKU YA TATU
MALAIAKA WALISEMA YESU ATAKUTANA NANYI GALILAYA.


PETRO UNAENDA WAPI?
KWA KABURI.


YOHANA AKAMFUATA NA AKAMZIDI PETRO
YOHANA SUBIRI SIWEZI KIMBIA KAMA WEWE


NI TUPU




YOHANA 20:2-9


YOHANA MAVAZI YA KABURI YAMEKUNJWA NIKAMA ALIAMUKA NAKUTEMBEA.
HAPANA HAIWEZEKANI.
LAKINI MALAIKA WAKO WAPI? WANAWAKE LAZIMA WAWE WANAONA VITU VISIVYO.


ULIONA WANAUME WAMEVALIA NGUO NYEUPE?
HAKUKUWA NA WANAUME ILA MALAIKA. MWILI WAKE UMEENDA.


SNIFF, SNIFF
MWANAMKE MBONA UNALIA?


KWASABABU WAMEUCHUKUA MWILI WA YESU NA SIJUI WAMEUWEKA WAPI.


MARIAMU


BWANA




YOHANA 20:7-17


WANAFUZI HAWAKUAMINI KWAMBA YESU ALIFUFUKA KUTOKA KWA WAFU.
PETRO NA YOHANA HAWAKUPATA KITU KABURINI. NATUDHANI KWAMBA KUNA MTU ALIUIBA MWILI WAKE. WALE WANAWAKE WENDAWAZIMU WANAFAA KUKOMA MAZUNGUMZO YAO YANAUDHI KILA MTU.
TUNAFAA KURUDI EMAU HAKUNA CHOCHOTE CHETU KILICHO SALIA HAPA.


HII NI SIKU YA TATU
NDIO MBONA ALIWARUHUSU WAMUUE NA ALIKUSUDIA KUFUFUKA KUTOKA KWA WAFU.
NDIO NA ANGETAKA KUWA MFALUME HANGEFANYA HAYA YOTE KWA SIRI. AU SIO?


HIVI, NAWEZA TEMBEA NA NYINYI?
*WHUUUUUU* UMENISHTUA ... UMETOKEA WAPI.
*KWELI* NI SIKU NJEMA *KWA* KUTEMBEA.


NILIWASIKIA MKIONGEA NIKIWAKARIBIA MNAONEKANA WENYE HUZUNI.
HAUJASIKIA YALE AMBAYO YAMETENDEKA SIKU TATU ZILIZO PITA KUMHUSU YESU WA *NAZARETI*?


TULIKUWA NA TUMAINI KWAMBA YEYE NI MASIHI LAKINI ALISULUBISHWA.
ASUBUHI YA LEO WANAWAKE FULANI WALIENDA KWA KABURI LAKE NA KUPATA MWILI WAKE HAUPO. WALIDAI KWAMBA WALIONA MALAIKA NA ALIWAMBIA YU HAI.




ZABURI 22, ZAKARIA 13:7, LUKA 24:13-26


HUYU YESU WA NAZARETI MWENYE WALISULUBISHA ALIDAI KUWA YEYE NI *KRISTO* NA KUWA YEYE NI SAWA NA MUNGU, SIVYO? ISAYA ALISEMA KRISTO ANGEITWA MWENYE NGUVU. MUNGU BABA WA MILELE. SI YESU ALISEMA MKIMWONA MMEONA BABA? MADAI YAKE YAMEDHIBITISHWA NA MAANDIKO MATAKATIFU.


ISAYA PIA ALISEMA KWAMBA KRISTO ATARUDI WAKATI HAKUNA MFALME MYAHUDI ISARAELI AMA YUDA, NA NI KWA WAKATI HUU SASA. ALIENDELEA KUSEMA YA KWAMBA MASIHI ATAZALIWA NA MAMA BIKRA. KULINGANA NA NABII MIKA ATAZALIWA BETHLEHEMU YA YUDA AMBAPO YESU ALIZALIWA.
UNABII UNATUFAHAMISHA KWAMBA ATAKUWA WA FAMILIA YA MFALUME DAUDI. YUSUFU NA MARIAMU WOTE NI WA FAMILIA YA DAUDI.


NABII ALISEMA KWAMBA KRISTO ATAFUNGUA MACHO YA VIPOFU NA ATAFUNGULIA WAFUNGWA NA ATAKUWA MCHUNGAJI WA ISRAELI NA ATAKUJA SAYUNI KAMA ***MKOMBOZI***.


ISAYA ALITABIRI YA KWAMBA ATAKATALIWA NA ISRAELI. MANABII PIA WALITABIRI KUTESEKA KWAKE. ATASALITIWA NA RAFIKI YAKE KWA PENI THELATHINI. HATAJITETEA MBELE YA HAKIMU. ATAPIGWA NA KUUMIZWA, NDEVU ZAKE ZITAVURUTWA, WATAUTAZAMA MWILI WAKE ULIO BILA NGUO NA KUMUTEMEA MATE USONI MWAKE, ATAPEANA MGONGO WAKE KWA WAPIGAJI WATAKAO MPIGA KULIKO MTU YEYEOTE YULE.


NABII ZAKARIA ANATUAMBIA YA KWAMBA MKOMBOZI ATANDUNGWA, NA KWAMBA MARAFIKI ZAKE WATAMCHAPA NA WATATENGENEZA VIDONDA KWENYE MIKONO YAKE NA MIGUU, PIA ATAONGOZWA KAMA MWANAKONDOO KUELEKEA KICHINJIONI NA HAYO YOTE YATAKUWA KWA SABABU YA KIFO CHAKE NA ATAZIKWA KWENYE KABURI LA TAJIRI.


LAKINI HUU HAUKUWA MSIBA AMBAO HANGEUZUIA. HIVI YESU HAKUSEMA KWAMBA HAKUNA BINADAMU ANAYEWEZA TOA UHAI WAKE? ISAYA ALISEMA KWAMBA ILIMFURAISHA MUNGU KUMUUMIZA YEYE KWA VILE ROHO YAKE ILITOLEWA KAMA DHABIHU. KWA SABABU YA DHAMBI ZA WENGINE ALIPIGWA NA KUBEBA DHAMBI ZA WENGI NA ATAOKOA WENGI KWA KIFO CHAKE.
BADO KIFO HAKIKUWA MWISHO ISAYA ALIONA KWAMBA MAISHA YAKE YATAENDELEA BAADA YA KIFO; ATAINULIWA NA KUSIFIWA NA KUFANYWA MKUU ZAIDI. ATAKUWA MWOKOZI WA DUNIA. HATAANGUKA MASIHI ATAKUWA AGANO JIPYA.




ZABURI 22:15, 41:9, ISAYA 7:14, 16, 9:6, 11:1, 4, 40:11, 42:4, 6-7, 45:23,49:6-7, 50:6, 52:13-14, 53:1, 3, 5, 7, 9-10, 12, 59:20, YEREMIA 23:5-6, MIKA 5:2, ZAKARIA 11:12-13, 12:10, 13:6-7, YOHANA 10:18.


HAPA NDIO KWANGU. TAFADHALI BWANA MUDA UMEYOYOMA NJOO NDANI UWE NASI USIKU WA LEO NINGEPENDA KUSKIZA WINGI WA UNABII KUMHUSU YESU.


BWANA TUNGESHUKURU SANA KAMA UNGEUOMBEA MKATE HUU.


UMEBARIKIWA EE MUNGU WETU MFALUME WA NCHI ANAYE LETA MKATE KUTOKA DUNIANI KWA HUU MKATE TUNATOA SHUKRANI.


CHUKUENI NA MULE.
YESU NI WEWE.
BWANA.


AMETOWEKA.
AMEENDA.
IMEKUWA YESU HUU MUDA WOTE HUO.
NDIO MAANA ALIKWA ANAJUA HUU UNABII WOTE.


YESU YU HAI KIFO HAKINGEMZUIA. YU HAI. TURUDI YERUSALEMU NA TUWAJULISHE WANAFUNZI WAKE.

LUKA 24:28-32


WAKATI HUO HUO PALE YERUSALEMU.
IFUNGE VIZURI MAKUHANI WAMEKASIRIKA KULIKO KAWAIDA, KWA VILE MWILI WA YESU HAUPO WANASEMA YA KWAMBA NI SISI TULIUIBA.
KUTOKA KWA KIKOSI KIZIMA CHA ASKARI?


ALISEMA YA KWAMBA ATAFUFUKA SIKU YA TATU.
SITAAMINI KWAMBA YU HAI HADI NIMWONE NA NIMWEKELEE MIKONO YANGU KWENYE ALAMA ZA MISUMARI.


NI PEPO!
NI YESU!
SAIDIA!
USIWE NA SHAKA TOMASO ULISEMA HAUTAAMINI HADI UONE. SASA NYOOSHA MKONO WAKO NA UGUZE MIKONO YANGU UHISI ALAMA ZA MISUMARI. NJOO GUZA KIDONDA KWA UPANDE WANGU.


WEWE NDIYE *BWANA* NA MUNGU *WANGU*.
TOMASO UMEBARIKIWA KWA MAANA UMEONA NA KUAMANI, LAKINI KWA WALE AMBAO WATANIAMINI BILA KUNIONA WAMEBARIKIWA ZAIDI.




LUKA 24:36-43,
YOHANA 20:26-31


NI LAZIMA MUAMBIE WANAFUNZI WOTE WANIKUTE GALILAYA, NITAWAONGELESHA HUKO.
ILIANDIKWA KITAMBO KATAIKA MAANDIKO KWAMBA KRISTO ATATESEKA KWA DHABI ZENU NA ATAFUFUKA KUTOKA KWA WAFU SIKU YA TATU NA INJILI ITAHUBIRIWA KWA JINA LAKE KATIKA NCHI ZOTE KUANZIA YERUSALEMU.


NGUVU ZOTE ZIMEPEANWA KWANGU HUKO MBINGUNI NA HUKU DUNIANI, ENDENI MKAFUNDISHE MATAIFA YOTE MWABATIZE KWA JINA LA BABA, LA MWANA NA LA ROHO MTAKATIFU. MWAFUNZE KUZINGATIA VITU VYOTE NIMEWAFUNZA NA NITAKUWA NANYI WAKATI WOTE, HADI MWISHO WA DUNIA.
KUNA VYUMBA VYENYU VIMETENGENEZWA KWA NYUMBA YA BABA YANGU. NAENDA KUANDAA MAHALI PENU. NITAKUJA TENA KUWACHUKUA BINAFSI, NITAKAPOKUWA PIA NANYI MTAKUWEPO.
MATHAYO 28:18-20, LUKA 24: 44-49, YOHANA 14:2-4


NENDENI *YERUSALEMU* NA MNGOJE ROHO MTAKATIFU AJE JUU YENU, NA AWAPE NGUVU ZA KUONGEA KWA JINA LANGU.
**ANAENDA JUU.**
ANAENDA KWA **BABA** YAKE.


NIKO NANYI WAKATI WOTE HADI MWISHO WA DUNIA.
ASHAENDA AMERUDI **MBINGUNI.**


MBONA BADO MNATAZAMA MBINGUNI.
NINI? NANI HUYO?
NIWALE MALAIKA NILIOWAONA KABURINI





LUKA 24:49-51, MATENDO YA MITUME 1:7-11


WANAFUNZI WA YESU WALIRUDI YERUSALEMU WALIVYOAGIZWA NA YESU NA HAPO WAKAENDELEA NA MAOMBI KWA SIKU KUMI WAKIONGOJEA ROHO MTAKATIFU, WALIKUWA WANAHOFIA KUONGEA KUHUSU KUFUFUKA KWA YESU ILI WAO WASIUWAWE PIA.


MAHALI WALIKUWA WAKIOMBEA PALITETEMESHWA, NA UPEPO MKALI UKAVUMA NA NDIMI ZA MOTO ZIKASHUKA JUU YAO.


WALIJAWA NA ROHO MTAKATIFU NA WAKAANZA KUMSIFU MUNGU KWA LUGHA TAFAUTI ZISIZO FAHAMIKA KWAO.


WAKATI ROHO ALISHUKA KWAO WALIPOTEZA UONGA WA BINADAMU WAKATOKA NJE WAKAANZA KUMSIFU MUNGU.
AMEBARIKIWA MUNGU NA BABA WA YESU KRISTO.
NINGESEMA WOTE NI WALEVI LAKINI WANAONGEA LUGHA YANGU BILA TATIZO.


MATENDO YA MITUME 1:12-14 ,2:1-13,32,36
WANAZUNGUMZA LUGHA YANGU PIA. HAWA WATU WANAFAHAMU AJE HIZI LUGHA ZOTE VYEMA NAMNA HII? HAO NI WATU AMABAO HAWANA ELIMU.
ENYI WATU WA ISRAELI, MLISHUHUDIA MIUJIZA AMBAYO YESU ALIFANYA. HII NI DHIHIRISHO KWAMBA MUNGU ALIKUWA NAYE, NA INGAWA MLIMSULUBISHA, MUNGU ALIMFUFUA KUTOKA KWA WAFU.


MIAKA 1000 ILIYOPITA DAUDI ALITABIRI KUMHUSU AKISEMA "KWA MAANA HUTANIACHA KABURINI, WALA HUTAMWACHA MTAKATIFU WAKO KUONA UHARIBIFU."
HIVYO BASI WACHA NYUMBA YOTE ZA ISRAELI IJUE HAYA KWAMBA MUNGU AMEMFANYA YESU ALIYE SULUBISHWA KUWA BWANA NA KRISTO.



TUTAFANYA NINI IKONENAKANA KWAMBA *TULIMSURUBISHA KRISTO?*
BADILISHENI MAWAZO YENU KUHUSU YESU KISHA MTII KWA KUBATIZWA KWA MAJI MENGI. ATAWASAMEHE DHABI ZENU NA MTAPOKEA ROHO MTAKATIFU.


YESU NI **BWANA**
NAAMINI YESU **NIBATIZE.**
BASI WALE WALIO POKEA NENO LAKE WALIBATIZWA NA SIKU HIYO HIYO WALIBATIZWA WATU ELFU TATU.


MIEZI BAADAE.
INAONEKANA KAMA JANA YESU ALIKUWA PAMOJA NASI HAPA.
HIVI SASA KUNA MAELFU YA WAFUASI WA YESU WENGI KILA LISAA.
NDIO LAKINI WAJUA NAWEZA HISI UWEPO WAKE ZAIDI HIVI SASA KULIKO ALIPOTEMBEA NASI.
ZABURI 2,16:10; MATENDO YA MITUME 2:27,34-31


TAFADHALI BWANA NAOMBA PESA KIDOGO YA MASIKINI NA WASIO JIWEZA.
PETRO SINA PESA YOYOTE UNA CHOCHOTE?
SINA LAKINI TANGU ROHO MTAKATIFU AJE KWETU TUKO NA KITU CHA KUWAPEA.


SINA FEDHA WALA DHAHABU LAKINI NITAKUPA NILICHO NACHO. KWA JINA LA *YESU KRISTO* AMKA NA *UTEMBEE*.
USIWE MKATILI. HUYU HAJAWAJI TEMBEA TANGU AZALIWE MIGUU YAKE HAIWEZI TEMBEA.


YESU KRISTO AMEKUFANYA UWE MZIMA.


GASP AHAAAAA.
BWANA MUNGU MTUKUFU.
MIGUU YAKE INAKUWA.


SIAMINI KUWA YULE KILEMA ANATEMBEA.
HAPANA ANACHUCHUMAA.
ASIFIWE MUNGU. ASANTE YESU.
MATENDO YA MITUME 3:1-11


NDIYE YULE ALIYE KUWA KILEMA MIGUU YAKE ILIKUWA IMELEMAA.
MBONA MWATUANAGALIA IVO KANA KWAMBA TUMEFANYA HUU MUUJIZA? MUNGU WA IBRAHIMU, ISAKA NA YAKOBO AMEMTUKUZA MWANAWE YESU ***KRISTO*** MLIYE MSULUBISHA.
WANASEMA ALIPONYWA NA JINA LA YESU YULE ALIYE SULUBISHWA.
MLIUWA MKUU WA MAISHA LAKINI MUNGU AKAMUINUA KUTOKA KWA WAFU NA TULIMWONA AKIWA HAI, NI KUPITIA KUAMINI NA JINA LA YESU AMBAPO HUYU KIWETE AMETEMBEA.


NAJUA NI KUPITIA KUPUUZA MLIMSULUBISHA YESU LAKINI MANABII WALITUONYA KUWA HIZI VITU ZITAKUJA KUTIMIA.
MNANIFAHAMU NYINYI WOTE. NI MUNGU TU ANGENIPA MIGUU ZANGU. AMININI NA MFUATE *YESU*.


BADILISHENI MAWAZO YENU KUHUSU YESU NA MUWE WANAFUNZI WAKE NDIPOSA DHABI ZENYU ZIWEZE KUSAMEHEWA.

WALE VIONGOZI WA DINI WALIO MSULUBISHA YESU WALITUMANA PETRO NA YOHANA WAKAMATWE.




MATENDO YA MITUME 3:12,14-19:4;1-3


SASA WANAWAKAMATA VILEMA KWA KUTEMBEA.
ILIKUWA NI MUUJIZA KAMA VILE YESU ALIVYOFANYA AKIWA HUKU.
NINA JIRANI ANAYE DAI ALIMWONA YESU AKIWA HAI BAADA YA KIFO, WANASEMA ALITOKEA WATU MIA TANO KWA WAKATI MMOJA.
NAENDA KUWATAFUTA HAO WANAFUNZI WAKE WENGINE NIJIFUNZE MENGI.


NILIDHANI TUMEMAMALIZANA NA HAO WATU TULIPO SULUBISHA KIONGOZI WAO.
WANADAI YUKO HAI.
BASI TUTAMUUA PAMOJA NA WAFUASI WAKE WOTE.
WANASEMA AKO NA BABA YAKE MBINGUNI.
SAWA HAO WAWILI WATAUNGANA NAO.
MATENDO YA MITUME 4:3-6


TUNAJUA MTU HUYU AMEKUWA KILEMA TANGU KUZALIWA KWAKE MMEWEZAJE KUMPONYA? NI KWA JINA LA NANI MMEYAFANYA HAYA?
KWA JINA LA YESU KRISTO WA NAZARETI. YULE MLIYEMSULUBISHA NA ALIYEFUFULIWA NA MUNGU KUTOKA KWA MAUTI, MTU HUYU ALIPONYWA. KUMBUKA MAANDIKO, "JIWE AMBALO WAJENZI WALILIKATAA NDILO LIMEKUWA JIWE KUU LA PEMBENI."


NA PIA HAKUNA WOKOVU KWA JINA LINGINE. KWA KUWA HAKUNA JINA LINGINE CHINI YA MBINGU LIMEPEANWA KATI YA WANADAMU, AMBALO SISI TWAWEZA KUOKOLEWA KWALO.


HAWA WATU WANAFAA KUWA WAPUUZI. HAWANA ELIMU NA WANAJUA MANENO YA MANABII.
HAKUNA HAJA YA KUKANA MIUJIZA YAKE. KILA MTU ANAJUA ALIMPONYA MTU YULE, NA WANAJUA NI WANAFUNZI WA *YESU* WANAFANYA HIVYO KWA JINA LAKE. TUNA TATIZO HAPA.
NINAWAFAHAMU. WALIKUWA NA YESU.


ZABURI 118:22, MATENDO YA MITUME 4:7-21
WAFUKUZENI WATOKE HAPA!
MKIENDELEA KUONGEA NA KUPONYA KWA JINA LA *YESU ALIYEAGA*, MTAPATA SHIDA ILIYOMPATA. MNANIELEEWA SASA? SASA ONDOKENI NA MUENDE NA NISIKIE UPUUZI HUO KUHUSU ***UFUFUO***.
MNAHUKUMU IWAPO NI VYEMA MACHONI MWA MUNGU, KUWAHESHIMU NYINYI KULIKO MUNGU. ILA LAZIMA TUZUNGUMZE MANENO TUNAYOONA NA KUSIKIA.


INJILI ILISAMBAA ISRAELI KOTE WENGI WALIAMUAMINI YESU NA WALIBATIZWA KWA MAJI.
MMESKIA HABARI NJEMA YA YESU KRISTO?
KANISA LIKAWA FAMILIA YA MAELFU WA WATU WALIOJAWA NA UPENDO NA AMANI.
YESU ALIFUFUKA NA YUKO HAI PAMOJA NASI. HATA SASA.


KANISANI WANAWAKE WALIHESHIMIWA.
TANGU FAMILIA YANGU IMUAMINI YESU KRISTO, KUMEKUWA NA AMANI KWA FAMILIA YETU KWA MARA YA KWANZA.


WAKRISTO WALIIMBA WAKIFANYA KAZI.
WAKRISTO WALIONGEZEKA NA WALIENDELEA KUGAWANA VITU VYAO. WALIMHUBIRI YESU NYUMBA KWA NYUMBA, NA HATA MIJINI WALIPOPATANA NA WATU.
MATENDO YA MITUME 13:30-32


NYINYI WATU WA ISRAELI, MNAJUA KWAMBA MUNGU ALIWAAMBIA BABA ZETU KUWA UZAO WAO INGEENDA NCHI NGENI, NA KUISHI HUKO KAMA WATUMISHI MIAKA 400. BAADAYE MUNGU ALISEMA KUWA ATAHUKUMU TAIFA HILO NA KUWAKOMBOA WATU WAKE NA KUWAW3E.


LAKINI SULEIMANI ALIMJENGEA MUNGU NYUMBA. ILA MUNGU HAISHI HEKALUNI ILIYOJENGWA NA MIKONO YA WATU. KAMA NABII ALIVYOSEMA: "MBINGU NI KITI CHANGU CHA ENZI, NA DUNIA NI MAHALI PA KUWEKA MIGUU YANGU; MTANIJENGEA NYUMBA YA NAMNA GANI? NA MAHALI PANGU PA KUPUMZIKIA NI MAHALI GANI? MAANA MKONO WANGU NDIO ULIOFANYA HIVI VYOTE"
STEFANO, USIWE MJINGA.
UNAZUNGUMZA DHIDI YA HEKALU LETU!


ISAYA 66:1, MATENDO YA MITUME 7:1-57
NYIE NI WENYE SHINGO NGUMU NA WAASI. ROHO ZENU SIO SAWA NA MUNGU. MNAPINGANA NA ROHO MTAKATIFU KAMA BABA ZENU. NYINYI NA BABA ZENU MLIWANYANYASA NA KUWAUWA MANABII WALIOTABIRI UJIO WA YESU KRISTO, LAKINI MLIMSALITI NA KUMUUA PIA.


STEFANO, WEWE UNAJIITA MYAHUDI?
MNAWEZA KUHARIBU MILA NA SHERIA ZETU KISHA MBADILISHE NA NINI? MTU ALIYEKUFA NA HAJAONEKANA TANGU WAROMA WAMUUE?
NINAONA MBINGU IMEFUNGUKA, NA MWANA WA MUNGU AMESIMAMA KWENYE MKONO WA KULIA WA MUNGU. *UTUKUFU MKUU!*


FUNGENI MASIKIO YENU MSISKIZE UKAFIRI KAMA HUU!
ANASTAHILI KUULIWA!
MUONDOENI MJINI NA MMPIGE MAWE AFE.


KAFIRI!
ANAJARIBU KUHARIBU DINI YETU.
TULIMSULUBISHA YESU. WEWE TUTAKUUWA KWA MAWE.
YESU ATABAKI KUWA MUNGU HATA MKINIUA.


AMEKUFURU DINI YETU. TUNASEMA LAZIMA AFE. SAULI, TUNA RUHUSA YA SERIKALI?
NITAPIGA SAHIHI ILI AULIWE. YEYE NI MMOJA WA WANAOFUATA YESU WA NAZARETI ALIYEAGA. LAZIMA HII KUKUFURU IISHE. MPIGENI MAWE.


SAULI, NISHIKIE KOTI LANGU.
BWANA YESU, POKEA ROHO YANG UNA USIWAHESABIE MAKOSA KWA KUNIUWA.
MATENDO YA MITUME 7:58-59


CLUNK!


NA WAKATI HUO KUKAWA NA MATESO MAKUU JUU YA KANISA LA YERUSALEMU, NA KILA MTU ALIONDOKA MJINI ISIPOKUWA MITUME.
HUU NDIO MWANZO TU!
MALIZENI MAMBO HAYA YA YESU!
MUANGAMIZENI KUFURU HUYU!


KUNA WAFUASI WENGINE WA YESU HUMU?
MSIMUUMIZE BABA YANGU!
MKAMATENI MKE WAKE PIA.
MFARISAYO SAULI ALIPIGANA DHIDI YA KANISA, AKIINGIA KILA NYUMBA NA KUWAKAMATA WANAWAKE NA WANAUME NA KUWAPELEKA GEREZANI.
MATENDO YA MITUME 7:59, 8:3


MKRISTO FILIPO AKIWA ANASALI, MALAIKA ALIMZUNGUMZIA.
FILIPO SIMAMA NA UENDE KUSINI MWA NJIA INAYOELEKEA GAZA KUTOKA YERUSALEMU.


SIJUI MBONA ANANITAKA HUKO LAKINI MUNGU AKISEMA NITAKWENDA.


NI KAMA NIMEFIKA. BWANA NIFANYEJE?


BWANA, UNATAKA AJE?


MSAFARA! BWANA, HII NDIYO SABABU ULIYONITUMA HUKU? KUNA MTU HUKO UNAYEMTAKA KUWA WAKO?
NENDA UKAUNGANE NA MSAFARA HUO.
MATENDO YA MITUME 8:26-29


KULIKUWA NA MTU ALIYEKUWA NA MAMLAKA ALIYEMHUDUMIA MALKIA WA ETHOPIA. ALIKUWA MWEKAHAZINA ALIYE AMINIWA NA UTAJIRI WOTE WA UFALME. ALIKUWA AMEKUJA YERUSALEMU ILI KUABUDU KIYAHUDI, NA ALIKUWA ANAREJEA ETHOPIA. ALIKUWA ANASOMA MAANDIKO.
“ANAONGOZWA KAMA KONDOO KWENYE KICHINJIO, KWA HIVYO HAKUFUNGUA MDOMO WAKE, KWA KUWA MAISHA YAKE YALITOLEWA DUNIANI.”


NASKIA UNASOMA KUTOKA MAANDIKO YA *ISAYA.* *UNAELEWA* UNACHOSOMA?
UMEJUA NINASOMA ILA SIWEZI KUELEWA. NJOO UKETI NAMI ILI UNIELEZE MAANA.


UMETOKA YERUSALEMU?
NDIO. NIMETOKA UKO KUABUDU DINI YA KWETU HAIKUWA NA AMANI NI KANA KWAMBA MUNGU ALIKUWA MBALI.


NIMESOMA KUHUSU MASIHI ALIYEAHIDIWA. NIKIENDA YERUSALEMU WENGI WANASEMA KUWA ALIKUJA, ILA ALISULUBIWA NA BAADAE KUFUFUKA.
NIMEKUWA NIKICHUNGUZA MAANDIKO YA MANABII ILI NIONE KAMA KUNA JAMBO KAMA HILO LILILOTABIRIWA.
ISAYA 53; MATENDO YA MITUME 8:27, 30-34


KAMA UNAVYOFAHAMU, KITABU HIKI CHA ISAYA KILIANDIKWA ZAIDI YA MIAKA 800 ILIYOPITA. SURA HII YA 53 NI MOJAWAPO YA UTABIRI WA MASIHI. INASEMA "ANGEDHARAULIWA NA KUTENGWA"
UMETOKA YERUSALEMU, HIVYO UNAFAHAMU YESU ALITENDA MIUJIZA MINGI NA BADO VIONGOZI WALIMTENGA.


MSTARI WA 7 NI ULE UTABIRI AMBAO YESU ALISIMAMA MBELE YA MAHAKIMU ILA ***HAKUWEZA KUJITETEA.***
ISAYA ALITABIRI KUWA YESU ANGETESEKA KWA AJILI YA DHAMBI ZETU. NA KATIKA MSTARI WA 5 UNASEMA ADHABU YETU ITAKUWA JUU YA YESU.
DHAMBI


MSTARI WA 8 UNASEMA KUWA ALITOLEWA GEREZANI NA ANGEULIWA KWA SABABU YA DHAMBI ZETU.
HASWA NINAUPENDA MSTARI WA 6 UNAOSEMA "SISI KAMA KONDOO TUMEENDA MRAMA, KILA MTU AMEGEUKA KWA NJIA ZAKE," HIYO INATUELEZA KUWA KILA MWANADMU AMEWACHA NJIA ZA MUNGU NA KUFUATA NJIA ZAKE ZA DHAMBI, LAKINI MUNGU ALIWEKELEA YESU DHAMBI ZETU ILI ALIPOKUFA ALILIPIA UASI WETU.
INRI
DHAMBI


INRI
MSTARI WA 9 UNASEMA YESU ANGEZIKWA PAMOJA NA WATU WEMA NA WAOVU PIA.
NA MSTARI WA 9 UNASEMA KUWA YESU HAKUKUWA MTENDA DHAMBI KAMA WANADAMU WENGINE BALI ILIKUWA MAPENZI YA MUNGU YEYE ATESEKE ILI KULIPIA DHAMBI.


MSTARI WA 10 UNAONGEA KUHUSU UFUFUO NA HUDUMA AMBAYO ANGEKUWA NAYO BAADAE.
ISAYA 53:3-10, MATENDO YA MITUME 8:35, WARUMI 2:16, 2 WAKORINTHO 5:21
NA UTABIRI MWINGINE MWINGI UNATUELEZA KUWA BAADA YA KUFUFUKA, YESU ATAKETI KATIKA KITI CHA ENZI ILI BAADA YA SISI KUFA TUSIMAME MBELE YAKE NA KUTOA HESABU YA MAISHA TULIYOISHI.


NIMEWASIKIA MAKUHANI WAKIZUNGUMZIA UTABIRI WA MASIHI MARA NYINGI. MBONA WENGI WAO WALIMKANA YESU?
BAADHI YA MAKUHANI WALIMKUBALI YESU, ILA WENGINE WALIMCHUKIA SABABU ALIZUNGUMZIA UNAFIKI WAO. WALITAKA MASIHI AMBAYE ANGEWAANGAMIZA WARUMI NA WALA SIO KUFICHUA DHAMBI ZAO.


JE, KUNA UTABIRI MWINGINE AMBAO YESU ALITIMIZA?
ZABURI 22 NI UTABIRI WA KIFO CHAKE KWA ***KUSULUBIWA***.
LAKINI SI ZABURI ILIANDIKWA ZAIDI YA MIAKA 1000, KABLA YA MTU YEYOTE KUTUMIA ***KUSULUBIWA*** KAMA NJIA YA ADHABU?




KATIKA ZABURI 22:16 INATUAMBIA KWAMBA MIKONO YAKE NA MIGUU INGEDUNGWA – KAMA ILIVYODUNGWA NA MISUMARI. FUNGU LA 14 LA ZABURI 22 LAELEZEA JINSI ANGEWEZA KUWA NA KIU NA KWAMBA MIFUPA YAKE INGETOLEWA NJE YA VIUNGO KATIKA KIFO CHAKE, LAKINI BASI ZABURI 34:20 INATUAMBIA KWAMBA HAKUNA MFUPA HATA MMOJA UNGEVUNJWA ATAKAPOSULUBIWA. NA KAMA UNAVYOJUA, NI MTINDO WA KIMILA KUVUNJA MIFUPA YA WALE WALIOSULUBIWA, LAKINI YESU ALIKUFA KABLA MIFUPA YAKE KUVUNJWA. FUNGU LA 17 LA ZABURI 22 ILITABIRIWA KWAMBA WATAUTAZAMA UCHI WAKE NA MSTARI WA 18 UNAELEZEA JINSI WANGEWEZA KUPIGA KURA KWA MOJA YA MAVAZI YAKE NA KUGAWANYA MENGINE VIPANDE VIDOGO MIONGONI MWAO.

PIA, ZAKARIA 12:10 INATUAMBIA KWAMBA MIKONO YAKE ITATOBOLEWA, NA KWAMBA BAADAYE, WAYAHUDI WANGEONA ALAMA MIKONONI MWAKE. ISAYA 50:6 INASEMA KWAMBA MGONGO WAKE UTAKUWA AMEPIGWA NA KWAMBA ANGEPIGWA KWENYE SHAVU. ZABURI 16:10 INATUAMBIA KWAMBA INGAWA ANGEZIKWA, MWILI WAKE HAUNGEKAA KABURINI MUDA MREFU WA KUTOSHA KUOZA. UNABII UNATUAMBIA KWAMBA ATAKUWA AKISALITIWA NA RAFIKI ZAKE, NA KWAMBA MSALITI WAKE ANGEJINING'INZA MWENYEWE, AMBAYO INGESABABISHA MWILI WAKE KUANGUKA NA KUTAPAKAZA MATUMBO YAKE ARDHINI. MAMBO HAYA YOTE NA MENGI ZAIDI YALITIMIZWA KAMA MANABII WALIVYOANDIKA. BILA SHAKA YESU KRISTO WA NAZARETI NI MASIHI, MWOKOZI WA ULIMWENGU.

ZABURI 22:6, 17-18, 16:10, 34:20; ISAYA 50:6; ZAKARIA 12:10



NINAAMINI KWAMBA YESU NI *MASIHI*. YEYE NDIYE MWANA-KONDOO ALIYEAHIDIWA KUONDOA DHAMBI ZETU. HATUHITAJI DHABIHU TENA. YESU NDIYE MLANGO WA KUINGIA KWA MUNGU. NITAKUWA *MWANAFUNZI* WA YESU.


HAPA KUNA MAJI. NI NINI KINACHONIZUIA KUBATIZWA?
NITAKUBATIZA IWAPO UNAAMINI YESU KWA MOYO WAKO WOTE.
OH! LAKINI MIMI NINAAMINI!


NINAKUBATIZA KWA JINA LA BABA WETU NA *MKOMBOZI*, **YESU KRISTO.**


MUNGU ASIFIWE!


MTU HUYO AMEENDA WAPI?
AMETOWEKA TU.
MUNGU LAZIMA ALIKUWA ANAMHITAJI MAHALI PENGINE. TWENDE ZETU NYUMBANI ETHIOPIA NA TUMUELEZE MALKIA KWAMBA TUMEJUA KUHUSU *MASIHI*.
KANISA LILIANZISHWA NCHINI ETHIOPIA NA ILIENDELEA HADI NYAKATI ZA KISASA WAKATI WENGI WA WAKRISTO WALIUAWA NA WAISILAMU.
MATENDO YA MT.8:36-39



# SURA YA 13

# KWA ULIMWENGU WOTE


KWA KUHOFIA MAISHA, WAKRISTO WALIKUTANA KWA SIRI KUSIKIA NENO LA MUNGU NA KUIMBA SIFA.
MARAFIKI WAPENDWA, BWANA ALITESEKA ILI TUPATE ONDOLEO LA DHAMBI ZETU. SI AJABU KWAMBA TUNAWEZA PIA KUTESEKA KWA AJILI YAKE. USISHANGAE KWA MATESO TUNAYOPATA.
YESU ALISEMA, *"IWAPO MTU ANATAKA KUWA MWANAFUNZI WANGU, BASI ANAPASWA KUTWAA MSALABA WAKE ILI ANIFUATE."* HIYO INAMAANISHA KUWA KILA MTU ANAPASWA KUBEBA MSALABA WAKE NA KUELEKEA MLIMA WA KUSULUBISHWA INAPOBIDI KUAFANYA HIVO. ZABURI 22 INATUELEZA....



MUNGU TUSAIDIE. NI *SAULI* YULE MUUAJI.
*KAENI PAPO HAPO!* DINI HII YENU YA KIGENI HAITAKUBALIKA HUKU. MNAKUFURU MUNGU NA TAIFA LETU. *WAJINGA NYINYI*. NI LAZIMA *MUACHE AMA MUAGE.*
MCHUKUENI KIONGOZI WAO ILI AWE FUNZO KWAO.


TUMEKUWA NA MASIHI WENGI AMBAO TUNGEWEZA. MBONA TUMUABUDU SEREMALA *ALIYEKUFA?*
BWANA WETU YESU YUKO *UHAI* NA NDIYE MUUMBAJI WA ULIMWENGU.
UNAWEZA KUBADILISHA MAWAZO YAKO TUTAKAPOMUEKA MKE WAKO GEREZANI AOZEE HUKO.





MATHAYO 16:24, MARKO 8:34, MATENDO YA
MT.9:1-2


HUYU PIA NI MMOJA WAO WA KUMPENDA YESU.
TULIJUA HAYA YANGETENDEKA TULIPOAMINI YESU KRISTO.


NI YULE MFARISAYO ANAYEITWA SAULI. YEYE HUPUMUA CHUKI NA KUUA.
SAULI AMEJAWA NA CHUKI.
NDIO. LAZIMA TUMUOMBEE. TUOMBE KWAMBA MUNGU ATAMFANYA ROHO YAKE IWE NYEPESI NA AWEZE KUONA UKWELI.
KUMBUKA SISI PIA HAPO MWANZO TULISHUKU.


SAULI NAFIKIRIA UMEFAGIA WAKRISTO WOTE YERUSALEMU.
LA. TUNAVYOENDELEA KUWAUA NA KUWAFUNGA NDIVYO WANAVYOZIDI KUONGEZEKA. WAMETAWANYIKA KATIKA MIJI MINGINE. KATIKA MAHEKALU YA DAMASKA WAMEJAA HUKO.


NITAKUPATIA RUHUSA YA KUWAKAMATA.
NITAKWENDA SASA HIVI.
SAULI ALIJUA NI JUKUMU LAKE KULINDA DINI YAKE NA TAIFA LAKE ILA ILIMSUMBUA KUWA WAKRISTO WALIKUWA NA UTULIVU NA AMANI AMBYO YEYE HAKUWAI KUSHUHUDIA.


GHAFLA KUKATOKEA MWANGAZA MKUBWA SANA MBELE YA SAULI.
SAULI, SAULI, MBONA UNANITESA?
FARASI WA SAULI ALISHTUKA HADI AKAMUANGUSHA SAULI.


WEWE NI NANI, BWANA, KWAMBA NINAKUTESA?
MIMI NI YESU UNAYETESA UNAPOWANYANYASA WAKRISTO.
BWANA UNGEPENDA NIFANYE NINI?
SIMAMA, NENDA MJINI NA UTAELEZWA UTAKACHOFANYA.
MATENDO YA MITUME. 9:1-6


ULISIKIA SAUTI?
MIMI PA. ILIKUWA KAMA RADI.
NDIO ILA SIKUELEWA ALICHOSEMA.
SIONI! MTU ANISAIDIE NIENDE MJINI.
ILIKUWA NI SAUTI YA MUNGU.


JINA LANGU NI ANANIA. YESU ALIZUNGUMZA NAMI NA ALINIELEZA KUWA UTAPATA KUONA TENA.
MIMI NI KIPOFU KAMILI.


KWA JINA LA YESU KRISTO ANZA KUONA TENA.


NINAONA!
NA UMESEMA YESU AMEYATENDA HAYA? NIELEZE ZAIDI KUHUSU YESU.


KWA HIVYO ANANIA ALIFUNGUA MAANDIKO NA KUMUONYESHA SAULI KUHUSU UTABIRI WA MASIHI.
NDIO, NIMEKUWA MJINGA. HAYA YOTE YALIKUWA KWENYE MAANDIKO. NATAKA KUBATIZWA NA KUWA MKRISTO.
MUNGU ALIBADILISHA JINA LA SAULI KUWA PAULO.
MATENDO YA MITUME. 9:7-19


SAULI, SASA PAULO ALIKUWA MTU MPYA ALIYE NA UJUMBE MPYA. HAKUTAKA TENA KUWAUA WAKRISTO. ALITAKA KUWASHAWISHI WATU KUMUAMINI YESU.
NINAELEWA KUTOAMINI KWAKO. MIMI PIA SIKUAMINI MARA YA KWANZA ILA NAKUELEZA YESU MNAZARETI ALIWEZA KUYAFANYA AMBAYO MASIHI ALITABIRIWA KUFANYA.
ILA USHAHIDI ***MKUBWA*** NI KUWA MUNGU ALIMFUFUA KUTOKA KWA WAFU.


WEWE NI MPUMBAVU KIASI GANI? MASIHI ANGEWEZAJE KUKUBALI KUULIWA NA MAADUI WAKE?
ALIKUWA MWANA KONDOO WA MUNGU WA KUONDOA DHAMBI ZETU.


MUNGU ALIWAFIKIA WATU WA MATAIFA PIA. KULIKUWA NA ASKARI MRUMI ALIYEKUWA AKIMTAFUTA MUNGU.
MUNGU NAJUA WEWE NI MMOJA. MUUMBAJI WA WATU WOTE. DINI YA WATU WANGU NI FISADI NA HAINA AMANI. NIONYESHE NJIA ZAKO NAMI NITAZIFUATA.



NANI? NINI? WEWE NANI? NA UMETOKEA WAPI?
MAOMBI YAKO YAMESIKIKA NA NIMETUMWA NA MUNGU. TUMA WATU JOPA KWA NYUMBA YA MTU AITWAYE SIMONI. ULIZIENI MTU ANAYEITWA PETERO NAYE ATAWAELEZA UKWELI KUMHUSU MUNGU.



MUNGU AMEFANYA *AMANI* KUPITIA DAMU YA MSALABA WAKE.
PETRO, BWANA WETU NI MTU WA DINI SANA, MTU MZURI ILA ANA TAABU NYINGI. YEYE HUSALI KILA WAKATI NA KUWASAIDIA MASKINI ILA HANA AMANI NA MUNGU.
HIYO INAMAANISHA *AJE?*
NITAMUELEZA MKUBWA WENU.


MKUBWA WAO ALIPATANA NA PETRO MLANGONI NA AKAINAMA MBELE YAKE.
INUKA. USINIIINAMIE KWANI MIMI NI KAMA WEWE TU. WAKUSANYE WENGINE NA NITAWAELEZA HABARI NJEMA.


LEO NI SIKU NJEMA. MUNGU AMEMTUMA PETRO, MMOJA WA WANAFUNZI WA YESU KUTUELEZA KUHUSU YESU.
MATENDO YA MITUME.9:20-22, 10:1-27, 38-41
NDIO. NILITEMBEA NA YESU KWA MIAKA MITATU NA NUSU. NLIMUONA AKISULUBIWA NA ALIPOFUFUKA. ALIKULA NASI NA KUSHIRIKIANA NASI. KULIKUWA NA WATU 500 WALIOKUSANYIKA KUMSIKILIZA AKIZUNGUMZA BAADA YA UFUFUO WAKE. ALIKULA NASI NA TULIMGUZA. ALITUFUNZA KUWAPENDA ADUI ZETU NA KUOMBEA WANAOTUHUKUMU. ALITUMA ROHO WAKE......


KORNELLI NA WATU WAKE WOTE WALIAMINI INJILI YA YESU NA WALIBATIZWA WOTE SIKU HIYO.


PAULO ALIENDA KWA SINAGOGI ANTIOKI NA ALIWAHUBIRIA WAYAHUDI SIKU YA SABATO.
MNANIJUA. NILIWANYANYASA WAKRISTO HADI KIFO, ILA YESU ALINITOKEA KWA ISHARA KUU NA KUNIELEZA NIHUBIRI NENO LAKE. NIMETAFUTA KWENYE MAANDIKO NA NIMEPATA UTABIRI WOTE KUHUSU MASIHI NA NIKAPATA KUWA YESU ALITIMIZA UNABII WOTE.


MUNGU ALISEMA KWAMBA ANGEMTOA MWANA WA DAUDI KUWA **MKOMBOZI** WA ISRAELI. NA KWAMBA VIONGOZI WA YERUSALEMU WANGEMHUKUMU KUFA. IMEANDIKWA KWA ZABURI YA PILI *"WEWE NI MWANANGU, LEO MIMI NIMEKUZAA"*.


KATIKA ZABURI NYINGINE IMEANDIKWA KWAMBA MUNGU HATARUHUSU MTAKATIFU WAKE KUPATA UHARIBIFU. HUU NI UNABII KWAMBA INGAWA ANGEKUFA, MWILI WAKE HUNGEFIKIA KUOZA. NA IJULIKANE KWAMBA KUPITIA KWA YESU, MSAMAHA WA *DHAMBI* UNAPATIKANA. JAMBO AMBALO *MUSA* KUPITIA SHERIA HANGEWEZA KUFANYA.




ZABURI 2:7, 16:10, MATENDO YA MT.2:27, 13:33-35


UNAWEZA KUULIWA KWA MAWE SABABU YA MANENO HAYA.
SABABU MNAPINGA HABARI NJEMA YA UZIMA WA MILELE, TUTAUPELEKA UJUMBE WETU KWA WATU WENGINE WA MATAIFA KAMA VILE MANABII WALIVYOSEMA.


ILIPOKUWA WAZI KWA PAULO KWAMBA WAYAHUDI KAMA TAIFA WANGEENDELEA KUMKANA YESU ALIAMUA KUSHUGHULIKA NA MATAIFA MENGINE BALI NA ISRAELI.
SIFA ZIWE KWA MUNGU NA MWANAWE YESU. *UKOMBOZI* UMEKUJA KWA *WATU WA MATAIFA!*
*PAULO, NIBATIZE MIMI!*
TUELEZE MENGI KUHUSU UTABIRI WA UJIO WA *MASIHI.*
WENGI WALIAMINI INJILI NA WALIENDELEA KWA NEEMA YA MUNGU.


WAYAHUDI WALIKASIRIKA NA KUWAFUKUZA PAULO NA BARNABA KUTOKA MJINI NA KUWATISHIA KUWAUA IWAPO WANGERUDI. HIVYO PAULO NA BARNABA WALIENDA ASIA NA WALIHUBIRI INJILI KWA KILA MTU WALIYEPATANA NAYE.
BARNABA, NIKIANGUKA WEWE ENDELEA KUKIMBIA. USISIMAME.


KATIKA LYSTRA, WAYAHUDI WALIMPIGA PAULO KWA MAWE HADI KIFO NA KUTUPA MWILI WAKE NJE YA MJI.
*MUNGU WASAMEHE!* WAMEMUUA PAULO.
MATENDO YA MITUME. 14:19-20


LAKINI MUNGU ALIFANYA MUUJIZA NA KUMFUFUA PAULO.
PAULO, NLIDHANI UMEKUFA!
BADO, MUNGU AMENIONYESHA MATESO MENGI YALIYO MBELE YETU NA NDIO SASA TUMEANZA. TURUDI MJINI.


KATIKA FILIPI YA MAKEDONIA PAULO NA BARNABA WALIPIGWA MIJELEDI 39 NA KUFUNGIWA GEREZANI. LICHA YA KUPITIA MATESO. MIOYO YAO ILIKUWA NA FURAHA NA USIKU WALIIMBA SIFA KWA MUNGU.
EEH BWANA POKEA UTUKUFU, HESHIMA NA SIFA.


OOOH!
YESU NI
BWANA.


WHAAAP!
KWA MIAKA ILIYOFUATA PAULO ALIPIGWA KWA CHUMA MARA TATU TOFAUTI, LAKINI ALIENDELEA KUMHUBIRI YESU.
MATENDO YA MITUME.14:19-20, 16:23-25, 2 WAKORINTHO 11:24-25, UFUNUO 4:11


PAULO ALIPOKUWA AKISAFIRI AKIHUBIRI, MELI ALIYOPANDA ILIZAMA MARA TATU TOFAUTI.
SIKU MOJA ALIZAMA MAJINI NA SIKU MOJA BADAYE MELI ILIYOKUWA IKIPITA ILIMUOKOA.
PAULO ALIPIGWA NA WAKORA MARA KWA MARA.
LAKINI ALIENDELEA KUHUBIRI.


PAULO ALIGONJEKA, KUPITIA BARIDI, JOTO, NJAA, NA MAMBO MENGINE MENGI YA KUSUMBUA ALIPOKUWA AKISAFIRI DUNIANI AKIWAELEZA WATU KUHUSU YESU.
BABA, NIPONYE ILI NIWEZE KWENDA KUHUBIRI KATIKA MIJI MINGINE.


PAULO ALITEMBEA KUTOKA MJI HADI MJI AKIHUBIRI NA KUWAONYA WATU DHIDI YA KUABUDU SANAMU, NA KUELEZA HABARI NJEMA YA YESU KRISTO.
MUMEMGEUKIA MUNGU NA KUACHANA NA SANAMU. SASA NYINYI NI WANA WA *MUNGU.*
*MUNGU ASIFIWE!*


1 WAKORINTHO 10:14, 12:12-13, 18, 2 WAKORINTHO 11:25, WAGALATIA 2:16, WAEFESO 2:19
VITU HIVI HAVIJAWAI KUNIPA AMANI.
WATU WALIPOMGEUKIA MUNGU WALIACHANA NA SANAMU. WALICHOMA KILA KITU KILCHOHUSIANA NA DINI YAO YA AWALI. KATI YA MIAKA ISHIRINI KULIKUWA NA WAAMINI DUNIANI KOTE WALIOMUABUDU MUNGU KUPITIA KWA YESU KRISTO.

YESU ALIKUWA AMEWAONYA WANAFUNZI, “WAKATI HUO WATAWASALITI NINYI MPATE DHIKI, NAO WATAWAUA; NANYI MTAKUWA WATU WA KUCHUKIWA NA MATAIFA YOTE KWA AJILI YA JINA LANGU. NDIPO WENGI WATAKAPOJIKWAA, NAO WATASALITIANA, NA KUCHUKIANA. NA MANABII WENGI WA UONGO WATATOKEA, NA KUDANGANYA WENGI.”






WAKATI AMBAO WALIOKUWA WAMEMWONA KRISTO WALIKUWA WAZEE NA KANISA LILIKUWA LIMEENEA KOTE KATIKA ROMA, WARUMI WALIANZA KUTAFUTA WAKRISTO NA KUWATESA HADI KIFO. NA IWAPO WAUMINI HAWAKUMKANA KRISTO, WANGEWEZA KUWAWEKA KATIKA UWANJA, NA WATU WANGETAZAMA KAMA SIMBA NA CHUI WANAWASHAMBULIA NA KUWALA VIPANDE VIPANDE.


GRRRR!
IEEEEE!

WAKATI MWINGINE WAKRISTO WALIPIGWA HADI KUFA. WATU WALISHANGAA JINSI WAUMINI WALIKUWA WATIIFU. HAWAKUKANA IMANI YAO. WALIKUWA TAYARI KUFA KWA AJILI YA YESU.




MATHAYO 24:9-11




MIAKA AROBAINI BAADAYE, KATIKA 70 A.D., WARUMI WALIKUJA NA KUHARIBU MJI NA HEKALU. WAKATI KUNI NDANI YA HEKALU ZILIKUWA ZINATEKETEZWA DHABIHU IKICHOMWA, DHAHABU YA HEKALU ILIYEYUKA NA KUINGIA KATIKA NYUFA KATI YA MAWE, SAKAFUNI NA KWENYE MSINGI. WARUMI WALIPOVAMIA, WALIPOKUWA WAKIJARIBU KUTOA ZILE DHAHABU, WALITOA MAWE NA KUBOMOA HEKALU. HIVYO UNABII WA YESU ULITIMIZWA.

WAYAHUDI KATIKA YERUSALEMU NA ISRAELI AMBAO WALINUSURIKA VITA WALIKIMBILIA MATAIFA MENGINE, AMBAKO WENGI WAO WANAISHI MPAKA LEO.




WAYAHUDI WA KIKRISTO PIA WALIKIMBIA KWA NCHI NYINGINE AMBAPO WALIHUBIRI INJILI YA KRISTO, NA KANISA ZIKAKUA.


POPOTE WALIPOKIMBIA, TAYARI KULIKUWA NA WAKRISTO HUKO KUWAKARIBISHA.





MATHAYO 24:2; LUKA 19:43-44

MITUME WA YESU WALIENDELEA KUHUBIRI UFUFUO WA YESU KRISTO HADI VIFO VYAO. MMOJA KWA MMOJA WAO WALIUAWA. WOTE WALIKUFA KWA UJASIRI, WAKIJUA KWAMBA WALIKUWA NA NYUMBA BORA MBINGUNI.




WENGINE WALILISHWA KWA WANYAMA PORI.
BAADHI WALIPIGWA MAWE HADI KUFA.
WENGINE WALINYONGWA.


PETRO ALISULUBIWA MIGUU IKIWA JUU NA KICHWA CHINI.
YOHANA 21:18, MATENDO YA MITUME. 12:2
WENGINE WALICHEMSHWA KWA MAFUTA.
NINAENDA MAHALI PEMA. MUNGU AWASAMEHE.
SISTAHILI KUFA KIFO KAMA CHAKO BWANA.
WOTE WALIAGA NA UHAKIKA KUWA WANGEPATA MIILI MIPYA NA MAKAO MAPYA.


MIAKA SITINI BAADA YA YESU KUFUFUKA, YOHANA ALIKUWA MTUME PEKEE ALIYEBAKI. ALIHAMISHWA KWA KISIWA CHA MIAMBA KINACHOITWA PATMOS. ROHO MTAKATIFU ALIMTWAA YOHANA HADI MBINGUNI AMBAPO MUNGU ALIMWONYESHA SIKU ZIJAZO.
YOHANA, NITAKUONYESHA MAMBO AMBAYO YATATOKEA KATIKA SIKU ZIJAZO. ANDIKA YALE UNAYOONA NA UWEKE KATIKA KITABU KISHA UYAPELEKE KATIKA MAKANISA SABA YA ASIA.


WAKATI KIZAZI HIKI KITAKARIBIA MWISHO, YESU ATARUDI NA KUFUNGUA MAKABURI YA WAFU WOTE WALIOMWAMINI, PAMOJA NA WAAMINIO WALIO HAI, WATAINUKA KUKUTANA NA YESU HEWANI NA ATAISHI NAO MILELE.
MWISHOWE, MUNGU ATATEMBELEA DUNIA KWA MAAFA YA KUTISHA. MOTO UTAANGUKA NA KUTAKUWA NA MAPIGO MENGINE AMBAYO YATAHARIBU ZAIDI YA WATU WANAOISHI DUNIANI.


MTU ATAKUJA AMBAYE ATADAI KUWA MASIHI, NAYE ATADANGANYA WATU WENGI. ATAWAFANYA WATU WAONYESHE UAMINIFU WAO KWAKE NA SERIKALI YAKE KWA KUWEKA ALAMA KATIKA VIPAJI VYA USO WAO AU KWENYE NYUMA YA MIKONO YAO YA KULIA
666
1 WATHESALONIKE 4:14, 16-17; 2 WATHESALONIKE 2:3-4; UFUNUO 1:9, 11, 8: 1-13, 9:18, 13:16, 20:4
WALE AMBAO HAWATAKUBALI ILE ALAMA WATAUAWA KWA KUKATWA KICHWA. UTAKUWA WAKATI WA DHIKI KUU KWA WALE WALIOACHWA DUNIANI.


KAMA ILIVYOTABIRIWA, YESU ATARUDI TENA NYAKATI ZA MWISHO.
ATAKUJA KATIKA UTUKUFU WAKE NA NGUVU NA SIO KAMA MTU TENA. MBINGU ITAFUNGUKA NA ATASHUKA AKIWA JUU YA FARASI MWEUPE.
ATAANGAZA KAMA JUA NA KICHWANI MWAKE ATAVAA TAJI NYINGI. MKONONI MWAKE ATASHIKILIA NYOTA SABA NA NDANI YA MDOMO WAKE UTATOKA UPANGA WA UKWELI.

ATAKABILIANA NA SHETANI NA ATAMTUPA KATIKA ZIWA LA MOTO AMBAPO ATAKUWA MILELE AKITESWA NA KAMWE HATAJARIBU MWANADAMU TENA. YESU PIA ATATUPA KIFO KATIKA ZIWA LA MOTO NA ULIMWENGU UTAFANYWA MPYA.




HAKIKA MWENYEZI MUNGU ATAWAKUSANYA WOTE, AMBAO WALIMWAMINI MWANAWE NA ATAWAPATIA UZIMA WA MILELE KATIKA DUNIA MPYA. MUNGU ATAYAFUTA MACHOZI YOTE NA HAKUTAKUWA NA MAUTI TENA, HUZUNI, KILIO AU MAUMIVU, KWA SABABU MAMBO YA ZAMANI YATATUPILIWA MBALI. YESU ATATAWALA KAMA MFALME NA MWOKOZI JUU YA WATU WEMA KATIKA ULIMWENGU HURU KUTOKANA NA DHAMBI NA KIFO.

1 WATHESALONIKE 4:16; UFUNUO 1:16, 19:11-21, 20:10-15, 21: 1-4


INJILI YA YESU KRISTO IMEHUBIRIWA KWA MIAKA 2,000. YESU ALITABIRI KWAMBA UJUMBE WA UFALME UTAENEA KOTE DUNIANI KWA KILA TAIFA, KABILA, NA KIKUNDI CHA FAMILIA KITAKACHOKUWA NA WATASIKIA HABARI NJEMA.


KUNA MUNGU MMOJA TU NAYE ANA MWANA MMOJA TU. KUNA IMANI MOJA TU NA KITABU KIMOJA KITAKATIFU. KUNA NJIA MOJA YA KUINGIA MBINGUNI BAADA YA MAISHA HAYA. YESU NI NJIA, UKWELI, NA UZIMA.


INJILI YA KRISTO NI TOFAUTI NA DINI ZINGINE ZOTE ZA DUNIA KWA KUWA HAIENEZWI KWA KIKWAZO AU VITISHO. YESU ALIWAFUNDISHA WAFUASI WAKE KUPENDA MAADUI NA KUJAZWA NA FURAHA NA KUIMBA. LEO, WATU WA KILA UTAIFA NA LUGHA HUFURAHI KATIKA MSAMAHA NA UZIMA WA MILELE.
YOHANA 3:16, 14:6
HATA HIVYO, IMEKUWA KARIBU MIAKA 2,000 TANGU YESU ALIFUFULIWA KUTOKA KWA WAFU, NA BADO KUNA WENGINE AMBAO HAWAJASIKIA HABARI NJEMA. MTU LAZIMA AWAAMBIE.


# HADITHI YA KISASA YA HUKUMU IJAYO





WEWE NI MALAIKA? UNANIPELEKA WAPI?




WAEBRANIA 9:27


ANAANGALIA KUONA KAMA JINA LAKO LIMEANDIKWA KATIKA KITABU CHA UZIMA CHA MWANA-KONDOO.
"NIKAWAONA WAFU, WAKUBWA KWA WADOGO, WAMESIMAMA MBELE YA HICHO KITI CHA ENZI; NA VITABU VIKAFUNGULIWA; NA KITABU KINGINE KIKAFUNGULIWA, AMBACHO NI CHA UZIMA; NA HAO WAFU WAKAHUKUMIWA KATIKA MAMBO HAYO YALIYOANDIKWA KATIKA VILE VITABU, SAWASAWA NA MATENDO YAO"


YOHANA DOE, UNAWEZA KUKARIBIA KITI CHA ENZI
"MUNGU ATAHUKUMU SIRI ZA WANADAMU KWA YESU KRISTO."


JOHN DOE, HII NI SIKU YAKO MAHAKAMANI. UNATUHUMIWA KWA JUTENDA IDADI KUBWA YA DHAMBI. UNASIHIJE?
NDIO, NILITENDA DHAMBI ILA NLIKUWA MTU MZURI. MUULIZE YEYOTE ALIYENIJUA.





WARUMI 2:6, 16; UFUNUO 20:12


LETA KITABU CHAKE.


MAISHA
YA
YOHANA
DUE.


KITABU HICHO KINA JINA LANGU
MAISHA YA YOHANA DUE.


KIELEZO DHAMBI
KUDANGANYA 1-48
TAMAA 49-74
CHUKI 75-91
MATAMANIO
MAOVU 92-115
KIBURI 133-175
UZINZI 176-204
IBADA YA SANAMU 116-132
KUTOAMINI 205-250
ULAFI 251-271
MAUAJI 272
MATENDO YA KISHOGA
273-274


KITABU CHAKO KINAONYESHA UMETENDA DHAMBI *NYINGI*.


ULIZA YEYOTE ALIYENIJUA, NILIKUWA MTU *MZURI*.
"SI KWA MATENDO YA HAKI ULIYOFANYA, LAKINI KULINGANA NA HURUMA YAKE ALITUOKOA."

TITO 3:5


ULIKUWA MTU MZURI ULIPODANGANYA?


ULIKUWA MTU MZURI ULIPOKUWA NA TAMAA?
ULIKUWA MT MZURI ULIPOKUWA NA HASIRA?


LAKINI SIKUTENDA DHAMBI MBAYA. NILIKUWA MTU WA KIDINI.
BADO UNATOA VISINGIZIO. DHAMBI ZOTE NI DHAMBI MBAYA.

NIONDOKEENI NYOTE MLIOTENDA DHAMBI. SIWAJUI.


EEH MUNGU, HII HAIWEZI KUWA KWELI.
POLE. SAA HII UMECHELEWA SANA KUMLILIA MUNGU.


IEEE!


WAOVU... WATATUPWA KATIKA ZIWA LA MOTO; KUTAKUWA NA KUOMBOLEZA NA KUSAGA MENO.

# KITI CHA HUKUMU CHA KRISTO




YOHANA 11:25-26


JINA LAKO LIKO KATIKA KITABU CHA UZIMA.
NI WAKATI WA KUPOKEA ZAWADI YAKO.


"KWA MAANA AMEWEKA SIKU ATAKAYOWAHUKUMU WALIMWENGU KWA HAKI, KWA MTU YULE ALIYEMCHAGUA;
NAYE AMEWAPA WATU WOTE UTHABITI WA MAMBO HAYA KWA KUMFUFUA KATIKA WAFU."




MATENDO YA MITUME.17:31

Our desire is that after reading *Good and Evil®* you will be motivated to read the entire Bible and that it will come alive to you. Make it a daily habit to read a portion of the Bible and then pray that God will help you understand and apply it.

Copyright © 2008, 2017
Michael and Debi Pearl.

ALL RIGHTS RESERVED.

*Author:* Michael Pearl

*Artist:* Danny Bulanadi

*Coloration:* Clint Cearley

https://goodandevilbook.com/